

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Thelathini na Saba - Tarehe 30 Julai, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ushirika na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MHE. DR. AARON D. CHIDUO (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MASWALI NA MAJIBU

Na.345

Viwanda/Mashirika Yaliyobinafsishwa

MHE. BERNARD K. MEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeweka mikakati maalum ya kuwasaidia Wananchi katika kumiliki mashirika yanayobinafsishwa ikiwa ni pamoja na kuuza baadhi ya mashirika kwa Watanzania kwa kutumia thamani ya vitabu badala ya thamani halisi kwenye soko; na kwa kuwa, moja ya matatizo yaliyopo ni kwa baadhi ya watu waliouziwa mashirika

hayo hawajaanza ukarabati na uzalishaji katika mashirika/viwanda hivyo na kusababisha ukosefu wa ajira kwa vijana wetu:-

(a) Je, ni mashirika na viwanda vingapi ambavyo havijaanza uzalishaji hadi sasa?

(b) Je, sasa Serikali ipo tayari kupokea lawama kwa kuwaendeleza hao wanaolegalega katika kufufua viwanda/mashirika yaliyobinafsishwa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)(k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mashirika na viwanda vipatavyo 13 havijaanza uzalishaji tangu vibinafsishwe. Baadhi ya mashirika/viwanda hivyo ni *Morogoro Tanneries, Moshi Tanneries, Mwanza Tanneries, Tanzania Bag Corporation (Moshi), Moshi Hotel, TAFICO* (Dar ed Salaam), baadhi ya mashamba ya mkonge yaliyobinafsishwa kwa *Katani Ltd., Kiwanda cha Chai Dabaga, Iringa, Mkata Saw Mills Ltd., UFI, Pugu Kaolin Mines Ltd., Morogoro Polyester Textile Mills Limited* na *Mikumi Wildlife Lodge*.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu mbalimbali zimefanya mashirika na viwanda husika kushindwa/kuchelewa kuanza kufanya kazi. Baadhi ya sababu hizo ni viwanda kuwa katika hali mbaya sana na hivyo kuhitaji mitaji mikubwa. Vilevile teknolojia katika mashirika/viwanda vingi imepitwa na wakati. Hali hii huwalazimisha wawekezaji kutafuta teknolojia ya kisasa ambayo gharama yake ni kubwa na pia inahitaji kufundisha wataalam wa kuitumia kwa ufanisi na tija. Baadhi ya sera zetu kuwa kikwazo kwa wawekezaji. Mfano hapa ni viwanda vya ngozi ambavyo vilishindwa kuanza kazi kwa sababu sera zilizokuwepo miaka michache iliyopita, zilikuwa zikiwavutia zaidi wauzaji ngozi ghafi katika masoko ya nje ya nchi badala ya kuzisindika hapa nchini. Kwa bahati nzuri, Serikali imeshughulikia tatizo hili kwa kutoza kodi (*Export Tax*) kwenye ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi. Baadhi ya wawekezaji kushindwa kupata mikopo ya Mabenki kutohana na riba kubwa na kukosekana kwa dhamana za mikopo na kadhalika. Pia baadhi ya wawekezaji kupeleka malalamiko yao Mahakamani huko tukisubiri maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewasiliana na wahusika wote na kubaini matatizo yanayowakabili. Imedhihirika kwamba, wawekezaji wengi wana sababu za msingi na hivyo Serikali imewapa muda zaidi wa kutekeleza mipango yao kulingana na mikataba ya ubinafsishaji.

Kwa wawekezaji ambao imebainika kuwa hawana sababu za msingi, Serikali imechukua hatua za kisheria kwa lengo la kuyachukua (*repossess*), mashirika/viwanda

husika ili waweze kutafutwa wawekezaji wengine watakaoweza kukidhi malengo ya ubinafsishaji.

Kwa vile hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kutatua tatizo hili, Serikali haipo tayari kupokea au kubebeshwa lawama kuhusu suala hili. Serikali ipo tayari kupokea ushauri na kuufanyia kazi kikamilifu kutoka kwa Mheshimiwa Bernard Membe na Waheshimiwa Wabunge wengine wote, unaolenga katika kuboresha utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa.

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa wawekezaji wote wanafuata *business plan* na kwenye *business plan* wanaji-*commit* kwamba watazalisha, wataleta ajira na wataendeleza ufanisi wa viwanda hivyo na kukiuka hilo maana yake ni kwamba, tayari wamejiondoa katika shughuli hizo na Serikali hasa *PSRC*, inatakiwa kuchukua hatua za mara moja za kuwafukuza na kuyatoa mashirika/viwanda hivyo kwa Watanzania wenyе moyo huo. Kwa nini *PSRC* haifuatili kwa makini na kwa haraka pale mikataba inapokiukwa ili mashirika haya yaweze kutolewa kwa Watanzania wenyе moyo wa kuyaendeleza?

(b) Kwa vile Mheshimiwa Waziri anasema Serikali haistahili lawama lakini ushauri, atakuwa tayari, sasa kwamba katika kipindi cha mwaka huu kabla ya Desemba, mashirika/viwanda vyote vilivyochukuliwa na watu hawa viorodheshwe, viondolewe ili Serikali iwaondoe na kuwapatia watu wengine na isipofanya hivyo ichukue lawama mwisho wa mwaka?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, Serikali imeyafuatilia mashirika haya na nimeta sababu mbalimbali zilizowafanya hao waliobinafsishiwa viwanda hivi kutoviendeza, hii ni dhahiri kwamba, Serikali imekuwa ikifuatilia. Kama nilivyoorodhesha mashirika hayo 13, ina maana Serikali imefuatilia wapi wamekwama.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna sababu ya msingi, kutokana na swali lako la pili kwamba, mashirika hayo tuyarejeshe, kuna sababu kubwa kwamba, Serikali imechukua hatua kupeleka Mahakamani. Kunapokuwa na *Court Injunction*, Serikali haiwezi kuchukua hatua nyingine tena zaidi ya hivyo, lakini bado inafuatilia. Lakini kama nilivyosema, Serikali ipo tayari kushauriana zaidi na Wabunge juu ya masuala haya sio kwamba ilitulia tu, ilikuwa inachukua hatua zinazohitajika ili kuyarejesha mashirika haya.

MHE. ABDULA S. LUTAVI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa mimi naamini kwamba viwanda hivi vinavyozungumziwa sasa havikuwa vimeanzishwa tu kiholela na vilikuwa na mchango kwa Taifa hili, baada ya

mashirika haya kubinafsishwa na kupewa watu binafsi kuyaendesha ni nini imekuwa athari kwa uchumi wa Taifa hili kwa mashirika haya kutoendelea kufanya zile kazi zilizokuwa zimedhamiriwa toka mwanzo wakati huo huo wao walipokuwa wanaji-*commit* watafanya kazi hiyo sisi tulikubaliana nao kwamba kazi hizi watakuwa wameanza kuziendeleza katika muda gani baada ya wao kuchukua viwanda hivi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):
Mheshimiwa Spika, bila shaka athari za kiuchumi ni kwamba, Wananchi waliopo karibu na viwanda hivyo au mashirika hayo, wamekosa ajira, vilevile Serikali itakuwa imekosa kodi, mapato, bila shaka haya yanatuathiri.

Mheshimiwa Spika, lakini narudia tena kama nilivyojibu kwenye swalii la msingi kwamba, hata kama alikuwa na *business plan*, kwa kuongeza ufanisi, matatizo mbalimbali waliyoyapata katika kuwekeza ili viwanda hivi viweze kujiendesha ndio yaliwazuia wasiendelee. Bila shaka natumai Mheshimiwa Mbunge, amenisikiliza vizuri sana, nimeorodhesha kama mambo matano ambayo yamewarudisha nyuma na mojawapo ni teknolojia. Wakati viwanda hivi vimeundwa vilikuwa na teknolojia ya zamani ambayo sasa hivi vingi vyao haviwezi kutumika lazima wabadilishe teknolojia na hili ni jambo ambalo linazuia wasiendelee mbele kuviendeleza viwanda hivi.

Na. 346

Malipo ya STABEX ya Chai 1995/1996

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa malipo ya STABEX kwa wakulima ni njia nzuri sana ya kuwashamasisha wakulima hapa nchini ili waongeze bidii zaidi katika kuzalisha mazao yenye ubora wa kuweza kuingia katika ushindani wa kidunia; na kwa kuwa Serikali ilikubali kuwalipa wakulima STABEX ya Chai ya mwaka 1995/1996 na baadhi yao wamelipwa mwaka 2002 na baadhi hawajalipwa katika Vijiji vya Sagara, Mayo, Mbokoi, Kwehangala, Kweminyasa na Balangai:-

(a) Je, Kampuni ya E.K. Mangesho and Company iliyopewa mkataba wa kusimamia malipo hayo ya STABEX ilipewa mwongozo gani na Serikali kuhusu ulipaji?

(b) Je, katika Wilaya ya Lushoto walipaji hao walionana na nani kati ya hawa wafuatao, yaani Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Katibu Tarafa wa Tarafa za Bumbuli, Mgashi na Soni, Maafisa Watendaji wa Kata za Mgashi, Mayo, Bumbuli, Mponde na Funta?

(c) Je, ni nani mwenye uamuzi wa mwisho wa kulipa au kutolipa wakulima wa vijiji nilivyovitaja kati ya Waziri mhusika na kampuni niliyoitaja?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kampuni ya *E.K. Mangesho* ya Dar es Salaam iliajiriwa na Jumuiya ya Ulaya na *National Authorizing Officer*, kwa niaba ya Serikali ya Tanzania kama Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za malipo ya *STABEX* ya chai ya mwaka wa 1995/1996. Utaratibu wa kulipa fidia chini ya *STABEX 1996 - Tea*, umeelezwa kwa kirefu katika mwongozo ulioandaliwa kwa ajili hiyo. Majukumu ya Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu yamefafanuliwa chini ya utaratibu huo. Tayari Mheshimiwa William Shellukindo, amepatiwa nakala ya kumbukumbu hiyo.

Chini ya mwongozo ulioandaliwa kwa ajili ya malipo ya *STABEX ya chai*:-

(a) Malipo yanzeingatia kiasi cha majani mabichi ambayo wakulima waliwasilisha kwenye viwanda vya kusindika chai au kwenye vituo vya kununulia chai kati ya tarehe 1 Julai, 1995 na tarehe 30 Juni, 1996. Malipo yangefanyika kikamilifu bila makato yoyote. Kinachohitajika hapo ni kumbukumbu za manunuza ya majani mabichi za viwanda vya chai. Wakulima ambao wangestahili malipo ni wale walioandikishwa katika skimu za wakulima wa chai na ambao wangakuwa wamefikishwa majani mabichi moja kwa moja kwenye viwanda.

Kiasi cha malipo kwa kilo ambacho kingelipwa kwa kila mkulima kingetangazwa katika vyombo vya habari pamoja na jumla ya malipo ambayo yangelipwa kwa wakulima kupitia kwenye kila kiwanda. Habari hizi zingetolewa pia kwa kila Kamati ya skimu na kuwekwa kwenye mbao za matangazo ya kila kiwanda.

Muda wa wiki sita kuanzia siku fedha zilipochukuliwa kutoka Benki ultolewa kwa ajili ya kufanya malipo. Kila mkulima alitakiwa kujitambulisha kupitia kwenye Kamati ya Kijiji au kwa kuonyesha kitambulisho.

Uliwekwa utaratibu wa kukata rufaa na wahusika walitakiwa kutoa malalamiko yao na ushahidi unaohusika katika muda wa siku tano tangu kutolewa kwa orodha za walipwa na katika muda wa wiki sita uliotengwa kwa ajili ya kukata rufaa. Mkaguzi wa Ndani alipewa uwezo wa kukubali au kukataa rufaa yoyote.

(b) Kuna ushahidi kwamba viwanda vya chai viliwasiliana na vijiji na kwamba uongozi wa *STABEX* uliweka mipango ya kukutana na viongozi wa vijiji na wakulima ili kuthibitisha usahihi wa kumbukumbu za mauzo ya chai. Kwa mfano, tarehe 11 Desemba, 2001, Meneja wa Mashamba ya *New Mponde Tea Factory* aliviandikia vijiji vya Kwabora, Mayo, Mgashi na mashamba ya Sagara na Kwevumo akiwataka wakutane na uongozi wa *STABEX* tarehe 12 Desemba, 2001. Barua hizo zilinakiliwa kwa Maafisa Watendaji wa Kata.

(c) Mwongozo wa malipo uliweka utaratibu ambao haukuhitaji maamuzi ya kiutawala na haukumhusisha Waziri wala Wizara. Kilichohitajika ni kumbukumbu sahihi tu.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenyeye maelezo mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mimi natoka katika Jimbo la Bumbuli na hakuna huduma za posta za kuweza kuchukua barua kwa siku moja na kuwapata watu siku ya pili. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba hapo ndipo tatizo lilipoanzia?

(b) Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunipa mkataba lakini kwa kuwa katika sehemu ya mwisho ya mkataba, Kifungu cha 8, kinataja suala la *procedures for errors and omissions relating to the amount payable* na vitu vingine, je, kazi hii ilifanyika ambapo mlipaji alitakiwa aifanye bila kuondoka katika sehemu ile?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kweli hakuna posta iliyotumika lakini mashamba hayo yako karibu sana na maeneo walikowasilisha chai mbichi na kwa hiyo mawasiliano yalikuwa ya karibu. Vilevile ukiangalia katika muda wa kuwasiliana na kufanya *appeals* ulikuwa muda mrefu wa wiki sita bado mtu aliweza kufanya *appeals* zilizotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkataba, naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane nami kwamba, suala hili halikuwa na utata kama anavyoelezea kwa kuwa lilihusisha watu wengi sana. Lilihusisha *Internal Auditor, CMU-Dar es Salaam, EC Delegate, National Authorizing Officer, Tea Factory, Scheme Committee* ya wanachama wenyewe na Benki, hawa wote walihusika pamoja na mawasiliano na Makatibu Kata, naamini nafasi ilikuwa nzuri kuamua utata wowote uliotokea.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa *STABEX* hii ambayo kawaida analipwa kwa wakulima wa chai vilevile hulipwa kwa wakulima wa kahawa, napenda kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni sababu zipi za msingi ambazo zilipelekeea kuwalipa wakulima wa chai *STABEX* kama alivyoelezea lakini wakulima wa kahawa wasilipwe. Je, haoni kwamba hii ni *double standards* na anataka wakulima wa kahawa waielewe vipi Serikali?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, *STABEX* ya chai ulikuwa utaratibu pekee na *STABEX* ya kahawa una utaratibu pekee tumeshauyeleza na mafao yao hayakuwa ya aina moja kama ilivyoelezwa. Kwa hiyo, naomba tufuate taratibu za kahawa kama zilivyo na hizi za chai kama zilivyo lakini haya mawili sio kitu kimoja.

Mradi wa Farkwa Multipurpose Dam Scheme

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilibuni Mradi wa *Farkwa Multipurpose Dam Scheme* na lengo mojawapo likiwa ni kuanzisha kilimo cha umwagiliaji wenyewe ukubwa wa hekta 10,000 eneo la Mpendo Wilayani Kondoa. Je, Serikali haioni hivi sasa ni muda muafaka wa kutekeleza mradi huo ili kupunguza umaskini na kuondoa njaa Mkoani Dodoma?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza tarehe 14 Julai, 2003, wakati nikijibu swalii Na.224 la Mheshimiwa Paschal Degera, eneo la *Farkwa Multipurpose Dam Scheme* liko kwenye Mto Bubu mpakani mwa Wilaya za Dodoma na Kondoa.

Mwaka 1983/1984, Mpango wa Uwiano wa Mkoa wa Dodoma uliandaa usanifu wa awali (*pre-feasibility study and preliminary design*) wa mradi wa kujenga Bwawa la Farkwa. Gharama za kujenga bwawa hilo zilikuwa kubwa zaidi ya shilingi bilioni 5.5 kwa wakati huo miaka ya themanini. Kutokana na gharama hizo kuwa kubwa, Serikali ilishindwa kuutakeleza mradi huo. Hata hivyo, Serikali inatambua kuwa kama bwawa hilo litajengwa, baadhi ya Wananchi wangenufaika kwa kupata maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, kunyweshea mifugo yao na kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kuwa na uhakika zaidi wa chakula na kujiongezea mapato.

Serikali iliona umuhimu wa kujenga Mradi wa Farkwa tangu mwaka wa 1983 lakini tatizo limekuwa ni uwezo mdogo wa Serikali kutokana na gharama za ujenzi kuwa kubwa mmo. Hata hivyo, nia ya Serikali ya kuujenga mradi huo bado ipo na utatekelezwa fedha zitakapopatikana.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula. Kwa kuwa Mradi huu ulipobuniwa ulikuwa na malengo ya kuzalisha umeme, kumwagilia hekta 10,000 kama ilivyoelezwa katika swalii na pia kuleta maji katika Mji wa Dodoma na ndio maana gharama imekuwa kubwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni sasa kwamba ni busara kutekeleza Mradi huu awamu kwa awamu kwa sababu ukitekeleza kwa pamoja ndio maana gharama zinakuwa kubwa na sasa nashauri waanze na ujenzi wa bwawa badala ya kuanza na miradi yote kwa pamoja?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakubaliana Mradi huu una faida sana lakini ukififikiria gharama za mwaka 1983,

shilingi bilioni 5.5 leo hii ni bilioni nyingi sana. Kwa hiyo, ukianza kuutekeleza hata kwa awamu ni kwamba, kusogezasogezo gharama bado ni gharama kubwa, uchumi wa sasa hauruhusu. Tusubiri hali itakapokuwa ahueni, tutafanya kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

Na. 348

Umiliki wa Kisheria wa Nyumba na Ardhi

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kuwawezesha Wananchi wa Tanzania kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kumiliki kisheria rasilimali zao kama nyumba na ardhi linatiliwa mkazo na Serikali kiasi cha kumleta hata Mtaalam kutoka Peru kuja kutoa elimu hiyo kwa Viongozi Wakuu wa Serikali yetu:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba karibu asilimia 70 ya Wananchi waishio mijini, kama Jimbo la Ukonga, wanaishi katika nyumba zisizo na hati na zilizopo kwenye maeneo yasiyopimwa na kwamba wenye nyumba hizo ni maskini kutokana na kutokuwa na haki miliki za nyumba zao?

(b) Je, ni lini Serikali itaidhinisha na kutekeleza miradi ya uhakika na endelevu ya kupima na kutoa hakimiliki (*regularization*) kwa makazi holela mijini kama Buguruni, Vingunguti, Kipawa na Ukonga Jimboni Ukonga na maeneo mengine nchini Tanzania ili kuwawezesha Wananchi hao kuwa na uwezo wa kuweka rehani nyumba/ardhi zao ili waweze kukopa na kujiondoa katika umaskini?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inafahamu kuwa karibu asilimia 70 ya Wananchi waishio mijini, wanaishi katika nyumba zisizo na Hati katika maeneo yasiyopimwa. Hata hivyo, tafiti za makazi zilizowahi kufanyika hazonyeshi uhusiano chanya (*Positive Relationships*) kati ya umaskini na nyumba zisizokuwa na Hati. Ukweli ni kwamba, makazi katika maeneo yasiyopimwa ni moja kati ya viashiria vingi (*indicators*) vya umaskini. Serikali inaendelea na juhudzi za kutekeleza Mkakati wa Kuondoa Umaskini nchini kuititia sekta zote hasa sekta za vipaumbele.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kupambana na tatizo la makazi yasiyopimwa na hayana Hati, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imebuni mpango wa kuwatambua Wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Mara Wananchi watakapotambuliwa, watapatiwa Leseni ya Makazi (*Residential Licence*), ambayo itasajiliwa na Serikali. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka

1999, kifungu cha 23, Leseni ya Makazi itakuwa na nguvu kisheria na mwananchi atawea kuitumia kuomba mkopo kutoka taasisi za fedha. Mpango huu utatekelezwa kwa awamu na mradi wa kwanza utaanza kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam mwaka huu wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, mpango wa kutambua maeneo yasiyopimwa na kutoa Leseni za Makazi, hauwalengi Wananchi waliojenga kwenye maeneo hatari ambao kwa mujibu wa sera, sheria, taratibu na kanuni zilizopo wanatakiwa waondoke mara moja.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa mpango huu wa kupima na kutoa hakimiliki au leseni ungewawezesha pia Wananchi hawa kupata mikopo kutoka kwenye vyombo vya kifedha kwa ajili ya kuendeleza au kujenga upya nyumba zao na kwa kuwa katika bajeti ya mwaka huu, Wizara haikuzungumzia lolote kuhusu uanzishwaji wa Benki za kutoa mikopo ya nyumba kama ambavyo imeainishwa katika ule mpango wa *National Housing Finance Programme*, ambao na mimi nimeshiriki katika kuuandaa kama Mtaalam kwenye masuala haya, je, mpango huu wa kuanzisha vyombo vya kutoa mikopo ya nyumba umekufa?

(b) Kwa kuwa katika mazungumzo yake na hotuba kadhaa ikiwemo hotuba yake humu Bungeni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, amekuwa akisisitiza umuhimu wa kuanzisha vyombo hivi vya kutoa mikopo kwa ajili ya nyumba ambayo inapelekea hata watu kujihusisha na rushwa ili waweze kujenga nyumba zao, je, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Fedha haioni kwamba kwa kutelekeza suala hili wanakwenda kinyume na kukiuka kauli ya Rais?

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli suala hili la kuanzisha chombo au utaratibu wa kuwawezesha Wananchi kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini, tumekuwa nalo kwa muda. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, Serikali iko katika hatua za mwisho kufikia maamuzi ya mwisho ya jinsi ya kuanzisha utaratibu au chombo cha aina hiyo.

Kwa hiyo, napenda nimwombe Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga kwamba, Wizara ya Fedha ipo katika hatua za mwisho za kushughulikia suala hili na wadau wote pamoja na Wizara yangu, tumekwisha wasilisha mapendekezo. Tunamshukuru Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia suala hili. Namhakikisha kwamba, katika utekelezaji tutajitahidi kumshirikisha ili tuweze kufanikisha katika utekelezaji wa suala hili muhimu kwa maendeleo ya makazi katika Taifa letu.

Kufunga Kiwanda cha TIPER

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:

Kwa kuwa uwezekano wa kugundua mafuta hivi sasa ni mkubwa kuliko miaka ya 1960 -1990. Je, Serikali inafanya maandalizi gani ya kuinufaisha Tanzania baada ya kuipunguzia *TPDC* majukumu yake, kufunga Kiwanda cha *TIPER* na kuweka soko huria la mafuta ya petroli nchini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kusafisha Mafuta Ghafi cha *TIPER*, ambacho kilijengwa kwa ushirikiano baina ya Serikali za Tanzania na Italia mwaka 1963 na kuanza kufanya kazi mwaka 1966, ni kiwanda kidogo, teknolojia yake ni ya zamani na kutokana na kukosekana kwa fedha za kigeni kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara, hali ya kiwanda hicho ilikuwa siyo ya kuridhisha. Aidha, uzalishaji wa kiwanda cha *TIPER* ulikuwa chini ya nusu ya mahitaji ya nchi ambapo kiasi kilichobaki ilibidi kuagizwa kutoka nje kama mafuta yaliyosafishwa. Kutokana na hali ya udogo wake wa teknolojia iliyokuwa ikitumika, mafuta yaliyozalishwa kiwandani *TIPER* yalikuwa ni ya gharama ya juu zaidi ikilinganishwa na mafuta yanayoagizwa kutoka nje.

Tathmini iliyofanywa mwaka 1998 na wataalam wa *Stork Engineers, Chem Systems* na *COWI Consult*, ilibaini kuwa uzalishaji katika Kiwanda cha *TIPER* ulikuwa unaliingizia Taifa hasara ya kiasi cha wastani wa Dola za Marekani 15 milioni (sawa karibu na Sh. 17bn/=) kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yaliyofanywa na Serikali ni kuruhusu kuanzishwa kwa soko huria la biashara ya mafuta ya petroli na pia kuipunguzia majukumu *TPDC* ya kujihusisha na uagizaji wa mafuta ya petroli na badala yake wajikite katika shughuli za utafutaji wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, matokeo hasa ya kuanzishwa kwa soko huria ndiko kulikosababisha kiwanda cha *TIPER* kufungwa na kuacha uzalishaji kwani kisingewenza kuendelea na uzalishaji pasipo kupata ruzuku ya Serikali, gharama ambazo ni mzigo mkubwa kwa Serikali.

Aidha, matokeo mengine ya kuanzishwa kwa soko huria la mafuta ya petroli ni kuokoa gharama ya takriban Dola za Marekani 15 milioni kama nilivyosema awali kwa mwaka ambazo uchumi wetu ulikuwa unabeba ili kukiwezesha Kiwanda cha *TIPER*

kuendelea kusafisha mafuta. Pia uwekezaji kwenye biashara ya mafuta nchini umeongezeka.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa jukumu mojawapo la *TPDC* lilikuwa ni kuagiza mafuta na kuza mafuta ya petroli na kwa kuwa *TPDC* ina hisa katika Mradi wa Songsongo. Je, ni kwa nini sasa wakati mradi huu unapoanza majukumu yote ya Kampuni ya *Songas* yamekabidhiwa *Songas* ikiwa ni pamoja na utafutaji, usafirishaji wa gesi na uuzaaji wa gesi badala ya kuishirikisha *TPDC* angalau katika sehemu hii ya usimamizi na udhibiti wa mauzo ya gesi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili ni kwamba, kiwanda cha *TIPER* wakati kikifanya kazi ndicho kilikuwa kiwanda kinachotoa malighafi kwa kiwanda kipyka kabisa cha lami kilichojengwa pale Kigamboni na kwa muda wote huu tangu *TIPER* imefungwa, kiwanda kile kimesimama. Je, Serikali haioni kwamba kuna sababu kwa *TPDC* sasa kupewa jukumu la kuagiza malighafi ili kiwanda hiki cha lami kiweze kutengeneza lami kwa ajili ya Taifa hili? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati natoa majibu kwa swali la msingi, majukumu ya msingi yaliyobakishwa katika *TPDC* ni ya utafiti na utafutaji wa mafuta nchini. *TPDC* imeondolewa majukumu ambayo hapo nyuma kama nilivyosema awali, yalikuwa ni pamoja na majukumu ya kibiashara na ndio sababu hasa hata katika uhusiano wa *TPDC* na *Songas* au katika mradi wa Songsongo, *TPDC* kama ambavyo Mheshimiwa Herbert Mntangi amesema, ni wabia katika mradi huo, lakini wamejiondoa katika masuala ya utawala wa siku hadi siku ili waweze kunufaika zaidi na mapato yanayotokana na mradi huo na wajikite zaidi katika kufanya utafiti na kutafuta mafuta nchini. Hii ndio sababu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiwanda cha *TIPER*, uzalishaji wa lami ulikuwa unaendana sambamba na uingizaji wa mafuta nchini. Kwa hiyo, wakati utaratibu wa kuingiza mafuta nchini ulipobadilishwa kutoptana na uanzishwaji wa soko huria na kiwanda kile kikasimama na kutoptana na sababu ambazo nimezieleza, ni dhahiri kwamba, suala la uzalishaji wa lami pia lilibidi lisimame.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii niseme kwamba, kama kuna wawekezaji wanataka kuwekeza ama katika *refinery* au katika utengenezaji wa lami, Serikali ipo tayari kuwapokea na kwa kweli tumekuwa tukiwapokea baadhi ya watu ambaeo wamekuwa wakifutilia masuala haya.

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Spika, nashukuru na nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa eneo la chini ya jengo la *Mafuta House* lilijengwa kwa sababu ya kuhifadhi *base* za mafuta ambazo hivi sasa zinaagizwa nje ya nchi za Norway na Canada na kwa kuwa jengo hilo hivi sasa wamepewa *NSSF*, je, Serikali

inatuambiaje leo hapa kwamba ile sehemu ya *basement* itakuwa *TPDC* kwa kuwa hifadhi za mafuta sasa hivi zipo nje ya nchi? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, jengo ambalo lilikuwa linajengwa na *TPDC* kwa pamoja na *National Housing* limekabidhiwa *NSSF* ili waweze kulikamilisha jengo hilo na liwe la kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hilo limefanyika kwa sababu jengo hili lilikuwa limeshindikana kabisa kumpata mbia wa kuweza kulimalizia na limekaa zaidi ya miaka mitano na kuna vifaa vilikuwa vimekaa bandarini zaidi ya miaka mitano na vingine vilikuwa vimewekwa kwenye *basement* na vilikuwa vimeanza kuharibika na *contractor* alikuwa tayari anadai fedha za kumwondoa katika kazi zaidi ya Sh. 5bn/=.

Kwa hiyo, ilibidi kwa kweli Serikali iingilie kati kuokoa jengo hilo na liweze kuendelezwa na kukamilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba jengo hilo sasa sehemu ya chini kutumika na Shirika la Mafuta, tumewakutanisha wahusika wote na kwa sababu *NSSF* wao hawatakuwa wakijaza hilo jengo kwa vyovyote vile watalipangisha, wataelewana na *TPDC* namna ya *TPDC* kuweza kutumia hiyo sehemu ya chini kwa kazi yao hiyo ambayo ndio walikuwa wamedhamiria kuitumia kama wangekamilisha kujenga jengo hilo. (*Makofi*)

Na. 350

Ununuzi wa Nguzo za Umeme Sikonge

MHE. SAID J. NKUMBA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*), lilifikisha umeme Wilayani Sikonge kwa nia ya kutoa huduma na vilevile kufanya biashara:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazofanya shirika hilo kuwaomba baadhi ya wateja kuchangia kununua nguzo ili wasogezewe huduma ya umeme?

(b) Kwa kuwa shirika linafanya biashara, je, Serikali haioni kuwa kutowafikisha Wananchi umeme kwenye nyumba zao zilizoandalialiwa na kufungwa vifaa vya umeme kusubiri umeme ni kulipa hasara shirika na Serikali?

(c) Je, nini mpango wa Serikali baada ya kufikisha umeme Mji wa Sikonge kuufikisha vilevile kwenye Kata za Chabutwa, Ipole, Mibono, Igigwa na Pangale?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Sikonge umepata umeme mwaka 2002. Kazi za mradi huu zilishisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33, umbali wa kilomita 90, ujenzi wa njia za umeme volti 400, urefu wa kilomita 17 pamoja na kuunganisha wateja wapya. Gharama za mradi huu ziliwa zaidi ya Sh. 1.2bn/. Baada ya kukamilika kwa Mradi, hatua iliyofuata ni kupeleka umeme maeneo na Vijiji ambavyo havijapata umeme hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, sio Sera ya Shirika ya kutaka mteja yeote yule kuchangia kununua nguzo ili asogezewe huduma ya umeme kwani hilo ni jukumu la Shirika. Hata hivyo, iwapo eneo alilopo mteja husika halipo katika mpango wa Shirika wa kupatiwa umeme kwa wakati huo lakini mteja anasisitiza kupatiwa huduma hiyo, basi Shirika ndipo linapomshauri mteja kulipa gharama zote za kufikishiwa umeme mahali alipo. Vilevile iwapo mteja anayeomba umeme yuko umbali zaidi ya mita 30 toka ilipo njia ya umeme (*0.4 KV*), pamoja na malipo ya *service line*, mteja atatakiwa kulipa gharama za kusogeza njia ya umeme. Hivi sasa gharama ambayo mteja anayolipa ya umbali usiozidi mita 30 kwa matumizi ya majumbani ni Sh. 180,000/= pamoja na kodi ya *VAT*, pamoja na Sh. 20,000/= kwa ajili ya *meter deposit*.

Aidha, gharama za kuvuta umeme pia zinategemea kuwa mteja anavuta umeme kwa matumizi gani, yaani kundi la mteja (matumizi ya nyumbani, biashara au viwanda). Gharama za kusogeza *service line* zinategemea umbali mteja alipo kutoka kwenye nguzo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufuata mpango wa Shirika wa kueneza umeme, Shirika pia linatambua kuwa wapo Wananchi wenyewe uwezo na wangependa wapate huduma mapema zaidi ya ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuwfikishia umeme Wananchi wake wote hususan wenyewe nyumba zilizoandaliwa na kujengewa vifaa vya umeme. Hata hivyo, uhaba wa fedha ndio kikwazo kikubwa cha kutekeleza azma hiyo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufikisha umeme Sikonge Mjini, Serikali itaendelea na zoezi la kufikisha umeme kwenye Vijiji na maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Sikonge. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, kutokana na uhaba wa fedha na wingi wa miradi kama hiyo inapunguza kasi ya utekelezaji. Kwa kuanzia, Kijiji cha Pangale ambacho kipo katika njia ya umeme kwenda Sikonge, kitapatiwa umeme kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2004.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa matumizi ya umeme ni muhimu na ya lazima duniani kwa ajili ya maendeleo na pia kupunguza suala la kutokuathiri mazingira. Je, *TANESCO* kuwataka Wananchi wajivekee umeme wao wenyewe, Waziri haoni huko ni kukwamisha juhudji zote ambazo nimezitaja hapo juu na kwamba hiyo siyo biashara hasa hasa kwa watu ambao wapo *serious* kufanya biashara?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, *TANESCO* hawawataki watu wajivekee umeme wao wenyewe. *TANESCO* kama nilivyoleza katika majibu ya msingi, huwataka wateja wachangie kulingana na hali ambayo nimeeleza wakati najibu kutokana na umbali na kadhalika. *TANESCO* inatambua umuhimu wa kupata wateja wengi nchini na kwa hakika kwa mwaka huu kwa mfano, walikuwa wamepanga waunganishe karibu wateja laki moja kama isingekuwa ni matatizo ya ukame ambayo yamejitokeza na kuhitaji kutumia fedha nydingi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme. Kwa hiyo, *TANESCO* wanafahamu sana umuhimu wa biashara na wanajua kadri wigo wa wateja unavyopanuka, ndivyo na wao watakavyoweza kufaidika na halafu pia kwa hivyo hivyo kutimiza wajibu wao wa kusambaza huduma hii muhimu kwa nchi yetu.

Na. 351

Barabara ya Nyashimo - Ngasamo, Lamadi - Sapiwi na Magu - Mahaha

MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Nyashimo - Shighala - Ngasamo na barabara ya Lamadi - Mkula - Sapiwi - Magu - Mahaha ni kiungo muhimu sana kwa Wananchi wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara katika shughuli mbalimbali za huduma za jamii na uzalishaji mali na kwa kuwa idadi kubwa ya wakazi wa Mikoa hiyo huitegemea sana barabara hiyo:-

- (a) Je, Serikali inatambua kuwa barabara hizo ni za Mikoa, japo hazina hadhi ya kufanana na barabara za Mikoa?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuziimarisha barabara hizo kwa kiwango cha kudumu badala ya kuwa inatenga fedha kiasi kidogo kisichokidhi mahitaji halisi ya Wananchi hasa pale zinapokuwa hazipitiki kabisa wakati wa masika?
- (c) Je, Serikali katika harakati za kutatua tatizo hilo inatoa tamko gani kwa Wananchi wa maeneo hayo pamoja na Mikoa jirani ambamo barabara hiyo inapitia?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mbunge wa Busega, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyashimo - Shighala hadi Ngasamo yenyе urefu wa kilomita 43, Lamadi - Mkula hadi Sapiwi yenyе urefu wa kilomita 16 na ile ya Magu - Kabilia hadi Mahaha yenyе urefu wa kilomita 48 ni barabara za Mikoa zinazohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mikoa wa Mwanza na ni kiungo kati ya Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zimekuwa zikifanyiwa matengenezo makubwa (*Spot Improvement*), kwa kiwango cha changarawe ili kuzifanya zipitike kwa wakati wote kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha wa 2001/2002, jumla ya Sh. 72m/= zilitumika kugharamia matengenezo ya kawaida na dharura kwa kilomita 20 za barabara ya Nyashimo - Ngasamo katika maeneo ya Busega, Shighala hadi Nyashimo.

Katika mwaka wa fedha wa 2002/003, jumla ya Sh. 300m/= zilitumika kwa matengenezo ya barabara hizo kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya kilometa 16 za barabara ya Lamadi - Sapiwi zilifanyiwa ukarabati kwa ghamama ya Sh. 100m/=.

(ii) Jumla ya kilometa 14 katika barabara ya Nyashimo hadi Ngasamo zilifanyiwa ukarabati kwa ghamama ya Sh. 100m/=.

(iii) Jumla ya kilometa 14 za barabara ya Magu - Mahaha zilifanyiwa ukarabati kwa ghamama ya Sh. 100m/=.

Katika mwaka wa fedha wa 2003/004, jumla ya kilometa 26 zimefanyiwa matengenezo makubwa ya sehemu korofi katika barabara za Nyashimo - Ngasamo, Magu - Mahaha na Lamadi - Sapiwi, kwa ghamama ya Sh. 200m/. Hadi sasa jumla ya kilometa 70 za barabara hizo zimefanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe na ziko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa barabara hizi ni za Mkoa na ndio maana matengenezo yaliyofanyika kama nilivyoainisha katika maelezo yangu ya awali, yamefanywa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mwanza. Aidha, Serikali imeshaanza kutekeleza Mkakati Kamambe wa kuzitengeneza barabara hizo kwa awamu kwa kiwango cha changarawe ili kuziwezesha kupitika katika majira yote ya mwaka, hivyo kuwaondolea Wananchi wanaozitumia barabara hizo kero ya usafiri na katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, barabara hizi zimetengewa jumla ya Sh. 177m/= kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya sehemu korofi. Wizara ya Ujenzi inawaomba Wananchi wa maeneo zinakopita barabara hizi, kuchangia nguvu zao katika kuzitunza barabara hizo na kuheshimu mipaka ya hifadhi ya barabara.

MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, napenda niwapongeze Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri. Lakini pamoja na pongezi hizo, napenda tu kusema kwamba, barabara ya Lamadi - Mkula - Sapiwi imefanyiwa matengenezo, lakini kiwango cha

matengenezo ni kibovu, hakitoshelezi kukidhi mahitaji ya matumizi ya barabara hiyo. Kuna daraja pale Lamadi limebomoka baada ya kujengwa kwa mwaka mmoja. Sasa swalı langu ni kwamba, je, Wizara inaweza ikafuatilia tatizo liko wapi kwa sababu gharama nyingi zimetumika kutengeneza daraja lile lakini halikuweza kudumu hata kwa mwaka mmoja? (*Makofi*)

Pili, katika ziara ya hivi karibuni ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Bariadi, alikiri kwamba, barabara hizi ni muhimu sana kama kiungo kwa Wananchi wa Mikoa hii na akaahidi kwamba zinapaswa kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, hii ahadi ya Mheshimiwa Rais, itatekelezwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja bovu ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumzia, bahati nzuri tunalifahamu na tunalifuatilia ili kujua nini kimetokea na kwa nini mkandarasi ametengeneza barabara hii kwa kiwango cha chini na tukipata majibu kutoka kwa *Regional Manager*, Mheshimiwa Mbunge tutamhusisha ili aweze kuyapata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Rais, Rais anatoa ahadi nyingi sana na sisi tunazipokea tunaziweka kwenye mkakati na utaratibu wa utekelezaji. Kwa hiyo, wakati wa utekelezaji wa suala hili ukifika, tutatekeleza.

Na. 352

Barabara ya Busisi - Nyang'holongo

MHE. JAMES P. MUSALIKA aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Busisi hadi Nyang'holongo yenyeye urefu wa kilomita 113 ambayo inapita katika Vijiji vya Ngoma, Busolwa, Nyang'hwale, Nyijundee, Nyarubele, Kharumwa, Kayenze na Bukwimba; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha kidogo kidogo za matengenezo ya barabara hiyo kuanzia miaka ya fedha ya 2000/2001, 2001/2002, 2002/2003 na 2003/004 na kwamba kipande cha kutoka Kharumwa hadi Nyang'holongo yenyeye urefu wa kilomita 30 kimejifunga kutokana na uharibifu uliopo; na kwa kuwa sasa hivi kipande hicho kinaleta usumbufu mkubwa kwa Wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali itatoa lini fedha za kutosha kuweza kukamilisha barabara hiyo hususan eneo liliojifunga?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo imekuwa kero kwa Wananchi wote wa Majimbo ya Nyang'hwale na Sengerema, je, Serikali itakubaliana nami kwamba Wananchi hao wanastahili kupewa haki yao ya huduma ya usafiri kama Wananchi wengine hapa nchini?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kupokea shukrani toka kwa Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kwa kuwatengeneza kipande cha barabara toka Ngoma hadi Nyarubele?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swal la Mheshimiwa James Phillipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), imekuwa ikifanya matengenezo makubwa ya maeneo korofi na ujenzi wa madaraja makubwa katika barabara hii ya Busisi hadi Nyang'holongo yenye urefu wa kilometra 113 kuanzia mwaka wa fedha 2000/2001 hadi 2003/2004. Barabara hii ambayo ilijifunga kutokana na kubomoka kwa madaraja ya Nyaluhwa, Ngoma na tuta la Nyang'holongo, sasa inapitika baada ya ujenzi wa madaraja hayo ya Nyaluhwa, Ngoma na Nyang'holongo. Kazi ya matengenezo ya barabara inaendelea kwa awamu kwa jinsi fedha zinapopatikana na tunatarajia kuendelea na matengenezo ya sehemu korofi iliyobaki katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 ambapo Sh. 50m/= zimetengwa kwa ajili ya barabara hii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni haki ya kila mwananchi kupata huduma ya barabara na ndiyo maana Wizara yangu inaendelea na matengenezo kadri ya upatikanaji wa fedha ili barabara yote ipitike na kutoa huduma ya usafiri kwa Wananchi wa Majimbo ya Nyang'hwale na Sengerema.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, napenda kupokea shukrani toka kwa Wananchi wote wa Majimbo ya Nyang'hwale na Sengerema waliyotoa kwa kutengenezewa barabara hii.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na shukrani za Wananchi wa maeneo yaliyotajwa, kwa kutengenezewa barabara hiyo iliyokuwa imesahauliwa kwa muda mrefu nataka kuuliza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa nimekuwa nikipigiwa simu na Wananchi kwamba kipande cha barabara kilichotengenezwa mwaka huu cha kutoka Kayenze hadi Nyang'holongo kwenye barabara hiyo kwamba barabara hiyo ni nyembamba yaani kipande ni chembamba. Serikali inatamka nini kuhusu malalamiko hayo kwa barabara hiyo na barabara zote nchini zinazojengwa bila kufikia kiwango kinachotakiwa? (*Makofit*)

(b) Kwa kuwa barabara sasa imekuwa njia ya mkato kutoka Kahama kwenda Sengerema hadi Mwanza na kwa kuwa sasa magari mazito yenye tani zaidi ya 30 yanapitia barabara hiyo na kuharibu madaraja ya Ligembe na Nyaluhwa na barabara yenye na kwa pia kule hatuna vituo vya Polisi wala Matrafiki. Serikali inashauri Wananchi wakiona hayo wachukue hatua gani za haraka? (*Makofit/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, juu ya swal la kipande cha Kayenze hadi Nyang'holongo, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia hili na sisi tumepata habari ya malalamiko hayo. Lakini hayo ni malalamiko ambayo

Wananchi wanafananisha na barabara ya kipande cha nyuma kilichotengenezwa kwa ajili ya mafunzo ya ukandarasi, lakini hii barabara pale upana wake ni sahihi kabisa ni mita 5.5 na tumekwenda kufuutilia hapa na tukaona mkandarasi ametengeneza kama Mkataba ulivyohusika. Kwa hiyo, si barabara nyembamba kama Wananchi wanavyoionna.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari mazito kuharibu madaraja kwenye barabara hii, Wananchi hawa wanafuata barabara nzuri ili wapite huko. Sasa Wananchi wanapoona haya magari mazito wayafanye nini? Mimi nawashauri wasiyashambulie, ni vizuri wakayaacha magari hayo yapite na tufanye jitihada za ulinzi tu wa haki ambayo itaruhusu mtu yejote kutumia barabara nzuri katika nchi hii bila kushambuliwa ili mradi haharibu barabara na pale anapoharibu daraja Wananchi wakiona basi wana haki ya kusimamisha na kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake.

Na. 353

Mikopo ya Wanawake na Vijana

MHE. JOEL N. BENDERA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imebuni mikakati mizuri ya kuwakwamua wanawake na vijana katika umaskini kwa kuwapatia mikopo ili waweze kujipatia kipato na hatimaye kujipatia uwezo wa kumudu maisha, lakini utafiti umebaini kwamba, mikopo hiyo haiwafikii walengwa wengi amba ni wanawake na vijana wanaoishi Vijijini badala yake mikopo hiyo inaishia Mijini tu na kwa kuwa utafiti umebaini pia kwamba, Maafisa Maendeleo ya Jamii Wilayani wanaogawa mikopo Vijijini hujibu kuwa ni vigumu kuwafikia na kuwadhibiti na kwa kuwa utafiti umegundua kwamba, wanawake na vijana wa Vijijini hawawezi kuandika maandiko ya miradi *project write up* kwa ajili ya kuomba mikopo na kuna ukosefu wa wataalam wa kuwasaidia kuandika na matokeo yake mikopo huishia Mijini tu:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha haki inatendeka kwa wanawake na vijana wote wa Mjini na Vijijini wanapata mikopo badala ya kuegemea upande mmoja tu?

(b) Katika kuhakikisha kwamba mikopo inafika Vijijini, je, Serikali haiioni kuwa ni busara mgao ukaelekezwa kwenye Kata ili kuziwezesha kupata mgao wao na kuzzungusha fedha hizo katika Vijiji vilivyo katika Kata husika, nikiamini kwamba utaratibu huo utapunguza sana malalamiko mengi ya wanawake/vijana katika Vijiji kama vile Vijiji vya Kalalani, Mtoni Bombo, Mgaza, Kerenge, Makorora, Makumba, Mgambo, Ubiri na kadhalika katika Jimbo la Korogwe Mashariki?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mshariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ikishirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa fedha chache zinazopatikana, haki inatendeka na Halmashauri katika kutoa mikopo kwa wanawake wa Mijini na Vijiji, wenye sifa za kukopa kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inapeleka fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa Halmashuri zote, ziwe za Mijini au Vijiji bila upendeleo wowote. Kwa sasa hivi kila Halmashauri inatengewa Sh. 4m/. Kimsingi fedha zinazotumwa na Mfuko huu ni ujazilishi (*complementary*) kwa ile michango ya asilimia tano ya mapato ya kila Halmashauri inayochangiwa katika Mfuko huu. Fedha zote zinawekwa pamoja na mwongozo unaohusika katika kutoa mikopo hiyo ni mmoja.

Adiha, mikopo hiyo inatolewa kwa wanawake kwa kuzingatia michanganuo inayowasilishwa na kikundi husika kwenye Kamati za Mikopo ya Halmashauri zilizopewa jukumu la kuidhinisha mikopo hiyo. Ni matumaini yangu kuwa, Kamati hizi zinatenda haki katika kutoa mikopo hiyo. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati hizi, ninawaomba kushirikiana katika kuhakikisha kuwa fedha chache zilizopo zinatumika na waliokopa ipasavyo ili kumkomboa mwanamke kiuchumi.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki kuwa, wazo la kuelekeza fedha za mikopo kwenye ngazi ya Kata ni zuri. Wizara yangu inatambua kuwa waombaji wa mikopo hii hutoka katika ngazi ya Mtaa, Kijiji na Kata.

Hivyo, fedha hizi tunaamini zinawafikia waombaji wote. Kinachofanyika ngazi ya Wilaya ni usimamizi na uratibu wa mkopo huu.

Aidha, kutokana na zoezi la ufuatiliaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake lililofanyika mwezi Februari, 2004, Halmashauri ya Korogwe ilikuwa bado haijagawa fedha zote ilizopokea kiasi cha Sh. 8m/ zilizopelekwa na Wizara yangu za mwaka 2001/2002 na 2002/2003. Namwomba Mheshimiwa Joel Bendera, ashirikiane na Halmashauri ya Korogwe ili awezeshe utoaji wa mkopo huu.

Hii ni pamoja na kushirikiana na Kamati ya Mikopo ya Halmashauri ambayo Mheshimiwa Joel Bendera ni Mjumbe, kuweza kukaa na kujadili maombi ya wanawake ambao wamekuwa wanasubiri wakati fedha zipo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tushirikiane ili tuweze kufikisha huduma za Mfuko huu kwa walengwa wote wa Mijini na Vijiji ili kuhakikisha kwamba, mikopo inawafikia wanawake wote.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba zipo Halmashauri ambazo zinakaa na fedha bila kuzipeleka kwa walengwa. Je,

ikigunduliwa hivyo kama alivyogundua Serikali inachukua hatua gani kwa wahusika? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

La pili, kwa kuwa ukienda vijijini yapo malalamiko kwamba uchumi kweli umekua lakini mzunguko wa fedha vijijini kwa Wananchi haupo na njia ya kuwawezesha waweze kupata fedha vijijini ni hii mikopo kufika kwa walengwa amba ni wanavijiji. Serikali haioni ingefuata utaratibu kama vile wa MMEM ambapo kila kijiji kimepata fedha na wamejenga shule na wameziona. Kwa mikopo hii kwa nini wasifanye utaratibu huo ili fedha ziweze kuwafikia wanawake na vijana walioko vijijini?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba, Wizara yangu ilifanya mapitio kuboresha uendeshaji wa Mfuko huu na ninafurahi kusema kwamba, Halmashauri nyingi zimeitikia na marejesho yamekuwa mazuri sana na mifano halisi ni Halmashauri zilizomo katika Mkoa wa Tanga, Halmashauri zote zimeweza kurejesha mikopo isipokuwa Halmashauri ya Korogwe. Sasa mimi naomba nitoe wito kwamba, wanawake wa Korogwe wanaonewa, shilingi milioni nane zipo.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Mbunge, aende kwenye Kamati hiyo wakatafute dawa. Kwa sababu dawa mnayo ninyi watu wa Korogwe, fedha zipo shilingi milioni nane, mkafanye kazi hiyo. Hii kupeleka Mahakamani itakuja baada ya kushindwa kabisa. Lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge, tusiwaonee wanawake wa Korogwe, shilingi milioni nane zipo zimekaa bure. Kwa hiyo, hili naona nimejibu maswali yote. Pia namwomba Mheshimiwa Mbunge, nina Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ule tuliuoboresha, kila Mbunge hapa tayari amepewa. Lakini kwa Mheshimiwa Joel Bendera, namwomba tuonane. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, nimeulizwa wapi, kwa wakati na mahali muafaka. (*Kicheko*)

Na. 354

Tatizo la *Fluoride* Katika Maji

MHE. PAUL N. MAKOLO aliuliza: -

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Maganzo uliopo katika Kata ya Songwa unakabiliwa na tatizo la *Fluoride* kwenye maji ya visima na hali hiyo inasababisha usumbufu mkubwa wa upatikanaji wa maji ya kunywa kwa wakaaji wa Mji huo:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kupunguza *fluoride* kwenye maji ya Mji huo?

(b) Je, ni nini matokeo ya utafiti wa kupunguza *fluoride* kwenye maji uliofanywa na wataalamu kwa kushirikana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, niliwahi kujibu swali Na.34 la tarehe 25 Mei, 2001, swali Na. 1020 tarehe 9 Novemba, 2001 na swali Na.2228 la tarehe 4 Februari, 2003 kwenye Mkutano wa Bunge wa Nne, wa Tano na wa Kumi sawia, kuhusiana na tatizo la madini ya *Fluoride* nchini. Miaka ya nyuma teknolojia ya kupunguza *fluoride* kwenye maji ilikuwa tatizo. Lakini katika Mkutano wa Kumi, nililifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu teknolojia iliyopatikana ya kupunguza madini hayo ya ziada kwenye maji ambayo ilijaribiwa huko Arusha na Wilaya Hanang na kuonekana inafaa. Kwa sasa majoribio kama hayo yatafanywa Mkoani Shinyanga, kwa kuwatumia wataalamu wetu na hivyo kipaumbele kitatolewa maeneo ya Maganzo yenyne matatizo ili kuwapa Wananchi mbinu za kupata majisafi na salama.

(b) Mheshimiwa Spika, matokeo ya majoribio yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kushirikiana na watalaam wa Wizara yetu, yanaonyesha uwezo wa mafanikio ya teknolojia hii ya kupunguza madini ya *fluoride* hadi viwango vinavyokubalika. Maji yenyne *fluoride* kiwango cha miligramu 2.8 hadi 15.6 katika lita moja yalipotumika kwa muda wa miezi 12 ya majoribio, mtambo uliweza kuchuja maji na kupunguza *fluoride* hadi miligramu 0.3 hadi 1.5 katika lita moja, viwango vinavyokubalika na Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, watalaamu wa Kijapani wakishirikiana na wataalamu wetu, wameuthibitisha uwezo wa teknolojia hii katika Wilaya ya Hanang.

SPIKA: Nashukuru Mheshimiwa Paul Makolo ameridhika na muda wa maswali umekwisha. Sasa tunaendelea na kazi nyingine.

Kwanza, matangazo ya vikao mbalimbali. Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, anawatangazia Wajumbe kwamba, kutakuwa na kikao leo chumba Na. 428, ghorofa ya nne kuanzia saa 4.30 asubuhi hii. Kamati nyingine ni ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, naye anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya PAC wakutane leo saa 5.00 asubuhi chumba Na. 219 ghorofa ya pili. Kamati nyingine ni Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anne Makinda, anawaomba Wajumbe wakutane saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Na. 432 ghorofa ya nne.

Kamati ya mwisho ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Njelu Kasaka, anatangaza kikao cha Kamati hiyo kifanyike saa 5.00

asubuhi hii katika chumba cha Kamati Na. 231 ghorofa ya pili. Kikao kingine ni cha Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote, katika maandalizi yao ya usiku wa leo, Mheshimiwa Anne Makinda, anawaomba wakutane saa 7.00 mchana kwenye viwanja vya burudani kule kule.

Kuhusu siku ya Jumamosi, kesho, kutakuwa na Semina kama kawaida itakayoanza saa tatu asubuhi inahusu tathmini ya Sensa iliyofanyika mwaka 2002. Kabla ya Semina kuna *VIP Race* kama tulivyokwisha kutangaziwa ambayo itaanza saa 12.00 alfajiri kama tulivyokwisha kuelezw. Ile *Race* inakusudiwa kumalizika kwenye saa 2.00 asubuhi hivi. Kwa hiyo, tutakuwa na nafasi ya kuanza semina saa 3.00 asubuhi. Halafu Usiku wa Mwanamke wa Afrika ni kama tulivyokwisha kutangaziwa majira ya jioni katika viwanja vyetu vya burudani.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*. Katibu.

KAULI ZA MAWAZIRI

Mwenendo wa Bei ya Zao la Pamba katika Msimu wa Ununuzi wa 2004/2005

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu mwenendo wa bei ya zao la pamba katika msimu huu wa ununuzi wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Taifa letu, hutegemea kwa kiasi kikubwa uzalishaji na uuzaaji wa mazao yetu ya kilimo, hasa mazao asilia kama kahawa, pamba, korosho, chai, tumbaku, katani na kadhalika na kwa kiwango kidogo mazao yasiyo asilia kama maua, mbogamboga, viungo vya vyakula, matunda na kadhalika. Huko nyuma tulikotoka hasa kwa mazao makuu ya biashara, biashara hiyo ilikuwa inafanywa na vyombo vya Serikali. Serikali ilikuwa inapanga bei kutegemeana na bei katika masoko ya dunia na mara nyingi bei hiyo ilikuwa haibadiliki kutokana na mabadiliko katika masoko ya dunia kwa bei kushuka au kupanda. Hali hii haikutoa motisha kwa wakulima kuzalisha zadi kwa sababu mkulima hakupata faida ya ushindani katika soko. Aidha, pale hasara ilipotokea ilibidi Serikali kufidia kwa kutumia kodi za Wananchi kuziba hasara hiyo na kuathiri shughuli zingine za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mabadiliko ya sera zetu na ili kumpatia mkulima uhuru wa kuuza mazao yake na kufaidika na ushindani, Serikali iliruhusu biashara hii ya mazao kuwa huru. Hivi sasa wanunuzi katika biashara huria ni Vyama vya Ushirika na wanunuzi binafsi na Serikali imebakia na shughuli za usimamizi na udhibiti. Hali hii sasa ni kwa mazao yote, lakini ni utaratibu ambao wakulima wetu hawajauzoea sana. Katika biashara huria, kwa kawaida mkono wa Serikali usingelikuwepo zaidi ya uangalizi. Hata hivyo, kwa kujua upya wa utaratibu huu na ili wakulima wetu wasije wakaonewa au kunyonywa na wafanyabiashara wenye ujuzi zaidi wa masoko, tumekuwa na utaratibu wa kuwakutanisha wadau wote ili kwa pamoja, wapange bei ya dira kwa mazao yanayohusika kwa kuhusisha vipengele vyote muhimu kama bei katika soko la dunia, mwelekeo wa bei katika soko, gharama za uzalishaji na gharama zinginezo za

biashara, kodi na ushuru mbalimbali, hadi kufikia bei ya dira ambayo wadau wote wanakubaliana.

Kutokana na utaratibu huu, ningependa ieleweke wazi kuwa, bei ya dira siyo bei ya Serikali na siyo bei ya Bodi na wala siyo bei ya zao husika. Ni bei inayotoa mwelekeo wa wapi pa kuanzia. Mara nyingi pale ambapo bei ya kununulia imekuwa kubwa kuliko bei ya dira kwa maana ya bei kupanda katika soko la dunia, hapajawahi kutokea matatizo. Hata hivyo, pale ambapo bei halisi imekuwa chini kuliko bei ya dira, malalamiko makubwa yametokea kwa wakulima na hata wawakilishi wao. Katika hali hiyo, bei ya dira hugeuzwa kuwa bei ya Serikali. Hali hii imetokea kwa mazao ya kahawa, korosho, tumbaku na sasa pamba. Zao la kahawa limekumbwa sana na matatizo haya mpaka Bodi sasa imeamua kuacha utaratibu huu wa kutangaza bei ya dira. Bila shaka Bodi nyingine za mazao nazo zitajifunza kutoka Bodi ya Kahawa na kuamua kama kweli ina maana yoyote kutangaza bei ya dira wakati huna uwezo wowote wa kushawishi nguvu za soko, wala huna uwezo wa kuingilia kati kwa maana ya kutoa ruzuku endapo bei itakuwa tofauti na utabiri ulioutoa. Katika utaratibu wa soko huria ni vyema kuachia nguvu ya soko ikafanya kazi ya kuamua bei kwa wakulima wetu kama inavyoamua katika soko la dunia. Kazi ya Serikali iwe ni kusimamia nguvu hiyo ya soko kufanya kazi yake vizuri na kwa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, mazao yetu mengi tunayuza yakiwa ghafi na bei za mazao ghafi ni ndogo sana, huyumba sana na hazitabiriki. Hali hii husababisha wakulima wengi kupata hasara na mara nyingine kukata tamaa. Hali kama hii ikitokea katika nchi tajiri, Serikali zao huwakinga wakulima wao kwa kutoa ruzuku ili kufidia gharama za uzalishaji. Sisi tulio maskini hatuna uwezo wa kufanya hilo japo hatukatazwi na mtu, nchi wala Shirika lolote kama tungelikuwa na uwezo wetu wa kufanya hivyo. Hata hivyo, yapo mambo ambayo tunaweza kuyafanya ili kupunguza hasara au kuongeza mapato ya wakulima wetu.

Kwanza, ni kuongeza tija katika uzalishaji. Tuchukulie mfano wa zao la pamba. Leo Tanzania tunazalisha wastani wa kilo 250 hadi 300 kwa ekari moja wakati kuna nchi zinazalisha zaidi ya kilo 4,000 kwa ekari hiyo hiyo. Kama walau tungefikia uzalishaji wa hata kilo 1200 kwa ekari, hata bei katika soko la dunia ingelianguka, mapato ya mkulima kwa ekari yangelikuwa mara nnne au zaidi ya anayoyapata sasa. Hivyo, ili kuepuka hasara kwa wakulima, wadau wote tujielekeze katika kuwasaidia wakulima waongeza tija katika uzalishaji.

Pili, kama nilivyosema, bei ya mazao ghafi hazitabiriki, ni lazima sasa tuelekeze nguvu mpya katika kusindika mazao yetu. Mazao yaliyosindikwa yana bei nzuri na soko lake linatabirika. Serikali tumeweka eneo hili katika maeneo ya kipaumbele katika uwekezaji na wanaowekeza hupata vivutio vingi na vizuri sana. Naomba wawekezaji wajiingize katika sekta hii.

Tatu, mazao yanapokuwa mengi sokoni, wanunuzi huchagua mazao yenyе ubora mkubwa. Hivyo, dawa ya kupata bei nzuri pia ni kuzalisha mazao yenyе ubora unaohitajika na soko. Tuwasaidie wakulima wetu kuzalisha mazao yaliyo bora.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba katika msimu wa ununuzi wa 2004/2005, limekumbwa na matatizo ya bei kushuka katika soko la dunia na hivyo kufanya bei halisi ya mkulima kuwa chini kuliko bei ya dira iliyotangazwa awali.

Katika misimu ya 2000/2001 hadi 2002/2003, bei ya wastani kwa kilo moja ya pamba mbegu ilikuwa shilingi 180/= kwa kilo. Katika msimu wa 2003/2004, bei ya pamba mbegu ilipanda hadi kufikia shilingi 350/= kwa kilo; bei ya wastani ikiwa shilingi 280/= kwa kilo wakati bei ya dira iliyotangazwa ilikuwa shilingi 225/= kwa kilo. Kutokana na kupanda kwa bei ya pamba katika msimu wa 2003/2004, wakulima waliongeza sana kilimo cha pamba katika msimu wa kilimo wa 2003/2004. Kutokana na ongezeko hilo, katika msimu wa ununuzi wa 2004/2005, ambao unaendelea sasa, uzalishaji wa pamba mbegu unatarajiwa kufikia tani 250,000 kutoka tani 140,000 za msimu uliotangulia. (*Makofî*)

Hali hii ya kupanda kwa bei ya pamba ilitokea katika maeneo yote yanayolima pamba duniani na ilitokana na hali mbaya ya hewa iliyokumba nchi ya China katika msimu uliopita na kusababisha kuwepo kwa upungufu mkubwa wa zao la pamba duniani. Wakulima katika maeneo mbalimbali yanayolima pamba duniani, walivutiwa na ongezeko hilo kubwa la bei na kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani milioni 20.04 za pamba nyuzi katika msimu wa 2003/2004 hadi tani milioni 22.2 za pamba nyuzi zinazotarajiwa kuuzwa katika msimu huu wa 2004/2005. Kutokana na matarajio hayo, bei ya pamba katika soko la dunia imeshuka kutoka dola za Kimarekani 0.79 au senti 79 za dola kwa ratili moja ya pamba nyuzi mwezi wa Oktoba, 2003 hadi senti 44 za dola ya Marekani mwezi wa Julai, 2004, sawa na anguko la asilimia 44.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazingira haya magumu ya soko la pamba katika soko la dunia, mnamo tarehe 14 Juni, 2004, wadau wa zao la pamba, yaani Bodi ya Pamba, wawakilishi wa Chama cha Wafanyabiashara wa Pamba (*TCA*), Wizara husika za Kilimo na Chakula na Ushirika na Masoko, walikutana Mwanza kupanga bei ya dira. Mkutano huo ulizingatia mwenendo wa kupanda kwa bei ya pamba katika msimu uliopita, yaani 2003/2004 na bei katika soko la dunia wakati huo ikiwa ni senti 52 za Kimarekani kwa ratili kwa pamba nyuzi katika soko la dunia katika msimu wa 2003/2004 na kuamua kwamba, katika msimu wa 2004/2005, bei ya dira ya kilo moja ya pamba mbegu daraja la kwanza ingekuwa shilingi 300/= kwa kilo na shilingi 150/= kwa kilo kwa daraja la pili. Msimu wa ununuzi ulianza tarehe 21 Juni, 2004 na muda mfupi baada ya msimu kuanza, bei ya pamba katika soko la dunia ilishuka hadi senti 44 za dola kwa ratili ya pamba nyuzi.

Kutokana na kushuka huko kwa bei, wanunuzi wa zao ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika, waliona hawawezi kununua zao hilo kwa bei ya shilingi 300/= kwa kilo bila kupata hasara. Benki zilizokuwa zimekopesha fedha za ununuzi wafanyabiashara hao, nazo zilisita kuendelea kutoa mikopo ya ununuzi wa pamba kwa kuogopa mikopo yao kutokurudishwa kwa vile bei ya pamba imeshuka sana. Ili kutathmini hali hii iliyojitokeza upya, wadau wa zao la pamba walikutana tena Mjini Mwanza tarehe 13 Julai, 2004 na kukubaliana kupunguza bei ya dira hadi shilingi 250/=

kwa kilo ya pamba mbegu. Wadau waliokutana siyo wanunuzi peke yao bali ni pamoja na Bodi ya Pamba, Wawakilishi na Wizara pamoja na Viongozi wengine wa Serikali. Kushuka kwa bei ya pamba mbegu kwa shilingi 50/= kwa kilo kumesababisha malalamiko mengi kutoka kwa wakulima na pia kutoka kwa wanasiasa, ambao wameitaka Serikali iangalie uwezekano wa kuingilia kati ili kumpunguzia mkulima hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mukutano wa kutathmini hali ya bei ya zao la pamba baada ya bei kushuka katika soko la dunia, wadau walifiki bei ya shilingi 250/= kwa kilo baada ya kufanya hesabu kutokana na bei ya senti za Marekani 44 kwa ratili moja ambayo ndiyo bei iliyokuwa sokoni. Hata hivyo, hali hiyo ilifikiwa baada ya wafanyabiashara kupunguza faida yao kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10, vinginevyo bei ingelikuwa hata chini ya shilingi 250/= kwa kilo. Hata hivyo, pamoja na kuwa bei ya shilingi 250/= ni ya wastani sana kwa zao la pamba, bado kuna manung'unico kwa sababu ya mazoea tu kuwa bei ya dira ikishawekwa huwa haijawahi kushuka hasa kwa zao la pamba. Kwa ajili ya kuungana mkono na wadau wengine hasa wanunuzi wa pamba, Serikali nayo imewajibika kuangalia sura ya bei (*Price Structure*), ya pamba ili kuona kama kuna lolote linaloweza kufanya kuhusu kushuka huko kwa bei. Ilelewka wazi kuwa, Serikali haina fedha inazoweza kuzitoa kwingineko kufidia hasara hiyo bali ni kuangalia katika sura (*structure*), ya bei yenyewe ya zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu katika sura ya bei ni kama ifuatayo:
Bei ya zao katika soko la dunia, faida kwa mnunuzi, gharama za ununuzi/biashara/uchambuaji na kodi na ushuru mbalimbali kama vile Mfuko wa Maendeleo ya Pamba (*CDF Levy*), Ushuru wa Zao (*District Cess*), Mfuko wa Elimu (*Education Levy*), gharama za Mbegu (*Seed Reserve Cost*) na gharama za Bodi

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia bei ya soko la dunia ya senti za Marekani 44 kwa ratili katika sura ya bei iliyoelezwa, bei hali ya sasa kwa mkulima inakuwa shilingi 250/= kwa kilo ya pamba mbegu. Bei hii ndiyo iliofikiwa na wadau kama nilivyoeleza awali. Bei hii halisi inaweza kubadilika kwa kupanda au kushuka kutegemeana na hali halisi ya bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa vipengele vyatya ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kuhusu faida ya wanunuzi. Katika kikao cha wadau cha kutathmini upya mwenendo huu wa bei, tumeelezwa kuwa wanunuzi walipunguza faida yao kutoka asilimia 15 mpaka 10 na ndiyo kupatikana bei ya shilingi 250/= kwa kilo.

Pili, ni kuhusu gharama za ununuzi na uchambuaji. Tumezungumza na wanunuzi ambao wamekubali kubana gharama zao za biashara ambapo sasa watachangia shilingi 10 kwa kilo katika bei ya mkulima. Mchango huu unafikisha bei ya mkulima kuwa shilingi 260/= kwa kilo. (*Makofi*)

Tatu, ni kuhusu kodi ya Ushuru mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Katika Mfuko wa Maendeleo ya Pamba mkulima hukatwa shilingi 20/= ambazo zimegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni shilingi 15/= kwa kilo, hizi hukatwa na kuingizwa katika kitabu cha mkulima kwa ajili ya kununulia pembejeo baadaye. Hizi kwa kweli ni fedha zake mkulima ambazo anawekewa kama akiba. Shilingi 5/= zilizobaki zinakatwa kwa ajili ya maendeleo ya zao lenyewe. Eneo hili kwa vile linasimamia zaidi shughuli muhimu za zao lenyewe na mkazo sasa hivi ni mazao yajigharamie zaidi, tunaliacha liliyo. Kwa sababu sehemu kubwa hata hivyo ni fedha za mkulima mwenyewe.

(b) Ushuru wa zao wa Halmashauri au *District Crop Cess*. Ushuru huu ni asilimia tano ya bei, kwa hiyo, kwa bei ya sasa ya shilingi 250/= ushuru huu unakuwa shilingi 12.50/= kwa kila kilo. Kwa vile zao la mwaka 2003 ni asilimia 60 ya uzalishaji wa mwaka huu na kwa kuwa mwezi Desemba, 2003, bajeti ilipotengenezwa, mantiki ya kawaida inaelekeza huwezi kutengeneza bajeti iliyo tofauti sana na iliyopita hasa kwa vyanzo usivyokuwa na udhibiti navyo, mapato yatokanayo na ushuru wa zao yatafanana na mapato ya mwaka huu yakitzwa kwa asilimia 60 ya zao la sasa. Hivyo, ushuru huu utatozwa kwa asilimia tatu au makato ya shilingi 7.50 kwa kila kilo. Halmashauri hazitegemewi kupata hasara kwa badiliko hili. Hii inabakiza shilingi 5/= kwa kilo kuchangia bei ya mkulima na kufanya sasa mapato ya mkulima kuwa shilingi 265 kwa kilo. (*Makofi*)

(c) Mfuko wa Elimu hutozwa shilingi 5/= kwa kilo. Mfuko huu hautozwi katika eneo lote linalolima pamba, hivyo, haustahili kuwa katika sura (*Price Structure*) ya bei ya pamba. Aidha, utozaji wa utaratibu huu humwadhibu yule anayezalisha pamba zaidi na humwacha anayezembea kilimo au yule ambaye halimi pamba kabisa. Wilaya zinashauriwa zitafute utaratibu mzuri zaidi ambapo kila mtu atachangia elimu badala ya mzigo kuwaelemea wale wanaolima na kuzalisha pamba nyingi. Fedha hizi zinaondoka katika sura ya bei na kwenda kwa mkulima, lakini mkulima bado anaweza kuchangia elimu kwa michango ya kaya na kadhalika. Aidha, elimu haitaathirika kwa sababu tunayo miradi ya MMEM na MMES ambayo itaziba pengo kama litajitokeza. Utaratibu huu utaongeza shilingi 5/= kwa kilo ya mkulima na kupandisha sasa mapato yake kuwa shilingi 270/= kwa kilo. (*Makofi*)

(d) Gharama za mbegu hufikia shilingi 7.50/= kwa kilo. Kwa vile zao litakuwa kubwa zaidi shughuli hizi zinaweza kufanya bila athari kwa asilimia 60 ya gharama hii, yaani shilingi 4.50/= kwa kilo na kumwachia mkulima shilingi 3/= kwa kilo na kufanya sasa mapato ya mkulima kuwa shilingi 273/= kwa kilo.

(e) Gharama za Bodi ni shilingi 5/= kwa kilo. Kama tulivyo fanya kwa wengine, Bodi nayo inaweza kufanya kazi yake bila kuathirika kwa kutumia asilimia 60 ya kiwango hiki kwa ajili ya wingi wa zao. Hii inabakiza shilingi 2/= kwa kilo katika mapato ya mkulima na kufanya sasa mapato ya mkulima kuwa shilingi 275/= kwa kilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya makato mbalimbali kutoka kwa wadau wa biashara hii, nataka ieleweke kuwa, fedha hizi zimepatikana baada ya maafikiano na wadau hao na kwa sekta yenye we kujichangia. Hivyo, zaidi ya bei ya msingi ya shilingi 250/= kwa kilo, mkulima atapata shilingi 25/= zaidi kwa kilo hiyo hiyo. Fedha hii haijumuishi shilingi 15/= anazokatwa mkulima na kuingizwa katika kitabu chake. Ukiongeza hizo, ambazo anawekewa akiba kwa kweli mapato ya mkulima yanakuwa shilingi 290/= kwa kilo. Pamoja na kuperomoka kwa bei, juhudhi kubwa imefanywa na wadau wote katika biashara hii ikiwepo Serikali yao ili angalau mapato ya mkulima yasiwe chini sana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, bei ya msingi ya shilingi 250/= kwa kilo ndiyo bei inayolipika hivi sasa kutokana na bei ya soko iliyoko. Hii siyo bei ya Serikali, narudia, bei ya shilingi 250/= kwa kilo ni bei ya soko, siyo bei ya Serikali. Wakulima wajue bei hii inaweza kubadilika wakati wowote kutegemeana na hali ya soko. Kwa mwelekeo wa jumla wa bei unavyokwenda, kuna dalili kuwa bei hizi hazitapanda hivi karibuni na labda zitaendelea kuteremka, hivyo wakulima wanashauriwa kuuza mazao yao ya pamba hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, Serikali inaagiza yafuatayo:-

Kwa wale wakulima ambao waliuza pamba yao na kulipwa shilingi 250/= kwa kilo, wanunuzi waliohusika wafanye marekebisho kama yalivyoelezwa kwa kurekebisha viwango vya makato yaliyoelekezwa ili fedha za nyongeza zinazookolewa kutoka makato hayo zipewe wakulima hao kwa kiwango cha shilingi 25/= kwa kilo, kwa pamba ya mbegu daraja la kwanza. Hesabu za bei ya pamba daraja la pili zifanywe kwa kufuata vipengere na sura hiyo ya bei inayohusika. Wizara husika, Bodi na TCA, wakamilishe hesabu hiyo kabla ya tarehe 1 Agosti, 2004, yaani keshokutwa. (*Makofî*)

Nataka nifafanue sehemu hiyo. Kwa hiyo, wale wakulima ambao wamekwishauza mazao yao kwa bei ya shilingi 250/=, watahitajika kuongezewa shilingi 25/= kwa kilo kwa wale ambao wamewauzia mazao hayo. (*Makofî*)

Utaratibu huu utaendelea kutumika na utaacha kutumika kama bei ya pamba itapanda na bei ya mkulima kufikia shilingi 300/= au zaidi kwa kilo. Katika hali hiyo utaratibu wa zamani utarudia.

Bodi ya Pamba isimamie maamuzi haya ya Serikali kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, inaonekana dhana ya biashara huria na sera ya Serikali kutokufanya biashara bado haijaleweka vizuri kwa Wananchi wetu. Biashara ya zao lako ni baina ya wewe mkulima na mnunuzi kama ilivyo kwa mnunuzi wa bidhaa na mwenye duka. Serikali mnakutana nayo kama kuna kukata leseni au kulipa kodi ama ushuru na labda katika kuweka mazingira mazuri ya biashara. Mnapolipana fedha hazipitii mikononi mwa Serikali na hii ndivyo ilivyo kwa mazao yetu yote ikiwepo zao la pamba. Mkulima unamkabidhi mnunuzi zao lako naye anakulipa fedha zako. Fedha hizo huendi kuzipokelea Ofisi ya Mkuu wa Wilaya au Ofisi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu hali ya kushuka kwa bei ya zao inapotokezea kama ilivyokuwa sasa kwa zao hili la pamba, wapo wanasiasa tayari wameanza kuzungukazunguka na kuwadanganya wakulima kuwa, fedha zenu shilingi 50/= kwa kilo zimekatwa na Serikali kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya CCM. Huu ni uwongo usio na aibu na wala wakulima msikubali kudanganywa. CCM haijawahi na wala haitawahi kukata fedha za wakulima au za kundi lolote la Wananchi kiujanja ujanja kwa ajili ya kugharamia shughuli zake. CCM siku zote ndiyo Chama tetezi wa wanyonge na itaendelea hivyo. Ningewashauri sana wanasiasa wenzangu, tusipende kutumia matatizo ya kweli ya Wananchi kwa maslahi ya kisiasa kwa sababu watakapong' amua kuwa unawadanganya hawatakuwa tena na imani na wewe. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/2005 Wizara ya Ushirika na Masoko

SPIKA: Namwita mtoha hoja ya leo, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Lakini subira kidogo, Mheshimiwa Waziri, ili wanaotoka kwenda kwenye chai wafanye hivyo. Tuko tayari kuanza sasa, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, muda wako wa kusema unahesabiwa kuanzia sasa.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, inayohusu Wizara ya Ushirika na Masoko na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005. Pamoja na Hotuba hii, nawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara katika kipindi cha 2003/2004, yaliyowasilishwa na kujadiliwa na Kamati hiyo tarehe 2 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wasemaji walionitangulia kutoa salamu za rambirambi kwako Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kutokana na vifo vyta Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Kapteni Mstaafu Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Natoa pole sana kwa familia za Marehemu na Wananchi wa Majimbo ya Mbeya Vijijini na Ulanga Mashariki, kwa misiba hii mikubwa. Aidha, nawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge wa Viti Maalum, kwa msiba wa kufiwa na baba yao mzazi, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Vijijini na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze hotuba yangu kwa kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake makini ambao umeweza kuiletea Jamhuri yetu maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii kwa muda mfupi wa miaka takribani nane na nusu ambapo amekuwa madarakani. Watanzania wote tunalo deni la kumshukuru na pia kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, aweze kupona haraka maradhi yanayomsibu ili aendelee na juhudzi zake za kuliongoza Taifa hili katika vita ya kuondoa umaskini na kuimarisha amani katika Eneo la Maziwa Makuu si tu katika kipindi chake kilichobaki cha Urais, lakini pia hata katika miaka itakayofuatia baada ya hapo.

Watanzania wote vile vile inatubidi tumshukuru Mwenyezi Mungu daima kwa kutujalia neema ya kuwachagua viongozi makini na waadilifu wa kuiongoza nchi yetu tangu harakati za kupigania uhuru hadi sasa. Uongozi huo ndio umetuwezesha kujenga Taifa lenye umoja, mshikamano, utulivu na amani ambavyo ndiyo misingi mikuu ya kuleta maendeleo katika nchi yoyote ile. Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala*, tunamwomba aendelee kutuongoza vyema katika kuwachagua viongozi shupavu wa kuliongoza Taifa letu katika muda wote wa uhai wa Taifa letu, *Amen. (Makofi)*

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Mtanzania mwenzetu Profesa Anna Tibajuka, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (*Habitat*) kwa kuteuliwa na Waziri Mkuu wa Uingereza kuwa Makamishna katika Kamisheni ya Afrika ambayo itatathamini matatizo ya maendeleo yanayoikabili Afrika. Uteuzi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa unatokana na uzoefu na juhudzi zake katika kupambana na matatizo ya Afrika, hususan matatizo ya maendeleo na umaskini uliokithiri. Sote tunajivunia uteuzi huo wa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na wa Profesa Tibajuka. Nachukua nafasi hii pia kumpongeza Balozi Ali Mchumo, kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pamoja wa Bidhaa (*Common Fund for Commodities - CFC*) mwezi Juni, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, iliyojadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa 2003/2004 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, tarehe 2 Juni, 2004 na kuyapitisha. Ushauri uliotolewa na Kamati utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wasemaji waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, aliyeshinda katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bariadi Mashariki tarehe 30 Mei, 2004. Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mbunge kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, Bunge la kwanza la Afrika liliundwa mwezi Machi, 2004. Napenda kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha katika Bunge hilo amba ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Kissassi, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe. Aidha, ninatoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Balozi Getruda Mongella, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa kwanza wa Bunge hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah V. N. Chibulunje, Katibu Mkuu wa Wizara, Dr Ladislaus C. Komba, pamoja na Wakuu wa Idara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara, Watumishi wote na Wadau wa Ushirika na Masoko, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, hususan katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 hadi 2005 na kufanikisha maandalizi ya taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2004/2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimechambua na kufafanua masuala mengi ya kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na hali ya Ushirika na Masoko na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha, kufufua na kuendeleza Ushirika na Masoko nchini. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliota michango mizuri ya ushauri kuhusu Ushirika na Masoko, ambayo tuliyachukua na tutayaafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Vyama vya Ushirika imara na endelevu kama njia mojawapo muhimu ya kuwawezesha Wananchi wengi nchini kuondoa umaskini, ni mchakato wa kijamii na kiuchumi amba huchukua muda kufikia matokeo yaliyokusudiwa. Ushirikishwaji wa wadau wote wa ushirika katika kutekeleza wajibu na majukumu yao ni muhimu katika kuhakikisha kuwa, mchakato huu unaharakishwa na mafanikio yanapatikana katika kipindi kifupi kadiri inavyowezekana. Kwa kutambua umuhimu wa Ushirika katika kuwawezesha Wananchi kujilettea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali yetu kwa ushirikiano na wadau mbalimbali, imeandaa mazingira yanayofaa kwa ajili ya ustawi wa Vyama vya Ushirika. Hatua zilizochukuliwa na Serikali kufikia azma hiyo ni pamoja na kukamilisha Sera mpya ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002 inayozingatia mazingira halisi ya kibiashara, kiuchumi na Kijamii na kupitishwa kwa Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika ya 2003 itakayoanza kufanya kazi Mwezi Agosti, 2004.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba, hatua mbalimbali zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zitasaidia kwa kiasi kikubwa katika kutatua matatizo yaliyokuwa yanavikabili Vyama vya Ushirika, hususan uongozi mbovu na uendeshaji usio makini, ukosefu wa mitaji, elimu duni ya ushirika na ya kuendesha vyama kibiashara. Jitihada za Wizara ya Ushirika na Masoko na wadau mbalimbali

katika kufufua, kuimarisha na kuendeleza Vyama vya Ushirika, zimejielekeza katika kuleta mwamko mionganoni mwa Wanaushirika na Wananchi kwa ujumla wa kuanzisha na kuendeleza Vyama vya Ushirika katika Sekta mbalimbali za uchumi kwa manufaa yao. Kutohada na jitihada hizo idadi ya Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali imeongezeka kutoka Vyama 4,903 mwezi Mei, 2003 hadi kufikia Vyama 5,462 mwezi Mei, 2004 sawa na ongezeko la asilimia 11.4. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vyama ambavyo vimeduwa na ongezeko kubwa ni pamoja na Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*), ambavyo vimeongezeka kutoka vyama 1,236 (778 Mijini na 458 Vijijini) Mwezi Mei 2003 hadi kufikia Vyama 1,509 Mwezi Mei 2004, sawa na ongezeko la asilimia 22. Aidha, katika kipindi hicho, Vyama vya Ushirika wa Mifugo navyo vimeongezeka kutoka Vyama 84 hadi Vyama 116, sawa na ongezeko la asilimia 38, Vyama vya Ushirika wa Uvuvi, vimeongezeka kutoka Vyama 86 hadi Vyama 110, sawa na ongezeko la asilimia 28 na Vyama vya Ushirika wa Viwanda, vimeongezeka kutoka vyama 232 hadi vyama 262, sawa na ongezeko la asilimia 13. Ongezeko la idadi ya Vyama vya Ushirika ni ishara kuwa wananchi sasa wamehamasika kuanzisha na kuimarisha Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za uchumi, kama njia mojawapo ya kuwapatia mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, suala la kupanua wigo wa Ushirika ni muhimu katika kuunganisha nguvu za wazalishaji wadogo na wa kati katika sekta mbalimbali za uchumi ili kuwawezesha kuboresha shughuli wanazofanya, kutumia vizuri fursa zilizopo katika uchumi wa soko na kuongeza tija kadri ya mahitaji yao. Kama takwimu zinavyoonyesha, uanzishaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika umegusa katika sekta mbalimbali za uchumi kulingana na mahitaji ya wananchi. Aidha, Vyama vya Ushirika vimeongezeka katika sekta za Fedha, Mifugo, Uvuvi, Madini, Viwanda, Usafirishaji, Huduma na Kilimo.

Hali hii inaonyesha jitihada zinazofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Ushirika na Masoko za kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika kwa kushirikiana na Wadau wengine, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Fedha, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania. Jitihada hizo zimeanza kuleta mafanikio na zitaimarishwa zaidi ili kuhakikisha kuwa Ushirika unatoa mchango mkubwa zaidi katika kuimarisha shughuli za wazalishaji wadogo na wa kati, hususan katika suala zima la kuondoa umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo la ukosefu wa mitaji ndani ya Vyama, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi, kujiunga na au kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*). Uzoefu umeonyesha kuwa uanzishaji na uendelezaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*Savings and Credit Cooperative Societies - SACCOS*) unawapa wananchi fursa ya kupata huduma za kifedha, ambazo wengi wao wasingeweza kuzipata kwa kutumia taasisi nyingine za fedha. Aidha, ushirikiano baina ya *SACCOS* na Asasi nyingine za fedha, hususan Benki za Biashara umeimarishwa na hivyo kutoa fursa kwa wananchi ya kupata mikopo kutoka Benki kwa masharti nafuu kupitia *SACCOS* zao mahali walipo bila kulazimika kwenda

Benki ya Biashara husika. Kwa kutambua manufaa hayo kwa Wananchi, Wizara imeweka msukumo mkubwa katika kuwawezesha wananchi, kuanzisha na kuendeleza *SACCOS* ili waweze kuondoa tatizo la ukosefu wa mitaji ya kuendeshea shughuli zao. Kutokana na jitihada hizo Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo vimeendelea kuwa na mvuto mkubwa kwa wananchi sehemu mbalimbali na kuongezeka kwa wingi kama ilivyoelezwa hapo awali.

Aidha, idadi ya Wanachama iliongezeka kutoka 157,774 mwezi Mei, 2003 hadi 219,345 mwezi Mei, 2004 sawa na ongezeko la asilimia 39. Hisa, amana na akiba za Wanachama zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 20.9 na kufikia shilingi billioni 29.7 katika kipindi hicho, sawa na ongezeko la asilimia 42. Katika maeneo mengi, hususan Vijijini Vyama hivi vinatumika kutoa huduma muhimu za Kibenki kwa wananchi, huduma ambazo zinawawezesha kuongeza uzalishaji na kujipatia mahitaji ya kila siku na hivyo kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa na *SACCOS* kwa wanachama wake imeendelea kukua kwa kasi mwaka hadi mwaka na hivyo kuwanufaisha wanachama wengi wakiwemo wakulima, wavuvi, wafanyabiashara wadogo, wafugaji na wafanyakazi. Katika mwaka mmoja uliopita mikopo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 19.3 mwezi Mei, 2003 hadi shilingi bilioni 43.2 mwezi Mei, 2004 sawa na ongezeko la asilimia 123. Aidha, katika kipindi cha miaka minne iliyopita mikopo iliyotolewa na *SACCOS* imeongezeka kutoka shilingi bilioni 11.5 mwezi Juni, 2000 hadi shilingi bilioni 43.2 mwezi Mei, 2004 sawa na ongezeko la asilimia 275. Mafanikio hayo ya utoaji mikopo pamoja na bidhaa nyingine za fedha kwa wanachama yametokana na mambo mengi yakiwemo: Mwamko wa Wananchi ama kujiunga au kuanzisha Vyama hivi na kushiriki kikamilifu katika shughuli zake, kuimarika kwa uendeshaji wa Vyama, kukua kwa ushirikiano baina ya *SACCOS* na Benki za biashara na kukua kwa Mfuko wa Kukopeshana wa *SACCOS* (*Central Finance Programme*), unaoendeshwa na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (*Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania - SCCULT*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *SACCOS* ni asasi za kifedha kama vile Benki za Biashara, zinahitaji kuwepo kwa uendeshaji na usimamizi makini ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi na kuchangia katika maendeleo yao. Kwa kuzingatia hili na mabadiliko ya Sera na Sheria zinazohusika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha (Benki Kuu), inaandaa miongozo mbalimbali ya uendeshaji na usimamizi wa *SACCOS* nchini ili kuziwezesha kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria husika na Viwango vya Kimataifa vya uendeshaji wa asasi hizo. Aidha, hatua hii itaziwezesha *SACCOS* kuajiri watendaji wenye sifa za kutosha, kuimarisha uongozi, uendeshaji na uwajibikaji kwa wanachama. Tayari hatua mbalimbali za kuleta mabadiliko ya uendeshaji wa *SACCOS* zimekwishaanza kutekelezwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania, Benki ya CRDB na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya *FISEDA* na *DID*, imeendelea kuviwezesha Vyama kufanya maandalizi ya kubadili mfumo wa uendeshaji.

Katika kipindi hiki kazi zilizofanyika ni pamoja na kutoa elimu na mafunzo kwa Wanachama 2,210, Watendaji 518 na Viongozi 956 kutoka *SACCOS* 414. Kazi nyingine ni ujenzi wa Ofisi zenye kuvutia wateja (*Frontal offices*), uhamasishaji wa Wananchi ili kuongeza idadi ya wanachama na kuhakikisha kuwa huduma za fedha zinawafikia wananchi wengi zaidi, na uimarishaji wa usalama wa fedha za Wanachama. Idadi ya *SACCOS* zilizobadili mfumo wa uendeshaji na kuboresha utoaji huduma imeongezeka kutoka 50 mwezi Mei, 2003 hadi 90 mwezi Mei, 2004 sawa na ongezeko la asilimia 80. Juhudi za makusudi zinafanyika kuongeza idadi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika wa mazao pia vinaendelea kufanya marekebisho ya uendeshaji kwa lengo la kujiimarisha ili viweze kuwahudumia wanachama wake ipasavyo. Kwa kutumia utaratibu wa Udhagini wa Mikopo kwa Mauzo ya nchi za Nje (*Export Credit Guarantee Scheme*), idadi ya Vyama Vikuu vya Ushirika vilivyoweza kupata mikopo kutoka Benki kwa ajili ya kukusanya mazao ya wakulima imeongezeka kutoka Vyama tisa msimu wa 2002/2003 hadi kufikia Vyama 12 msimu wa 2003/2004. Aidha, Vyama vya Msingi vitano vya Wilaya ya Mbinga, Mkoa wa Ruvuma vimepata mikopo chini ya utaratibu huu kwa miaka miwili mfululizo na vimeweza kurejesha kikamilifu mikopo iliyopata. Vilevile, baadhi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi vya mazao vinavyojitegemea pamoja na baadhi ya Vyama Vikuu vya Ushirika, vimeweza kutoa malipo ya pili na ya tatu kwa Wanachama wao. Kwa mfano, *ISAYULA* na *MBOCU*, baada ya malipo ya awali ya shilingi 350 kwa kilo ya kahawa wamelipa malipo ya pili ya shilingi 200 kwa kilo. *ACU* ililipa malipo ya pili ya shilingi 100 na malipo ya tatu ya shilingi 100 kwa kilo ya kahawa baada ya malipo ya awali ya shilingi 550/= kwa kilo. Vyama vya Msingi vya *RUMAKO* Mkoani Kigoma vimeweza kuwalipa wakulima jumla ya shilingi 1,150/= kwa kilo ya kahawa na hivyo kuwa mionganoni mwa malipo ya juu yaliyotolewa kwa wakulima wa kahawa aina ya *Arabica* katika msimu wa 2003/2004. Aidha, Vyama hivi vimeweza kununua Kinu cha kukobolea kahawa ambacho kinatarajiwu kuanza kufanya kazi msimu wa 2004/2005, baada ya kazi ya usimikaji kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu wa *ECGS*, Serikali imekuwa ikichukua hatua pale inapobidi, za kuvinusuru Vyama vya Ushirika visifilisiwe na badala yake viimarike na kuwa katika hali ya kukopesheka. Kwa mfano, madeni ya Vyama vya *KCU*, *KDCU* na *NCU* kwa Benki za *CRDB* na *NBC* kwa msimu wa 1999/2000, yenye thamani ya shilingi bilioni 3.0 na madeni ya Chama cha *KNCU* kwa *CRDB* kwa msimu wa 2001/2002 ya shilingi 667,750,353/= yalichukuliwa na Serikali ili kuvinusuru visifilisiwe. Awali mkopo wa fedha katika msimu huo ultolewa kwa utaratibu wa *ECGS*.

Aidha, katika msimu wa 2000/2001, bei ya Kahawa katika Soko la Dunia iliposhuka sana na kusababisha Vyama vya *KCU* na *KDCU* vishindwe kuwalipa wakulima, Serikali iliingilia kati na kutoa shilingi bilioni 1.7 kuwalipa wakulima waliokuwa wanavidai Vyama hivyo. Vilevile, kwa upande wa zao la Pamba, kwa sababu ya kuporomoka kwa bei katika msimu wa 2001/2002, Serikali ilivisaidia Vyama vya *SHIRECU*, *NCU* na *BCU* kulipa deni la jumla ya shilingi bilioni 3.79 kwa Benki ya *NBC* ili kuvinusuru visifilisiwe. Awali mkopo wa fedha katika msimu huo ultolewa kwa utaratibu wa *ECGS*.

Mheshimiwa Spika, juhudi kama hizi zimefanywa pia na Serikali ili kuwanusuru wakulima wa Pareto katika Mikoa ya Iringa na Mbeya kutokana na hasara ambayo wangeipata kwa matatizo ya soko tangu msimu wa 2001/2002. Katika mwaka 2003/2004, Serikali ilitoa dhamana kwa Kampuni ya *Tanzania Pyrethrum Processing and Marketing Company Ltd. (TPPMCL)* na hivyo kuiwezesha kukopa shilingi bilioni 1.48 kutoka Benki ya *Standard Chartered*. Mkopo huo umeiwezesha *TPPMCL* kununua pareto yote liliyolundikana mikononi mwa wakulima pamoja na kuwalipa shilingi milioni 200 walizokuwa wanaidai. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuendeleza ushirika, tatizo sugu la ukosefu wa ajira kwa vijana linaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa Mkoani Tanga (*TDCU*) kwa kuititia mradi wa *Pingoni Youngsters Dairy Settlement Scheme*, kimewezesha vijana zaidi ya 350 kujipatia ajira kwa kufanya shughuli ndogo ndogo zinazohusu uzalishaji na uuzaji wa maziwa. Kwa kushirikiana na *TDCU* na Chuo cha Ushirika Moshi, Wizara yangu itaandaa mafunzo kwa vijana hao ili waweze kupata stadi za ushirika na biashara ili wafanye shughuli zao kiufanisi zaidi. Napenda kutoa wito kwa vyama vingine vya ushirika kuiga mfano wa *TDCU* katika kupambana na tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa utendaji wa Vyama vingi vya Ushirika bado una upungufu, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imeendelea kuviwezesha Vyama vya Ushirika kuboresha uendeshaji. Mkazo mkubwa umewekwa katika utoaji elimu kwa wanachama ili waweze kuvisimamia inavyostahili ikiwa ni pamoja na kudhibiti uendeshaji mbovu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ushirika Moshi katika kutekeleza shughuli zake za kitaaluma, ushauri, utafiti na elimu ya ushirika kwa wanachama, kimekuwa na mafanikio katika uenezaji wa mbinu za ujenzi wa ushirika shirikishi wenyewe mwelekeo wa biashara zaidi kuliko ule wa huduma za jamii. Aidha, idadi ya wanafunzi imongezeka kutoka 341 mwaka 2002/2003 hadi kufikia wanafunzi 556 mwaka 2003/2004, sawa na ongezeko la asilimia 63. Aidha, idadi ya wanafunzi kwenye kozi fupi iliongezeka toka 66 mwaka 2002/2003 hadi kufikia 82 mwaka 2003/2004. Usajili katika kozi ya Shahada ya Uzamili katika Menejimenti na Maendeleo inayotolewa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Leicester, Uingereza ulibaki kuwa wanafunzi 42 kama mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Chuo cha Ushirika Moshi kimeweza kupanua wigo wa ushirikishwaji katika shughuli za utafiti na usambazaji wa taarifa zitokanazo na utafiti huo. Chuo kimeendelea na Uchapishaji wa jarida la *Journal of Cooperative and Business Studies* kwa ajili ya, pamoja na mengine, kusambaza taarifa mbalimbali za ushirika. Matawi 19 ya Chuo yaliyoko Mikoani yameendelea kuimarishwa kwa kuajiri na kuwapa mafunzo walimu wapya, kukarabati majengo yake na kuyapatia vitendea kazi. Aidha katika mwaka huu wa 2003/2004, tawi jipya limeanzishwa Kibaha (Pwani). Kabla ya hapo Mkoaa wa Pwani ulikuwa unahudumiwa na tawi la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ushirika Moshi kimeendelea kutoa elimu, kufanya utafiti na kutoa ushauri kwa ajili ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika ndani na nje ya nchi. Chuo kimeweka msukumo mkubwa katika utoaji Elimu ya Ushirika Shirikishi kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika ili kuwapa mbinu za ujasiriamali ambazo ni muhimu katika usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika katika mazingira ya uchumi wa Soko huru. Aidha, elimu hiyo itasaidia kuwajasirisha, wawe wabunifu wenye kuthubutu na kujiamini. Kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Ujasirishaji Wanachama (*MEMCOOP*), Chuo cha Ushirika Moshi kiliendesha mafunzo juu ya dhana na mchakato wa elimu ya Ushirika Shirikishi kwa wadau wote muhimu ikiwa ni pamoja na wanachama 600, watendaji 54 na Viongozi 60, wa baadhi ya Vyama vya Msingi, Vyama Vikuu na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania. Aidha, mafunzo hayo yametolewa kwa Maafisa ushirika wa Wilaya 294, Washauri wa Ushirika wa Mikoa 21, Wakaguzi wa Mikoa minane wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), Walimu wa Matawi 30 na wa Makao Makuu wa Chuo cha Ushirika Moshi pamoja na Viongozi na Maafisa waandamizi 25 wa Wizara. Programu ya *MEMCOOP* itaanza kutekelezwa mwaka 2004/2005 katika Mikoa yote na Wilaya 60. Vyama vya Ushirika na vikundi 2000 vitashiriki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nilipowasilisha Hotuba yangu nilieleza kuwa lengo kuu la Serikali ni kukiongezea uwezo wa kitaalam Chuo cha Ushirika Moshi. Katika kufikia lengo hili nafurahi kulifahamisha lako Bunge Tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imekamilisha maandalizi ya kukipandisha hadhi Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*The Moshi University College of Cooperative and Business Studies - MUCCOBS*). Hatua hiyo imefikiwa baada ya Baraza la Mawaziri kuupitisha Waraka husika Aprili, 2004 na Mheshimiwa Rais kukubali na hatimaye kuweka saini Tangazo Rasmi (*Declaration Order*), ambalo limewekwa katika Gazeti la Serikali tarehe 28 Mei, 2004.

Mheshimiwa Spika, programu maalum ya kuondoa viforo vya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika imeendelea kutekelezwa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*). Programu hii imevisaidia Vyama vya Ushirika kuwa na hesabu zilizokaguliwa kwa wakati na hivyo kuwapa wanachama fursa ya kusomewa hesabu mapema ili waweze kuchukua hatua zinazostahili. Katika kipindi hiki Shirika limekagua hesabu za Vyama 3,023 kati ya Vyama 3,530 vilivyotarajiwa sawa na asilimia 85.6. Kutokana na utekelezaji wa programu hii idadi ya Vyama vya Ushirika vyenye hesabu zilizokaguliwa kwa wakati imeongezeka kutoka Vyama 2,888 mwaka 2002/2003 hadi Vyama 3,023 mwaka 2003/2004 sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa shirika, watumishi 44 walipatiwa mafunzo katika fani mbalimbali. Aidha, shirika lilifanya uhamisho wa baadhi ya watumishi waliokaa kwenye vituo kwa muda mrefu ili kuongeza tija na ari ya kufanya kazi. Watumishi pia walipatiwa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari manne yaliyopelekwa mikoani. Juhudi za kulipatia Shirika wataalam wenye sifa zinazostahili zimeweza idadi ya wakaguzi na wahasibu wenye CPA kuongezeka kutoka wawili waliokuwepo mwaka 2000/2001 hadi kufikia tarehe 16 Juni, 2004. Kutokana na mafanikio hayo katika mwaka wa

2003/2004, Shirika limeidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania kuweza kufanya ukaguzi kwenye Taasisi za kifedha zikiwemo Benki za Biashara.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walio wengi ni maskini na hutegemea shughuli za kilimo na ufugaji kwa maisha yao. Kwa kuzingatia hali hiyo Serikali inaelekeza kila jitihada zake katika kuimarisha sekta ya kilimo ili kuweza kuwakwamua wananchi walio wengi kutoka katika hali ya umaskini. Upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo ni moja ya kichocheo kikuu cha kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Aidha, upatikanaji wa masoko ya uhakika huwezesha wakulima kuzalisha mazao hayo kibiashara kwa kuzingatia mahitaji ya masoko hayo, hususan ubora, madaraja na ufungashaji. Vilevile Serikali inahimiza usindikaji wa mazao kabla ya kuyauza kila inapowezekana, kwani usindikaji sio tu huongeza nafasi za ajira kwenye vinu na viwanda vya kusindika mazao, bali pia huongeza uwezekano wa kupata soko la uhakika na fursa kwa mzalishaji kupata malipo mazuri zaidi, hususan kwa mazao ya korosho, pamba, mbegu za mafuta, muhogo, nafaka, matunda na bidhaa zitokanazo na mifugo. Hii inatokana na ukweli kwamba mazao mengi na bidhaa nyingi za Tanzania huuzwa kabla hazijaongezewa thamani kwa kuzisindika na hivyo hushindwa kuhimili ushindani katika masoko ya nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo kadhaa ambayo yanaathiri juhudzi za upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao nchini. Makubwa katika hayo ni pamoja na uduni wa miundombinu ya masoko ambao husababisha gharama za kusafirisha mazao kutoka sehemu za uzalishaji kwenda kwenye soko kuwa kubwa, ukosefu wa taarifa za mahitaji ya masoko hasa ya nchi za nje, wafanyabiashara wadogo kukosa stadi za biashara na mitaji ya kuendeshea shughuli zao na uwezo mdogo wa wazalishaji hususan wakulima katika kujadiliana bei na wanunuzi. Aidha, bidhaa kutoka nchi za nje zinazoingia kwa wingi nchini huwapunguzia uwezo wa ushindani wazalishaji wa Tanzania kwa kuwa bidhaa hizo mara kwa mara huwa na bei ndogo kuliko zilizozalishwa hapa nchini. Vilevile, Watanzania walio wengi wana kasumba ya kupenda kutumia bidhaa kutoka nchi za nje kuliko zile zinazozalishwa hapa nchini hata kama bidhaa hizo zina ubora na viwango vinavyolingana. Uimarishaji wa soko la ndani utasaidia sana katika kupunguza matatizo haya hususan kwa mazao yanayozalishwa nchini, kwa mfano nafaka, mbogamboga, matunda, pamba na bidhaa za mifugo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo hayo, mfumo wa soko huru haujawasadida sana wakulima wadogo wadogo. Badala yake pale ambapo kuna upungufu katika usimamizi wa taratibu za soko, wanunuzi binafsi wasio waaminifu huwapunjwa wakulima kwa kununua mazao kwa bei ya chini, kupanga bei bila kujali madaraja ya ubora wa mazao, kutumia vipimo visivyothibitishwa kisheria. Aidha, kwa sababu ya udhaifu wao na kwa kutokuwa na uwezo wa kupata mikopo, wakulima hulazimika kuza mazao yao kwa bei ya chini mara baada ya mavuno badala ya kusubiri wakati bei zinapokuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2003/2004, hali ya masoko kwa baadhi ya mazao ya biashara imekuwa ya kuridhisha kutokana na ongezeko la bei katika soko la dunia. Ongezeko hilo liliwezesha bei za wakulima kupanda kwa wastani wa kati ya

asilimia 7.5 na 56 ikilinganishwa na bei katika msimu wa 2002/2003. Hata hivyo, bei ya kahawa aina ya mild arabica haikubadilika na kubakia kuwa shilingi 500/= kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina fursa kubwa ya kukuza soko la nje kwa mazao yake kwa kupitia mikataba na makubaliano mbalimbali kama vile Soko la Amerika kwa mujibu wa *African Growth and Opportunity Act (AGOA)*, Jumuiya ya Ulaya (EU) chini ya utaratibu wa *Everything But Arms*, utaratibu wa upendeleo maalum kwa nchi zinazoendelea wa Jamhuri ya China na nchi ya Canada, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Makampuni machache yanayosafirisha mazao ya biashara asilia (*Traditional Export Crops*) kama kahawa, chai, tumbaku, mkonge na pamba na makampuni yanayozalisha mazao ya biashara yasiyo asilia kama maua, mbogamboga na sukari wanatumia fursa hii kwa kuuza bidhaa zao katika soko la Jumuiya ya Ulaya (EU). Ili kukuza soko la mazao na kuwawezesha wafanyabiashara wetu kuingia katika masoko hayo, Serikali inaendelea kuwawekea mazingira mazuri ya kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kimataifa. Hii ni pamoa na kuanzisha maeneo maalum ya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi, yaani *Export Processing Zones (EPZ)*.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa mazao ya kahawa, korosho, tumbaku ya moshi na pamba kwa msimu wa 2003/2004, ulipungua ikilinganishwa na msimu wa 2002/2003. Ununuzi wa zao la kahawa ulipungua kwa asilimia 28, korosho asilimia 17.3, tumbaku ya moshi kwa asilimia 29 na pamba asilimia 25.9. Kushuka kwa ununuzi wa mazao hayo kulitokana na kushuka kwa uzalishaji kulikosababishwa na ukame ulioikumba sehemu kubwa ya nchi msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa zao la tumbaku ya mvuke uliongezeka kwa asilimia 48.8 ikilinganishwa na ongezeko dogo la asilimia mbili katika ununuzi kwa zao la chai na asilimia moja katika ununuzi wa zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, zao la pareto bado linakabiliwa na tatizo la soko tangu msimu wa 2001/2002. Hata hivyo, ununuzi wa zao hilo kutoka kwa wakulima umepatiwa ufumbuzi baada ya Kampuni ya *Tanzania Pyrethrum Processing and Marketing Company Ltd. (TPPMCL)* kufanikiwa kupata mkopo wa Shilingi bilioni 1.48 kutoka Benki ya *Standard Chartered* chini ya Udhamini maalum wa Serikali kwa utaratibu wa *Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)*. Kampuni ililipa madeni ya wakulima na kununua tani 300 za pareto iliyokuwa imelundikana kwa wakulima na wanunuzi binafsi. Aidha, Kampuni inaendela kununua pareto msimu wa 2003/2004, ambayo inakisiwa kufika tani 1,000. Kampuni inalipa malipo ya awali ya shilingi 100/= kwa kilo ya maua ya pareto ya misimu iliyopita na shilingi 360 kwa kilo kwa pareto ya msimu wa 2003/2004. Malipo ya pili kwa ajili ya pareto ya misimu iliyopita yanafanywa na Kampuni mara baada ya kufanya tathmini ya kiasi cha sumu kilichopo katika maua hayo wakati ambapo malipo ya pili kwa maua ya pareto ya 2003/2004, yatafanywa baada ya kuuza sumu iliyoziduliwa. Vilevile Kampuni inaendelea kuzidua maua ya pareto na kuhifadhi sumu inayopatikana. Kiwanda kinaendelea na juhudzi za kutafuta soko la sumu hiyo.

Mheshimiwa Spika, wastani wa bei ya mkulima kwa mazao ya biashara msimu wa 2003/2004, iliongezeka kwa viwango tofauti ikilinganishwa na bei za msimu wa 2002/2003. Bei ya kahawa aina ya robusta iliongezeka kutoka shilingi 135 hadi shilingi 180 kwa kilo ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 33. Bei ya kahawa aina ya arabica kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 300/= kwa kilo kufikia shilingi 350/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.6. Wakati huo huo, bei ya Kahawa aina ya *arabica* ambayo huzalishwa katika mikoa ya Kaskazini ilibakia kuwa na wastani wa shilingi 500 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, bei ya mkulima kwa zao la korosho iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 360 kwa kilo msimu wa 2002/2003 hadi shilingi 500/= kwa kilo msimu wa 2003/2004. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 39. Bei ya mkulima wa zao la pamba iliongezeka kwa asilimia 55.5 kutoka shilingi 180 msimu wa 2002/2003 hadi shilingi 280 kwa kilo msimu wa 2003/2004. Katika kipindi hicho bei ya mkulima wa tumbaku ya mvuke iliongezeka kutoka shilingi 574/= kwa kilo hadi shilingi 729/= ambayo ni sawa na asilimia 27 ambapo bei ya tumbaku ya moshi iliongezeka kutoka shilingi 470 hadi shilingi 679/= kwa kilo ikiwa ni ongezeko la asilimia 44. Bei ya mkulima wa zao la chai iliongezeka kutoka shilingi 80 msimu 2002/2003 hadi kufikia shilingi 86/= kwa kilo msimu wa 2003/2004, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.5.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bei ya mkulima kwa mazao ya biashara katika msimu wa 2003/2004 kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa bei za mazao hayo katika soko la dunia. Bei za mazao hayo ziliongezeka kama ifuatavyo: Bei ya kahawa aina ya robusta iliongezeka kutoka wastani wa Dola za Marekani 0.52 hadi Dola 0.53 kwa kilo, *arabica* kutoka Dola za Marekani 1.11 hadi Dola za Marekani za 1.48 kwa kilo. Bei ya kuuzia nje pamba nyuzi iliongezeka kutoka Dola za Marekani 0.87 hadi Dola za Marekani 1.54 kwa kilo. Bei ya tumbaku ya mvuke iliongezeka kutoka Dola za Marekani 2.18 hadi Dola za Marekani 2.36, bei ya tumbaku ya moshi iliongezeka kutoka Dola za Marekani 1.78 hadi Dola 2.05 kwa kilo. Bei ya chai katika mnada wa Mombasa iliongezeka kutoka Dola za Marekani 1.24 msimu wa 2002/2003 hadi Dola 1.34 msimu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa sukari msimu wa 2003/2004, ulikuwa tani 223,839 ikilinganishwa na mahitaji ya takriban tani 360,000 kwa mwaka. Uzalishaji wa sukari uliongezeka kwa asilimia 17.7 ikilinganishwa na tani 190,120 zilizozalishwa mwaka 2002/2003. Mauzo ya sukari katika soko la ndani kwa matumizi ya nyumbani yalifikia tani 201,089 hadi kufikia Mei, 2004. Aidha, mauzo ya sukari katika soko la Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) chini ya utaratibu wa *Everything But Arms (EBA)* kwa msimu wa 2003/2004 yalikuwa tani 22,750. Kiasi hicho kiliingizia Taifa jumla ya shilingi bilioni 16 ikilinganishwa na shilingi bilioni 12 zilizopatikana baada ya kuuza tani 22,700 katika msimu wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya sukari kwa matumizi ya viwandani mwaka 2003/2004, ilikadiriwa kufikia tani 54,515. Sukari hii hadi sasa haizalishwi katika viwanda vyetu vya ndani na hivyo Serikali iliruhusu wenyе viwanda kuagiza sukari ya aina hiyo kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, wazalishaji wengi wa mazao ya mboga mboga, na matunda hutegemea sana soko la ndani. Pamoja na lengo la kuimarishe soko la ndani la mazao hayo kwa kiasi kikubwa hushindwa kupanya katika masoko ya nje kutokana na kutokidhi viwango vya mahitaji ya masoko ya kimataifa. Mahitaji ya soko la kimataifa ni pamoja na kupanga mazao katika madaraja ya ubora, masharti ya ukaguzi wa usafi na magonjwa (*sanitary and phytosanitary*), ufungashaji na uhakika wa upatikanaji. Hata hivyo, wazalishaji wachache wametimiza viwango hivyo na kufanikiwa kupata soko la mazao yao katika nchi za Jumuiya ya Ulaya. Wazalishaji hao ni pamoja na makampuni ya *Gomba Estate Limited* na *Serengeti Fresh Limited* ambayo huzalisha na kuza mbogamboga. Makampuni mengine ni *Kiliflora Limited*, *Tengeru Flowers Limited* na *La Fleur d'Afrique Limited* ambayo huuza maua na Kampuni za *Tanzania Zanzibar Organic Producers (TAZOP)* na *Zanzibar Organic Producers (ZANOP)*, ambazo huuza viungo vya chakula.

Makampuni hayo yalipata fursa ya kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ya mbogamboga, maua, matunda na viungo vya chakula yaliyofanyika mjini Rostock, Ujerumani mwaka 2003 na kushinda tuzo mbalimbali, zikiwemo nishani za dhahabu 14, za fedha 12 na za shaba saba. Aidha, Serikali ya Tanzania ilitunikiwa medali kubwa ya fedha kutokana na mafanikio katika maonyesho hayo. Kufuatia usoefu uliopatikana kwenye maonyesho ya Rostock, Ujerumani, nchi yetu ina nafasi kubwa ya kupanua soko la mazao ya mbogamboga, maua na matunda katika soko la Jumuiya ya Ulaya. Kwa hivi sasa uzalishaji wa mazao hayo kwa ajili ya soko la Ulaya bado ni mdogo. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kuwezesha wawekezaji katika sekta hii kuongeza uzalishaji na hatimaye kuweza kuzalisha kiasi ambacho kitawezesha upatikanaji wa bidhaa hizo moja kwa moja katika masoko hayo kutoka kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro ambacho kwa sasa hakitumiki kikamilifu. Napenda kutoa pongezi sana kwa wazalishaji hawa na natoa wito kwa wazalishaji wengine waige mfano wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alivyoleza wakati akitoa hotuba ya Bajeti ya Wizara yake, katika msimu wa 2003/2004, kulikuwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame uliokuwepo sehemu nyngi za nchi. Upungufu huo ulisababisha kuongezeka kwa bei kwa mazao makuu ya chakula kama vile mahindi, mchele na maharage. Kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam, wastani wa bei ya jumla kwa gunia la mahindi lenye uzito wa kilo 100 uliongezeka hadi kufikia shilingi 20,500 mwezi Desemba, 2003 ikilinganishwa na bei ya shilingi 12,500 mwezi Desemba, 2002. Ongezeko hilo ni la asilimia 64. Katika kipindi hicho wastani wa bei ya mchele katika Jijini Dar es Salaam uliongezeka kwa asilimia 17.7 hadi kufikia shilingi 46,330 kwa gunia la kilo 100. Wakati huo huo katika jiji la Mwanza, wastani wa bei ya mahindi uliongezeka kutoka shilingi 13,250 hadi kufikia shilingi 20,500, sawa na ongezeko la asilimia 54.7. Aidha, wastani wa bei ya mchele kwa gunia lenye uzito wa kilo 100 katika jiji hilo uliongezeka kutoka shilingi 24,500 hadi kufikia shilingi 45,000, ikiwa ni ongezeko la asilimia 83.67.

Mheshimiwa Spika, bei ya mazao ya chakula hadi kufika Juni, 2004 inaashiria kuwepo kwa chakula kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano, katika Jiji la Dar es

Salaam wastani wa bei ya jumla ya mahindi imeshuka kutoka shilingi 20,500/= kwa kilo 100 hadi shilingi 12,500/= katika kipindi cha Desemba, 2003 na Juni, 2004 sawia. Vivyo hivyo bei ya jumla ya mahindi katika Jiji Mwanza imeshuka kutoka shilingi 20,500 kwa kilo 100 hadi shilingi 13,500/= katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ununuzi na uuzaji wa mazao makuu ya chakula uliendelea kukabiliwa na tatizo la uduni wa miundo mbinu ya masoko hususan barabara za vijijini, magulio au vituo vya kuuzia na kununulia na upungufu wa vinu au viwanda vidogo vya kusindika mazao hayo. Hali hii imesababisha kuwepo kwa gharama kubwa za kununua na kuuza mazao na pia sehemu kubwa ya mazao kuharibika kabla au baada ya kufikishwa sokoni. Aidha, wafanyabiashara wadogo wa mazao ya chakula wameendelea kukabiliwa na ukosefu wa mitaji ya kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo na mazao yake, hususan nyama, maziwa, ngozi na mayai, hutegemea kwa kiwango kikubwa soko la ndani kutokana na mifugo hiyo na mazao yake kutokidhi viwango vya soko la kimataifa. Kutokana na kuwepo kwa magonjwa ya mifugo katika ukanda wetu usafirishaji na uuzaji wa mifugo na bidhaa zake katika masoko ya Kimataifa umezuiwa. Hata hivyo, wafugaji hawa wanaweza kunufaika zaidi na soko la ndani ambalo linazidi kukua kila siku endapo juhudhi za makusudi zitafanyika katika kuendeleza miundombinu ya masoko ya mifugo na pia uhamasishaji wa matumizi ya bidhaa za mifugo zinazozalishwa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe uliongezeka kutoka tani 341,500 msimu wa 2002/2003 hadi kufikia tani 348,800 msimu wa 2003/2004 ikiwa ni ongezeko la asilimia 2. Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 980.5 na kufikia lita bilioni 1.18. Aidha, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai milioni 790 na kufikia milioni 910 sawa ni ongezeko la asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo kutoka kwa wakulima msimu wa 2003/2004, uliongezeka kwa asilimia 38.8 ikilinganishwa na idadi ya ngozi zilizonunuliwa msimu wa 2002/2003. Mauzo ya ngozi nje ya nchi katika kipindi hicho yaliongezeka kwa asilimia 56. Mauzo hayo yaliliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 5.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.6 zilizopatikana msimu wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara yangu ilipanga kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyolenga kuimarisha na kuendeleza huduma muhimu za ushirika na maendeleo ya masoko. Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa kiasi kikubwa. Pamoja na mafanikio katika shughuli za kawaida za kila siku za kiofisi, kiutawala na zinazohusu masilahi ya watumishi, mafanikio makubwa ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la sera, sheria na mipango, Wizara ilifanya kazi zifuatazo: Kuandaa Sheria ya Vyama vya Ushirika 2003, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ilikamilisha zoezi la kufanya mapitio ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1991 na kuandaa Muswada wa Sheria mpya ya Ushirika. Muswada huo

ulipitishwa na Bunge mwezi Novemba, 2003 na mwezi Januari, 2004, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliidhinisha uwe Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003. Wizara imekamilsha uandaaji wa Kanuni za Sheria hiyo na hivyo itanza kutumika rasmi hivi karibuni.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Wizara imekamilisha maandalizi ya kukipandisha hadhi Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*The Moshi University College of Cooperative and Business Studies - MUCCOBS*). Kwa sasa taratibu zinafanywa za kuwasilisha taarifa hii Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

Maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Policy*), yamefikia hatua ya kuridhisha. Kwa kushirikiana na mshauri mwelekezi, Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (*Economic and Social Research Foundation - ESRF*), maandalizi yalianza kwa kupata maoni ya wadau mbalimbali ambapo warsha za wadau katika kanda saba zimefanyika na taarifa kuhusu hali ya Masoko ya mazao hayo imeandaliwa. Inatarajiwa kuwa rasimu ya Sera hiyo itakamilika na kuwasilishwa mwezi Septemba, 2004.

Wizara imefanya mapitio ya Sheria Na. 15 ya mwaka 1982 ya Shirika la Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) na kubaini kuwa sheria hiyo inahitaji kufanyiwa marekebisho. Kwa sababu hiyo hatua za kurekebisha sheria hiyo zimeanza kuchukuliwa. Tayari rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri imeandaliwa. Rasimu hiyo ipo katika hatua ya kujadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu.

Maandalizi ya sheria ya kusimamia Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala (*Commodity Warehouse Receipt System*) yameendelea vizuri. Waraka wa kuelezea mfumo unavyofanya kazi na faida zake uliandaliwa na tayari umejadiliwa na kukubaliwa na Baraza la Mawaziri. Hatua inayofuata ya kutunga sheria itakayowezesha utekelezaji wa mfumo huu imeanza kutekelezwa. Sheria hiyo inatarajiwa kuwasilishwa Bungeni katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Kuandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula na Maji na Mifugo katika kukamilisha maandalizi ya Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*). Halmashauri zimewezeshwa kutumia mwongozo ulioandaliwa na kuandaa miradi ya Kilimo, Mifugo na Ushirika. Katika ushirika zilitengwa Shs.288,000,000/= kwa Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*).

Mheshimiwa Spika, katika masula yanayohusu maendeleo ya ushirika yafuatayo yametekelozwa:-

Kuratibu Uanzishaji wa Benki ya Ushirika ya Kitaifa. Wizara imeendelea kuratibu zoezi la uanzishaji wa Benki ya Ushirika ya Kitaifa. Kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*TFC*) ameteuliwa Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya *Ernst and Young* kufanya upembuzi yakinifu kuhusu uanzishaji wa Benki

hiyo. Kazi hiyo imeanza mwezi Julai, 2004. Upembuzi huo unatarajia kubaini umuhimu wa kuwepo kwa Benki hiyo, muundo wake na utaratibu wa kuianzisha na namna itakavyoendeshwa.

Kudhamini Vyama vya Ushirika kupata mikopo. Chini ya utaratibu wa dhamana kwa mauzo ya nje (*Export Credit Guarantee Scheme*) Wizara iliendelea kuviwezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo kutoka Benki kwa ajili ya kununulia mazao. Katika msimu wa 2003/2004, Serikali ilitenga shilingi bilioni 8.0 kwa ajili ya utaratibu huu. Aidha, Benki ya *CRDB* ilitenga jumla ya shilingi bilioni 18.7 na iliidhinisha mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 13.7 kwa Vyama Vikuu vya Ushirika na shilingi bilioni 2.2 kwa vyama vya msingi vitano katika Wilaya ya Mbinga. Wizara imefuatilia matumizi ya mikopo hiyo na kuhakiki kuwa ilitumika ipasavyo na urejeshaji wake ni wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2004 shilingi bilioni 8.1 kati ya shilingi bilioni 9.6 zilizotolewa na Benki zilikuwa zimerejeshwa, sawa na asilimia 84. Aidha, Wizara imewezesha kupatikana kwa dhamana ya mkopo wa shilingi bilioni 1.48 kwa ajili kununua maua ya pareto ambayo yalikuwa mikononi mwa wakulima na hivyo kunusuru kuharibika kwa maua hayo. Hadi hivi sasa wakulima wamelpwa shilingi milioni 200.0 na hivyo kuondoa kero ya madeni ambayo kiwanda cha kuzidua pareto kilikuwa kinadaiwa.

Kuhamasisha uanzishaji Vyama vya Ushirika. Uhamasishaji wananchi kuunda Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali umeendelea vizuri. Jumla ya Vyama 559 vimeanzishwa ambapo 273 (sawa na asilimia 48.8) ni Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*). Vyama vingine ni Vyama vya Mazao 197, Umwagiliaji 3, Mifugo 32, Viwanda 30 na vinginevyo 24.

Kuandaa Programu Kamambe ya Mageuzi ya Ushirika nchini (*Cooperative Reform and Modernisation Programme*). Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imekamilisha rasimu ya Programu hii. Malengo ya Programu hii ni pamoja na:-

- Kuhimiza na kuwezesha uibuaji wa mfumo wa Ushirika ambao msingi wake ni Vyama vya Ushirika vya Msingi, vinavyoendeshwa na kuwajibika kwa wanachama;
- Kuainisha kazi maalum za ngazi mbalimbali za Vyama vya Ushirika;
- Kusisitiza kuwepo kwa Viongozi wa Ushirika wanaowajibika kwa Wanachama na ambao ni wabunifu kibiashara;
- Kujasirisha Wanachama kwa kuwawezesha kupata elimu na stadi zinazohitajika ili waendeleze Vyama vyao;
- Kuhimiza na kuhamasisha uanzishaji/uendelezaji wa Vyama vya Ushirika vyenye nguvu za kiuchumi na endelevu na vinavyotumia mifumo ya kisasa ya biashara na menejimenti;

- Kuhamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali katika sekta mbalimbali za kiuchumi;
- Kuhimiza na kuwezesha mabadiliko katika mfumo wa Vyama vya Akiba na Mikopo na Benki za Ushirika ili vyombo hivyo viweze kuwahudumia wanachama kikamilifu;
- Kuimarisha uwezo wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika, Taasisi na Asasi mbalimbali zinazohusika na maendeleo ya ushirika nchini; na
- Kuunganisha vyama vya mazao ya kilimo na Makapuni ya Kimataifa ya ununuzi.

Utekelezaji wa Programu Kamambe ya Mageuzi ya ushirika nchini utahusisha Wizara, Chuo cha Ushirika, *COASCO, SCCULT, TFC* na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Wadau wa nje ni pamoja na Shirika la kazi Duniani (*International Labour Organisation - ILO*), ambalo litakuwa Kiongozi wa jukumu hili, Shirikisho la Vyama vya Ushirika Ulimwenguni (*International Cooperative Alliance - ICA*) na *DID Canada*. Tayari mazungumzo yamefanyika kati ya Wizara na *ILO* kuitisha mkutano wa wahisani (*Donors Conference*) kuwezesha utekelezaji wa programu hiyo.

Utekelezaji wa programu hiyo ni muhimu sana ili kuwezesha Vyama vya Ushirika kutoa mchango wake stahili sio tu kwa ajili ya kumwezesha mwanachama mmoja mmoja kiuchumi na kijamii, lakini pia kuvwezesha Vyama vya Ushirika kuchangia kikamilifu katika harakati za taifa za kupunguza umaskini mionganoni mwa jamii za Tanzania.

Kutoa Elimu ya Ushirika Shirikishi. Kwa kushirikiana na Chuo cha Ushirika Moshi, Wizara imetoa elimu shirikishi kwa waraghbishi 345 kutoka wilaya mbalimbali. Waraghbishi hao wataendelea kuendesha mafunzo ya elimu ya ushirika shirikishi kwa wanaushirika katika maeneo yao. Mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya kitaifa ya Ujasirishaji wa wanachama (*Member Empowerment in Management of Cooperatives - MEMCOOP*).

Kuimarisha Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Shughuli za Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika zimeendelea kuimarishwa. Shirika la *COASCO* liliwezeshe wa kuapeleka watumishi 44 kwenye mafunzo ya muda mfupi na kununua vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na magari mawili na kompyuta tano. Aidha, kufuatia uwezeshaji huo shirika limefanikiwa kukagua hesabu za vyama 3,023 kati ya vyama 3,530 vilivyotarajiwa sawa na asilimia 85.6.

Wizara imeendelea kuwawezesha maafisa ushirika katika Halmashauri za Wilaya ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kwa kutumia mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi, Wizara ilipeleka fedha shilingi 95,510,780/= kwa ajili hiyo. Fedha hizo zinatumika kwa kazi za uhamasishaji wa vyama, ukaguzi wa mara kwa mara na ukusanyaji wa taarifa zinazohusu vyama na usambazaji wake kwa wahusika. Aidha, ili

kurahisisha usafiri wa maafisa ushirika Wizara imenunua na pikipiki 29 kwa ajili ya kuzisambaza kwenye wilaya mbalimbali. Hivyo, idadi ya pikipiki zilizonunuliwa kwa ajili hiyo kutoka mwaka 2002/2003 imefika 46.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kuhusiana na maendeleo ya Ushirika, pamoja na uwekaji wa mazingira muafaka ya kisera na kisheria, Wizara imeendelea kuziimarisha taasisi zifuatazo ambazo ndio mihimili mikuu ya Serikali katika juhudzi za kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini. Taasisi hizo kwa upande wa Serikali ni Idara ya Maendeleo ya Ushirika na Ofisi za ushirika zilizoko Mikoani na Wilayani, Chuo cha Ushirika Moshi na *COASCO*, aidha, kwa upande wa Vyama vya Ushirika ni *TFC* na *SCCULT*. Wizara itaendelea kuziimarisha taasisi hizo muhimu katika Programu Kamambe ya Mageuzi ya Ushirika nchini inayotarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka huu wa 2004/2005. Aidha, kupitia Programu hiyo majukumu na uhusiano kati ya taasisi hizo utawekwa bayana ili kuongeza ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha masoko ya ndani na nje ya mazao na bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, Wizara ilifanya yafuatayo:-

Kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za Masoko. Wizara inaendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za Masoko kwa lengo la kuwasaidia wazalishaji wafanyabiashara na walaji kufanya maamuzi muafaka. Taarifa hizo zinazohusu mazao makuu ya chakula na mifugo, zimekuwa zikisambazwa kupitia Redio, Magazeti, Majarida na mawasiliano ya moja kwa moja kupitia barua. Ili kuimarisha ukusanyaji wa taarifa na takwimu maafisa 75 walipatiwa mafunzo na vitendea kazi. Aidha, kwa kupitia mradi wa Kuendeleza Mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing System Development Programme - AMSDP*) pikipiki 20 zilinunuliwa na kugawiwa kwa wakusanyaji takwimu katika miji mikuu ya mikoa ya Tanzania Bara. Vilevile, kompyuta 27 zimenunuliwa kwa ajili ya kukidhi na kuchambua takwimu za masoko. Vifaa hivi vitasambazwa kwa wakusanyaji wa taarifa na takwimu za masoko.

Kuimarisha soko la ndani la mazao na bidhaa za kilimo. Wizara inakamilisha taratibu za kufanya Kongamano maalum la Kitaifa la kuimarisha soko la ndani. Lengo la kongamano hilo ni kuandaa mikakati ya kuhamasisha Watanzania kujenga tabia ya kupenda kununua na kutumia mazao na bidhaa za kilimo zinazozalishwa hapa nchini. Aidha, kongamano hilo litasaidia kuwatayarisha watanzania kushiriki kikamilifu katika makubaliano mbalimbali ya kibashara (*Regional and International Trade Agreements*). Kongamano litashirikisha wakulima, wasindikaji, wafanyabiashara, wasafirishaji, walaji, wanataaluma na wadau wengine. Katika kutumia fursa za soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambalo hapo baadaye litakuwa soko moja (*Common Market*), Wizara imeandaa na kufanya warsha ya kuhamasisha Watanzania kushiriki kikamilifu katika soko hilo, hususan kati ya Tanzania na Uganda. Hii ni kwa sababu, kuanzia mwezi Januari, 2005 bidhaa za Tanzania na Uganda hazitatozwa ushuru bali zile ziingizwazo kutoka Kenya. Fursa hii itawezesha Tanzania na Uganda kuiandaa na kujiimarisha kabla ya bidhaa zitakazotoka Kenya kuingia Tanzania na Uganda bila ushuru. Warsha ilifanyika mjini Mwanza mwezi Julai, 2004 na ilishirikisha wadau mbalimbali kutoka

sekte ya umma na sekte binafsi. Katika mada zilizotolewa, Wizara iliainisha bidhaa ambazo zina fursa kubwa kuingia katika soko la nchi ya Uganda, nazo ni mazao ya vanilla, kahawa, nyuzi za pamba, chai, mchele na samaki.

Kushiriki katika shughuli za Jumuiya Afrika ya Mashiriki na *SADC*. Wizara, imeshiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan katika kuandaa sera na mkakati wa Kilimo na Maendeleo Vijijini (*Agricultural and Rural Development Policy and Strategy*) na kukamilisha Itifaki ya Ushuru wa Forodha wa Jumuiya (*The EAC Customs Union Protocol*). Itifaki hiyo iliwekwa saini na Marais wa nchi za Jumuiya tarehe 2 Machi, 2004. Aidha, Wizara ilishiriki kikamilifu katika maandalizi ya Mkakati wa Kuhakikisha Usalama wa Chakula katika nchi za *SADC* ulioidhinishwa tarehe 15 Machi, 2004, Jijini Dar es Salaam na Wakuu wa nchi hizo Chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, Wizara iliendelea kutekeleza masuala yafuatayo yanayohusu maendeleo ya watumishi na uboreshaji mazingira ya kazi:-

Wizara imeendelea na mpango wake wa kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake, ambapo jumla ya watumishi 57 wa Wizara walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali hapa nchini na nchi za nje. Aidha, watumishi wawili walipata nafasi ya kusoma shahada ya uzamili. Maafisa ushirika 132 wa Mikoa na Halmashauri walidhaminiwa na Wizara kwa mafunzo mbalimbali Chuo cha Ushirika Moshi. Sambamba na utoaji mafunzo zoezi la upandishwaji vyeo iliendelea ambapo watumishi 129 Walipandishwa vyeo. Ili kuziba nafasi zilizo wazi Wizara iliomba na kupatiwa kibali cha ajira mpya 10.

Kukamilisha Ujenzi wa Jengo jipya la Wizara, Dodoma. Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo jipya ambayo ni sehemu ya upanuzi wa majengo ya Wizara la ghorofa mbili lenye sehemu ya ukumbi wa mikutano, sehemu ya maonyesho yahusuyo masoko, maktaba na ofisi za watumishi. Kukamilika kwa jengo hilo lilogharimu takriban shilingi milioni 280, kunatoa fursa kwa Wizara kutekeleza mikakati yake ya kuhamasisha upatikanaji wa masoko kwa njia ya maonyesho na mfumo wa upashanaji habari za masoko (*Marketing Information System*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ifuatayo:-

(i) Mradi wa Kuendeleza na Kuboresha biashara na masoko ya mazao ya Pamba na Kahawa. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Mazao (*Common Fund for Commodities - CFC*), unaojihusisha, pamoja na mambo mengine na kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye maghala (*Commodity Warehouse Receipt System*) kama dhamana ya kupata mikopo. Katika mpango wa majaribio mfumo huu umeonyesha mafanikio katika Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo Vyama vya Ushirika vya Msingi 27 na Wilaya ya Mbinga ambapo Vyama vya Ushirika vya Msingi 50 vilinufaika. Benki zilizoshiriki ni *CRDB, EXIM* na *KCB*.

(ii) Mradi wa Uendelezaji wa Miundo Mbinu ya Masoko Vijiji. Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa unatekelezwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) katika Wilaya za Kongwa, Morogoro na Mvomero. Pamoja na mambo mengine, mradi huu unajenga miundombinu ya masoko likiwemo Soko la Kimataifa la Mahindi katika Mji Mdogo wa Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa. Ujenzi wa soko hilo unahusisha pia ujenzi wa barabara yenyе urefu wa mita 800 (0.8 km) kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Soko hilo na barabara kuu ya Dodoma - Morogoro. Masoko mengine yanayojengwa ni pamoja ya masoko ya matunda katika Vijiji vya Tawa na Kinole katika Wilaya Morogoro na soko la matunda na mbogamboga linalojengwa huko Nyandira katika Wilaya Mvomero. Aidha, barabara zenyе urefu wa kilomita 39.2 zimeimarishwa, madaraja makubwa mawili yanajengwa ili kuimarisha usafirishaji wa biashara ya mazao. Mradi pia unaimarisha miundo mbinu ya umwagiliaji na upatikanaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani. Katika Wilaya zote tatu vituo vya mafunzo kwa wakulima na wafanyabiashara vinajengwa. Utekelezaji wa mradi ni zaidi ya asilimia 75 na ifikapo Desemba, 2004, ujenzi wa miundo mbinu yote chini ya mradi huu utakuwa umekalimika. (*Makofî*)

(iii) Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme*). Programu hii inatekelezwa kwa muda wa miaka 7 na utekelezaji huo unafanyika katika mikoa 8 na jumla ya wilaya 36 zilizopo katika Kanda za Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Utekelezaji wa Programu hii umejielekeza zaidi katika maeneo yafuatayo:

Kusaidia uandaaji wa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo: Maandalizi ya Sera ya Mazao ya kilimo yamefikia hatua nzuri na ifikapo Septemba 2004, rasimu ya Sera hiyo itakuwa imekamilika.

Kujasirisha Wakulima na Wafanyabiashara wa Mazao na Bidhaa za Kilimo na Kuwaunganisha na Masoko: Katika mwaka wa 2003/2004, Wilaya nane za awali zilitewa ili kuanza ujasirishaji wa wakulima na wafanyabiashara. Idadi ya Wilaya hizo itaongezeka na kufikia 20 katika mwaka wa 2004/2005. Utekelezaji wa sehemu hii ya programu unafanywa kwa kushirikiana taasisi zisizo za kiserikali kama vile FAIDA Mali, *Techno Serve, Di Stefano na Farm Africa*. Kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa kutumia programu hii, Wizara imewapatia mafunzo na vitendea kazi wakusanyaji taarifa na takwimu 75.

Ili kusaidia jitihada za Serikali za kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, programu itaendelea na zoezi la uhamasishaji wa matumizi ya Mfumo wa kutumia Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo. Ili kufanikisha uhamasishaji huo Programu imetenga fedha kwa ajili ya mikopo ya kuwezesha ukusanyaji wa mazao ya awali katika mfumo huu.

Uimarishaji wa Miundombinu ya Masoko. Utekelezaji wa sehemu hii ya Programu imezinduliwa rasmi mwezi Mei, 2004 baada ya taratibu za upatikanaji wa fedha kutoka *ADB*. Hadi kukamilika kwa sehemu hii ya programu, inatarajiwa kwamba,

barabara za vijiji (*Feeder Roads*) zenye jumla ya urefu wa kilometra 1,136 zitafanyiwa tathmini na kuimarishwa, madaraja 115 na makalvati 575 yatajengwa au kukarabatiwa na masoko na magilio yapatayo 60 yatajengwa na/au kuimarishwa. (*Makofi*)

Ili kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo inadumu na kuendelea kutoa huduma zinazotarajiwa, mafunzo kwa wahandisi katika ngazi za Mikoa na Wilaya yatasolewa. Aidha, mafunzo yatasolewa pia kwa Madiwani na wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kukarabati miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Ushirika na Masoko ilitengewa jumla ya shilingi 7,521,863,797/= kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,126,116,797/= ziliwu za Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengene) na shilingi 395,747,000/= ziliwu za Matumizi ya Maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2004 jumla ya shilingi 7,126,116,797/= fedha za Matumizi ya Kawaida ziliwu zimetolewa na kiasi cha shilingi 7,035,679,294.26/= zimetumika, sawa na asilimia 98.73 ya fedha zilizoidhinishwa. Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo jumla ya shilingi 2,325,848,938/= zimetumika. Kati ya fedha hizi shilingi 142,325,000 ni fedha za ndani na shilingi 2,207,523,938/= ni fedha za nje. Matumizi ya fedha za nje ni makubwa zaidi ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti kutoana na Serikali ya Ufaransa kuidhinisha fedha za ziada kwa mwaka wa 2003/2004, kwa ajili ujenzi ya miundombinu ya masoko katika Wilaya za Kongwa, Morogoro na Mvomero.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Wizara itaendelea na juhudhi za kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika na Masoko kwa kuzingatia mabadiliko ya sera za kijumla za uchumi pamoja sera na sheria za sekta. Aidha, Mpango huu wa kazi umeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Bajeti ya Serikali (*Medium Term Expenditure Framework - MTEF*) kwa kipindi cha 2004/2005 - 2006/2007, uliotolewa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafisishaji na Wizara ya Fedha. Kazi zilizopangwa kutelezwa zimeainishwa katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, kwenye eneo la Sera, Sheria na Mipango, Wizara itafanya kazi zifuatazo:-

- Kusambaza na kueneza Sera mpya ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka wa 2002 na Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika ya mwaka wa 2003;
- Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Policy*), ikiwa ni pamoja na kuandaa Mkakati wa kutekeleza Sera hiyo. Sera hiyo ni mwongozo utakaosaidia katika upanuzi wa soko la mazao ndani (ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika) na nje ya nchi;

- Kuratibu utekelezaji wa Programu Kamambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini, ambayo itakuwa mhimili wa utekelezaji wa Sera mpya ya Maendeleo ya Ushirika na Sheria ya Vyama Vya Ushirika;
- Kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria ya kusimamia Mfumo wa Matumizi ya Stakabadhi ya Mazao kwenye Maghala (*Commodity Warehouse Receipt System*);
- Kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme*) kwa kuainisha miradi ya maendeleo, hususan Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo katika Wilaya (*District Agricultural Development Plans*); na
- Kuandaa taarifa ya Utekelezaji ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 - 2005 kuhusu maendeleo ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini inafanikiwa, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuratibu maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika ya Taifa mapema iwezekanavyo;
- Kuendelea kuvikutanisha Vyama vya Ushirika na Benki za Biashara kwa lengo la kuviwezesha kupata mikopo kwa ajili ya kuendeshea shughuli muhimu, hususan ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wakulima. Pia kuimarisha mitaji ya ndani ya Vyama vya Ushirika kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wanachama kuongeza hisa na kuanzisha na kuimarisha SACCOS;
- Kwa kushirikiana na wadau wengine Wizara itaendelea kuhamasisha Wananchi kwa kasi zaidi katika kuanzisha Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Lengo ikiwa ni kuhamasisha jamii kuhusu Ushirika kama chombo cha kumkomboa mkulima na mfanyabiashara mwenye kipato kidogo kutokana na umaskini;
- Kwa kutumia Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) kuendelea kutekeleza programu ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na kuhakikisha kuwa taarifa za ukaguzi zinasomwa kwa wanachama wote na kwa wakati unaofaa;
- Kushirikiana na Chuo cha Ushirika Moshi kuratibu utekelezaji wa Programu ya Ujasirishaji wanachama (*Member Empowerment in Cooperatives*) na kutoa elimu ya Ushirika shirkishi kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuwajasirisha ili wamiliki na kuviendesha vyama vyao. Aidha, Chuo cha Ushirika Moshi kitaanzisha Kituo cha Ujasiriamali Vijijini katika Bara la Afrika (*Centre for Rural Entrepreneurship in Africa*). Ili kupata uzoefu zaidi, Viongozi wa Wizara na Chuo cha Ushirika Moshi pamoja na maofisa wengine watatembelea Chuo Kikuu cha Earth nchini Costa Rica, Amerika ya Kusini, ambacho kimefanikiwa sana katika eneo la ujasiriamali;

- Kuendelea kutoa miongozo ya uendeshaji ili kusaidia kuboresha utendaji wa Vyama vya Ushirika, hususan Vyama vya Msingi;
- Kuendelea kuwawezesha Maafisa Ushirika Wilayani kutekeleza kazi zao ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo na vitendea kazi kama vile pikipiki na kompyuta.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza soko la ndani na nje ya nchi kwa mazao ya kilimo, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya masoko ambayo inategemea mahusiano na utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za masoko. Mafanikio ya mifumo bora ya masoko yanategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa miundombinu bora ya masoko, kupatikana kwa mitaji na mikopo, kuwepo kwa stadi za biashara na mahusiano kati ya wadau ambayo yanaongozwa na taarifa sahihi za masoko. Kwa sababu hiyo Wizara itayapa kipaumbele mambo yafuatayo katika kukuza soko la mazao ndani na nje ya nchi:-

- Kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao kwa walengwa (*Market Intelligence*). Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya vyombo vya habari vinavyotangaza taarifa za masoko ya mazao, kuongeza wigo wa mazao yatakayotangazwa na kuanzisha tovuti ya Wizara ambayo itaunganisha taarifa hizo na wadau wa masoko ndani na nje ya nchi;
- Kuandaa kitabu cha orodha ya Wanunuvi na Wasindikaji wa Mazao (*Agribusiness Directory*) na kuisambaza kwa wadau;
- Kufanya mapitio ya mahitaji ya taarifa za masoko kwa wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba taarifa zitolewazo zinakidhi mahitaji ya watumiaji;
- Kutoa mafunzo ya jinsi ya kutumia taarifa mbalimbali za masoko kwa vikundi vya wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara wa kati ili waweze kuzalisha na kuza kwa kufuata mahitaji ya soko;
- Kuwezesha Hal mashauri za Miji na Wilaya kuwa na vitendea kazi vya kukusanya, kuchambua na kutunza taarifa za masoko katika maeneo yao;
- Kutoa elimu ya kanuni na taratibu za masoko na biashara na nchi za nje hususan nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na nchi nyingine ambazo zimetoa mfumo wa upendeleo kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zinazoendeleo.
- Kushiriki katika majadiliano na maandalizi ya Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za kukuza biashara ya mazao katika nchi za Jumuiya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Jumuiya ya Ulaya na nchi nyingine duniani;
- Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za masoko kwa kushirikiana na washauri waelekezi kutoka Taasisi za utafiti ndani na nje ya nchi zikiwa ni pamoja na Vyuo Vikuu,

asasi nyingine za utafiti, kama vile *International Food Policy Research Institute (IFPRI)* na *DECILION*. Lengo ni kuainisha vyanzo vya matatizo mbalimbali ya masoko na kutoa mapendekezo ya kuyaondoa au kuyapunguza;

- Kuendelea kuhamasisha wazalishaji na wanunuzi wa mazao kutangaza bidhaa zao kupitia njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa;
- Kuandaa mikakati ya kuendeleza soko la ndani;
- Kushirikiana na Vikundi na Taasisi zisizo za Kiserikali (*NGOs, CBOs* na Makampuni) zinazojishughulisha na biashara ya mazao ya kilimo kwa lengo la kuviunganisha vikundi hivyo na masoko maalumu; na
- Kuratibu na kufanya tathmini ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko; na
- Kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Masoko ili iwe na uwezo wa kufanya shughuli zilizoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara itaendelea kuratibu, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ifuatayo:

(i) Mradi wa Kuendeleza na Kuboresha Biashara ya Pamba na Kahawa (*Coffee/Cotton Marketing Development and Trade Promotion Project*). Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko Maalum wa Mazao (*Common Fund for Commodities*) pamoja fedha za hapa. Katika mwaka wa 2004/2005, kazi zifuatazo zitatekelezwa chini ya mradi huu:-

Kukamilisha taratibu za kisheria, uhamasishaji na kutoa mafunzo kwa wadau ili kuwezesha matumizi ya Stakabadhi za Mazao yaliyopo ghalani kama dhamana ya mikopo kutoka katika vyombo vya fedha. Kuendeleza juhudzi za kuimarisha ubora wa mazao ya kahawa na pamba.

(ii) Mradi wa kuendeleza Masoko ya Mazao ya Kilimo katika Wilaya za Kongwa na Morogoro Vijijini. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2003 katika Wilaya za Kongwa na Morogoro Vijijini kwa msaada kutoka Serikali ya Ufaransa na kuratibiwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania - MVIWATA. Katika mwaka wa 2004/2005, kazi zifuatazo zimepangwa kufanyika:

- Kukamilisha ujenzi na kukabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa soko la mahindi la kimataifa katika Mji Mdogo wa Kibaigwa;
- Kukamilisha ujenzi wa magilio ya mazao katika vijiji vya Tandai, Tawa na Nyandira katika Wilaya ya Morogoro Vijijini na Mvomero na kukabidhi masoko hayo kwa Halmashauri husika;

- Kukamilisha ukarabati wa barabara zinazounganisha vijiji vya Kinole, Tandai, Tawa, Nyandira;
- Kukamilisha ujenzi wa Vituo cha mafunzo ya Vikundi vya Wakulima katika mji mdogo wa Kibaigwa, vijiji vya Tawa, na Kinole;
- Kuweka Utaratibu wa Kusimamia na Kuendesha masoko yatakayokamilishwa; na
- Kufuatilia na kufanya tathmini ya matumizi ya miundombinu ya masoko katika Wilaya hizo kwa lengo la kupata usoefu ili kuiwezesha Serikali kujenga vituo vya masoko (*Commodity Exchange Centres*) vya kanda vitakavyotumika kama minada mikuu ya mazao.

(iii) Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme - AMSDP*). Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia programu hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wengine katika maeneo yafuatayo:-

- Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao.
- Kupitia na kuboresha Sheria, Kanuni na Taratibu za ununuzi wa mazao ili zikidhi mahitaji mbalimbali ya mfumo wa soko uliopo hivi sasa;
- Kuboresha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko kwa kuongeza wigo wa taarifa hizo;
- Kuvijengea uwezo vikundi vya uzalishaji, usindikaji na vya wafanyabisha kwa lengo la kuvunganisha vikundi hivyo na masoko maalumu, na
- Kukamilisha maandalizi na kuanza uimarishaji wa miundombinu ya masoko katika wilaya 20.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watumishi wa ngazi zote yakiwemo ya taaluma ya yale ya kupiga vita rushwa sehemu za kazi. Jumla ya watumishi 130 wamepangwa kuhudhuria mafunzo hayo;
- Kuimarisha ufanisi wa utendaji wa taasisi zinazoshughulikia maendeleo ya ushirika kwa kutoa mafunzo kwa watendaji wake na kuboresha upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi;
- Kuendelea na upandishwaji vyeo na kuthibitisha kazini watumishi wa Wizara. Jumla ya watumishi 50 wa kada mbalimbali wanatarajiwu kupandishwa madaraja kulingana mfumo mpya wa utendaji kazi Serikalini unaozingatia matokeo ya kazi;

- Kushughulikia ajira za watumishi pamoja na kujaza nafasi zilizo wazi. Jumla ya watumishi 44 wataajiriwa;
- Kuimarisha utendaji kazi na upimaji wa malengo (*Performance Management System*) kulingana na maelekezo ya programu ya uimarishaji wa utumishi wa umma;
- Kushirkisha sekta binafsi katika utoaji huduma (*Private Sector Participataion*). Wizara imelenga kuingia Mkataba na Kampuni binafsi zitakazotoa huduma mbalimbali kwa kuanzia na huduma za uhudumu, usafi wa mazingira, ulinzi na mapokezi; na
- Kuimarisha kampeni ya kutoa elimu kwa wafanyakazi juu ya janga la UKIMWI. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imepanga kuendesha semina mbalimbali kwa wafanyakazi wake kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa huo na kutoa ushauri nasaha kwa waathirika ili waweze kuishi kwa matumaini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirika na Masoko imeendelea kushirikiana na Wizara za Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika na Viwanda, Biashara na Masoko za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibarkatika masuala yanayohusu ushirika na masoko. Wizara imeanza utaratibu wa kutoa nafasi katika Chuo cha Ushirika Moshi na kugharamia mafunzo kwa wanafunzi kutoka Zanzibar. Katika mwaka 2003/2004, maafisa ushirika watano walinufaika na ufadhili huo. Aidha, katika mwaka wa 2004/2005 maafisa ushirika watatu kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar watanufaika. Vilevile, katika mstakabali huo Wizara iliwawezesha Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushiriki katika maonesho ya kimataifa ya Mboga mboga Maua na Matunda yaliyofanyika mjini Ristock Ujerumani mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara yangu katika juhudzi za kuendeleza Ushirika na Masoko. Kwanza, napenda kuzishukuru nchi za Norway, Ufaransa, Kenya na Afrika ya Kusini. Vile vile napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zikiwemo Benki ya Dunia, *International Cooperative alliance, ILO, ICO, IFAD, ADB, CFC, UNCTAD* na *UNOPS*. Pamoja na shukrani hizo napenda kuwaomba waendelee kutusaidia kwani bado tunahitaji sana misaada yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Viongozi na Wanachama wa Vyama vya Ushirika nchini, Bodi za Mazao na vikundi vya uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali kwa kazi nzuri wanayofanya kwa pamoja katika kuimarisha na kuendeleza ushirika ili kufanikisha malengo yao. Vilevile, tunawashukuru wadau wote wengine wanaoshughulika na biashara ya mazao ya kilimo na mifugo na bidhaa nyingine ndani na nje ya nchi. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 11,403,061,500/=. Kati ya fedha hizo, shilingi

7,336,242,500/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 4,066,819,000/= ni kwa ajili ya shughuli za Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 169,300,000/= ni fedha za hapa na shilingi 3,897,579,000/= ni fedha za Kigeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, naafiki

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Watakaochangia tutakapoanza mchango wa jumla ni hawa wafuatao: Ambao hawajachangia hata mara moja wapo wawili, Mheshimiwa Hasnain Murji na Mheshimiwa Major Jesse Makundi. Halafu watafuatiwa na ambao wameishachangia mara moja tu ambao ni Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Jacob Shibili na Mheshimiwa Leonard Derefa, wajiandae. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Msemaji wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, atoe maoni ya Kamati. (*Makofî*)

MHE. DR. AARON D. CHIDUO (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 81(1), Toleo la mwaka 2004, kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 na kutoa ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti na Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Fungu 24, Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa masikitiko makubwa, nitumie nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole na rambirambi kwa mjane, familia na Wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Mbeya Vijijini, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Yeteh Sintemule Mwalyego. Aidha, natoa pole na rambirambi kwa mjane, familia na Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wao, ndugu yetu mpendwa, Marehemu Mheshimiwa Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu wote wawili mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara walikwisha tambulishwa tulipowasilisha Taarifa za Kamati kuhusu Wizara za Nishati na Madini na Viwanda na Biashara. Hivyo, sikusudii kurudia kuwatambulisha tena Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, ilipokuwa inajadili na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali ambao ilibidi Wizara kuutolea maelezo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri uliotolewa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

Kwanza, Wizara itoe elimu na kuhamasisha wadau ili washiriki kikamilifu katika mchakato wa kujenga Vyama vya Ushirika endelevu na shirkishi na vyenye kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Ushirika Moshi, iliendesha mafunzo ya majuma mawili kwa Maafisa Ushirika 256. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na *COASCO*, walishiriki kwenye Mkutano Mkuu wa Vyama Vikuu vya Ushirika vinane.

Pili, Wizara ikamilishe kazi ya uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika itakayotoa mikopo kwa masharti nafuu na kuviunganisha Vyama vya Ushirika na huduma za fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania, imeteua Kampuni ya *Ernest and Young* kufanya kazi ya upembuzi yakinifu wa kuanzisha Benki ya Ushirika ya Kitaifa, kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2004.

Tatu, Wizara ihamasishe Wananchi katika Mikoa yote ili waanzishe Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa kuzingatia mazingira yao na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, jumla ya Vyama vya Ushirika 292 vimeanzishwa kote nchini. Kati ya hivyo, *SACCOS* 218, Vyama vya Ushirika vya Umwagiliaji Maji Mashambani vitatu, Vyama vya Wavuvi 12, Vyama vya Wafugaji 17, Vyama vya Mazao 16, Viwanda vitatu na Vyama vya aina nyingine 23. Vilevile Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), liimarishwe ili liweze kuhudumia ipasavyo Vyama vya Ushirika pote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, *COASCO* ilipatiwa jumla ya Sh.526,852,300/= ili kuliwezesha Shirika kufanya kazi zake kwa ufanisi. Aidha, Shirika limeajiri watumishi wenye sifa wa kada mbalimbali na kujaza nafasi zilizokuwa wazi. Sheria iliyoanzisha *COASCO* (Sheria Na.15 ya mwaka 1988) ipitiwe upya ili muundo wake na majukumu yakidhi mahitaji ya ushirika wa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya *COASCO*. Wizara itekeleze azma yake ya kuanzisha Kituo cha Kuendeleza Masoko (*Market Development Centre*) ili kuweza kuwa kiungo muhimu cha *trade hubs* ambazo ziko katika mpango wa *AGOA*.

Kamati ilielezwa kuwa, kwa kuzingatia gharama kubwa za uanzishaji wa kituo hicho (kiasi cha Shilingi bilioni 7.4) ambapo kati ya hizo asilimia 90 zinatakiwa kuchangiwa na Wahisani, Wizara imeamua kuimarisha Idara ya Masoko badala ya kuanzisha Taasisi mpya na

Pia, Wizara iipatie Idara ya Ushirika Wataalam, fedha na nyenzo zinazokidhi mahitaji halisi ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, iliajiri na kuzipatia Halmashauri za Wilaya Wataalam mbalimbali wakiwemo Wataalam wa fedha. Aidha, jumla ya Sh.95,510,710/= zilipelekwa kwa Halmashauri za Wilaya katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhika na maelezo yaliyotolewa kuhusu utekelezaji wa ushauri wa Kamati kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha 2003/2004, Wizara iliweza kukusanya mapato ya kiasi cha Sh.6,820,000/=. Mapato hayo yalitokana na ada za zabuni na uandikishwaji wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirika na Masoko ilitengewa kiasi cha Sh.6,881,500,900/=. Aidha, matumizi halisi ya kawaida hadi kufikia tarehe 28 Mei, 2004 yalikuwa Sh.5,721,623,265/= sawa na asilimia 83.8 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara ilipata baadhi ya mafanikio yafuatayo: -

- Wizara iliandaa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003;
- Chuo cha Ushirika Moshi kimepandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Nawapongeza wote waliofanikisha hatua hiyo kufikiwa; (*Makofi*)
- Maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao yalifikia hatua ya kuridhisha;
- Wizara inachukua hatua za kurekebisha Sheria ya COASCO ya mwaka 1982;
- Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye maghala (*Commodity Warehouse Receipt System*) inaandaliwa;
- Wizara inaratibu uanzishaji wa Benki ya Ushirika ya Kitaifa;
- Hatua za kudhamini Vyama vya Ushirika ili kupata mikopo zinachukuliwa;
- Uhamasishaji uanzishaji wa Vyama vya Ushirika unaendelea;
- Mpango wa Mabadiliko ya Ushirika (*Cooperative Reform Programme*) unaandaliwa; na
- Ujenzi wa jengo jipya la Wizara Dodoma umekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Wizara ilikabiliwa na matatizo ya utekelezaji yafuatayo: -

- Upungufu wa vitendea kazi kwa Wakaguzi wa Vyama vya Ushirika, hususan katika Halmashauri za Wilaya na Sekretarieti za Mikoa;
- Kushuka kwa bei za mazao ya biashara katika soko la dunia kunakosababishwa na ziada za uzalishaji toka nchi nyingine na kupungua kwa ubora wa mazao yetu;
- Upungufu wa Wafanyakazi na Maafisa Ushirika katika Idara za Wizara, kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa;
- Baadhi ya Vyama vya Ushirika bado vinakabiliwa na Uongozi mbovu;
- Elimu ya Ushirika shirkishi bado haijawafikia Wanachama wengi ili waweze kuvitawala na kuviendesha Vyama kwa manufaa yao;
- Bado kuna hali duni ya miundombinu ya masoko (barabara za vijijini, magilio/masoko ya mazao na maghala) ambayo husababisha kuongezeka kwa gharama za kusafirisha na kuhifadhi mazao;
- Uduni wa vifaa vya mawasiliano unaodhoofisha usambazaji wa taarifa za masoko kwa wakati; na
- Bado kuna kasi ndogo ya uhamasishaji wa Wananchi kuanzisha na kijiunga na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, baadhi ya kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 ni kama ifuatavyo: -

- Kusambaza na kuelezea Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003;
- Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo;
- Kukamilisha maandalizi ya Kanuni za Vyama vya Ushirika;
- Kuratibu maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika ya Taifa-
- Kuendelea na maandalizi ya kutekeleza programu ya kurekebisha uendeshaji wa Vyama vya Ushirika;
- Kuendelea kuvikutanisha Vyama vya Ushirika na Benki za Biashara;

- Kuhamasisha Wananchi kuanzisha Vyama vya Ushirika kwa kasi zaidi katika Sekta mbalimbali;
- Kuwawezesha Maafisa Ushirika Wilayani kutekeleza kazi zao kwa ufanisi;
- Kuimarishe na kuendeleza Mfuko wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za ushirika na masoko; na
- Kuratibu na kufanya tathmini ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kuchambua kwa kina mpango na makadirio ya matumizi na mapato ya Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka 2004/2005, Kamati inapenda kutoa ushauri ufuatao ili kuboresha utekelezaji wa mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ilizochukua kuimarishe Idara za Ushirika kwenye Halmashauri za Wilaya katika mwaka wa fedha uliopita. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kusambaza pikipiki 27 kwa Maafisa Ushirika katika Halmashauri za Wilaya. Aidha, Wizara ilipeleka kiasi cha Sh.95,510,780/= ili kuwawezesha Maafisa Ushirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua zaidi ili kuimarishe Idara za Ushirika kwa kuzipatia Wataalam, fedha na nyenzo za kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi walio wengi bado hawajahamasishwa kuhusu umuhimu wa kuanzisha Vyama vya Ushirika. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhamasisha na kuwashimiza Wananchi kuanzisha Vyama vya Ushirika kulingana na mazingira na mahitaji yao. Aidha, elimu zaidi itolewe juu ya umuhimu wa kuanzisha Vyama vya Akiba na mikopo (*SACCOS*) katika ngazi ya Vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na juhudhi zinazofanywa na Wizara za kuanzisha Benki ya Ushirika ya Kitaifa (*National Cooperative Bank*). Benki hii siyo tu itakuwa inatoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika kwa masharti nafuu, bali pia itakuwa kiungo muhimu kati ya Vyama vya Ushirika na Taasisi nyingine za kifedha. Kamati inaishauri Wizara kubadilisha jina la Benki hiyo na kuwa Benki ya Maendeleo na Ushirika (*Cooperative and Development Bank*) ili kupanua wigo wa shughuli zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maeneo ya migodi ya machimbo ya madini yana nguvukazi kubwa ya vijana ambao hawajahamasishwa kuijunga katika vikundi vya ushirika. Hali hiyo inasababisha ongezeko la vitendo vya uhalifu kama ubakaji, wizi, uvutaji bangi, utumiaji wa dawa za kulevyaa na kadhalika. Hivyo, Kamati inashauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuhamasisha vijana hao kuanzisha vikundi vya ushirika wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa azma yake ya kukamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo na kuandaa mkakati wa utekelezaji wake. Sera hiyo itakapokamilika, itaiwezesha nchi yetu kunufaika na fursa mbalimbali za mauzo ya bidhaa nchi za nje kama vile *AGO4*, Jumuiya za Kikanda za Afrika ya Mashariki (*EAC*) na Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Kamati inashauri kuwa, Sera hiyo pia ikabiliane na ongezeko la wimbi la uuzaji wa bidhaa bandia (*Counterfeit Items*) kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kubuni Mradi wa Ujenzi wa Masoko ya Kimataifa ya Mazao katika Wilaya za Kongwa na Morogoro Vijijini. Kamati inaishauri Wizara kuanzisha miradi kama hiyo kwenye Mikoa na Wilaya nyingine nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea kwa furaha taarifa za mafanikio ya mradi huu kwa zao la pamba katika Wilaya ya Babati, Mkoani Manyara na Mikoa ya Mbeya, Kagera, Ruvuma na Kilimanjaro kwa zao la kahawa kwa kutumia Benki ya *CRDB* na *Kilimanjaro Cooperative Bank*. Kufuatia mafanikio ya mradi huu kwenye maeneo hayo, Kamati inaishauri Wizara kuusambaza mradi huo kwa Wananchi wanaolima mazao mengine ya biashara kama mkonge, korosho na kadhalika ili nao wanufaika na mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo wa ushirikiano na mawasiliano kwa Wizara ambazo masuala yake si ya Muungano kama vile masoko, maji, viwanda, elimu na kadhalika kwa faida ya pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kujadili mpango wa kazi za Wizara kwa kipindi cha 2004/2005, Wizara imepanga kutoa elimu kupitia warsha, semina na mafunzo ya kompyuta ili kuwahamasisha wakulima na wafanyabiashara wadogo jinsi ya kutumia taarifa mbalimbali za masoko ili kuendelea kuuza/kununua mazao kulingana na mahitaji ya soko. Pamoja na juhudhi hizo na kwa kuzingatia mazingira magumu ya shughuli zao, Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, kuunda chombo maalum ili kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kuanzisha Programu ya Kuendeleza Mfuko wa Masoko ya Mazao (*Agricultural Marketing System Development Programme*) uliojielekeza katika uimarishaji, ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko na kujasirisha wazalishaji. Kamati inashauri Serikali kuhamishia mradi huu Wizara ya Ushirika na Masoko ili kuwepo uwajibikaji wa karibu katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Balozi George Clement Kahama na Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa ushirikiano na kwa Kamati na uwasilishaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa ufahasa. Aidha, nawapongeza Watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dr. Ladislaus Komba, kwa ushirikiano na maandalizi mazuri ya bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William H. Shellukindo na Wajumbe wa Kamati, kwa ushirikiano wao na kwa kunipa heshima ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili nitoe ushauri wa Kamati. (*Makofi*)

Mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Kipenka M. Mussa na Katibu wa Kamati hii, Bwana Daniel Eliufoo, kwa kuihudumia Kamati hii ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo, Kamati imekubaliana na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko na kuyapitisha bila mabadiliko. Kiasi cha fedha kinachoombwa chini ya Fungu 24 ni Matumizi ya Kawaida Sh.7,336,242,500/=, Matumizi ya Maendeleo Sh.4,066,819,000/. Jumla ni Sh.11,403,061,500/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. AISHA P. MAGINA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5)(b) na (c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuungana na wenzangu kutoa rambirambi zetu za dhati kabisa kwa Wananchi na familia za Marehemu Mheshimiwa Yeti Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa msiba mkubwa wa kuondekewa na waliokuwa wapendwa Wabunge wao. Mwenyezi Mungu, awalaze Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara hii ni pamoja na kusimamia na kuratibu Vyama vya Ushirika na kutafuta na kusimamia masoko ya bidhaa zake ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na uchumi huria, lakini ni wazi kuwa bila ya kutoa motisha na msukumo maalum kwa Vyama vya Ushirika sio rahisi kwa Vyama hivyo kushindana na wafanyabiashara binafsi. Pahala popote ushirika uliposhika nguvu ni pale Serikali kwa makusudi zimekuwa zikitoa upendeleo maalum kwa Vyama hivyo, katika kuvipatia mikopo yenye masharti nafuu, pembejeo zenye bei nafuu na uhakika wa masoko mazuri ya bidhaa zao. Lakini pia Serikali hizo zimekuwa haziingilii Vyama kama ilivyotokea hapa kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii ya ushindani na kama kweli Serikali imekusudia kuendeleza ushirika, ni vyema Waziri akatueleza ni upendeleo gani unaotolewa na Serikali kwa Vyama vya Ushirika ili viweze kuingia katika mtandao wa soko huria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara inalo jukumu la kusimamia masoko ya bidhaa za Tanzania za mazao ya kilimo na bidhaa nyingine. Hivi sasa bidhaa zetu za mazao zinashindwa kuingia kwenye masoko ya nje kutokana na gharama kubwa za uzalishaji na zinazoongezwa na mamlaka za mazao. Kwa mfano, zao la korosho, wakulima wanalipa si chini ya asilimia 40 ya bei wanayouzia ni kodi tupu hivyo mkulima wa korosho ameendalea kuwa maskini na Wakuu wa Mamlaka ya Korosho wanazidi kunufaika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri aelezee ni hatua gani anazochukua za kuwapunguzia mzigo wa kodi wakulima na Vyama vya Ushirika ili viweze kuwanufaisha wazalishaji wao. Aidha, kwa nini pale ambapo Vyama vya Ushirika vina uwezo wa kusimamia shughuli zao, wabebeshwe mzigo wa kulea ukiritimba wa bodi za mazao?

Mheshimiwa Spika, Waziri ni vyema pia akatuelezea, je, jukumu la Wizara yake ni kusimamia masoko ya bidhaa za kilimo tu au na bidhaa nyingine kama madini? Aidha, ni vyema akatuelezea uhusiano wake na Bodi ya Biashara za Nje katika kuwasaidia Watanzania katika kupata masoko bora ya bidhaa zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, uchumi wowote duniani ambao hauna bidhaa za kuuza nje, hauwezi kuwa ni uchumi endelevu na sisi Tanzania bado uwezo wa kusafirisha bidhaa zetu nje ni mdogo mno, hivyo, ni vyema Serikali ituelezee ni mkakati gani ulioandaliwa wa kupanua masoko yetu ya ndani ya nchi jirani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ili kuvipa uhuru Vyama vya Ushirika, waziondolee mzigo wa kuziendesha Bodi za Mazao, mzigo huo ubebwe na Serikali Kuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ufuatiliaji wa miradi inayofadhiliwa na *JICA*, katika nchi za Tanzania na Malawi, kwa kipindi cha 2001/2002 inaonyesha kuwa kwa kipindi hicho jumla ya vyama vya msingi 4,566 vilikuwa vimesajiliwa hapa. Kati ya hivyo 2,590 vilikuwa ni maalum kwa ajili ya Mazao ya Kilimo, 887 vilikuwa ni vya kuweka na kukopa, 119 vilikuwa ni vya wafugaji, 81 ushirika wa wachimbaji madini na 624 vya wazalishaji wa viwandani.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa wametoa taarifa kuwa kati ya vyama hivyo 3,480 ndivyo vinavyofanya kazi na vingine vimeshindwa kuendelea na shughuli zake. Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa vyama vingi vinaanzishwa kwa msukumo wa kutamiza malengo ya kisiasa na ndiyo maana havidumu. Aidha, Watendaji wake Wakuu wanakuwa na uelewa mdogo kwenye nyanja za ushirika na malengo ya uanzishwaji wa vyama vyenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vyama hivyo kwa ujumla vilikuwa na idadi ya wanachama 575,651 na gharama za uanachama wao ilikuwa ni Sh. 6.58 bilioni kwa vyama vya msingi pekee na vyama 44 vya kati ya Mikoa pamoja na Benki tatu za Ushirika, Muungano huu ulikuwa na jumla ya vyama 2,411 ambavyo vilikuwa vinamiliki hisa 26,514 zilizokuwa na thamani ya Sh.360 milioni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna *Tanzania Federation of Agricultural Cooperatives*, hii ndio iko juu ya vyama vyote vya Ushirika kama vilivyogawanya kutokana na mazao manne Kitaifa, yaani, Tumbaku, Kahawa, Pamba na Korosho, *TFAC* ina wanachama wanne tu, Chama Kikuu cha Ushirika cha Pamba, Kahawa, Tumbaku na Korosho.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia majukumu ya *Federation* ni mengi na yanawafanya watendaji katika Vyama vya Ushirika vya Kati na vya msingi, kuwa na majukumu ya kusimamia tu, badala ya majukumu ya msingi ya kutafuta soko zuri ili kupata bei nzuri ya mazao ya wanaushirika badala ya washirika kufanya kazi ya kutafuta wao masoko. Watendaji wa vyama vya msingi wafanye kazi hiyo ya kutafuta masoko kwa mazao ya wanaushirika badala ya *Primary Societies* kuwa ni *Collection Centre on behalf of Regional Cooperative*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2003/2004, ukurasa wa nne, kuhusu hali ya Ushirika na Masoko nchini, alisema kuwa hali ya vyama vingi vya ushirika ilikuwa mbaya sana, iliyogubikwa na matatizo mengi sugu, pamoja na uongozi mbovu, ubadhirifu, hujuma na wizi ikiwa ni pamoja na muundo duni wa ushirika na kadhalika.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa mbali na yale aliyoeleza Waziri kuwa Wananchi walipoteza imani iliyokuwepo juu ya ushirika ni kuwa muundo wa ushirika uliopo sasa hivi ni ule wa kuwa *imposed* kwa watu badala ya kuwa *formed* na watu wenyewe. Hii imesababisha Wananchi wawe na *feelings* ya kuwa, huo ushirika unaoundwa, sio wa kwao, bali ni wa Viongozi wa Serikali, kitu kinachosababisha matatizo sugu kama Mheshimiwa Waziri alivyoyabaini. Tunaiomba Serikali ijaribu kurekebisha kasoro hizo kwa manufaa ya historia nzuri ya ushirika katika nchi yetu na wanaushirika kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wamezaliwa na kulelewa na Ushirika na hivyo bado wana imani kubwa na ushirika, mfano ni kule Kagera, Wananchi kuna msimu walikuwa wanauza kahawa Uganda na kuacha kuuza kwenye vyama vyao. Serikali iliweka vyombo vya dola kuhakikisha Kahawa haiendi Uganda. Tunadhani matatizo yalikuwa ni kati ya Vyama vya Ushirika na wanachama wake na wangekaa wakaona ni kwa nini wanachama hawataki kuuza kwenye Ushirika, Serikali haikutakiwa kuingilia kwa kutumia vyombo vyake. Kuingilia kwa Serikali ina maana ya kulinda watendaji wabovu wasio wabunifu katika masuala ya msingi ya uanzishwaji Ushirika. Kuwazuia wakulima kuuza mazao yao kwenye nchi ambayo inakuwa na bei nzuri ni kuwakatisha tamaa wakulima hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia na lengo zuri la ushirika, bado haujakidhi lengo lake kuhusu bei kwa wanaushirika kwa ujumla, bei itolewayo kwa wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kagera, malipo ya mwanzo ni shilingi 60/= na nyongeza ya shilingi 25/= kwa kilo ya kahawa ya maganda, bei hii ni ndogo mno. Sasa mkulima ili aweze kuona kahawa inamsaidia na ushirika unamsaidia ni mpaka auze tani ngapi? Aidha, inaonyesha kuwa kuna tofauti kubwa sana ya bei kwa wakulima wa kahawa Mkoa wa Kilimanjaro na Kagera, kitu kinachoweza kusababisha malalamiko na kuona kuwa wanabaguliwa, tunaiomba Serikali iliangalie suala hili, bei ya Kahawa ilingane kwa wakulima wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Ushirika ni kuwatafutia wanachama wake masoko na pembejeo. Vitu ambavyo mmoja mmoja ni adimu kuvipata au ni usumbufu kuvipata, haya ndiyo majukumu ya msingi katika ushirika. Kambi ya Upinzani, inamwomba Waziri, alieleze Bunge ni vyama vingapi vya Ushirika vimeshafanikiwa kupata soko la mazao au malighafi moja kwa moja nje ya nchi na kukwepa ukiritimba wa *middlemen*, kitu kinachowafanya wakulima kuona kuwa kilimo hakiwasaidii wao bali kinawanufaisha watu wengine, kama ambavyo imekuwa ikijitokeza sehemu mbalimbali kwa wale wanaojihusisha na biashara ya mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa vyama vya ushirika hapa Tanzania vimekuwepo kwa zaidi ya miaka 70 hadi sasa na historia inaonyesha Vyama vya Ushirika vya Mikoa ya Kagera, Mwanza, Tabora na Kilimanjaro ndiyo vilivyokuwa na nguvu katika Bara la Afrika na pengine Duniani, kwani vilimiliki mashule, vilisomesha watoto wao nje ya nchi, katika kozi tofauti kulingana na waombaji. Nadhani hili Mheshimiwa Waziri, analielewaa vizuri sana. Kambi ya Upinzani, inamwomba Waziri aeleze nini kilichokuwepo wakati huo mpaka Ushirika ukawa ni nguzo kubwa katika kilimo kwa ujumla na sasa hivi ushirika umebakia kupangiwa bei na kuwayumbisha wanachama wake, vyama vya ushirika vilikuwa na nguvu ya kujadili bei na wanunuvi. Leo ushirika unakosa nguvu za ku-*bargain* kwa manufaa ya wanachama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa siku za hivi karibuni, soko la Pamba limeshuka toka shilingi 300/= hadi shilingi 250/= na inavyoonyesha bei inaendelea kushuka zaidi. Je, Serikali inasema nini juu ya suala hili na ni kwa nini haijaingilia kati suala hili? Hii inasababisha kupungua ubora wa mazao yetu na wakulima kukatishwa tamaa kutokana na mfumo mbovu wa soko na biashara holela na soko kushuka. (*Makofi*)

Aidha, tunaona matatizo na migogoro ni kutokana na Ushirika kukosa dira katika uwajibikaji ya kuwa ni nani anatakiwa kuwa wa kwanza, Mwanachama au Serikali. Tusipositisha mambo ya viongozi wa siasa kuwa walezi na wadhamini wa Vyama vya Ushirika, basi mafanikio hayatakuja kuonekana katika sekta ya ushirika. Kuna viongozi wengi wa ushirika ambao ni wanasiwa na wengine wamekuwa wabadhirifu wa mali za Vyama vya Ushirika. Lakini wanataka kinga ya kisiasa na hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi yao. Tuna imani Waziri analifahamu hilo. Je, hatua gani wamewachukulia wabadhirifu hao? Mara nyingi kumetolewa kauli na Serikali kwamba, wale wote waliofilisi Vyama vya Ushirika sasa watakiona, mbona hatujawahi kuona hata

mtu mmoja kashtakiwa na hukumu kutolewa? Hii inawafanya Wananchi waamini kuwa viongozi hao wanapata kinga ya kisiasa toka Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kusikia kuwa hivi sasa kuna wanachama takriban 600,000 kwenye Vyama vya Ushirika na huduma zake zinawagusa maskini wapatao milioni kumi. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Watanzania sio maskini, kwani kila mkulima anachozalisha kinalingana na mahitaji yake, tatizo ni kwa viongozi kukosa ubunifu kumwezesha mzalishaji kupata bei nzuri ya anavyozalisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Kigoma, baadhi ya Wilaya za Mbeya na kadhalika, wakisema kuwa, Wilayani kwao chakula hakijawahi kuwa ni tatizo ila tatizo ni jinsi ya kuuza. Kambi ya Upinzani inawapongeza Wananchi wa Wilaya hizo, aidha, inashangaa ushirika kwenye Wilaya hizo ni wa nini na unawasaidiaje wanachama wake? Hivyo, tunashauri Wizara kuwa, suala siyo kuwa na vyama vingi ila ni mitandao ya vyama hivyo, ndicho kitu cha msingi. Mifano iliyotolewa hapa Bungeni inatosha kutuonyesha kuwa Tanzania ina chakula cha kutosha ila tatizo ni ufahamu wa sehemu gani ya Tanzania chakula kinapatikana kwa muda huo. Ndiyo maana nasisitiza mtandao katika Vyama vya Ushirika ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayodhoofisha vyama vya ushirika hapa Tanzania ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuingizwa siasa ndani ya Vyama vya Ushirika. Uendeshaji wa vyama vya ushirika kisiasa ni kuvinyima uhuru vyama hivyo kujiendesha kwa malengo na madhumuni walijokubaliana wanaushirika. Kwa vile Vyama vya Ushirika kazi yake ni ama kufanya biashara au kutoa huduma, basi ni lazima Serikali itoe uhuru kwa vyama hivyo kufanya kazi zake kitaalamu na kibiashara bila kuviingilia au kuvibagua kwa misingi ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa tatizo hili ni kwa Serikali kuona kuwa ina wajibu wa kumkomboa kiuchumi na kumwendeleza kila Mtanzania bila kujali msimamo wake wa kisiasa. (*Makofi*)

(ii) Ufinyu wa Mitaji, Elimu na Utaalamu ndani ya Vyama vya Ushirika. Kati ya vikwazo vikubwa vinavyozua ukuaji wa maenedeleo ya vyama vya ushirika hapa nchini ni pamoja na ufinyu wa mitaji, elimu na utaalamu ndani ya vyama hivyo. Hii inatokana na ukweli kuwa, kwa vile wanaounda ushirika ni watu wa vijijini ambaa ni maskini na elimu yao ni ndogo juu ya ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wakati sasa umefika kwa Serikali kuanzisha mpango na utaratibu wa kuvisaidia na kuviwezesha Vyama vya Ushirika kupata mitaji na utaalamu utakaoviwezesha kukua kiuchumi na hivyo kutoa mchango mkubwa katika juhudzi za kuondoa umaskini hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Mambo ya kuzingatiwa katika kuimarisha Vyama vya Ushirika, hasa vyama vya wakulima wadogo wadogo ili viwe na manufaa kwa wanachama wake na kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu kwa ujumla ni:-

(i) Serikali iache kuingilia uundaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika vya sekta zote, sio tu vyama vya ununuzi wa mazao.

(ii) Serikali iviwezeshe Vyama vya Ushirika kupata mikopo kwa kuvidhamini vyama hivyo wakati wa kuomba mikopo toka benki kwani vyama hivyo havina *collateral*. Mikopo hiyo iwe kwa riba ndogo kabisa na ipatikane bila usumbufo. Vyama vya Ushirika vinavyostahili kupata mikopo, vipewe mikopo hiyo mapema kabla msimu wa ununuzi wa mazao haujaanza. (*Makofî*)

(iii) Serikali itoe elimu, hasa kwa njia ya redio, juu ya mambo muhimu yanayohusiana na ushirika. Kama vile kuelezea umuhimu wa kila Chama cha Ushirika, cha sekta yoyote ile, kianzishe utaratibu wa kuweka na kukopa (*Saving and Credit Societies*), kila Chama cha Ushirika kununua hisa katika masoko ya hisa baada ya kushauriwa na Serikali ni kampuni gani iliyo bora katika soko na pia kila Chama cha Ushirika kununua *bonds* za Serikali (treasury and premium bonds)

(iv) Serikali itilie mkazo *Specialisation of Co-operative Societies*. Kwa mfano, ni vigumu wakulima kuunda Chama cha Ushirika cha mazao pamoja na wavuvi au wachimba madini.

(v) Serikali iachie vyama vya ushirika kujiunga pamoja na kuanzisha jumuiya zao mpaka juu (*the apex*), yaani hata nchi nzima bila kuingiliwa, yaani Serikali kazi yake iwe ni kuratibu tu. (*Makofî*)

(vi) Serikali iibadilishe *NMB* kuwa Benki ya Ushirika badala ya kuanzisha Benki nyingine. *NMB* ina mtandao hadi Wilayani hivyo itaipunguzia Serikali gharama ya kuanzisha Benki mpya na majengo mapya na watumishi wapya. Serikali hivi sasa ipo mbioni kuanzisha Benki ya Wakulima, lakini ikumbukwe kwamba, *CRDB* ilikuwa Benki ya Ushirika na ilikuwa na majukumu ya kukopesha vyama hivyo. Vyama vilikuwa na hisa ndani ya *CRDB*. Katika mtazamo na jitihada hizo hizo, tuijulize, zile hisa za Serikali kwenye *CRDB* zimeishia wapi? (*Makofî*)

(vii) Serikali ihakikishe kuwa utaratibu wa sasa wa uandikishaji Vyama vya Ushirika unabadilishwa mara moja kwani umejaa urasimu usio wa lazima. (*Makofî*)

(viii) Serikali ihakikishe kuwa mpango wa *Export Guarantee Scheme* unalenga na kunufaisha Vyama vya Ushirika zaidi kwa kuupanua katika mazao mengine badala ya kilimo tu.

(ix) Serikali kuanzia sasa iwashirikishe vijana wanaohitimu Vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini katika mpango wa kujiajiri wenyewe kwa kuwawezesha kuijundia

vikundi nya ushirika badala ya kutegemea na kungojea kuajiriwa. Mpango huo ni budi uzingatie mambo yafuatayo:-

Ili kupenyeza utaalamu na uongozi bora kwenye Vyvama nya Ushirika, ni vizuri Serikali, ikasimamia na ikahamasisha vijana wanaomiliza Vyuo nya Elimu ya Juu, kujiunga kwenye vikundi kama vile nya watu kumi mpaka ishirini na kuanzisha ushirika wa shughuli ya kiuchumi watakayochagua wenye na kisha Serikali ikawadhamini kupata mkopo wa benki ili uwawezeshe kununulia vifaa na nyenzo za kuzalishia. Mfano wa Vyuo nya Elimu ya Juu tunavyovizungumzia ni kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chuo Kikuu cha Kilimo, Chuo cha Ushirika Moshi na kadhalika. Ili kikundi cha ushirika kiwe ni chenye elimu na utaalamu wa kisasa, ni vyema kikawa na vijana wawili wenye ujuzi wa *Irrigation Engineering*, Vijana wawili wenye ujuzi wa Kilimo na Ufugaji, Vijana wawili wenye ujuzi wa Usimamizi wa Fedha, Vijana wawili wenye ujuzi wa Uongozi, Vijana wawili wenye ujuzi wa *Mechanical Engineering*, Vijana wenye ujuzi wa kuendesha Vyama nya Ushirika na kadhalika.

Uzuri wa Serikali kuwezesha uundwaji wa vikundi kama hivi vyenye kujumuisha wasomi toka vyuo vinavyofundisha fani mbalimbali, ni kuwa sasa vijana wetu wanaomiliza masomo yao watakuwa na uhakika wa kujijiri na pia itasaidia kutoa ajira kwa vijana wengine wengi katika yale maeneo ambayo vikundi hivi nya ushirika vitakuwa vinaendesha shughuli zao. Hii ndiyo njia sahihi ya kuutokomeza umaskini. Baada ya vikundi nya ushirika kuanzishwa, Serikali iwajibike kutoa udhamini kwa vyama hivyo wakati wa kuomba mikopo toka benki kwani vyama hivyo havina *collateral*.

Ni wajibu wa Serikali ikishirikiana na maafisa wa benki zinazokopesha fedha, kuratibu njia bora ya kusimamia urudishwaji wa mikopo hiyo kwa wakati na bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa nguvu kifedha kwa wakaguzi wa vyama nya ushirika nalo ni tatizo linalozidisha utendaji mbovu na ubadhirifu wa mali za ushirika, mfano, katika taarifa ya Waziri inasema kuwa ni asilimia 56.7 tu ndiyo vilikuwa vimekaguliwa na asilimia 43.3 havikukaguliwa, uwezekano ni mkubwa kuwa asilimia ambayo haikukaguliwa ndiyo muhimu zaidi na ndipo kwenye matatizo mengi ya kiutendaji, wizi, ubadhirifu na uwajibikaji kwenye ushirika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haiilewi ni vipi Programu ya kuendeleza mfumo wa masoko ya mazao ya Kilimo unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu wakati ni jukumu la Wizara hii au Wizara ya Kilimo? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri, kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, ina majukumu mengi na ndio msimamizi mkuu wa shughuli za kiutendaji Serikalini, tunashauri kitengo hicho cha Programu ya kuendeleza mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo kihamishiwe Wizara ya Ushirika na Masoko. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Bodi za mazao na Watendaji wake, wanafanyaje kazi zao, kwani hazina vyanzo vyovoyote vya mapato wala ruzuku toka Wizarani, kwa mantiki hii, utendaji kazi wake inakuwa ni mzigo mkubwa kwa Vyama Ushirika vya Ushirika vya Msingi (*Primary Societies*). Tunashauri mzigo huu ubebwe na Serikali, Serikali itoe ruzuku ya kuendesha bodi hizo.

Mheshimiwa Spika, kituo cha kuendeleza masoko, katika utekelezaji wa ushauri na maagizo ya Kamati kuhusu kuanzisha kituo cha kuendeleza masoko ilikuwa kiungo muhimu na *Trade hubs* ambazo zipo katika Mpango wa *AGOA*. Tunashukuru Wizara imeamua kuiimarisha idara yake ya masoko. Sasa kitu cha muhimu hapa kwanza ni kuimarisha uzalishaji na masoko ya ndani. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, bidhaa nyingi zinazalishwa hapa nchini, lakini Watanzania wengi hawajui wapi wauze bidhaa hizo, mifano mizuri Waheshimiwa Wabunge, mmeshuhudia, maonyesho mbalimbali yaliyomalizika hapa kwenye Viwanja vya Bunge, bidhaa mbalimbali zilizoletwa zimezalishwa hapa kwetu. Mkakati wa Wizara usiwe ni kulenga soko la nje tu, kwanza tuhakikishe bidhaa zetu zinafurika kwenye soko la ndani na kuwahamasisha Wananchi wapende bidhaa zinazotengenezwa nchini. Tunaamini kama bidhaa zina ubora unaotakiwa, tunaweza tukauza ziada nchi za nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kugeuzwa kwa Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu, Kambi ya Upinzani haipingi jambo hili lakini inashauri sababu zilizofanya kuanzishwa kwa chuo hiki zisipuuzwe, mafunzo ya awali ya ushirika yabakie palepale. Kambi ya Upinzani, inauliza, je, chuo hiki kinavyobadilishwa kuwa Chuo Kikuu, kwa nini kisiwe chini ya Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu? Je, mambo ya Ushirika yatabaki pale pale?

Tunashauri Chuo hiki kiendelee pamoja na kutoa *degree*, kitoe pia vyeti na *Diploma* ya ushirika kama ilivyokuwa hapo awali. Pia vyuo vingine vya ushirika kama Kizumbi, viendelezwé. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuanzisha vyuo kuna maandalizi ikiwa ni pamoja na ikama ya wataalamu. Je, Chuo hiki kimejiandaaje?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni hayo na mapendekezo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, katika kuendelea kuwapatia Wenyeviti wa Bunge uzoefu, sasa namwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, aje aliongoze Bunge. Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ataendelea mpaka jioni. (*Makofî*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja hii ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yeté Mwalyego na familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Watendaji wake katika Wizara hii ya Ushirika na Masoko. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, anajitahidi kadri ya uwezo wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge ninatoka Jimbo la Newala na jimbo langu ndiyo jimbo linalozalisha korosho kwa wingi. Usije ukashangaa kwamba, katika kuchangia kwangu nikawa nachangia tu suala la korosho. Uchumi wetu, mambo yetu kuwa mazuri, maendeleo yetu na mambo yote tunategemea zao la korosho, hatuna zao lingine mbadala zaidi ya korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo nichangie kwa masikitiko makubwa sana katika msimu wa korosho wa mwaka 2000/2001, Serikali ilikopa korosho kutoka kwa wakulima wa zao la korosho na mpaka leo hii bado hawajalipwa mazao yao yaliyokopwa na Serikali. Nataka kusema Serikali ilikopa kwa sababu Serikali ndiyo ilishinikiza Bodi ya Korosho ikope hizo korosho. Lakini cha kushangaza katika ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, utaona kwamba, katika msimu wa mwaka 2000/2001, bei ya kahawa katika soko la dunia iliposhuka sana na kusababisha Vyama vya *KCU* na *KDCU* vishindwe kulipa wakulima, Serikali iliingia katia na kutoa shilingi bilioni 1.7. Pia kwa wakulima wa pamba ilikuwa hivyo hivyo, walisaidiwa na Serikali na kulipa deni la shilingi 3.79 bilioni. Pia Serikali imesaidia kuwanusuru Wananchi katika zao la pareto. Sasa je, Mheshimiwa Waziri, hivi kwenye korosho umeshindwa nini kuwalipa madeni wale wakulima? Kama kweli mmeweza kulipa kwenye kahawa, kama mmeweza kulipa kwenye pamba na kama mmeweza kulipa kwenye pareto, kwenye korosho kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nataka nikuambie kwamba, Mheshimiwa Waziri mwaka 2000, alipata bahati ya kusafiri kwenda China, India na Singapore, kwa ajili ya kutatua tatizo la soko la korosho. Sasa bahati hii sisi tulikupa watu wa zao la korosho kwenda India, China na Singapore. Sasa tuna haki ya kukudai hata nauli uliyokwenda nayo Singapore na India, uturudishie kwa sababu uliporudi kule ulifanya kikao na sisi Wabunge tunaotoka mikoa inayolima zao la korosho, ukatuahidi kabisa kwamba, mambo yatakuwa mazuri na kwa kweli umetutafutia na umewekea misimamo mizuri. Lakini Mheshimiwa Waziri, mpaka leo na sasa sisi wenzako Wabunge wenzio tunakwenda kwenye uchaguzi, wale Wapiga Kura wanatuuliza fedha yetu vipi kabla hatujapiga kura?

Sasa tunaomba utakapokuwa una-*wind up*, Mheshimiwa Waziri, ujitalidi kutuelezea suala hili la mkopo mliokopa kutoka kwa wakulima wa zao la korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wakulima wa korosho hawana matatizo, kwa kweli hizi korosho zilikopwa kwa bei ya shilingi mia mbili kwa *grade* ya kwanza na *grade* ya pili ilikopwa kwa shilingi mia moja, fedha ambayo ni ndogo sana ambayo Serikali mngeweza kulipa kabisa. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri, mliangalie wenzeni tuko katika matatizo makubwa, hawa wakulima wamekwama, kama mnavyoju sasa hivi pembejeo zimepanda bei. Sasa hivi mfuko mmoja wa *sulphur* umefika Sh.15,000/= na haipo hata hiyo Sh. 15,000/= pia. Sasa Mheshimiwa Waziri, jinsi ulivyofanya kwenye pamba, jinsi ulivyofanya kwenye kahawa na jinsi ulivyofanya kwenye pareto, tunakuomba pia katika korosho utusaidie hilo pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uhamisho wa baadhi ya watumishi alioufanya. Kwa kweli mimi binafsi niliandika barua katika Wizara yako, kuna baadhi ya watumishi wamekaa kwenye Halmashauri zaidi ya miaka 30, sasa mtu anakaa miaka 30 usitarajie kuwa na mabadiliko ya aina yoyote, kwa kweli mimi ninakushukuru na ninakuombe mengine ambayo yaliyobaki, basi uyafanye kama maeneo haya mengine uliyofanya uhamisho wa hawa waliokaa zaidi ya miaka 20, miaka 25 na miaka 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Watanzania wengi ni maskini, hutegemea shughuli za kilimo kwa maisha yao. Sasa sisi katika Mkoa wa Mtwara, tuna matatizo kadhaa ambayo yanaathiri juhudhi za upatikanaji wa masoko. Hii inasababishwa na biashara holela inayofanywa na wafanyabiashara kutoka nje. Hawa *processors* wa zao la korosho ambaao wako nje ya nchi hii, huenda mpaka kijijini wenyewe kwenda kununua korosho. Sasa hawa *processors* wanapokwenda kule vijijini wanawavunja moyo wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijapata kutokea, katika msimu wa mwaka 2000/2001, hawa *processors* walikwenda vijijini na *ku-check* kwa kuchoma sindano *quality* za korosho. Mimi sijawahi kusikia *quality* inachekiwa kwa kuchomwa sindano. Sasa hawa kwanza tani wanazonunua ni tani 1,000 hawanunui zaidi ya tani 1,000, lakini wanatoka nje wanakwenda kwa wakulima, wanawavunja moyo kwa kuwaambia korosho zenu chafu, korosho zenu hazifai, kumbe ni uongo korosho zile ni nzuri, zinakuwa *maintained* vizuri, zinapulizwa dawa kwa gharama kubwa kabisa, lakini wanavunjwa moyo kwa sababu ya kupunguza bei ya wakulima wa zao la korosho. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri, hawa *processors*, wafanyabiashara wakubwa wanaokuja, wasiende moja kwa moja vijijini. Sisi katika Mkoa wa Mtwara, tuna mfumo mzuri sana wa ununuzi wa zao la korosho. Kwa kweli vyama vyetu vya ushirika vinafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Kila zao la korosho linalonunuliwa, sisi linanunuliwa kutoka kwenye chama cha ushirika halinunuliwi nje ya chama cha ushirika, tuna utaratibu mzuri sana. Lakini hawa *processors* na wafanyabiashara wanaotoka nje wanatuvunja moyo. Pia Mheshimiwa Waziri, nataka kukuhakikishia kwamba, tuna wafanyabiashara wazawa wazuri wanaotoka Mkoa wa Mtwara, wanununua korosho vizuri bila matatizo yoyote na hawatuharibii jina lolote katika Mkoa wa Mtwara. Lakini cha kushangaza utakuta kwamba, mgeni aliyetoka nje ndiyo anaibiwa hela. Lakini mzawa hajawahi kuibiwa hela

hata siku moja. Sasa wanatuharibia jina kwamba, kuna ujambazi, kuna matatizo mengi kwenye korosho na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni tatizo kubwa, ni tatizo mojawapo linalosababisha kuangusha bei ya korosho kwamba mtu anatoka moja kwa moja India anakwenda zake mpaka kijijini kwenda kununua korosho. Huu utaratibu naomba uuangalie Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie katika suala la *EPZ*. Sisi zao la korosho hatujapewa upendeleo wa aina yoyote katika *EPZ*. Sasa hivi Mtwara tuna kiwanda cha *OLAMU*, ambacho kinabagua korosho kimetoa ajira kubwa kwa Wananchi wa Mkoa wa Mtwara, tuna kiwanda kingine cha export trading ambacho kiko pale Mtwara. Tuna kiwanda kingine kipo Naliendele na tuna kiwanda kingine tena cha Mama Mkapa, ambacho amefungua pale Mtwara. Lakini Mheshimiwa Waziri, nataka kukuambia kwamba, kama zao la korosho halikuingizwa katika *EPZ*, viwanda hivi havina maisha, nakuhakikishia mpaka kufika mwakani, hakuna kiwanda ambacho kitafanya kazi. Sasa hivi viwanda vinavyofanya kazi vinatoa ajira kubwa sana kwa akina mama na vijana, vinatusaidia sana kutoa ajira, kwa sababu kazi kubwa inayofanywa na hivi viwanda ni kazi za mkono. Sasa ni ajira kubwa sana. (*Makofi*)

Leo angalia kile kiwanda kilichokuwepo pale Vingunguti cha *Premier Cashew*. Kile kiwanda kilikuwa kinatoa ajira ya akina mama 2,500. Leo kile kiwanda kimefungwa kwa sababu hakikingizwa katika mpango wa *EPZ*. Sasa katika suala la *EPZ*, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie hivi viwanda vyta kubangua korosho na kuweza kupata soko la uhakika na kuweza kupata bei ya uhakika ya korosho na kubangua korosho nchini.

Hivi ndio tutaondoa tatizo lote la soko, bei na kila kitu. Viwanda hivi ukienda kuangalia, zaidi vinamilikiwa na Watanzania, ndio wanaomiliki viwanda hivi. Lakini Watanzania hao hao ndio wanaopata vikazo vingi. Sasa sijui mnataka waje Wawekezaji kutoka India ndio muwape nafasi ya *EPZ*? Mtueleze ili Watanzania wajue basi waagize watu kutoka nje ili waje wafungue hivi viwanda kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi tuna tatizo la wabanguji wadogo wadogo wa korosho. Wamekuja kutembelea Mtwara, wameona wale akina mama wanavyojianika pale barabarani kutafuta soko la korosho. Kwa kweli wale akina mama wanafanya kazi nzuri sana, wanabangua korosho kwa mikono yao na ile korosho inayobanguliwa ni *grade one* kabisa, lakini hawana soko! Leo wanakaa pale barabarani wanahangaika kutafuta soko. Hawana hata *packing machine* za *ku-pack* zile korosho zao kwa sababu zile korosho wanazobangua zikikaa zaidi ya mwezi mmoja zinaharibika, wanapata hasara kubwa sana wale akina mama. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri, katika mipango yake, aangalie jinsi ya kuwasaidia wale akina mama wabanguji wadogo wa korosho. Wale akina mama ndani ya Mkoa wa Mtwara, ndani ya Wilaya zote, kuna vikundi vyta akina mama ambavyo wanafanya vizuri sana, lakini tatizo lao hawana soko na tatizo lingine linalowakwamisha ni jinsi ya *ku-pack* zile korosho. Wale akina mama wanahitaji

packing machine ili korosho zao ziwe *packed* na *vacuum* ambayo inaweza ikakaa zaidi ya miezi sita na kuweza kutafuta soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo la watu wa nje kuja kununua korosho moja kwa moja Kijiji ni tatizo kubwa sana. Tunaomba sana hili liangaliwe na leo Mheshimiwa Waziri, atolee tamko rasmi kwamba wale watu ni marufuku moja kwa moja kwenda kununua korosho kwenye Vyama vya Ushirika. Tuna vijana wetu wanafanya kazi nzuri sana na hawana matatizo yoyote na wapo na *agents* wengi wanatoka pale Mtwara, Lindi, Newala, Masasi, Tandahimba, sehemu zote wapo *agents* wa kununua zile korosho, lakini tukiwaachia hawa watu kwenda moja kwa moja itakuwa ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia tunamwomba Mheshimiwa Waziri, leo atupe dira ya bei ya korosho. Leo katika Soko la Dunia linaonyesha kwamba, korosho mwaka huu itaanza kununuliwa kwa bei ya Sh. 800/= kwa kilo. Sasa isije ikaingia mizengwe mingine tena tukaanza kununua kwa Sh. 200=/. Leo Soko la Dunia linaonyesha kabisa zao la korosho ni karibu Dola 800. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri, aliangalie, atupe ufanuzi na pia kuhusu suala la ushuru, tuna matatizo makubwa sana. Tuna ushuru mkubwa sana unaosababisha mkulima kukosa bei nzuri ya korosho. Sasa na sisi tunaomba tupate mfumo wa wenzetu wa Msumbiji. Sasa hivi wenzetu wa Msumbiji wanachokifanya ni kwamba, ushuru wote wa korosho unatozwa pale Bandarini wakati unakuwa *exported*, yaani inachajiwa kama ni *export levy*, kama 4% au 5%. Lakini huku chini kunakuwa hakuna kitu chochote. Sasa zile 5% unazochajiwa kama *one percent* inakwenda kwenye Bodi ya Korosho, *one percent* nyingine inakwenda kwenye mfuko mwingine na zile *three percent* zilizobaki ndio zirudi kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, wao walikuwa wanakusanya ushuru wa korosho pale kwenye Halmashauri yao, lakini baadaye wao wakaikabidhi kazi ile Bodi ya Korosho na Bodi ya Korosho ilipoanza kutoa kodi ile, ilipata ongezeko la asilimia 50 zaidi ya makusanyo yaliyokusanya na Halmashauri ya Mkuranga. Kwa hiyo, sisi tunategemea kwamba, zao hili la korosho kama likitozwa ushuru wake pale Bandarini, basi na sisi tunaweza tukapata ongezeko la zaidi ya asilimia 50 ya pesa zile tunazokusanya kutoa kwenye Halmashauri. Hii tutakopesha katika mambo mengi na itasaidia sana kutoa hata *incentives* viwandani katika viwanda vinavyobangua korosho. Kwa sababu *automatically*, itakuwa ni *incentive* kwa viwanda vinavyobangua korosho kwamba, leo ile korosho ambayo ni *raw* inayokuwa *exported*, ndiyo inayotozwa kodi, ile ambayo inapelekwa viwandani inakuwa haina kodi, inakuwa ni *automatic* imeshapata *incentives* tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi, ni hayo tu. Naomba niunge mkono hoja mia kwa mia kwa kutegemea kuwa, maombi yangu ya madeni ya korosho sasa yatalipwa kwa wakulima. Nashukuru. (*Makofi*)

MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika kuwaombea ndugu zetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, wametutangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu,

azilaze roho zao mahali pema peponi, kwa kuwa yeye anatoa na yeye anatwaa, jina lake lihimidiwe. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbuke Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, ambaye bado yuko Hospitalini, ambaye amepata ajali. Namwomba Mwenyezi Mungu, amponyeshe mapema, ajiunge na sisi ili tusukume gurudumu la maendeleo la Taifa letu kwa pamoja.

Kwa pekee nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kumnusuru Mheshimiwa Rosemary Nyerere, aliposhambuliwa na majambazi na amerudi salama, makovu mengi sana, majeraha mengi sana, ninarudia kusema kwamba, kwa vile majambazi hayana huruma na mtu yejote yule, hata binti kama huyu walipomwona mwili wake mwembamba kiasi hicho ni hali yake ilivyo, wakaamua kumtia msukosuko na kumjeruhi nusura kumuua, hawana huruma! Nasema hivi, narudia kusema kwamba, majambazi wote wauawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa George Kahama, ni hotuba nzuri sana, ni hotuba inayotoa mwelekeo na dira kamili katika Wizara hii na sisi Watanzania kuweza kufaidika katika Ushirika na Masoko. Katika kufaidi huku kusiwe na mtu yejote yule ambaye anafanya ubadhirifu au anaiba au anafanya ujambazi katika kazi hii nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri, anaiongoza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasi katika Mkoa wa Kilimanjaro, tunao ushirikiano wa hali ya juu sana unaoongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. Huyu Mkuu wa Mkoa ni zawadi kwa Mkoa wa Kilimanjaro tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Ameweka *record* katika kutushirikisha sisi Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro kuwa kitu kimoja na kusahau itikadi zetu. Kwa kuwa baada ya Mbunge kuchaguliwa kuwa Mbunge kwa tiketi aliyoitumia, yeye anakuwa ni Mbunge wa Vyama vyote, itikadi zote, dini zote, viumbe vyote vilivyo hai na ambavyo sio hai. Hana budi kushirikiana na Wabunge wengine katika eneo hilo katika Mkoa huo ili kuleta ufanisi wa ushirikiano na ushirika katika kuendeleza maendeleo ya Mkoa husika hususan Jimbo husika. (*Kicheko/Makofi*)

Napenda kumtambua Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge wa Rombo, kwa tiketi ya CCM, pia napenda kumtambua Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai (CHADEMA), Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha (CCM), Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini (TLP), Mheshimiwa Daniel Yona, Mbunge wa Same Mashariki (CCM), Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi (CCM), Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga (CCM) na mimi mwenyewe, Mheshimiwa Major Jesse Jeremiah Makundi, Mbunge wa Jimbo la Vunjo (TLP). (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndio wanaunda ushirika na ushirikiano wa kusimamia na kuongoza Mkoa wa Kilimanjaro tukishirikiana na Jemadari wetu,

Mheshimiwa Mkoo wa Mkoa, Mama Hilda Ngoye, ambaye nampongeza kwa kazi yake nzuri sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaposhirikiana kiasi hiki, kunakuwa na watu ambao ni wanasiasa uchwara, wanatufuatafuata, wanatuzingira zingira ili kutuvurugia ushirikiano huu ili tushindwe kusimamia Vyama vyetu vya Ushirika, tushindwe kusimamia masoko kwa kututawanyisha na kutusambaratisha, kitendo ambacho nakilaani na sasa nasema sitaki kuona hawa wanasiasa uchwara, sitaki kuona watu wenyewe siasa za chuki na sitaki kuona wale wenyewe siasa za uchochezi. Mara tu baada ya Uchaguzi, tunaungana wote kwa pamoja kufanya kazi moja tu. Hawa viongozi wetu Wenyeviti wa Vyama Taifa, wana uzoefu mzuri sana wa kuongoza Vyama vyao na wanaongoza kwa kutumia Katiba na Kanuni, hawaongozi Vyama vyao kwa kutumia Magazeti. Hivyo, kabla sijaendelea na mchango wangu ambao ni mfupi sana, nakanusha katakata yale yote yaliyozungumzwa kwenye Magazeti ya kwamba ni ya uongo, uzushi, walitaka tu namna ya kutaka kupata chochote kuuza Magazeti na kuona kwamba wanatafuta njia ya kutuharibia uhusiano wetu na Vyama vyote vya Demokrasia hapa katika nchi yetu ya Tanzania. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, kutokana na uwezo mzuri, Viongozi wetu wa Kitaifa walionao, wana uzoefu, kwa hiyo, kamwe hawafanyi kazi kwa Magazeti, ila wanafanya kazi kwa uongozi kwa barua, kwa kuitana kwenye vikao mbalimbali na kukosoana. Hivyo, nafuta yote yale yaliyokuwa yamezungumzwa kuhusu *TLP* ni ya uongo kwa sababu sisi Wabunge husika hatujapata barua wala simu na kwamba tunashirikiana vizuri mno na Mwenyekiti wetu na hatujasambaratika hata kidogo. Wauza Magazeti na wenyewe kueneza siasa za uchwara waendelee huko huko, sisi tuko njia moja ili kudumisha demokrasia hapa nchini. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hilo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niingie kwenye nyanja moja tu katika Ushirika na Masoko. Nyanja hii ni akiba na mikopo. Mara tu baada ya kuingia madarakani kwenye Jimbo la Vunjo, nikiongoza vyema Kata za Kirua, Kilema, Marangu, Mamba, Mwika, Himo, Makuyuni na Kahe, nilijikuta kwamba, kuna wizi wa hali ya juu sana kwenye Benki hizi za akiba na mikopo kiasi kwamba, wale walioweka fedha zao kule hawakuruhusiwa tena kuzichukua kama ni akiba yao kwenda kutunza watoto wao kuwapeleka Shule na kuendesha maisha yao. Wale viongozi walioko kule, *signatories* walioko kule, waliowekwa katika Vyama hivi ndio waliokuwa wanachukua fedha hizi kujinufaisha, kujenga majumba, kununua viwanja, kununua magari na kila anayekwenda kuchukua kule mwenye amana na akiba alikuwa anaambiwa hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikajiuliza nani aliywajengea nguvu kiasi hiki hawa watu? Nikajiuliza, jambazi wa kwanza lazima awe Mrasisi ambaye ndiye anasimamia. Nikamtafuta Mrasisi wa Mkoa anaitwa Ndugu Makundi kama mimi na kila anapoitwa kuja kusimamia uongozi katika hivi Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo anapiga chenga, haji. Nikajua kwamba, huyu anayemficha mwizi naye ni mwizi vilevile. Anayemficha jambazi, naye ni jambazi vilevile. Nikajua kwamba, kunaelekeaa

kuna jambazi mwingine anamficha, basi huyo atakuwa Mrajisi wa Taifa. Nikamwenda, nikamwuliza hivi ni wewe? Akaniambia sio mimi, ni hao hao walioiba kule. Ni nani sasa washtakiwe wachukuliwe hatua? Akaniambia tunachukua hatua wakati muafaka. Siku zimekwenda, siku zimerudi! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vyao vya Ushirika ni pamoja na *Mwika North Rural Savings, SACCOS*, kwa hesabu zilizokaguliwa mwaka 2000/2001, hawa wezi waliiba Sh.34,727,262/= . Wanachama waliokuwa kule ni 2,380 na hao ndio niko nao sambamba, tunakimbizana na majambazi mpaka tuwapate na tukiwapata kama Wizara itashindwa kuchukua hatua za Kisheria, nakuhakikishia ifikapo Januari, 2005, hawatakuwa wanapumua kwa sababu wametuhabibia uwezo wetu wa kuendeleza maendeleo yetu. Kwa hiyo, hawana haja ya kupumua wakati wao ni majambazi kama majambazi wengine tu. Jambazi wewe umeweza kuchukua zile fedha nyepesi ukaweka mfukoni, majambazi wengine wanavunja nyumba na kuchukua vifaa taslim vya uzito mkubwa, majambazi wengine wanachukua kuku, sijui wanachukua magodoro na hivyo vijizi uchwara nawaambia huko Vunjo waache wizi huo maana yake nikija watapata moto na nimeshatoa matangazo kwamba wauawe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Ngakoma iliyoko Mwika Msae, wameiba Sh.25,900,000/=, nyingine ni *Mamba Rural Savings Account*. Mamba kule wameiba Sh.3,500,000/=, nyingine *Marangu East Rural Savings*. Marangu pale wameiba Sh.78,600,000/=, *Marangu West Rural*, wameiba Sh.2,200,000/=, nyingine ni *Legho Rural* wameiba Sh.151,000/. Hawa wote ni wezi na majambazi wa kawaida. Nilitaka kujua kama Waziri mwenyewe ni jambazi mwingine ili nichukue hatua ninazozijua kwa sababu lazima auwawe. Lakini jana alinihakikishia Ofisini kwake kwamba, yeye sio jambazi na kwamba, sheria ambayo ndiyo rungu la dola, litachukuliwa dhidi ya hao majambazi na nina hakika ninapozungumza sasa hivi, kama nitawakuta shauri yao na kama wanajua rungu hili linakuja kwa sababu sheria tunazozitunga, kanuni zinafuatwa, waikimbie nchi kabla hatujawakuta, kwa sababu nasema kwamba hakika hukumu yao ni miaka 30 na kufilisiwa mali zao, ninazifahamu fika. Wote hawa, Kirua, Kilema, Marangu, Mamba, Mwika, Himo, Makuyuni na Kahe, wale wote waliofilisi ole wao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu kengele ya pili inigongee, lakini nasema hivi, Ushirika mwingine huu wa Kahe Magharibi, ushirika wao ni wa kilimo cha umwagiliaji. Labda kwa bahati mbaya imetokea kwamba ile mifereji yote imeharibika na ninaomba sasa Serikali ya Kilimanjaro iingilie kati ile mifereji ili kilimo kile cha ushirika kiweze kuendelea vizuri na mazao yaingie kwenye ghala waweze kupata nafuu yao ya maisha. Kahe Magharibi hadi Mashariki hali ni ya unyesheaji. Lakini kwingine kote, Kirua, Kilema, Marangu, Mamba, Mwika nasema kwamba, wale waliofilisi Benki hizi ole wao, orodha ninayo. Walikuwa wanachukua kila baada ya siku mbili shilingi laki moja, shilingi laki tano, shilingi laki sita, shilingi milioni moja, shilingi milioni mbili. Katika Benki hizi walikuwa wanaweka akiba Wananchi wengi sana pamoja na Baba yangu mzazi ambaye ameshafariki na mimi niliweka pesa huko huko. Shule zote, makanisa yote walikuwa wameweka huko *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara muhimu ya Ushirika na Masoko. Naomba nianze kwa kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na Marehem Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo, utaongozwa na falsafa mbili. Falasafa ya kwanza ni kuwa, ukiamini katika kila kitu maana yake wewe hauamini katika chochote. Haiwezekani ukasema kwamba umesimama na wakati huo huo umekaa. Lazima uamue ama umesimama ama umekaa. Kwa hiyo, ukiamini katika kila kitu, maana yake hauamini katika chochote, falsafa ya kwanza itakayoongoza mchango wangu wa leo.

Falsafa ya pili itakayoongoza mchango wangu wa leo, natumia maneno ya busara aliyotupatia Baba wa Taifa, alisema: “Mtu mwenye akili akikwambia jambo la kipumbavu huku akitambua kwamba, jambo hilo ni la kipumbavu ukalikubali atakudharau sana.” Narudia kwa ambao hawakusikia ili wasikie. Mheshimiwa Baba wa Taifa alitufundisha na akasema, nanukuu: “ Mtu mwenye akili timamu akikwambia jambo la kipumbavu huku akijua ni la kipumbavu ukalikubali, atakudharau sana.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndizo falsafa mbili zinazoongoza mchango wangu wa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa na Serikali inaamini na Mheshimiwa Balozi George Kahama, alikuwa mtu wa kwanza alipokuja kwenye ziara katika Jimbo langu na kwa bahati nzuri akasema anaomba twende kwenye Kijiji tulikozaliwa na tulipokuwa pale akawaeleza Wananchi kwamba, *STABEX* ya kahawa inakuja na akawahakikishia wamwamini kwamba, *STABEX* hiyo watapewa kama ulivyokuwa utaratibu wa kawaida. Mimi nikampigia makofi na Wananchi wakampigia makofi na bahati nzuri aliyasema haya katika Kijiji ninachozaliwa na Shule ambayo nilianza kujifunza kusoma na kuandika. Lakini baadaye ikaonekana kwamba, sasa msimamo wanaotoa fedha hizo sasa fedha hizo kwa wakulima wa kahawa hawawezi kupewa fedha taslim ingawa wakulima wa chai wanaweza wakapewa, lakini wa kahawa hawawezi kupewa fedha taslimu. Kwa nini? Ni kwa sababu walielezwa hivyo na wanaotoa fedha hizo. Kwa hiyo, nasema hawa Wazungu wanaotoa fedha hizi, waliwaambia wataalam wetu mambo ya kipumbavu na wakayakubali, kwa hiyo wakawadharau. Sisi kama Bunge hili, hatuwezi kuelezwu mambo ya kipumbavu tukayakubali kwa sababu tutadharauliwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae kidogo. Mchango ni mzuri kweli, lakini naomba *u-make selection* kwa maneno yale yale kwa maana ile ile. Karibu.

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Bahati nzuri siyo maneno yangu ni falsafa ya Mwalimu Nyerere lakini kwa kuzingatia ushauri wako, nitayatumia kwa *style* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STABEX* hiyo hiyo, tulielezwa kabisa na kila mtu anaamini kwamba, fedha hizo lazima tuhakikishe zinamfikia mkulima ili aweze kunufaika nazo, lakini baadaye tunaambibiwa, waliota fedha hizo wanasema lazima mtaalam kutoka London ndiye aje kutusaidia kuzitambua barabara za maeneo inakozalishwa kahawa na Waziri wa Ujenzi hazijui barabara hizo, wataalam kwenye ushirika hawajui barabara hizo na wala Wabunge hawajui barabara hizo. Kwa hiyo, unaamini kwamba, fedha zile lazima zitumike vizuri zimfikie mkulima, lakini fedha hizo hizo unaamini lazima ulete mtaalam kutoka London kuja kusaidia kutambua ni barabara zipi zitengenezwe, potelea mbali hata ukimlipa asilimia 40 ya fedha hizo. Hii ni kuamini katika kila kitu, ni sawasawa na kutoamini katika chochote. Yeyote akikwambia maneno hayo kwamba chukua mtaalam kutoka London akusaidie kutambua barabara za Kahawa na ukakubali maneno hayo, sasa mengine sipendi kusema kwa ushauri wa Mwenyekiti. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelezwa kabisa na tunaamini kwamba, Wizara ya Ushirika na Masoko ni muhimu kwa kutusaidia kutafuta masoko. Tunaamini, lakini vilevile kwamba, mpango wa kuendeleza masoko hauwezi ukakaa kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko, lazima ukae kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii ni sawasawa na kwamba, unaamini katika kila kitu na hivyo huamini katika chochote. Unaamini Wizara ya Ushirika na Masoko ni muhimu na lazima iwepo kuwasaidia wakulima, lakini unaamini vilevile mpango mkubwa wa kuendeleza masoko, hauwezi ukakaa kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko, ni lazima ukae kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Unaamini katika kila kitu, hauamini katika chochote. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile unaamini kwamba, Wizara ya Ushirika na Masoko ni muhimu ili kutusaidia kutafuta masoko na unatambua vilevile ziko Bodi za Mazao ambazo kazi mojawapo ni kuhakikisha zinatafuta masoko, lakini vilevile unaamini Bodi hizi ni dhambi kubwa kukaa kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko na badala yake zikae kwenye Wizara ya Kilimo. Hapa ninachomaanisha ni kwamba, unajaribu kuwaambia Watanzania umuhimu wa Wizara ya Ushirika na Masoko, lakini wakati huo huo unahakikisha Wizara hiyo haipewi vyombo ambavyo vingefanya ifanye kazi yake vizuri. Kwa hiyo, unaamini katika kila kitu, maana yake hauamini katika chochote. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaamini vilevile kwamba, wakulima lazima wawezeshwe kuweka fedha kidogo kidogo na wajifunze tabia ya kuweka akiba. Kwa utaratibu huo wakulima wa Chama Kikuu cha *KCU* Kagera, wakaamua kuwa wanaweka fedha kidogo kidogo ili baadaye waweze kuwa na mfuko mkubwa, waepuke riba kubwa zinazotozwa na Mabenki na unasema hiyo ndiyo sera yetu na ndiyo sera yetu, mtu maskini lazima ajifunze kuweka akiba kidogo kidogo. (*Makofsi*)

Mkulima huyu anapojitahidi kuweka fedha kidogo kidogo, *TRA* inakimbia haraka sana na kumtoza kodi kubwa kwa sababu ameweza kukusanya zaidi ya shilingi bilioni moja kwa kukata kwenye fedha ambayo angepeta na kwa hiyo, unapunguza uwezo wake. Kwa hiyo, huku unaamini aweke akiba, huku unaamini kukatwa kodi fedha kidogo na kwa sababu hiyo lazima fedha zilizokatwa kwenye mfuko wa mazao wa wakulima wa

Kagera zirejeshwe mara moja kwa sababu ni haki ya wakulima na ilikuwa ni dhambi kubwa kukata fedha hizo. (*Makofi*)

Lakini unaamini vilevile kwamba, lazima tuwawezeshe Wananchi mmoja mmoja kwa kupitia ushirika, unaamini kabisa na tunasema kwamba, hiyo ndiyo sera yetu na tunasema kwenye ubinafsishaji wanapotokea Watanzania wakaunganisha nguvu zao, basi tutawapa kipaumbele. *KDCU* na *Tanzania Federation of Cooperatives* wakaungana wakawenza kununua hisa ya Kiwanda cha *TANICA*. Lakini hadi sasa ninapoongea ni miezi sita, Waziri muhusika amekalia uamuzi wa *PSRC* na kwa kuchelewesha uamuzi huo, maana yake siku moja tutaambiwa hapa kwamba, *KCU*, *KDCU* na wakulima ni wababaishaji, walitaka kununua kitu ambacho hawana uwezo wakati uwezo wanao, fedha wanazo lakini uamuzi unacheleweshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri muhusika ni askari wa mwavuli, ambaye kwa bahati mbaya hakupewa mwavuli, hana Bodi za Masoko, mipango ya kuendeleza masoko ya wakulima iko kwenye Ofisi nyingine. *STABEX* pia hana kauli nayo. Hana rungu la kupiga wanaonea ushirika, bajeti ya Wizara ni ndogo. Alichonacho ni uwezo wake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa uwezo wake, machache aliyofanya nampongeza. Lakini nasema na kusisitiza tuache kuamini katika kila kitu. Tuamini kwamba, Wizara ya Ushirika na Masoko ni muhimu kumkomboa mkulima na kwa hiyo, tuipe meno. Waziri muhusika tumpe silaha. Tumpe mwavuli, Bodi za mazao ziwe chini yake. Madaraka ya fedha za *STABEX* yawe chini yake. Mpango wa kuendeleza mpango wa masoko uwe chini yake na apewe bajeti ya kutosha. Ndiyo baadaye tutamwuliza amefanya kazi ipi. Vinginevyo tutaendelea kuamini katika kila kitu na kwa hivyo, tutakuwa hatuamini katika chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru na mimi kwa kunipa nafasi nichangie kwenye hoja iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Naomba nianze kwa kuungana na wenzangu kutoa pole kwa Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kumpoteza Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Capt. Thedeos Kasapira, tunamwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amina*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii ambayo sasa tunajadili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie katika maeneo machache sana. Nitakwenda moja kwa moja katika zao la korosho. Katika eneo hili, naomba nianze

kuishukuru Bodi ya Korosho kwa bidii yao iliyopelekea kupata wawekezaji katika viwanda saba vya korosho hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata watu wa kuchukua viwanda vile inaweza kuwa ni ukombozi mkubwa kwa Wananchi wenye maeneo ambayo viwanda vile visto. Kwa sababu ni wazi kwamba, watapata ajira na hii itasaidia kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nina mashaka, mashaka yangu ni kama kweli hawa waliopewa viwanda hivi wataweza kufanya kazi bila ya msaada mkubwa wa Serikali. Kwa bahati mbaya korosho ni zao ambalo halina kipingamizi kupeleka nje. Mazao kama pamba, kahawa, pareto, katani ni lazima kwanza waya-*process* hapa ndiyo yapelekwe nje, kisheria kabisa. Lakini korosho inaruhusiwa kwenda kama lilivyo. Inawezekana kukawa na ushindani mkubwa sana kati ya wale wanaopeleka korosho na hawa wabanguaji wa hapa nchini, itafika mahali watashindwa kufanya hiyo kazi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na mpango wa makusudi wa kuwasaidia hawa wazawa wenye viwanda waweze kumudu ushindani huo, waweze kupata uwezo wa kupata mitaji mikubwa, wawekewe taratibu ambazo wao wanaweza kupata korosho za kuwasaidia kufanya kazi hivyo viwanda, vinginevyo watapewa viwanda lakini watashindwa kuinua korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu vilevile uzingatie maslahi ya wakulima kwa maana kwamba, huu mpango usije ukawaumiza wakulima. Lakini nasema lazima wasaidiwe. Nashangaa tunapiga kelele kila siku kwamba ni vizuri bidhaa ziongezewe thamani hapa nchini, lakini korosho haizungumziwi katika hilo! Lazima ipelekwe nje ikiwa ghafi na kuwapatia ajira watu wa nchi nyingine hasa India ambako mara nyingi zinaenda huko.

Juzi Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, alikuwa anazungumzia suala la magogo hapa, akasema amepiga marufuku ili tuongeze ajira hapa nchini, iongeze thamani. Naomba Serikali ifikirie zao la korosho, inafikiria nini, kwa nini lazima iende ghafi tu isilazimishwe kufanyiwa *process* hapa nchini ili kutuongezea ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu pembejeo za korosho. Dawa ya *sulphur* hapa nchini mwagizaji ni mmoja na ni yeye tu anaruhusiwa kuagizia hiyo *sulphur*, matokeo yake ni kwamba, hakuna ushindani. Anapanga bei atakavyo yeye na hivi leo *sulphur* hakuna wakati Wananchi wanaihitaji. (*Makofsi*)

Ni kweli, Serikali imezia kufanya biashara, lakini jukumu la kuhakikisha kwamba, pembejeo zipo ni la Serikali. Haliwezi kuwa jukumu la mtu mmoja. Nilikuwa nashauri Serikali iangalie uwezekano wa Bodi ya Korosho kuwa ama mratibu au msimamizi wa uagizaji wa *sulphur* hapa nchini. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kwamba, nilikuwa naomba Bodi ya Korosho iwe mratibu na msimamizi wa kuagizia *sulphur* nchini ili ihakikishe kwamba,

bei inakuwa ya kumudu. Lakini vilevile kuhakikisha kwamba, *sulphur* inapatikana kama inavyotakiwa. Lakini hata ukienda nje ukitaka *sulphur* utaambiwa nenda Dar es Salaam kanunue kwa fulani. Hiyo kweli siyo haki. Inampa uwezo yeze kupanga bei anavyotaka mwenyewe, huo si ushindani wa kibashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho lina bahati mbaya. Kuna programu nyingi tu za kuendeleza mazao mbalimbali, lakini hakuna programu inayoleweka ya kulinuuza zao la korosho. Mikoa ya Lindi na Mtwara, mikoa ambayo inalima korosho nyingi, yako maeneo mengi ambayo yanaweza kupandwa mikorosho mipy. Serikali ingefanya jitihada ya kutafuta fedha tukawa na programu kubwa ya kupanda mikorosho mingi katika mikoa ile. Mikorosho mingi ilibaki porini wakati wa operesheni vijiji, imekufa. Maeneo tunayo mazuri, makubwa lakini uwezo wa Wananchi wenyewe ni mdogo na Bodi haina uwezo, naamini kwamba, Bodi ni nzuri, Watendaji wazuri, wana uwezo wa kuliinua zao la korosho na kulilettea Taifa fedha nyingi za kigeni. Naomba Serikali itazame uwezekano wa kuipa Wizara hii fedha maalum kwa ajili ya kuliendeleza zao la korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kuomba au kutaka kujua nini sababu za msingi za kuweka mpango wa kuendeleza soko kuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nini sababu za msingi? (*Makofi*)

Wizara hii ina kazi kubwa kabisa ya kujenga uchumi wetu. Maeneo muhimu wanapewa watu wengine na wala sina hakika kama Waziri ana kauli gani katika Kitengo hiki. Kwa sababu kiko chini ya bosi wake. Hawezi kumhimiza, hawezi kumwelekeza. Ninaamini kwamba, lazima kirudi chini ya Wizara Kitengo hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri katika hili naomba maelezo mazuri. Najua wewe maneno mazuri huna, lakini mwenye nayo namjua. Itabidi umwulize huyo mwenye maelezo akupe ya kutosha ili jioni tuelewane vizuri hapa. Ni kweli kabisa tunapoamini jambo, tunapomwamini mtu wa kazi fulani, tumpe kazi ile afanye. Unapotoa ni kunyofoa vitu, picha ile kwa watu wengine inamvunjia hadhi huyo uliyemwamini. (*Makofi*)

Mimi nasimama, asema aah! Mheshimiwa Balozi George Kahama amechoka, vitu vingine tumechukua tumeweka pembeni. Nani atabisha? Unamharibia, nasema Waziri wa Wizara hii ni Waziri mzoefu kuliko Mawaziri wote katika Baraza la Mawaziri. Hawezi kushindwa kuusimamia mpango huu kwa namna yoyote ile. Anao Watendaji wazuri, hawawezi kushindwa kusimamia mpango huu. Lakini hawajapewa nasema, mimi ninaomba sana, makof hayo ni kwa ajili ya kauli ya wengi. Tupate maelezo ya kutosha kabisa, sababu za msingi na kama tutazikubali tuambiwe ni lini Kitengo hiki kitarudi kuwa chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la Bodi za Mazao. Bado uko utata kati ya Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Ushirika na Masoko. Mimi nilidhani Bodi za Mazao zote zingekuwa chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko, Kilimo wana mambo mengi, wala hawayawezi. Wanabeba mzigo mwangi kwa watu wengine. Juzi hapa Wizara ya Kilimo na Chakula, ilikuwa tabu kwenye bajeti yao kutohakana na mambo

mengi yaliyokuwepo. Punguzeni mambo haya, muwape wenyewe wafanye. Lakini mahali pakiingia rupia pana udhia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupate maelezo vilevile ni muhimu kufanya Bodi za Mazao ziwe chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula badala ya Wizara ya Ushirika na Masoko ambayo hasa ndiyo inayoshughulikia masuala ya masoko na mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ulinipendelea, naomba yule mwenye nafasi yake asikose. Nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ROBERT K. MASHALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Kabla ya mchango wangu, niungane na wenzangu kutoa salamu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, lakini vilevile nitoe salamu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mungu alitoa na Mungu ametwaa, jina lake libarikiwe.

Naomba nianze kuipongeza Bodi ya Pamba Tanzania, kwa mchango wake mkubwa sana wa kueneza zao la pamba. Kazi iliyofanywa na Bodi ya Pamba ni kubwa. Uzalishaji ambao umefanyika mwaka huu ni mkubwa sana unaleta matumaini. Tumetoka kwenye uzalishaji wa tani 140,000 mpaka sasa tuna tani 250,000. Kwa hiyo, ni asilimia 80 ya mafanikio. (*Makofi*)

Pamoja na uzalishaji huu kuwa wa msingi na kwamba Watanzania wamepokea kweli ushauri wa wataalam wetu wa Bodi ya Pamba, lakini kama hatutaimarisha vyama vyta ushirika, juhudhi hizi ni bure. Vyama vyta ushirika mpaka sasa vinaonekana kusuasua sana na kusuasua kwa vyama vyta ushirika ndiyo vinapelekea wakulima wetu wanyanyaswe na wanunuzi binafsi. Mfano hai, ni pale wanunuzi walipoamua kuteremshiwa bei ya pamba, wanunuzi walikubaliana kwa makusudi kabisa, wakakutana Mjini Mwanza tarehe 13 Julai, 2004 na matokeo ya m Kutano wao huo ni kuteremsha bei ya pamba kutoka Sh.300/= kwa kilo ya pamba *AR* mpaka Sh.250/=. Hii inaonyesha jinsi gani wenzetu wanunuzi binafsi ambavyo lengo lao kubwa ni kujilimbikizia faida kuliko kutoa huduma kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2002 Serikali iliandaa Sera ya kuimarisha ushirika. Lakini mpaka sasa ushirika nchini bado una matatizo mengi. Moja ya matatizo ambayo kwa kweli vyama vyetu vyta ushirika vinayo ni pamoja na kutokwa na mitaji ya kutosha. Lingine ni upatikanaji wa mikopo ni mgumu sana na inapatikana kwa masharti magumu. Ikiwa ni pamoja na kupangiwa bei na wakopeshaji. Kitu ambacho kwa kweli kinaathiri sana vyama vyetu vyta ushirika. Lingine ni ushindani wa soko ambao hauzingatii Sheria. Unakuta wanunuzi binafsi hata hawana vituo. Wanaamua kununua, mfano wanafuata hata majumbani, hata ule ubora wa mazao sasa unakuwa ni mdogo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishajitoa kwenye biashara ya mazao, lakini inabaki kama mdhibiti. Hali hii Serikali imeshindwa kudhibiti na hasa pale wanunuzi

walipofanya makubaliano ya kuteremsha bei ya pamba, Serikali ilikuwepo na haikusema lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze tu tamko ambalo limetolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu kupanda tena kwa bei ya pamba kutoka Sh. 250/= sasa ni Sh. 275/=. Tamko hili limechelewa, wakulima wetu wameathirika. Serikali ingepaswa itoe tamko hili mara tu baada ya bei kuteremka hivi Wizara ya Ushirika na Masoko ilikuwa wapi mpaka ikafika mahali Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja wakapiga kelele ndiyo matokeo yake bei tena imepanda. (*Makofi*)

Hivi yawezekana pengine kweli kama ni mwamvuli sasa askari wa mwamvuli huyu bado hajapata kiwanja cha kutua anahangaika hewani. Pamoja na matatizo haya, Wizara imeshindwa kabisa kuviimarisha vyama vya ushirika. Vyama vya Ushirika vingi havina uhakika wa kujiendesha. Lakini hata masoko ya uhakika hayapo. Wizara ya Ushirika na Masoko kazi yake ni kutafuta masoko kumhakikishia mwanaushirika kwamba, kile anachozalisha kinakuwa na soko la uhakika. Lakini sasa leo msemaji mkuu wa masoko wamekuwa wanunuzi binafsi, hata baada ya kuteremsha bei wanunuzi binafsi ndiyo wamekuwa wakitangaza kila leo kwenye vyombo vya habari mwenendo wa bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2002, Serikali iliamua kuimarisha ushirika na moja ya jitihada zake za kuimarisha ushirika iliamua hata kuwatoa viongozi wa ushirika ambao ilidhani ni tatizo katika maendeleo ya ushirika. Mfano Serikali iliwaondoa Viongozi wa CChama cha Ushirika cha *SHIRECU* Mkoo wa Shinyanga na mpaka ikapeleka na menejimenti na hivi ninavyozungumza, Ushirika wa Shinyanga una menejimenti mpya ambayo inaongozwa na Watendaji wa Serikali. Hali ya ushirika wa Shinyanga kwa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoo wa Shinyanga (*SHIRECU*), ni mbaya. Hivi ninavyozungumza, Wafanyakazi wa *SHIRECU* hawajalipwa miezi 17. Sijui Serikali inasema nini? Ushirika wa *SHIRECU* sasa unakufa chini ya mikono ya Serikali, kwa sababu Watendaji Wakuu ni wa Serikali. (*Makofi*)

Serikali naomba leo itamke inawasaidia vipi Watendaji hao wa Chama Kikuu, wafanyakazi ambao hawajalipwa? Vilevile tatizo la *SHIRECU* ni kubwa sana kwa sababu *SHIRECU* ina watumishi wengi kiasi kwamba, inajiendesha kwa hasara na Serikali ilitoa ushauri kwamba, *SHIRECU* ipunguze watumishi. Lakini kazi kubwa kwa *SHIRECU* kupunguza watumishi ni kwamba, haina fedha ya kuwalipa watumishi watakaopunguzwa. Naomba tamko la Serikali, inakisaidia vipi chama hiki ili kipate uwezo wa kuwalipa watumishi hawa ambao watapunguzwa na hatimaye iweze kujiendesha kwa faida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linavikabili vyama vyetu vya ushirika, ni ukaguzi hafifu kwenye vyama vyetu vya ushirika na hasa vya msingi. Vyama vya ushirika vya msingi havina wakaguzi kabisa. Mfano hai ni Wilaya yangu ya Bukombe yenye vyama vya msingi zaidi ya 120, ina Maafisa Ushirika wawili tu. Mwaka 2002 Serikali ilitangaza nafasi 300 za Maafisa Ushirika ili waweze kuziba mapengo yaliyoko, lakini hao Maafisa Ushirika sijui walienda wapi, mimi sijawaona. Kitu ambacho

kinasababisha kwa kweli hujuma kubwa sana kwa vyama vyetu vya ushirika. Kazi ya Afisa Ushirika ni kuzuia hujuma kwenye vyama vya ushirika. Lakini sasa wamekuwa wakisubiri mpaka mwisho wa mahesabu ya mwaka ndiyo wanatoa taarifa, kama ni hujuma tayari ilishafanyika. Kwa hiyo, Serikali naiomba ijitahidi sana kuhakikisha kwamba, imeajiri watendaji wengine wa ushirika kwa maana ya Maafisa Ushirika ili waweze kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vyama vyetu vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imesikia kilio cha wakulima wa pamba na pamba imeongezwa bei, nadhani mchango wangu umepungua. Ninaiomba Serikali isimamie kwa ukaribu sana utekelezaji wa zoezi hili ili Wbananchi ambao watafuatilia haki zao basi wasipate matatizo tena ya kunyanyaswa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. Mheshimiwa Jacob Shibili na Mheshimiwa Leonard Derefa, wajiandae. Bunge linasitishwa.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Bunge lilirudia*)

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia za Waheshimiwa wenzetu waliotutangulia mbele ya haki na namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote wawili mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyoweza kumtuma Mtumishi wake, Baba Paroko wa Kiwanja cha Ndege, kuja kutoa neno la Mungu siku ya kumuaga mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Capt. James Kasapira. Kwa kweli Mwenyezi Mungu alimwezesha na akanena neno la Mungu ambalo limetusaidia sana sisi Wabunge ambao tumebakwi wakiwa, namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo mpaka sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Wizara ya Ushirika na Masoko sina matatizo nayo, bado nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayoifanya ya kufufua ushirika ambao ni kitu kilichokuwa kimeisha kabisa lakini picha inayoonekana sasa hivi ushirika umeanza kufufuka. Kwa hiyo, nampongeza sana na nina

imani naye kubwa sana. Matatizo yapo lakini matatizo yako wapi tutayaelekeza kwake lakini siyo yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la bei ya Pamba. Katika bei ya pamba nitaihusisha Bodi ya Pamba. Katika Bodi ya Pamba nitaihusisha Wizara ya Kilimo na Chakula. Ni masikitiko makubwa mno kwa kitendo kilichofanyika kwa wakulima wa zao la pamba katika msimu huu. Serikali imejitoa baada ya hotuba au ya tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa leo inaonekana kwamba bei ya shilingi 300/= haikupangwa na Serikali. Ni picha ya ajabu na imesononesha watu. Bodi ya Pamba ilisema kwamba bei itaanzia shilingi 300/= sio chini ya shilingi 300/=.

Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yako, Vyama vya Ushirika kwa mara ya kwanza Vyama vimeweza kupata pamba nyingi kuliko mfululizo wa miaka mitatu iliyopita. Watu wamehamasika, wamepeleka pamba kwenye vyama vyao vya Ushirika wiki ya kwanza kuanzia tarehe 21 na kuendelea yaani kufikia Ijumaa kwa Vyama vya Ushirika vya Mkoa wa Mwanza na Wilaya ya Biharamulo, Mwanza kulikuwa na kilogramu 4,900,000, Biharamulo ilikuwa kwenye kilogramu milioni 2, *SHIRECU* sina hakika nayo. Wiki ya pili, *NYANZA* ilikuwa na kilogramu milioni 11, *BCU* ilikuwa kwenye kilogramu milioni 4, *SHIRECU* sikupata taarifa zao.

Wiki ya tatu ambapo Bodi ya Pamba na wanunuzi *TCA* walikaa Mwanza hawakutamka kwamba bei imeteremka Vyama vya Ushirika vimeendelea kupokea pamba kwa shilingi 300/=. Sasa kwa hali hiyo ni lini bei ya shilingi 275/= itaanza, kwa Vyama vya Ushirika ni shida sana! Inakuwa ni kazi ngumu kupambanua waanzie wapi hao kwa sababu tamko la kuteremka kwa bei ndio leo tulikuwa hatujapata tamko lolote la kuteremka kwa bei.

Ombi kubwa sana kwa Serikali kwa niaba ya walima pamba wote kwa kweli mimi bei ya shilingi 275/= nimeipokea kwa shingo upande, kwa kweli sikurudihika. Naiomba Serikali kama inaweza kwa sababu wao ndio walikuwa waanzilishi wa bei hiyo ya shilingi 300/= waubebe mzigo huo na waendelee kulipa kwa shilingi 300/=. Kwa kweli mimi nitafurahi sana kama Serikali inaweza kurekebisha na kufanya hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bei ya soko la dunia kuteremka kufikia shilingi 250/= bado mnunuzi amebana kwenye matumizi yake akatoa shilingi 10/= akaongezea hapo, *Council* shilingi 5/=, elimu shilingi 5/=, mbegu shilingi 3/= na Bodi shilingi 2/=. Kwa hiyo, ukijumlisha hapa kuna kama shilingi 15/= ambazo zimetoka kwenye mikono ya mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi walima pamba wana hali mbaya kweli shilingi 300/= hana faida kwa sababu wanalima hawaangalii gharama zingine. Ukiingia kwa kina zaidi yaani hapo hana faida ni hasara, kumpa shilingi 300/= ni hasara lakini bado tena unamteremshia zaidi ya hapo. Hivi wanaolima zao la pamba wana makosa gani kwa Mungu? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Waziri wa Ushirika na Masoko hana matatizo, Bodi ya Pamba ina matatizo makubwa sana. Hata tukirudi nyuma kuanzia mwaka 1976 Vyama vya Ushirika vilipovunjwa, Mamlaka ya Pamba ndiye aliyechukua madaraka ya kubeba mali ya wanaushirika mpaka mwaka 1984 ndio akarudisha. Kwa hiyo, inatukumbusha mambo mengi mabaya ambayo tumeweza kufanyiwa na hawa watu. Bado kwenye mbegu, ni miaka miwili imepata hapa tumelalamikia suala la mbegu, hazioti, tumepewa za namna ipi, ikafika mahali tukasema haya. Kwenye bei tumeanzia shilingi 300/= wameteremsha wanetuachia wenyewe tungeweza kufanya kazi hiyo. Waziri wa Ushirika, nia kubwa ya kufufua ushirika unayo lakini baadhi ya watu Serikalini hawataki ufufue ushirika. Kama labda wangeona hakuna sababu wasingekupa Wizara hiyo, uwezo wa kufufua ushirika unao lakini hawataki kukupa nyenzo ili uweze kufanya kazi. Kwa kweli zao la pamba linachezewa visivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaokaa ni Bodi ya Pamba, ni *TCA* wanaihusisha kidogo na Wizara yetu ya Ushirika, Vyama vya Ushirika havihuishi kwenye kupanga mambo yote haya. Bila Vyama vya Ushirika umaskini utakuwa mkubwa zaidi nawahakikishieni ndugu zangu Wabunge. Ushirika ndio unao-*touch* zaidi kwa mtu maskini, Bodi ya Pamba bado inafanyabiashara. Pamba yote ya Mashariki yaani Dar es Salaam, Morogoro, Tanga inanunuliwa na Bodi ya Pamba ina maana hakuna wanunuizi binafsi ambao wanaweza kununua Pamba hiyo? Hakuna uwezekano wa kuungana wana ushirika katika Mikoa hiyo ya Pwani, Morogoro na Tanga?

Kwa nini Bodi ya Pamba anaingilia kufanyabiashara hiyo wakati Serikali kazi yake ni kusimamia? Nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, wana ushirika bado wako wengi sana, Morogoro, Pwani, Tanga wahuishwe kwenye shughuli yao wafanye wao wenyewe sio Bodi ya Pamba kazi yao wasimamie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu katika suala zima la jinsi Bodi ya Pamba ilivyokaa. Bodi ya Pamba ihamishwe iliko irudishwe kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko waweze kufanya kazi. Pindi watakaporudishwa huko Mheshimiwa Waziri usiwe na huruma ufanye *overhauling* kubwa zaidi ili angalau ikae katika mkao wa kufanya kazi, kuna watu wamezoea kuvuruga. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa nigusie mambo machache sana ili Wizara yetu ya Ushirika iweze kuimarika vizuri zaidi. Wizara ya Ushirika haina mamlaka na Maafisa Ushirika wa Wilaya na Mikoa kiutawala wako chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo, katika mpango wa mageuzi haya ili angalau twende kwenye utaratibu mzuri utakuwa na kazi ngumu zaidi kuteremka mpaka chini kwa sababu hawana madaraka nao. Naomba kama inawezekana basi sera hiyo isitishwe na baadaye wawe na madaraka kuanzia kwa Waziri mpaka kwenye Wilaya ili kazi iweze kwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, ushirika kwa mujibu wa kanuni na misingi ni chombo huru. Katika sheria mpya ya mwaka 2003, naiomba Wizara ijiepushe kuingilia Vyama vya Ushirika, waviache vifanye shughuli zao kwa uhuru. Wanaushirika wahuishwe katika uandaaji wa kanuni zao. Ni juzi tu tumepitisha sheria hapa zinazofuata ni kanuni lakini wanaushirika wengi hawakuhusishwa zaidi katika kuona

mambo hayo. Kwa hiyo, ni vema wakahuishwa ili mambo yaweze kwenda vizuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu za uchumi zinazotolewa mara kwa mara, hakuna takwimu zinazoonyesha mchango wa Vyama vya Ushirika katika Pato la Taifa. Kwa hiyo, ni vema pato la wanaushirika nao likaonyeshwe kwenye Pato la Taifa ili kwenye jamii ushirika uonekane unachangia nini. Ni vema ikawekwa kitu cha namna hiyo ili na wao waweze kuonekana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Kamati ya Rais ya kumshauri kuhusu kuendeleza ushirika nchini, kuna mambo mbalimbali ambayo yalijitokeza, Mheshimiwa Waziri anayafahamu. Kuna mali za wanaushirika baada ya kuvunjwa mwaka 1976, takwimu tumekwishazipeleka kwenye Wizara, ni shilingi ngapi, Serikali inasema nini? Naomba angalau leo basi wanaushirika waweze kusikia mali zao hizo zinalipwaje na Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003 hajatangazwa rasmi na kuanza kutumika. Itakapoanza kutumika kwa sababu sheria iliyopita kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika walikuwa wanahitaji kusiwe na chini ya wanachama kati ya 20 au 10 lakini katika sheria hii ni 50. Sasa ni vema kuwepo na mpito vinginevyo hatutabaki na Chama cha Ushirika chochote kile. Kuwe na mpito, vinginevyo mkivikatisha hivi namna ya kuiendeleta itakuwa ni kazi moja ngumu, muwaelekeze katika kuwasukuma ili waweze ku-*takeoff* halafu baadaye waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Vyama vya Ushirika vimejitokeza kikamilifu katika kununua mashirika ya umma yaliyobinafsishwa, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, alizungumzia, *TFC, KDCU* na *KNCU* wameamua na wametimiza masharti ya kununua *TANICA* bado kuna mizunguko mbalimbali. Napenda nieleze kuwa hapa maana hapa tayari kuna mitaji yao imebaki kule wanapata hasara hawa zaidi ya mwaka mmoja sasa ununuzi hapa umekuwaje, ubinafsishaji wa *TANICA* umekuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kipindi kifupi mno ambacho amekaa kwenye Wizara hiyo lakini baadhi ya mashirika au taasisi zilizo chini yake zinaonyesha kazi inaenda vizuri zaidi tukianzia na Chuo cha Ushirika Moshi mpaka kuja kufikia kuwa Chuo Kikuu ni kazi yako Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kazi hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofî*)

MHE. LEONARD N. DEREGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja hii iliyo mbele yetu.

Kwanza napenda nitoe pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego pamoja na wananchi wa Jimbo lake. Vile vile napenda nitoe pole sana kwa

familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, pamoja na wananchi wa Jimbo lake na naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba naunga mkono hoja iliyombele yetu na naomba nitoe ushauri ufuatao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu ushirika ndio mkombozi wa wanyonge, tukiwa pamoja tunaweza kuwa na nguvu zaidi kuliko tukisambaratika. Napenda niishauri Serikali kwamba bila ushirika kwa kweli wakulima wetu watahanganya sana na mpaka sasa hivi wanayo mahangaiko makubwa sana. Kwa kweli tukitaka kuwasheshimu watu waliotuweka hapa lazima tuhakikishe kabisa ushirika huu ambao ndio wa watu wengi, ndio wa wakulima tunaweka mikakati mizuri.

Mimi nimekuwa nikisema hapa kwamba *principles* za ushirika zinaeleweka. Ukioma kwenye ushirika kuna ile *Rochdale Principle* yaani ushirika unavyotakiwa kuwa lakini hapa Tanzania inavyoonekana tumechanganya mambo na sidhani kama kwa kweli tutafika tunapokwenda sababu ushirika na *private enterprise* (watu binafsi) ni kama kuchanganya mbuzi na fisi, mmoja lazima ataliwa. Hiyo ndio principle ya ushirika sababu wanatofautiana katika *interest*, mfanyakia biashara anataka apate faida ushirika unataka uhudumie wakulima lakini hapa *principally* ushirika tumerudisha lakini tumerudisha kwa kuchanganya mambo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi huwa nasema kwamba Tanzania tunalo kosa kubwa la kutojua kwa nini tumeshindwa mahali. Kitu tunapoona kwamba kimeshindikana badala yake *solution* tunafikiri labda ni kubinafsisha lakini lazima tuwe tunajifunza kwa nini kwa mfano ushirika tuliokuwa nao ulishindwa? Tungekuwa tunafanya *research* na kuona mapungufu yaliyotufanya tushindwe ndio tunayarekebisha lakini tunaposhindwa tunaamua labda ibinafsishwe halafu tulete mambo mengine, kwa kweli ni tatizo kubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la pamba, bahati nzuri mimi nimewahi kufanya kazi *Lint and Seeds Marketing Board*, Bodi ya Pamba ile ya wakoloni, halafu mwaka 1973 ikawa-reorganized ikawa Mamlaka ya Pamba vile vile nimefanya kazi kwenye *cooperatives*, matatizo ya zao la pamba ni makubwa sana na nilishangaa walipoingia hata watu binafsi kwenye pamba. Mkitazama baadhi ya watu waliongibia kwenye biashara ya zao la pamba ile *integrity* yao ukiipima unakuta kwamba baadaye kuna mapungufu makubwa sana.

Niliwahi kuuliza kwenye mikutano wakaniambia kwamba hawa watu wanafanya *study* lakini biashara ya pamba kwa kawaida inakuwa nzuri halafu baadaye inaharibika. Ninaamini kabisa bei ya zao la pamba Kimataifa inapoteremka lazima wale watu ambao wamejiingiza kwenye biashara hiyo lazima watapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa katika zao la pamba ni namna tunavyolihudumia na tatizo kubwa kabisa liko kwenye *financing*. Hapo nyuma wenzetu wakoloni waliweka utaratibu mzuri lakini baadaye tulipokuja tuka-*temper* nao na

baadaye ikaonekana tunapata matatizo. Wakati wa *Lint and Seed Marketing Board* bei inapokuwa nzuri zile hela zinawekwa kwenye *Price Stabilization Fund* lakini bahati mbaya tulipojitawala tukasema kwamba Serikali kwa kuwa ndio imekuwa ina nguvu hela hizi zikitumika. Wakati ule nakumbuka kulikuwa na *26 milioni Sterling Pound* ambazo zilikuwa zimewekwa kwenye *Moscow Narrobin Bank London* ni *Merchant Bank* ambayo huwezi kusema kwamba inaweza kafilisika hata siku moja, nafikiri imeanza kwenye *Century* ya 14 au 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhi kusema hapa makosa tunayafanya sisi wenyewe halafu tunakuja tunashangaa. Tumeuza Mabenki yetu, tumeuza hela sababu fedha ni kitendea kazi ambacho kinaleta maendeleo lakini tumebinafsisha benki kwa watu wengine.

Sasa hivi nakwambia tatizo kubwa kabisa, hela zilizopo hata kwenye *CRDB* ambao wana-*finance*, hazitoshi. Benki yetu ambayo ilikuwa inatusaidia tumeiuza badala ya kutafuta kuna matatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nasema ni kichekesho, *we are talking about a starting another bank* wakati hizi *bank* tulikuwa nazo, hivi, samahani Mwenyekiti naweza kusema maneno Waheshimiwa Wabunge wakafikiri nimewatukana lakini nafikiri kuna *u-craziness* sababu hizi Benki tulikuwa nazo, tulikuwa na *Tanzania Rural Development Bank* halafu tumeuza zote, sisi tumeishauri Serikali kwamba *National Microfinance* tuibadilishe angalau sasa ihudumie watu hawa. Wakati Waziri amesema kwamba *we are making a feasibility study* ya kuanzisha benki, huo sio wehu, sio wehu ule, benki si tunayo, kwa nini *tusii-convent* ile *bank* ikawa ndio benki labda hata ya *cooperatives* sababu vitu hivi vipo.

Nafikiri tunachezea hela za walipa kodi kwa nini tumpe mtu mwingine afanye *study* ya kuanzisha benki na hizi benki tulikuwa nazo? Kwa nini hatukusoma, kwa nini kwa mfano *Tanzania Rural Development Bank* ambayo ilikuwa ina-*finance* badala yake tukaamua kuiiza? *CRDB Bank Limited* tumeiuza, *National Bank of Commerce* tumeiuza halafu leo tena mtu anasema tunatoa hela za kununua *feasibility study* ya *bank*, *is that not craziness? No, that is craziness*, ule ni wehu wa aina yake. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri lazima sasa hivi tuweke mikakati, tukubaliane kwamba kama hela hizo hazijalipwa kufanya hiyo *feasibility study*, basi *NMB* iwe ndio benki yetu na kwa bahati nzuri ina mtandao kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazao ya Serikali, Serikali inapenda ipate hela za wakulima. Mimi nakumbuka mazao ya Serikali ni pamba, korosho, katani, kahawa, chai, pareto lakini sasa hivi naona pareto imekufa.

MBUNGE FULANI: Na karafuu.

MHE. LEONARD N. DEREFA: *Of course* Karafuu kule Zanzibar lakini sisi huku mazao ya Serikali yalikuwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikukumbushe kwamba Waingereza kabla hawajaondoka hapa walikuwa na *Director of Agriculture*, walikuwa nao hawa watatu. Mmoja alikuwa anakaa Mwanza, Mr. Gibbons kwa ajili ya *ku-supervise the cotton production in the Lake Zone, coffee in Bukoba* pamoja na chai kule Bukoba. Mwingine alikuwa anakaa Tanga, *to supervise sisal production in the Coast*, korosho na katani na mwingine ambaye ni mkubwa wao alikuwa anakaa Dar es Salaam lakini kazi yake ilikuwa ni *ku-supervise sisal production in the Coast* pamoja na korosho lakini sasa unajiuliza kwamba hivi Serikali haya mazao yakifa leo tutakuwa wapi? Hii *foreign currency* ya nchi hii mtaitoa wapi? Tunajua sasa hivi tuna madini lakini na sheria za madini na zenyewe ni za kipuuzipuuzi, sasa mimi sijui. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hautoshi lakini napenda niongelee suala moja, leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametangaza bei mpya na bahati nzuri wakati tuko kwenye mkutano nilimweleza kwamba sisi kule Shinyanga pamoja na kwamba hapa ni Kitaifa lakini sisi Mkoa wa Shinyanga tulikuwa tumekubaliana tangu mwaka 1984 kwamba wakulima walikubali ni principle na wala sio wakulima tu na wengine hata wafanyabiashara wachangie Mfuko wa Elimu na umetusaidia kujenga shule.

Kama mnavyofahamu taarifa zote za elimu zinaoonyesha kabisa Shinyanga sisi tuko nyuma sana lakini leo hii amefuta Bodi ya Elimu na nilimwambia kabisa zile shilingi 5/= ambazo wakulima tumekubaliana usiziguse lakini leo alivyotangaza hapa ni kama amefuta sababu amezitoa zile hela zote.

Mimi nilimwambia na hata Waheshimiwa Wabunge wenzangu niliwaambia na nilimwomba kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu usishike hizi sababu kuna Walimu ambao wanalipwa na hizi hela, halafu kuna *Secondary School* ambazo zinaendeshwa na mfuko huu na kuna hata *Contractors* ambao wanadai kwa ajili ya kujenga *secondary school*.

Kitendo cha kufuta leo hapa nafikiri sisi Wabunge wa Shinyanga tungelia badala ya kucheklea sababu sisi kama mnavyofahamu tuko nyuma sana, hatuna shule nyingi ni Mfuko huu wa Elimu umetuwezesha kujenga *secondary school* ili kusudi na sisi tujitahidi kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda niseme kwamba *system* ya *procurement* lazima uwekewe utaratibu. Hawa watu wa benki wanaokuja kufanya biashara hapa lazima wakubaliane na masharti. Zamani wakulima walikuwa wanakopa hela kwa kutumia *Letter of Hypothecation*, kwa kutumia *Maximum Liability Certificate* pamoja na *Insurance Cover Note* unakwenda Benki unakopa leo hii hawa watu tunaowapa leseni ya kufanya biashara ya benki hapa kwa nini hivi hawavifanyi. Zamani kulikuwa na *private banks* lakini walikuwa wanakubaliana na sheria hizi leo tatizo hili limekuwa gumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda nieleze kwamba lazima tujifunze kutoka India. Wahindi wana sheria kwamba 5% ya *all deposits* kwenye *Commercial*

Banks lazima ziwe directed kwenye Land Bank ama kwenye cooperatives kusudi zikopeshwe kwa wakulima at a very low interest rate. Hii ingetusaidia sana na naamini kabisa ile *feasibility study* ya bank ambayo mnaifanya sasa hivi haya mawazo yawekwe mle. Napenda niseme kwamba mimi kwa kweli siungi mkono kwamba tuanzishe another bank, tutoe hela kwa watu, haya matatizo yapo na yanajulikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umechemsha lakini napenda kusema kwamba kwa kweli watu tunaowaleta hapa kutufanya kazi sheria zetu lazima ziwe za kutusaidia sio za kututeketeza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa, naunga mkono hoja lakini muda wangu nafikiri umechemsha, vile vile nilifikiri niseme kwamba Bodi ya Pamba imefanya kazi nzuri sana matatizo hayakosekani, lakini wale watu bwana wamefanya kazi nzuri. Ukitazama kwenye *figure* sasa hivi ninaamini kabisa kwamba pamba imeongezeka kutohana na juhudhi zao. Tatizo hili la bei ni la wakubwa, *World Bank* na nini lakini ninaamini kabisa Bodi ya Pamba inajitahidi kufanya kazi hasa vijana waliopo sasa hivi mimi nawafahamu Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, wamekwenda karibu kila Jimbo ambalo linalima Pamba. Sasa lazima tuwapongeza kama kuna matatizo ya kushuka kwa bei hii lazima tueleze lakini kusema kweli Dr. Kabisa pamoja na uongozi wake amefanya kazi nzuri sana. Naamini kabisa mwaka huu pamba, mimi niko kwenye pamba, itakuwa nyingi zaidi. Mimi nilikisia marobota milioni moja wakanibishia, lakini kwa mwaka huu inawezekana kabisa wakafika zaidi ya laki tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. LYDIA T. BOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ili niweze kuungana na wenzangu kuchangia katika hoja ya Waziri iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nataka nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa jinsi wanavyojitahidi kuandaa mipango. Kama kawaada ninachoshauri ni kwamba wasimamie hiyo mipango ili iweze kutekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pole kwa kifo cha ndugu yetu Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, ambaye ametutoka tukiwa katika Bunge hili la Bajeti na Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipoingia humu Bungeni leo asubuhi niliandika mwenyewe kwa hiari yangu kikaratasi kutaka kuchangia, lakini aliposimama Waziri Mkuu jinsi alivyozungumza Kauli ya Serikali, amepitia kila eneo sijui alikuwa amefanya maandalizi ili Wizara hii tusiwe na maswali mengi au ni taratibu zipi. Lakini pamoja na kauli ya Serikali, mimi siwezi kujadili, nimeipokea vizuri sana ila nitakuwa na machache ya kuchangia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu zao la korosho. Zao la korosho katika nchi hii ni zao la pili katika kuingiza Pato la Taifa, lakini bado zao hili wakulima wanapata shida katika suala la uzalishaji. Wakulima sasa hivi wana shida ya

pembejeo kama *sulphur* na dawa ya kuzuia wadudu na mambo mengi tu. Sababu kubwa ambayo nataka niizungumzie kwa nini wanapata shida, mwaka 2003 nilipokuwa kwenye Bunge la Bajeti nilichangia kwamba Mkoa wa Mtwara umeingia ugonjwa, majani ya mikorosho yote yamewiva na kupukutika kabisa, hatima yake mikorosho ile haikuzaa. Walioweza kuzalisha korosho katika mashamba yao ni watu wachache. Halafu kwa mfululizo vipindi vitatu kumekuwa na ukame na uzalishaji ukawa mdogo. Sasa hivi *sulphur* bei ni ya juu na wakati huo huo hili zao linabidi lizalishwe. Linapozalishwa linasaidia Taifa lakini, je, Taifa linamsaidiae huyu mkulima au mkulima anafaidika nini na zao la korosho? Tunaona anafaidika kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba Serikali ijitahidi kuwaona wale watu wa Mkoa wa Mtwara na ikiwezekana wapatiwe *sulphur* kwa mkopo au kwa bei nafuu. Mimi sijui kama zoezi hilo lilifanyika, lakini kwa kuwa Waziri atasimama kufanya hitimisho la taarifa yake, nitapenda kusikia hatua zipi zilichukuliwa ili kuwaokoa wakulima wale ambao wana zao hilo la korosho. Mimi nataka niseme kwamba ni zao pekee ambalo mkulima wa Mkoa ule analitegemea kibiashara ukilinganisha na mazao mengine aliyonayo ambayo pia masoko hayana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana pia nikiwa hapa Bungeni niliuliza swalii kuhoji Serikali kuhusu mkopo katika Mfuko wa *STABEX*. Jibu lilikuwa kwamba mfuko huo sasa hivi haupo ulishasimamishwa kuanzia mwaka wa 2002. Lakini ukiangalia katika orodha ile hili zao la korosho liliachwa nje kabisa, halimo, lakini yapo mazao sina sababu ya kuyataja wenye wenye mazao wanajua, ambayo Mfuko huu ultumika vizuri sana, lakini zao la korosho halikuweza kuutumia Mfuko huu mpaka umesimamishwa.

Sasa je, mkulima huyu wa Mtwara anaachwa wapi na wakati huo huo narudia ndiye anayesaidia Taifa hili katika uzalishaji lakini mwenyewe anaishi katika mazingira magumu, anapalilia mashamba kwa mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nishukuru labda katika kupitia taarifa hii ya Waziri amesema kwamba sasa hivi kuna mpango wa Mfuko mwingine wa kukopesha wananchi na kutakuwa na Mikoa nane na Wilaya 36 ikiwemo na Mikoa hiyo ya Kusini. Sasa katika hilo nataka kushauri tuache tabia ya kuonyesha mgongo Mkoa wa Mtwara, badala yake tuangalie uso kule kwani wananchi wa Mtwara pia wanaitegemea Serikali ni ya wote.

Kwa hiyo, itakapokuwa inaanizishwa, basi kweli iwe kama ilivyoandikwa taarifa hii, anzisheni na kule katika Mkoa wa Mtwara kuliko kuanzisha Mikoa mingine, mnasema *pilot area*, wenzetu wanakwenda mbali, sisi bado tunabaki pale pale tumesimama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, safari hii huu Mfuko ni kweli muuanzishe mapema na ikiwezekana mwanzie Mkoa wa Mtwara kwa sababu kwa muda mrefu mmetuacha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo nashauri jambo moja, kuwe na Mfuko basi wa Taifa ambao utasaidia kwa sababu Mifuko mingine ina utata, lakini kuwe na Mfuko ambao utatambulika Kiserikali kwamba ni Mfuko wa wakulima wa Tanzania nzima ukiwemo na Mkoa wa Mtwara. Uwe na utaratibu mzuri na ukopeshaji kirahisi ili wale watu waweze kuwa na uhakika wanapata wapi kwa sababu sasa hivi tunavyoongea hapa katika kipindi hiki cha Bajeti ndio kipindi cha kuweka dawa ya *sulphur* katika mikorosho lakini tunaambiwa Mtwara hakuna *sulphur*. Ile ambayo walinunua haikutosha kulingana na hali ya ukwasi, pia kama nilivyoeleza kule nyuma, watapata wapi fedha za kununua *sulphur* na Serikali tunaiambia haitaki?

Kwa hiyo, sasa *sulphur* hawana, sijui hili nalo Waziri analifahamu na kama analifahamu atanishauri nini, jinsi gani wakulima wale wajikwamue kupata *sulphur* ya kuweza kusaidia mikorosho yao ambayo imesimama kwa sababu wataalam wanasema ukishapulizia mara moja basi, hakuna faida ya kupulizia. Inatakiwa uanze kupulizia tangu mwezi wa tano na upulizie mara nne au kama umekosa *sulphur* angalau mara tatu, lakini kwa taarifa nilizonazo wengine hawajapulizia kabisa na wengine wamepulizia mara moja moja. Hilo nalikabidhi mikononi mwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu akinamama kufanya biashara zao ndogo ndogo au kupata masoko. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mama Anna Mkapa, kwa jinsi anavyojitahidi kuwaunganisha akinamama, kuwaleta hata Dar es Salaam wapate mafunzo ya vitendo kuona jinsi gani wauze bidhaa zao. Lakini nataka niseme kwamba wanakuja wakati mwingine kutoka Mikoani kwa mazingira magumu, wengine hawatambuliki kabisa kupata fedha na wanahitaji waje wajifunze. Sasa hili nalo limekuwa ni gumu, lakini namshukuru tena yule mama kwa jinsi anavyojitahidi lakini naomba Serikali imwunge mkono, itoe maelekezo katika Mikoa au kwenye Wilaya, taratibu zifanyike za kuwatambua wale akinamama ambao wanakuja kuuza bidhaa zao hapa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama ndio wazalishaji, wengi wa akinamama ndio wanaolima mashamba ya nchi hii, lakini bado hatujawasaidia ipasavyo. Ukitosha kwenye makabarasha hayo wameandika vizuri sana, tutamkomboa mwanamke na tutamsaidia, kila sekta inamtaja mwanamke, lakini rudi ufanye tathmini huyu mwanamke anayezungumziwa wa Kijijiini na umwangalie anavyoishi kwa mazingira magumu. Lakini leo hapa tunazungumzia masoko kwamba huyu mwanamke vitu vile anavyozalisha anapata soko wapi? Tunaona bado hapati soko lolote kwa sababu tunavyotembea kule Vijijiini la kwanza ni kukwambia kwamba mimi nina bidhaa hii sijapata soko, mimi nina bidhaa hii, mimi nimetengeneza mikeka au nina mikorosho, sasa hivi soko liko wapi?

Tunaomba Serikali ituambie tatizo ni nini katika kuwawekea mazingira mazuri hawa wanawake wakafanye bidhaa sawa na malengo ambayo tunajiwekea ya kuwasaidia katika suala la uchumi badala ya kumwacha amebaki anazalisha lakini tatizo la mazingira ya masoko yanamatatiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia huko nyuma, kwa mfano, akinamama ambao wamejitokeza katika Mkoa wa Mtwara, kila Wilaya utakuta labda kuna vikundi mia mbili au mia moja hamsini kwamba wote wameamua kubangua korosho. Sasa hizi korosho tatizo kwanza ubanguaji na uandaaji mzuri, halafu *packing*. Hili nalo limezungumzwa ni mwaka wa nne sasa tumo ndani ya Bunge, sijajua jinsi gani akinamama wanawasaidia lakini taarifa ambazo mimi nimekuwa nikizisikia humu ndani utasikia kuna kikundi tulitoa mafunzo, sasa mwisho wa habari ni huo! Kikundi hicho kiko wapi na kinasaidia katika maeneo gani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki huduma kama matone, tunataka jumla yake kuu, watu watoke na bidhaa zao wafike mpaka Taifani mpaka nchi za nje. Japokuwa pia kufika nchi za nje kwao itakuwa ni tatizo kubwa tu maana Serikali yenye hapa ikisimama utasikia bidhaa haziwezi kwenda nchi za nje kwa sababu hazina ubora, hivi tunazungumza vitu gani? Ni nani sasa afanye bidhaa ziwe bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wameniuliza hivi Tanzania tuna wataalam au tuna wafanyakazi? Nimeshindwa kujibu swalî hilo. Kwa hiyo, kama wataalam wangekuwepo, wanasema wangekuwa wanashauri hili neno la kusema kwamba bidhaa sio bora lisingekuwepo. Wataalam hawa wana vyeti, wana shahada, lakini ni wafanyakazi, si wataalam wa kuweza kushauri au kuelekeza jambo lolote. Sasa hilo lianze kipindi hiki, tunachelewa, muda unatuacha na tuanze na akinamama, akinamama wanao uwezo wa kufanya kazi hizo kwa sababu wameshaonyesha njia, wameanza kupiga hatua ya kuandaa korosho kwa njia ya kienyeji tu, lakini zikikaa miezi miwili tayari zimeharibika. Sasa leo tuwasaidie *packing* yao iwe nzuri ili wapate masoko na korosho zao zisiharibike zikae kwa muda ili ziwafae. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Mtwara utawakuta akinamama wanatembeza korosho kwenye makapu, kwenye mifuko ya lambo, kwenye maboksi hawajui waende wapi, wanahangaika, wanapishana pishana na hili sio geni tumelizungumza kwa muda mrefu sana.

Sasa nina hakika Wizara ikikaa itapanga na *staff* yake ikiwa nzuri, wataweza kupata njia jinsi gani wawasaidie hawa akinamama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapowasaidia hawa akinamama na baraka utazipata kwa sababu akinamama ndio wazazi na ndio walezi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na machache ya kuzungumza. Nashukuru kwamba Waziri amenisikia na nilishamwambia anafanya kazi nzuri na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, anafanya kazi nzuri, anajibu maswali vizuri lakini katika haya niliyoongea bado. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko.

Kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapa pole wafiwa na wananchi wa Majimbo ya Mbeya Vijijini pamoja na Ulanga Mashariki. Tunawapa pole sana na sisi tunajipa pole, kwa kweli ni misiba ambayo ilituhusu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nasita kumpongeza Waziri wa Ushirika na Masoko. Nasita sana kwa sababu ya mambo ambayo nitayaeleza hapa. Wizara ya Ushirika na Masoko maana yake ni kushughulikia ushirika na masoko ya bidhaa zetu. Hiyo ndio hoja kamili katika Wizara hii.

Lakini kila mwaka tangu imeundwa Wizara hii sijaona ushirika hata uliokuwa umekomaa, sijaona namna gani unakwenda. Kila siku tunashuhudia unazidi kuzama, mimi natoka kwenye Mkao ambao ulikuwa na ushirika wenye nguvu sana, lakini sasa ushirika huo wa Mkao wa Shinyanga kwa maana ya SHIRECU umechemsha na umechemsha mpaka imeiva maana yake mpaka sasa afadhali na Nyanza, Nyanza imenunua karibu kilo milioni 17, SHIRECU haijafikisha hata milioni tano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuipa *guarantee* ya fedha lakini tuna tatizo hata la *management* pale. Kuna watu pale sijui walitoka wapi wameletwa pale kwenye ushirika wa Shinyanga. Hawajui hata mazingira, wamekwenda pale, hawana uchungu na SHIRECU. Kwa hiyo, mimi nafikiri hata hii *Care Take Committee* ya *Management* ya SHIRECU ni tatizo katika ushirika wa SHIRECU. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ginnery* zinakodishwa tu ovyo ovyo na watu wengine ambao ni matapeli wala hawajulikani wametoka wapi, hawalipi hata kodi, ni kuiba *spare* tu na kuziuba mahali pengine. Namwambia Mheshimiwa Waziri kama hajui SHIRECU imekufa kwa misingi ya uongozi aliouweka yeze mwenyewe pale. Hiyo *management* ni ovyo kabisa. Haifai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba ushirika ndio mkombozi wa mkulima, ndio mkombozi wa kutuondoa hata katika umaskini lakini uongozi mbovu hauwezi kutusaidia. Katika ushirika huu Waziri lazima akubaliane na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, ushirika huu hata kama ungepewa bilioni ngapi hautaendelea, kuna wafanyakazi zaidi ya mia sita SHIRECU tu peke yake, wanafanya nini, hata kama wamenunua kilo milioni moja lazima utawalipa mishahara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa naangalia kitabu hiki, katika ukurasa wa kumi na nne na kumi na tano, Vyama vya Ushirika anavilipia madeni, nimejumlisha hapa nimepata bilioni tisa *point* tisa tano lakini hajaangalia *over employment* ya Vyama hivi vya Ushirika ambayo ndio inafilisi. *Typewriter* moja wapiga chama kumi, gari mbovu iko gereji, madereva kumi wanaisubiri na wanalipwa mishahara. Sasa Waziri atafanyaje, kwa nini asitafute hela hata kama fungu la Serikali

likadhamini hawa wafanyakazi wakaondolewa, wakalipwa mafao yao, wakabaki wachache ambao kweli wanaweza kuendesha *SHIRECU* au Nyanza kisayansi kuliko kuwaacha pale huku wanalipwa mishahara kwa kukaa kujadili wizi tu kwa sababu hawana kazi nyingine pale zaidi ya kujadili namna ya kuiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kila *ginnery* basi ingekuwa ni *institution by itself*, iwe ni kitengo kabisa, kila *ginnery* ijitegemee, haya mambo ya kwenda *Apex Mkoani* au Taifani, haya ni mambo mengine, hatujafika huko. Taarifa za Bodi na yenyewe inataka hela tu. Halafu na hizi sheria za ushirika na zenyewe hazijakwenda na wakati, mambo ya soko huria sasa hivi, inatakiwa mtu unabadilisha bei *on the spot* unakuta bei ni shilingi 300/=, wafanyakishara wengine wanasema watu wanataka mia tatu na kumi, anamwambia nunua mia tatu na kumi, wewe *SHIRECU* mpaka uite Bodi, mpaka uite wazee, nao wana matatizo yao, wanaweza kukubali au wakakataa. Unachukua mwezi kuita kikao cha *SHIRECU*, watu wameshapandisha bei, umeshapitwa na wakati, kwa hiyo huwezi kununua pamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie vile vile kuhusu kazi ya utendaji katika Wizara hii. Kwa kweli nimeona kitabu hiki kina jengo zuri, sasa hili ndio tuliwaambia mkafanye kwenye ushirika kwenda kutengeneza jengo zuri badala ya kwenda kuimarishe ushirika na kutafuta masoko ya mazao yetu? Maana yake naona jengo zuri tu ndio mllichokifanya hapa kwenye ushirika, hakuna kingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naona hata ukiangalia ukurasa wa 34 mpaka 36 ni mikakati, rasimu zinaandaliwa. Mheshimiwa George Kahama, tangu amekuwa Waziri ni rasimu tu zinatengenezwa. Mimi nafikiri Mzee kama wewe unatakiwa sasa utuelekeze sisi vijana namna ya kuchapa kazi. Sasa rasimu, rasimu, masoko yanatafutiwa rasimu, ushirika unatafutiwa rasimu, Baraza la Mawaziri litakaa lini? Sasa nafikiri hakuna hata ukaguzi. Kukaguliwa vitu hivi bado hatujakwenda, kwa hiyo, ushirika naona kwa kweli bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia kwenye masoko na kwenyewe sijaona. Nilikuwa naongea na Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, hapa kuhusu viazi vya Gairo kama havijapata soko mahali popote. Anasema, bwana viazi vinaoza tu wakati Wizara hii ina wataalam wa kila namna. Kazi ni kununua pikipiki na magari lakini utaalam huu wa kutafuta masoko hakuna. Kila siku wanakwenda mara semina na humu nimeona warsha nyingi tu nyingine za Kimataifam wafadhili wengine ni *World Bank* wengine sijui *ADB* na wengine wengi tu. Sasa hawa wataalam wa masoko wa Wizara hii wanafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha mpaka imefika kwenye mazao muhimu kama ya pamba na kahawa, wataalam hawa hawa wanashauri Wizara *indicator price*, bei ya dira itakuwa shilingi 300/=, baada ya wiki mbili ni shilingi 250/=, halafu wanatoa sababu ambazo hata mtu ambaye hajakwenda shule hawezi kuambiwa. Eti wazalishaji wa China na Amerika wameongeza, walipewa ruzuku, kwani hukuliona hilo mpaka baada ya wiki mbili ndio unaliona hilo? Unataka kutwambiaje bwana! Baada ya wiki

mbili ile ruzuku imetolewa na wakulima wa Amerika wamelima sana katika wiki mbili na wamezalisha sana mpaka soko limefurika katika wiki mbili? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ipo haja ya Wizara sasa kukaguliwa, tuwe na *auditing* kila Wizara ina-*perform* vipi, zipo Wizara zina-*perform*, zinaondoa vitendawili ambavyo vilikuwa ni giza. Wizara ya Ujenzi tulikuwa tunazunguka Kenya kufika Bukoba, sasa tutatoka Mutukula kwa taksi mpaka Mtwara, hicho ni kitendawili. Wizara ya Elimu na Utamaduni, watoto walikuwa wanakaa chini, sasa wapo kwenye shule za msingi kama sekondari, hicho ni kitendawili. Sasa Wizara hii kitendawili cha viazi kuoza Gairo kitatolewa lini? Pamba kuchezewa soko tu kama unachezea maziwa, mara yanaganda mara yanachacha, tutakwenda wapi?

Mimi nafikiri ipo haja ya kuangaliwa Wizara hizi ziondolewe kama hazi-*perform* na mishahara hii waongezewe Mawaziri wanao-*perform*. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba ni zao nyeti, hatuwezi kulichezea na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa amesimama, mimi nikafikiri anaongeza shilingi 50/= kumbe shilingi 25/=, Waziri Mkuu mzima anasimama kutuongezea shilingi 25/=! Hapana bwana, hatuwezi kuchezea mazao muhimu. Zao la pamba ni zao muhimu na ndio rasilimali yetu sisi tunaolima pamba na ndio benki yetu. Watu wanapongeza Bodi, Bodi inafanya kazi gani? Bodi ni nini? Pamba imepatikana kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, mvua imenyesha vizuri. Sasa Bodi ilifanya nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi nataka kumweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba bado tatizo la wakulima wa pamba halijafikia muafaka. Tunataka kuiomba Serikali maana yake wamejaribu kuangalia kodi kodi hizi tu, sasa basi kwa nini Serikali isichangie hata shilingi 20/=. Kama tumepata shilingi 25/= basi Serikali nayo ijipapase katika mifuko yake iongeze ziwe shilingi 300/=. Nimepiga hesabu hapa kilo zinazotaka kununuliwa ni kilo 216,000,000 za pamba mbegu, ukitoa shilingi 20/= ni bilioni nne tu na *point* tatu, hizo hela kweli Serikali inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi inashindwa kupata hizi bilioni nne ili kuwafidia? Kama SHIRECU na Nyanza na hizi zote ziliweza kufutiwa bilioni tisa, watu wameiba lakini zikalipwa na Serikali, bilioni nne kuwapa wakulima wa pamba nchini hapa wakafaidika na hapa utakuwa umewasadidia kwa sababu sasa hivi tuna njaa katika nchi, hii bei nzuri ya pamba maana yake mtu atanunua chakula mapema na hatutakuwa na tabu tena ya kupeleka chakula, mbona hatuyaoni mambo haya! (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii inakaa na wanunuzi inatoka wapi? Soko huria maana yake mnakutana kule sokoni. Serikali inakaaje na wanunuzi mnapanga *indicator price*, ya kwenda wapi? Serikali wewe simama peke yako, fanya *analysis* ya kuzalisha kilo moja ni bei gani kwa mkulima. Mimi nimepiga hesabu ni shilingi 260/= na hii ni kwa kumpendelea tu kwa sababu nimepiga kilo mia nne zinazalishwa katika eka moja lakini Waziri Mkuu ametwambia ni kilo mia mbili mpaka mia tatu. Kwa hiyo, *it is more than two sixty actually*, kilo moja ya pamba mbegu. Sasa kama unampa shilingi 250/= tayari amekula hasara kwa shilingi kumi na mbili kwa hesabu hii ambayo nimeikisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima ifanye *research*, ione mkulima huyu inam-*cost* bei gani kuzalisha kilo moja ya pamba mbegu na atauza kwa *marginal profit* vipi na ndio unapanga wewe Serikali unatamka. Mtu ambaye anataka kununua pamba sasa asiteremke hapo sio kukaa, hao watakudanganya. Leo wamekwambia eti faida yao ni kati ya asilimia kumi mpaka kumi na tano kwa kigezo gani, unajua *analysis* za wafanyabiashara. Mfanyabiashara hawezi kutoa faida, haiwezekani tunadanganya tu.

Sasa mimi nasema soko huria halitaki mtu akae pamoja na wafanyabiashara kujadilia bei, haitakiwi. Sasa mimi nashangaa Serikali yetu ya Chama chetu kitukufu cha Mapinduzi inakaa na wafanyabiashara hawa inajadili bei ya kumlipa mkulima wa pamba, hapana. Naomba niisafishe hii Serikali, lazima ijiondoe kukaa na wafanyabiashara. Tunadanganya tu eti wanafadhili, hatutaki ufadhili, hawa wanakwenda kuwaibia wakulima, hivi sisi tutakubali kupata mikosi ya namna hii? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara hii ina kazi kubwa ya kufanya na kutuonyesha Watanzania kwa nini iendelee kuwepo pale. Lazima *i-perform*, iondoe vitendawili hivi. Nataka kushauri kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi amesema kwamba Serikali inajiondoa, haiwezekani. Yapo mazao ambayo Serikali haiwezi kujiondoa kama vile ni pamba, kahawa, korosho au tumbaku. Pia kuna vitu kama ng'ombe, huwezi kujiondoa, Serikali lazima iangalie huu ndio utajiri wetu. Sasa kama umejiondoa kwenye madini, watu wanachimba tu wanaondoka. Unajiondoa kwenye tumbaku, watu wanavuta bangi na tumbaku zile wanachanganya, wewe haupo. Unajiondoa kwenye pamba, watu wanauzu tu wanavyotaka, wewe utapata wapi fedha za kigeni? Lazima Serikali iwekeze katika mazao haya. Tunaiomba sana Serikali.

Kuhusu hili suala la kuzuia kilimo cha pamba katika Mikoa ya Kusini. Mheshimiwa Charles Keenja, alitwambia tutajadili lakini lazima pamba ilimwe katika Mikoa ya Kusini. Utaachaje, tunaambiwa eti kule kuna mdudu, mdudu huyo amekuwa wa UKIMWI, haonekani? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi pamba imekuwa na UKIMWI? Lazima kule Mbeya, Rukwa, Mtwara, Lindi, Ruvuma walime pamba, pamba, pamba. Hakuna mdudu, mdudu tunajua ni wa UKIMWI sio kwenye pamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Kuna watu ambao walikuwa kwenye orodha lakini waliniomba kwamba wangechangia dakika tano, tano. Kwa hiyo, waweke dakika tano hapo. Waliomba wameniandika hapa. Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, dakika tano na Mheshimiwa Dr. James Msekela, dakika tano.

MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia dakika tano. Kwanza, nikimaliza dakika tano bila kumshukuru Mheshimiwa Charles Keenja, nitakuwa siyo mwangi wa fadhila.

Wakulima wa Korosho Mtwara Vijijini wamepata fedha za Mfuko wa Pembejeo kwa kila Chama cha Msingi namshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea Serikali haina taarifa na matatizo ya wakulima wa Mtwara. Kwa dakika tatu tu naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yake niwaombe wachukue kalamu na karatasi niwape matatizo ya wakulima wa Mtwara Vijijini ili wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la wakulima wa korosho ni upatikanaji wa *sulphur*. Mwaka huu *sulphur* wamenunua mpaka shilingi 20,000/= kwa mfuko wakati mfuko mmoja ni shilingi 9,000/= tu. Naiomba Serikali itoe tamko au iweke utaratibu *sulphur* ifike kwa wakati na iuzwe kwa bei nzuri ya chini ili uzalishaji uendane na gharama za uzalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, bei ya korosho. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo juu ya Bodi zinazota mwelekeo wa bei na korosho inafanya hivyo hivyo, mwelekeo wa bei waweza kuwa shilingi 700/=, lakini hununua kwa shilingi 100/= mpaka shilingi 150/=. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alijue hilo ili siku nyingine pia atoe tamko hapa kwa zao la korosho kama alivyotoa la pamba. Maana sisi hatuelewi *STABEX* Kahawa, Chai ila Korosho, zii. Kauli ya Serikali kuhusu pamba, korosho zii, sisi inakuwa hatuelewi inawezekana Serikali haina taarifa juu ya zao la korosho.

Leo nawapeni taarifa matatizo ya zao la korosho bei ina kuwa ya chini tofauti na inavyotamkwa na *sulphur* inakuwa ya bei ya juu sana kiasi ambacho uzalishaji unakuwa wa juu na bei ndogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kutunza ahadi yako. Mheshimiwa Dr. James Msekela na wewe ufanye hivyo hivyo.

MHE. DR. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda niunge mkono hoja hii. Lakini pia napenda nizungumze kama mambo matatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ambalo kwa kweli ni suala *over due*, tulivyotunga Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001, huko ndani kulikuwa na *clause* ambayo ilikuwa ina *undo existences* ya *Association of Tanzania Tobacco Traders*. Hawa mabwana katika *Articles* za *Association* yao, hiyo ni *Association*, walikuwa na vipengele ambavyo vilikuwa vinakuwa *undone* sasa na ile sheria. Lakini nasikitika kusema kwamba *Association of Tanzania Tobacco Traders* bado wapo na wako *active* kwenye biashara ya tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuuliza swali hapa na wakulima wenzangu wa tumbaku waliwahi kuzungumzia haya masuala hapa Mheshimiwa Juma Nkumba, Mheshimiwa Ally Karavina, tumeuliza hapa maswali na bado tumepewa majibu ambayo

hayawezzi kusema *straight* kwamba *ATT* anatakiwa *ku-wind up* au ana ruhusa ya *ku-exist*. Sasa leo napenda hili waliseme *straight* hapa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nisingekuwa mkweli kama sitasema kwamba tumbaku kwa kweli mwaka huu masoko yake yamekuwa mazuri na hii ni mojawapo ya pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko *Sir George Kahama*, kwa jinsi ambavyo alifanya kazi nzuri sana kutusaidia kupata sheria nzuri sana ya mwaka 2001 ya tumbaku. Masoko yalikuwa mazuri kwa wastani kwa kweli tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo napenda nilisemee jioni hii ni pamba ambayo imeanza kulimwa na huu ndiyo msimu wa kwanza Jimboni kwangu Wilaya ya Uyui. Tunataka kuuza hiyo pamba. Pamba tunayolima kwetu ni aina ya *UK91* hii iko kwenye majaribio. Sasa hivi hawa wakulima wetu walitakiwa kuwa wanauzwa pamba yao mwishoni mwa mwezi Juni, 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hadi ninavyozungumza hivi hakuna aliyeuza hata mmoja pamba yake kwa njia ya kawaida. Waliouza wote wamefanya hivyo kwa njia za panya na isitoshe wamepeleka nje ya Wilaya yetu na hiyo inatusababishia hasara ya moja kwa moja kwa wakulima wenyewe, lakini hata kwa Ushirika na Wilaya yetu. Hili ni tatizo kubwa. Hivi sasa tumeambiwa amepatikana mnunuzi anaitwa *KACU* au *Kahama Co-operative Union*. Hawa mabwana mpaka sasa hivi jioni mimi nimezungumza nao kwa simu, mchana nimeongea na Dr. Kabisa, ambaye ni Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba akanieleza kwamba wale wamemwambia kwamba wanaanza kununua pamba kesho tarehe 31 Julai, 2004.

Nimempigia simu baadaye huyu Mhasibu, namtaja kwa jina kwa kweli anaitwa Ndugu Bukindu na ajisikie huko aliko, akaniamba wala si kweli wanaanza kuuza hiyo pamba Jumatatu, nikamuuliza *readiness* yako ikoje kama unaanza kununua hiyo pamba Jumatatu, akasema kuna watu wako hapa nitawa-*dispatch* sasa hivi kwenda kule, wakati *actually* dakika tano zilizopita amewafukuza hao watu ofisini kwake. Kutoka Kahama Mjini kwenda Bukumbi, ambako wanakwenda hawa watu nafikiri bado wako njiani sasa hivi ni kilometra kama 90 na ni barabara mbaya atawapata wapi ili aweze ku-*organize* soko Jumatatu liwepo. Huyu ni mwongo na uongo huu umekuwa una-*drag* kwa muda mrefu.

Sasa nimetoa hii historia fupi ili kumtaka Mheshimiwa Waziri hapa atusaidie kwa kweli tuliiitikia wito wa Bodi ya Pamba na Wizara hii walikuja wakatusaidia kuhamasisha watu wakahamasika wakaamua kulima pamba na wamelima pamba kweli kweli. Niseme kwa makisio ya mwanzoni kuna kilo 300,000 kule. Kilo 300,000 kwa hii bei ambayo imetangazwa hapa na kwa kuwa pamba yetu nimeambiwa na Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba kwamba inaongezewa shilingi 30/= kwa kilo, unahitaji kama shilingi 305 kwa kila kilo. Kwa hiyo, hizo kilo 300,000 unahitaji kama milioni 100 tu. Sasa hawa watu hata milioni 100 *KACU* tena wanaonekana wanatubabaisha. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aweke uzito wake wote kwenye hili na kwa kweli mimi niko tayari dakika yoyote ile kumpatia msaada wa aina yoyote *logistically* ili hao watu waende wakanunue pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. LEONARD M. SHANGO: Mhesahimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ushirika na Masoiko ni Wizara nyeti na kama itaelekeza nguvu zake kiutendaji na kimipango, itawagusa wananchi walio wengi na wenye hadhi ya chini kiuchumi na kipato katika sekta mbalimbali za uchumi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufufua ushirika katika kipindi cha utandawazi na ushindani wa kibiashara linakuwa gumu zaidi na kwa hiyo, ni muhimu malengo ya ushirika mpya yaelekezwe kuendana na hali halisi ya dunia ya leo ya ushindani na utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nionavyo mimi ushirika mpya katika Taifa letu, lazima uelekezwe katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, masoko ya ndani na nje yahushe mazao mchanganyiko ya kilimo na ufugaji. Eneo hili ni jipyä na hata wakati wa ushirika wa zamani, soko la ndani na mazao mchanganyiko lilitihau. Eneo hili linahusisha takriban 50% hadi 70% ya wananchi wakulima. Ukichanganya na ufugaji pamoja na viwanda vidogo vidogo kama usindikaji, patahusisha wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 39 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, vyama 559 vimeanzishwa. Kusema kweli katika Wilaya mbalimbali pamoja na Wilaya ya Iramba, hapatafanyika kazi yoyote ya kuanzisha vyama vya namna yoyote ya ushirika hasa kwenye mazao ya kilimo na misfugo vijijini. Wizara ifanye kazi ya ziada ya kupeleka wataalam wa ushirika wengi zaidi katika ngazi za Halmashauri na Vijijini. Haitoshi kwa sasa kuwa na Afisa mmoja tu wa Ushirika Makao Makuu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ushirika wa Vyama vya Akiba na Mikopo, vimeanzishwa na viro katika hatua ya Makao Makuu ya Wilaya. Hata hivyo, vyama hivi vina matatizo makubwa ya kukosa mitaji ya fedha na watendaji wazoefu. Mikopo midogo na michache inayotolewa, haisimamiwi kwa utaalam na uzoefu na hivyo kufanya marejesho ya mikopo kuwa madogo sana na hata kuathiri mwelekeo wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatakiwa kuimarisha usimamizi wa vyama hivi (*SACCOS*) katika ngazi ya Wilaya na kuwa na mpango unaoeleweka kuwafikia wananchi vijijini kama wateja muhimu. Kwa hiyo, elimu ya kuunda, kuendesha, kukagua na kuhimili ushindani wa vyama vya ushirika vya aina mbalimbali, uonekane vijijini na siyo Makao Makuu ya Wilaya, Mikoa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ushirika mpya unaoanzishwa uelekezwe kwenye sekta za kuzalisha mazao na mali na siyo kwenye kuuza au kufanyabiashara tu. Kwa mfano, kuhusu sekta ya kilimo, ushirika wa kuchimba mabwawa/malambo na mifereji ya kupeleka maji mashambani, utawasaidia wakulima katika kuleta mageuzi ya kilimo kutoka kutegemea mvua na kuingia kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji. Katika eneo hili, ushirika wa kuhodhi na kutoa huduma za vifaa na pembejeo za kilimo, uanzishwe na utoe huduma kwa wananchi wakulima, wafanyabiashara na wasindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Kwa sasa ni vigumu kwa wananchi binafsi waweze kupata/kununua vifaa na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ushirika katika kutoa huduma mbalimbali kama afya (zanahati, kliniki, hospitali), elimu, mawasiliano, usafiri na usafirishaji ni eneo ambalo linaweza kuboresha maisha na huduma vijijini kwa kuleta ushindani kibiashara na wahimili binafsi. Kwa kufanikisha hivyo, Wizara na Serikali kwa ujumla ifanye mambo muhimu ya uwezeshwaji na usimamizi wa vyama vya ushirika katika eneo/sektahii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano na mwisho, Benki za Ushirika zenyenye mitaji mikubwa ya uhakika, zianzishwe na matawi ya taasisi hizi za fedha zipatikane mpaka vijijini. Kwani vyama vya ushirika katika sekta mbalimbali, vitahitaji huduma ya kibenki na fedha vijijini, ambapo ndiko sekta za kuzalisha mazao na mali zina nafasi kubwa ya kufanikiwa, kuhimili ushindani na kuimarika. Pia benki hizi za ushirika zitangia kwa kiwango kikubwa kuimarisha mzunguko wa fedha vijijini. Kwa sasa vijiji vingi na Wilaya nyingi zina tatizo la mzunguko mdogo wa fedha (*liquidity circulation constraints*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa Makadirio ya bajeti ya mwaka 2004/2005.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na mikakati ya utekelezaji ni mizuri na ina upeo mpana. Kinachotakiwa ni utekelezaji wa mipango kwa mikakati iliyowekwa kivitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu, upo uhaba mkubwa wa watumishi. Afisa Ushirika wa Wilaya amekaa katika kituo hicho zaidi ya miaka 15. Ufanisi wake ni mdogo sana kutokana na uenyeji wake. Nashauri ahamishwe ili kupata kiongozi mpya mwenye ari na msukumo mpya wa kazi. Kwa sasa Afisa huyo amejikita kwenye siasa na kusahau wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *STABEX* ambazo zimepelekwa Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Kilimo na Chakula, nashauri Wizara ya Ushirika na Masoko isaidie kuratibu usambazaji wa fedha hizi ili ziwafikie walengwa wote ambao wengi ni

wanachama wa Vyama vya Ushirika. Maeneo hasa yale ya kahawa yanagusa vyama na wanachama wa ushirika. Naomba ushirikishwaji na ushirikiano wa walengwa uwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Ushirika cha *Usambara Co-operative Union* kipewe msaada maana ni kichanga. Msaada utolewe kwenye maeneo ya Elimu kwa watendaji na wanachama wa vyama wasaidiwe katika ukaguzi wa Vyama vya Msingi. Pia wasaidiwe katika kupata fedha za kununulia mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa masoko ya ndani na nje uimarishwe. Bei za mazao ziratibiwe ili wakulima wasipate hasara wakati bei zinaposhuka. Utafutwe uwezekano wa kuunda mifuko ya kusawazisha bei za mazao zinaposhuka ili kulinda wakulima wetu wasifilisike kabisa. Asante.

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ushirika na Masoko pamoja na Naibu Waziri wake, kwa kazi ngumu, lakini inayoonyesha mafanikio mazuri na makubwa katika kujenga na kuimarisha ushirika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwapongeza wataalam wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa kutayarisha hotuba nzuri yenye kuonyesha dira ya ushirika katika Taifa letu. Napenda kuchangia machache kwa nia ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya masoko. Hali ya masoko hasa kwa mazao ya biashara asilia, inakatisha tamaa kwa wakulima. Mfumo wa biashara huria unaathiri sana *performance* ya Vyama vya Msingi vya Ushirika, kwani wanunuzi binafsi wanafanya njama za kudhoofisha Vyama vya Ushirika na matokeo yake ni vyama hivi kushindwa kuijidesha na kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kama inawezekana Serikali itoe agizo kwamba Vyama vya Ushirika vipewe dhamana ya kununua mazao haya, halafu ndiyo wafanyabiashara binafsi wanunue kutoka kwao. Mheshimiwa Waziri, bila kuchukua hatua hii, ni dhahiri kwamba vyama vingi kama *KCU*, vitakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukosekana kwa uongozi wenye uadilifu katika Vyama vya Ushirika vya Msingi. Hali hii imesababisha kafilisika kwa vyama vingi vya ushirika hususan Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Waziri, wananchi wanavidai Vyama vya Msingi vya Ushirika na mpaka sasa hakuna mafanikio. Je, Serikali inawasaidiaje hawa wananchi wanaodai? Je, Wizara ina mikakati gani ya kuwajibisha wale wote ambao wamehujumu Vyama vya Ushirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirikiano kati ya Wizara ya Ushirika na Masoko na *NGOs* zinazoshughulikia kuondoa umaskini hapa nchini. Mheshimiwa Waziri, napenda kushauri Wizara itambue juhudzi za Mashirika yasiyo ya kiserikali katika

kuwapatia wananchi mikopo pamoja na kuwahamasisha kuanzisha vikundi vya kiuchumi na hatimaye hivi vikundi vinaungana na kuanzisha *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi hii imefanywa sana na Shirika la *Faraja Trust* la Morogoro. Faraja kupitia kitengo chake cha *Faraja Microfinance*, kimehamasisha wanawake na vijana Mkoani Morogoro kuunda vikundi vya kiuchumi ambavyo vimepewa mikopo. Baada ya vikundi kuimarika, wamehamasishwa kuunda *SACCOS* kwenye ngazi za Kata na Tarafa. Faraja imewasaidia kuijandikisha na kuwapatia mitaji, pamoja na kutoa mafunzo ya kutunza mahesabu na kumbukumbu za *SACCOS* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maofisa wa Wizara hii ya Ushirika, wanavifahamu vikundi hivi vya *SACCOS*, lakini hawajaonyesha nia ya kuwasaidia kwa namna yoyote. Mpaka sasa tunazo *SACCOS* 19 za wanawake na vijana katika Mkoa wa Morogoro. Naomba Wizara iwezeshe Shirika la Faraja ili liweze kuendelea na kazi nzuri ya kusaidia kuundwa kwa *SACCOS* hasa kwenye *Rural Districts*. Juhudi za Shirika hili zinaonekana katika Viwanja vya Maonyesho ya Kilimo vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya ushirika. Elimu ya Ushirika iingizwe kwenye mitaala ya Shule za Msingi na Sekondari, kwani umuhimu wa ushirika katika kuleta maendeleo ya kiuchumi Kitaifa hauna mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati muafaka wa kutoa maamuzi ya kuwapa vijana wetu elimu ya ushirika na masoko kama kweli Taifa limedhamiria kuondoa umaskini kwa njia ya kuwawezesha Watanzania kujisaidia wenyewe, kwani ni kwa njia ya kuweka nguvu zetu za pamoja, ili tuweze kuanzisha miradi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Wizara itoe *literature* (maandiko) ya ushirika katika maktaba za Shule za Msingi, Sekondari na kwenye Vyuo vya Ufundis Stadi. Hii itawapa mwanga vijana kwamba ushirika ni nini na utawasaidiaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Ushirika, Moshi. Baada ya Chuo cha Ushirika kuwa Chuo Kikuu, naanza kuwa na wasiwasi kuhusu huduma ya elimu ya ushirika katika ngazi ya vijiji, iliyokuwa inaendeshwa na *Extension Officers* wa Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sasa chuo kitaendelea kutoa elimu kwenye ngazi za chini kama walivyokuwa wanatoa au watakuwa *Academic and Research oriented* kama vyuo vikuu vingine? Kama lengo la mwanzo litabadilika, je, Wizara ina mipango ya kuanzisha mfumo mbadala wa kuelimisha wanavijiji kama mwanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia haya yote, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namwombe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wa Wizara ya Ushirika na Masoko, afya njema na baraka za Mwenyezi Mungu katika kuiongoza Wizara hii nyeti.

MHE. GEORGE F. MLAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii naiunga mkono bila kikwazo chochote. Wakati huo huo natoa pongezi za moyo kwa Waziri, Mheshimiwa *Sir* George Kahama, kwa uongozi wake wa Wizara hii, ulio makini na uhakika. Vile vile natoa pongezi kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu na Maafisa wa Wizara hii kwa utumishi wenye mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa kuhimiza ukuaji wa Vyama vya Ushirika kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi na hasa kuendelea hatua kwa hatua kuvi-*transform* kuwa pia Vyama vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*). Ni muhimu sana kuzidi kukiimarisha Chama cha *SCCULT* ili kiweze kusimamia uanzishwaji na ukuaji wa *SACCOS* nchini kote, hasa *SACCOS* za wakulima. *SCCULT* izidi kupewa uwezo mkubwa wa kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika na kuvi-*transform* kuwa pia *SACCOS* mpaka umoja huu wa *SACCOS* uwe na uwezo mkubwa wa kifedha na hatimaye ujitegemee katika utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono juhudzi za Wizara hii, nazidi kuhimiza Vyama vya Ushirika kupewa mikopo ya ununuzi wa mazao ya wanachama wao ili kuleta ushindani ufaao wa bei za mazao. Vyama vya Ushirika vya Msingi lvijenge ma-*godown* ya kuhifadhi mazao na kuuza mazao hayo wakati bei ni nzuri. Vyama vya Ushirika vitakuwa na *Bargaining power* kubwa katika upatikanaji wa bei za haki za mazao. Hivyo, ni vema kuharakisha uanzishaji wa Benki ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuanzisha programu ya kuendeleza mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme*) na kwamba inatekeleza kwa muda wa miaka saba na utekelezaji huo unafanyika katika mikoa nane na jumla ya Wilaya 36 zilizopo katika Kanda za Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini, pamoja na kutengeneza barabara za vijijini muhimu sana kujenga masoko ya Kimataifa ya mazao ya kilimo, mfano wa Soko la Kimataifa linalojengwa Kibaigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini, ni muhimu sana kuwa na masoko mengi ya aina hiyo ambayo yatatatuwezesha kufanya biashara ya ushindani katika Soko la *SADC*. Eneo hili lina uwezo wa kuzalisha aina mbalimbali za mazao ya chakula. Kwa kuongezea tija, inawezekana kabisa tukaweka ushindani mkubwa wenye kuleta maendeleo makubwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara hii iwahamasishe wawekezaji wajenge masoko ya Kimataifa mengi iwezekanavyo katika eneo hili la Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo la Kalenga, inawezekana kabisa kujenga Soko la Kimataifa katika moja ya *Trading Centres* za Tanangozi au Ifunda.

Tukiwa na masoko ya aina hiyo, basi utaratibu wa dhamana kwa mauzo ya nje Vyama vya Ushirika, (*Export Credit Guarantee Scheme*) utafanikiwa na kufana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kwa kusema kuwa naunga mkono hoja hii.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Balozi George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mzuri na bajeti ya utekelezaji wake ni matokeo ya kazi nzuri ya viongozi wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu na Wakurugenzi/Maofisa Waandamizi wa Wizara. Tunawapongeza wote na kuwahimiza waongeze juhudhi na ari ya kuendeleza sekta hizi za Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kumtuma Mtaalam wa Ushirika kuja Mwanga na kuiongea, kutoa mwongozo na maelekezo kwa vyama vyetu vya Ushirika vya Msingi ili viweze kupata *guarantee* ya Serikali, viweze kukopa kwa ajili ya kununua kahawa. Mtaalam huyo amefanya kazi nzuri sana.

Vyama vingi vya ushirika vya msingi Wilayani Mwanga, vimefanya jitihada kubwa kutimiza masharti yanayotakiwa ili waweze kukopa kwa ajili ya kununua kahawa na kuiuza mnadani, Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wamlele tena Ndugu Chilipaine, Afisa Ushirika Mwandamizi, aende tena Mwanga kuhimiza na kukamilisha kazi aliyoanzisha. Kwenda kwake kumekuwa na umuhimu mpya baada ya Wilaya yetu kuingizwa katika mradi wa *SELF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vyetu vyote vimeanzisha *SACCOS* zao. Matarajio yakiwa kuwa tukipata msaada kwa ajili ya hizi *SACCOS*, tutawawezesha wananchi wanachama wa Vyama vya Msingi waweze kukopa dawa za kahawa na kununua pembejoe zingine. Hivyo, kwa kuingia katika mradi wa *SELF*, imepatikana fursa kwa vyama hivi kupata mtaji wa kuviwezesha na kwa masharti nafuu. Sasa tunahitaji mtaalam huyu atusaidie kuingia katika *SELF* kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimia Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Sir George Kahama na Naibu Waziri, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Nawaomba waongeze jitihada ya kuimarisha ushirika na utafutaji wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kueleza kuwa hali ya ushirika kwa maana ya Vyama vya Ushirika, hαιaridhishi. Nimefutilia suala la uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika katika Halmashauri yangu, lakini bado sijafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003 nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipatie wataalam ili wakanisaidie kuhamasisha uundwaji wa Vyama vya Ushirika vya Msingi. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia Wataalam hao ambao walifanya kazi nzuri. Baada ya kuhamasisha wananchi, kazi iliyobaki ilikuwa ni kuunda Vyama vya Ushirika vya Msingi katika maeneo tuliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuwaeleza kuwa hadi sasa hakuna kilichofanyika. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, anisaidie namna ya kuifufua au kuanzisha Vyama vya Ushirika katika jimbo langu hasa Vyama vya Msingi. Katika Halmashauri yangu wapo Maofisa Ushirika wawili tu na hivyo wanashindwa kumudu kazi ya uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika. Nashauri wawepo Maofisa Ushirika katika kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho natoa pole kwa familia ya Marehemu Capt. Mstaafu Theodos Kasapira, kwa kufiwa na mpendwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watumishi wote wa Wizara na wanaushirika wote, kwa kazi nzuri sana inayoendelea kuifufua ushirika. Mafanikio yanaonekana, hivyo hapana budi kuongeza juhudhi katika kushauri, kuwezesha na kusimamia ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Kwanza nashauri tena Mheshimiwa Waziri awashauri wanaushirika wa Muleba, Bukoba na Karagwe waungane tena na kuwa na chama kimoja tu cha ushirika. Kugawanyika kwao kunapingana na dhana na msingi mkuu wa ushirika. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nashauri Mheshimiwa Waziri waingilie kati mgogoro wa Mahoteli ya *Coffee Tree Inn* na *Lake Hotel*. Mikataba walioingia bila ushauri na usimamizi wa Wizara ya Ushirika na Masoko, sasa ni mzigo kwa mujibu wa viongozi wa *Kagera Co-operative Union (KCU)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kusoma mkataba huo/hiyo. Kusema kweli ni aibu tupu. Ni vema kuwasaidia wanaushirika kupata suluhu mapema, hii itatuondolea aibu. Tumeunusuru ushirika wa *KCU* kwa tabu sana na bado kazi ni kubwa. Hailezeki iwapo wananchi watanyang'anywa mali ambazo tumesaidiwa na Mheshimiwa Rais kuzinusuru. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza tena Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri sana. Naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara kwa kukamilisha hotuba, ni nzuri na yenye mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 14 na 15, ameelezea namna Serikali ilivyosaidia kulipia madeni ya Vyama Vikuu vya Ushirika kama ifuatavyo:-

Madeni ya Vyama vya *KDCU* na *NCU* yaliyolipwa Benki ya *CRDB* na *NBC* ni shilingi bilioni 3.79, deni la Chama cha *KNCU* Benki ya *CRDB* ni shilingi 667,750,353/=, Vyama vya *KCU* na *KDCU* vilisaidiwa kuwalipia wakulima shilingi bilioni 1.7 na Vyama vya *SHIRECU*, *NCU* na *BCU*, madeni yao ya shilingi bilioni 3.79, Serikali iliwalipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yaliyofanywa na Serikali kwa vyama hivi vikuu na jambo zuri na linasaidia maendeleo katika mikoa hiyo. Jambo hili lingefanyika kwa madeini ya Vyama Vikuu vya Ushirika vyote nchini kama madeni ya Chama Kikuu cha Ushirika Mbinga (*MBICU*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la *MBICU* lilikuwa chini ya shilingi bilioni 2.0, lakini Serikali haikusaidia kulipa deni hilo na ilifilisiwa. Naomba kufahamu kwa nini madeni ya vyama vingine vinasaidiwa na *MBICU* haikusaidiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iokoe majengo ya *MBICU* ili kulinda haki ya wananchi wa Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hotuba hii kwa imani kwamba itasaidia kulipa madeni ya *MBICU*. Ahsante sana.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na programu nzuri za kufufua ushirika nchini, pamoja na ujenzi wa masoko ya mazao kama yale ya Kibaigwa, Kinole na Nyandira, chini ya umoja wa *MVIWATA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 51(iii), Wizara imepanga kujenga masoko kama hayo katika Mikoa nane na Wilaya 36 Kaskazini na Nyanda za Juu. Kwa vile Halmashauri ya Njombe tayari imetenga eneo la ekari 100 na fedha kidogo kwa madhumuni hayo na tayari imejibu barua ya Wizara kuhusiana na ujenzi wa soko pale Makambako. Vipi ujenzi wa soko la Makambako usipewe umuhimu wa kwanza katika kipindi hiki kuanzia mwaka 2004/2005?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makambako ni katikati ya Nyanda za Juu na mazao kutoka Wilaya jirani mara nyingi hulundikwa chini ya ardhi kwa vile hakuna soko pale

Makambako. Makambako panafaa kwa sababu ipo katika Reli ya *TAZARA* na barabara kuu ya Kaskazini, ni katikati ya Nyanda za Juu, ni lango la kuingilia na kutokea Nyanda za Juu na Mikoa ya Kusini, ni bandari ya nchi kavu (stesheni), wakulima kutoka Mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Mbeya na Iringa kuuzia mazao yao Makambako, Kijiji cha Makambako kinakua kwa kasi kubwa kuliko miji yote ya Nyanda za Juu. Sasa Makambako pana wakazi 51,000 wakati Njombe ni wakazi 41,000 tu, ni katikati ya Miji ya Songea, Iringa na Mbeya na Makambako imependekezwa kwa soko la mazao la Kimataifa na Halmashauri ya Wilaya, eneo limetengwa na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba ujenzi wa soko uwe katika programu ya mwaka 2004/2005 au 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii fupi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Idara mbalimbali na Wasaidizi wao katika Wizara ya Ushirika na Masoko. Nawapongeza sana kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kusonga mbele kuleta ufanisi katika kuimarisha na kuboresha ushirika nchini. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kubadilisha uongozi wa Utawala wa Serikali katika Chama Kikuu cha Ushirika (*SHIRECU*), Mkoani Shinyanga, kwani chama cha Ushirika katika uongozi wake mpya, utashindwa kuendesha ipasavyo kwa kuwa mkono wa Serikali unatumia nguvu ya dola. Achaguliwe *General Manager* wa *SHIRECU* wa kwao ili uongozi uwe wa *SHIRECU* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiimarishe kitengo cha masoko ili kiweze kusimamia bei ya mazao ya wakulima vizuri. Kutangaza ovyo ovyo bei ya mazao, kusiwe kunatangazwa na watu wasiokuwa na nyadhifa Serikalini. Atangaze Waziri mwenyewe, Naibu Waziri na Katibu Mkuu basi. Vikao kuhusu mazao ya wakulima, visifanywe na wafanyabiashara pekee na kutolewa matangazo. Serikali iwe macho sana kwa suala la bei ya mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya ushirika, bado tuko nyuma sana kwa suala la kueneza na kuimarisha Elimu ya Ushirika shirikishi hasa kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika. Uwepo mpango mahususi wa Kitaifa wa kufundisha wanachama wa ushirika na wakulima kwa jumla, elimu kwa uongozi wa Vyama vya Ushirika nchini, mbinu za kupambana na soko huru na mpango huu ulenge hasa kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi iimarishe na iwe inatoa taarifa ya ukaguzi wake mara kwa mara kunakohusika. Aidha, pale ambapo pana dosari ya kazi, basi hatua kali zichukuliwe haraka. Idara hii ipewe usafiri, vitendea kazi vinavyoihusu Idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. EDSON. M. HALINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu, kwa juhudhi wanazozifanya ili kumwezesha mkulima kwa ushirika kuweza kukabiliana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika usichukuliwe na kueleweka kuwa upo kwa kumsaidia mtu ama mtumishi binafsi anufaik. Inatakiwa ushirika uwe ni mafanikio ya pamoja na kuongeza uchumi wa kipato kwa pamoja katika ushirika na kupunguza harubu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, inapaswa ushirika upunguze gharama za wakulima kutokana na uzalishaji. Ushirika ni vema uendeshwe kwa kujituma, ikibidi hadi kujitolea kwa kiasi fulani. Tatizo la ushirika wetu ni kula zaidi ya uwezo wa Shirika wenye. Kwa hali hii, inabidi kazi za ushirika wa uzalishaji mazao, ni vema ukalenga msimu wa uzalishaji kuwa na watumishi wa kudumu wakati shughuli za ushirika ni za miezi sita tu. Matokeo yake ni kafilisika ushirika na kuzaa manung'unico ya wanachama na kuwa ndiyo mwanzo wa vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema kuwa Vyama Vikuu vya Iseyula na *MBOCU*, vililipa wakulima nyongeza, ni kweli. Bei ya mwanzo ilikuwa ni shilingi 300/= na malipo ya pili yalikuwa shilingi 200/>. Maana yake ni kwamba vyama vikuu hivyo vililipa shilingi 500/= hadi shilingi 600/= kwa kilo. Lakini vikundi vilivyojiunga vilipewa shilingi 600/= mpaka shilingi 900/= kwa kilo. Hii ilitokana na kupunguza gharama kwa watendaji na milango mingi ya ulaji. Aidha, usimamizi wa mali yao ulikuwa wa papo kwa papo na wanakikundi wote waliwajibika. Vikundi vya Isansa, Itompi na Hasaruba kwa uchache kama kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isijisahau kwa kuongeza nguvu katika ukaguzi wa mara kwa mara katika mazao yanayokusanya wakati wa soko. Vile vile wakati wa malipo kwa wakulima, utunzaji wa vitabu, hata mikopo inayokopwa na vyama, kwani mikopo hiyo hutumiwa kama posho kwa watendaji badala ya kununulia mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikitaka masoko yawe kwa manaufaa ya wakulima wa nchi, ni lazima itambue kuwa utaalam ni msingi muhimu. Nchi haiwezi kudhibiti masoko mpaka tu na wataalam wa masoko. Hatuwezi kufanikiwa kwa kunung'unika bila elimu ya kumbukumbu ya utafiti wa masoko na kuuanisha wa biashara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuipongeza Serikali ya kujenga soko Kibaigwa. Hiyo ndiyo njia pekee ya kumwezesha mkulima kuwa na mahali pa kuuzia mazao yake kirahisi. Aidha, masoko kama haya yaongezwe katika mikoa yote nchini kwa awamu, hata watu binafsi wahamasishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba soko lijengwe Tunduma ambapo tutaweza kudhibiti uchumi katika mpaka wa Zambia na wa Malawi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Binafsi sioni faida ya Bodi za Mazao kwa wakulima, bali ni gharama za kuwapunguzia wakulima mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti ya Ushirika na Masoko.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mmheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya msimu wa pamba kufunguliwa, wanunuzi wengi walinunua pamba kwa shilingi 300/= kwa kilo kama Bodi ya Pamba ilivyokuwa imetangaza bei ya dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 13 Julai, 2004 Bodi ya Pamba (*TCA*) walikaa Mjini Mwanza na kushusha bei ya pamba hadi shilingi 250/= kwa kilo. Uamuzi huu uliwakanganya wakulima. Bahati mbaya zaidi Serikali ilikaa kimya juu ya hali hii. Wakati huo huo wananchi wakafanya yafuatayo:-

(i) Wakazuia pamba iliyoko kwenye maghala hadi walipwe shilingi 300/= kwa kilo.

(ii) Wakashindwa kuamua iwapo wauze pamba yao kwa shilingi 250/= kwa kilo au labda Serikali itachukua hatua za kuongeza bei.

(iii) Wanunuzi waliokuwa tayari wamenunua pamba kwa shilingi 300/= kwa kilo, wakateremsha bei na wakataka walipe shilingi 250/= kwa kilo, wananchi wanalamika sana kupitia kwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi Waziri Mkuu ametoa tamko ambalo naamini limepokelewa kwa furaha katika maeneo hayo. Tamko limechelewa sana. Kuna suala moja ambalo Waziri Mkuu hakulitolea maelezo, nalo ni hatma ya wakulima waliouza pamba yao kwashilingi 300/= kwa kilo na sasa wanunuzi wanataka wasilipe kama walivyonunua, wanunue chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataka maelezo ya Waziri juu ya hatima ya wananchi hao. Naomba kuwasilisha.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naelekeza mchango wangu kwenye yafuatayo:-

Kwanza kuhusu Mradi wa kuendeleza mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMSDP*) na ule wa *Agricultural Sector Development Programme (ASDP)*. Mradi huu ulipotangazwa ulitupa matumaini kuwa miundombinu ya barabara kwenye maeneo ya mazao yangeboreshwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mradi huu bado kwa sehemu kubwa upo kwenye hatua za kujenga muundo tu badala ya kwenda moja kwa moja kwenye kuendeleza miundombinu kama ambavyo Miradi ya *TASAF* inafanya. Hii ni changamoto, kwani mradi ambao kwa miaka zaidi ya mitatu inaunda tu *structure* ya utawala, hauna sababu zaidi ya kuitia hasara nchi kupitia mikopo inayofadhili miradi nya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya naomba kupata kwa undani programu ya mradi huu Wilayani Babati, ikizingatia kwamba mwaka 2003 nilitoa mchango wa maandishi kama huu nikiulizia utaratibu wa kuendeleza barabara na masoko Wilayani Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la Chama cha Msingi cha Mlimani - Bonga, ambacho kiliathirika na dawa za kuua wadudu kwenye kahawa kutoka Kampuni ya *Balton (T) Ltd.* Tatizo hili liliwasilishwa kwa Waziri wa Ushirika na Masoko baada ya chama hicho kufanya mawasiliano mengi na Wizara ya Kilimo na Chakula bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo linagusa Chama cha Ushirika, Chama cha Msingi cha Mlimani kiliona ni vema Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko asaidie kutatua tatizo hili. Nami naungana na Mheshimiwa Waziri, baada ya kuchukua hatua za awali. Naomba basi kufahamu Mheshimiwa Waziri amefikia wapi juu ya tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni shahidi kuwa Wilaya ya Babati, Tarafa ya Mbugwe ni eneo zuri la kulima zao la pamba na ushahidi ni pale Mheshimiwa alipokipongeza Chama cha Msingi cha Orodoi kilichokopa fedha *CRDB* na kununua pamba ya kutosha na kupata faida ya shilingi milioni 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mamlaka ya Bodi ya Pamba itoe msaada zaidi kwa kuimarisha soko la pamba eneo hili, hasa kwa kututafutia wawekezaji wa kuweka *ginnery* pale Mwada ambao tunategemea mwaka huu umeme utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii.

MHE.ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu uliopita nchi yetu ilikumbwa na upungufu mkubwa wa chakula. Katika Wilaya yangu ya Masasi, kulikuwa na kampeni kubwa ya kilimo cha zao la muhogo kama kinga ya njaa. Matokeo yake ni kwamba wananchi wamelima kwa wingi zao hilo na tunategemea mavuno kuwa mengi kuliko mahitaji, hivyo kuwa na ziada ya muhogo ambayo inahitaji kutafutiwa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani kuwa kwa vile muhogo ni chakula cha kujikinga na njaa, Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*SGR*) ingekuwa soko la kwanza la zao hilo la muhogo. Lakini hakuna kinachosemwa na *SGR* juu ya ununuvi wa muhogo ili iwe tahadhari ya njaa. *SGR* imepanga kununua tani 100,000 za mahindi kama kinga ya njaa.

Ikiwa *SGR* nayo haitaki kununua zao la muhogo, Serikali ieleze wapi muhogo huo utauzwa ili kuepusha muhogo mwingi kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, elimu kwa wakulima inahitajika ya utunzaji bora wa zao la muhogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la msimu wa mauzo wa zao la korosho. Niliwahi kuomba huko nyuma kuwa msimu wa mauzo ya zao la korosho uongezwe muda ili kumwezesha mkulima wa zao hilo kuuza korosho wakati wote. Zao la korosho hivi sasa linaonekana kuzaa wakati wote wa mwaka, pengine kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na zao lenyewe. Kuna korosho zinazaa kifuku na zingine huzaa kiangazi. Hivyo, mwananchi anahitaji soko wakati wote ili auze korosho zake. Kwa kukosa soko, mwananchi analazimika kuuza korosho zake kwa walangazi kwa bei ya chini sana ambayo haimpatii tija mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pia kuwa ushirika pekee ndiyo mkombozi wa wanyonge. Lakini bado wananchi wengi wanasisita kujiunga na ushirika kutokana na historia mbaya ya ushirika nchini. Bado ile dhana ya wananchi kudhani kuwa fedha zao zinaliwa na viongozi wa vyama vyao, ipo na vile vile dhana ya baadhi ya viongozi wa Vyama vya Ushirika kuwa wamechaguliwa ili wale fedha za wanachama, bado ipo. Kinachotakiwa sasa ni elimu kwa wananchi na viongozi, ili kuwaondoa hofu na kuwapa imani juu ya ushirika mpya. Ni muhimu vile vile viongozi wa ngazi zote kuwa karibu na wananchi juu ya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. DR. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumzie uchelewaji wa kuanza kwa masoko ya pamba katika Wilaya ya Uyui. Kuchelewa huku, imekuwa ni kero kubwa kweli kweli kwetu hasa kwa kuwa Bodi ya Pamba ilifanya kazi nzuri sana ya kuhamasisha. Wananchi wa Uyui waliitikia vizuri sana na kulima pamba nyingi sana, ikiwa ni mara ya kwanza kufanya hivyo rasmi katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha hapa ni kwamba pamba hii ilitakiwa kuingizwa soko na kununuliwa tangu mwishoni mwa mwezi Juni, 2004, lakini hadi jioni hii tunavyozungumza, bado hatujauza hata *kilogram* moja ya pamba huko Wilayani Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na juhudi mbalimbali za kuleta mnunuzi, ikiwa ni pamoja na *KACU* amba hivi sasa wamepewa vibali sita kwa ajili ya kuanza kazi hiyo mara moja. Maelezo ya awali yalikuwa kwamba *KACU* wangeanza kununua pamba hiyo tarehe 31 Julai, 2004 baada ya kupewa vibali, yapata wiki mbili zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kuwa inaonekana hata huo uhakika sasa haupo tena na kwa mujibu wa taarifa ya simu niliyoipata jioni hii kutoka *KACU*, sasa wataenda kununua pamba hiyo kuanzia tarehe 2 Agosti, 2004. Nilipouliza maandalizi yao ya kuanza zoezi hilo, bado nimepata wasiwasi kama kweli *KACU* wataanza ununuzi huo hiyo tarehe 2 Agosti, 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiyumkiniki kama kweli haya yanawatokea wakulima wetu ambao walihamasishwa kweli kweli na wao kuitikia kwa kishindo. Namtaka Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi hili ili masoko yaanze si zaidi ya wiki ya kwanza ya mwezi wa Agosti, 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zingatio hapa pia ni kwamba, kuchelewa kwa masoko haya kunakopelekeea utoroshaji wa pamba hiyo iliyolimwa kwa mbegu ya *UK91*, kutapelekeea kupotea/*contamination* ya mbegu hiyo mbali ya kuwaongeza ufukara wakulima wetu ambao watashindwa pia kurejesha mikopo yao na vijana wao ushuru, hali kadhalika na Halmashauri ya Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa sana. Hebu Waziri aweke nguvu zake zote hapa ili awanusuru wakulima wetu wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Ushirika na Masoko kwa jitihada wanazozifanya katika kuboresha ushirika nchini. Pamoja na hayo, ninazo hoja tatu ambazo ningependa zipatiwe majibu na Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa katika nchi ya Uganda imeanza ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Kahawa kama kile cha *TANICA*, kwa Serikali ya nchi hiyo kutoa shilingi bilioni 30. Je, Serikali inachukua hatua zifi katika kuhakikisha Kiwanda cha *TANICA* kinafanya kazi ya kusindika Kahawa na kuwakabidhi Vyama vya *KDCU Ltd.* na *KCU (1986) Ltd.* na kufuutilia ili kama hawawezi, apewe mwekezaji mwingine? Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutembelea kiwanda hicho ili kujionea matatizo yanayowakabili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa Serikali iliweka ukiritimba kwa kuzuia kisheria makampuni makubwa kama *OLAM (T) Ltd.* na *TANCOF* yasinunue kahawa huko vijijini, lakini huko Uganda bei ya kahawa iko juu, kitu ambacho kinawavutia wananchi wa Kagera kutaka kuuza kahawa zao huko Uganda. Je, Serikali inaruhusu Mikoa ya Rukwa, Lindi na Mtwara kuuza mahindi yao kwa nchi jirani, kuna nini kwenye kahawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa kuwa wananchi wa Karagwe kupitia Halmashauri yao ya Wilaya, wamefanya utafiti wa kuweza kupika pombe aina ya rubisi na kupata gongo ambayo inaweza kusafirishwa kwenye viwanda, ili kuondoa sumu inayosababisha madhara kwa afya ya binadamu. Je, Wizara iko tayari kuwasaidia

wananchi hao, wakati Halmashauri imekwishapitisha hilo kwenye vikao vyao? Hii inawezekana kwani hata katani ambayo majimaji yake yakigusa mwili wa binadamu yanawasha, inatafitiwa ili kupata pombe. Kwa nini hili la gongo ya rubisi, Serikali isilichangamkie? Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda huko Karagwe kuona jitihada hizo za wananchi, ili msaada kuweza kutolewa na Wizara?

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kwamba soko la kisasa kama lile la Kibaigwa, linajengwa pia Tandai, Kinole, Tawa na Matombo. Mimi na Mheshimiwa hamza Mwenegoha, tunashukuru sana. Tunaomba mawe ya msingi ya masoko hayo aje Waziri Mkuu au Makamu wa Rais au Rais Benjamin William Mkapa, kule Kinole na Tawa, ili wananchi waone juhudhi zetu na *MVIWATA*. Nawapongeza sana *MVIWATA*.

MHE. ABIDILLAH O. NAMKULALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe matatizo ya soko la korosho.

Kwanza ni kuhusu bei kubwa ya *Surphur*. Mwaka huu tumenunua kwa bei ya shilingi 20,000/= kwa mfuko wa shilingi 9,000=/. Hii inapandisha gharama za uzalishaji. Tatizo ni kwamba *Agent* wa kuagiza *Surphur* ni mmoja tu, hana mshindani. Wakulima wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu soko la korosho kuwa na bei ya chini hata kama Bodi ikitoa mwelekeo wa bei. Kwa mfano, shilingi 600/= kwa kilo, wanunuzi watanunua shilingi 150/= hadi shilingi 200/= kwa kilo na Serikali inafumbia macho. Mbona kwenye pamba leo Waziri Mkuu amekemea, kwenye korosho je?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu viwanda vidogo vidogo vya ubanguaji wa korosho. Ni muhimu, maana korosho ghafi, mnunuzi ni India tu. Hivyo, anatalulalia atakavyo, ila zilizobanguliwa, soko tele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kwamba soko la zao la muhogo tutafutiwe. Zao linakufa na umaskini unapenyea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni kuhusu zao la pamba. Turuhusiwe kulima Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. FRANK M. MUSSATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya mwaka 2003/2004 na nawatakiwa wafanye vizuri zaidi kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yazingatiwe yafuatayo:-

Kwanza, soko la tangawizi inayolimwa Wilayani Kasulu. Katika Jimbo la Kasulu Mashariki, wananchi wanalima tangawizi nyingi tu na hivi niandikapo kuna tani zisizopuingua 100,000 kwa misimu mitatu au hata minne. Zao hili halina mnunuzi. Naomba Wizara itusaidie tupate soko la zao hili ili wananchi waweze kupambana na umaskini uliokithiri katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangawizi hii inalimwa bila kutumia kemikali zozote na hivyo mimi nina amini kwamba zao linalotokana na kilimo cha namna hii ndilo linalotakiwa na soko la kisasa. Tafadhalii sana naomba tutafutiwe soko la tangawizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu hamasa ya Ushirika mkoani Kigoma. Hali ya ushirika mkoani Kigoma siyo nzuri hata kidogo. Umoja au ushirika haupo kabisa pamoa na kwamba mkoani humo umaskini umekithiri na ushirika ndio tu unawenza kukabiliana na umaskini. Naiomba Wizara ihamasishe moyo wa ushirika Mkoani Kigoma hasa katika Wilaya za Kasulu na Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA S. KIDUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi na utendaji wa Wizara hii unastahili kupongezwa kwa jambo moja kubwa na la msingi. Jambo hili ni lile la kukifanya chuo cha Ushirika cha Moshi kuwa Chuo Kikuu na hivyo kuimarisha na kukuza dhana ya Ushirika nchini. Nimpongeze Waziri mzoefu, Ndugu yetu, Mheshimiwa Sir George Clement Kahama, kwa kuona umuhimu wa kuimarisha dhana ya ushirika na wakati huo huo kuendeleza mabadiliko ya kiutendaji kukabiliana na matatizo ya wakulima kila yalivyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara itoe kipaumbele cha kwanza kukiimarisha chuo cha ushirika haraka ili kiwe chimbuko la ubunifu wa mbinu za kisasa za ushirika wa kisayansi unaolingana na mazingira ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu kama nchi inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Waziri na Katibu wake Mkuu wa kuona umuhimu wa kuajiri wasomi wazuri kama viongozi na watendaji wakuu Wizarani. Ubora wa jambo hili umedhihirika katika ujenzi wa mwelekeo mpya wa Wizara kidhana na kiutendaji.

Pendekezo moja la msingi ni kwamba Wizara inahitaji kuweka uzito na msisitizo katika vyama vyaya ushirika vinavyoshughulikia usindikaji wa mazao. Tatizo la uduni wa bei za mazao yetu linatokana na kuyauza katika hali ghafi. Kwa mfano, pamba yetu isingekuwa na bei ya kuyumba kama tungekuwa na viwanda vyaya kutengeneza nyuzi na hata vitambaa na hivyo kuuza nguo au angalau hata nyuzi.

Aidha, sehemu kubwa ya Kahawa na Korosho zetu zingesindikwa kabla ya kuuzwa nje ya nchi. Muhimu hapa ni kuwa ushirika uhamasishe viwanda vidogo na hata vyaya kati vyaya *processing* vyaya mazao yetu, hasa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuipongeza tena Wizara hii kwa kazi nzuri na hivyo naunga mkono wapewe fedha walizoomba.

MHE. BUJIKU K. P. SAKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na viongozi wengine wote wa Wizara hii changa wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri, ngumu na kubwa wanayoifanya katika kuimarisha Wizara hii changa na muhimu kwa wakulima na wazalisha mali wa nchi hii. Nawapongeza vile vile kwa hotuba nzuri ya mwaka huu ambayo kwa maoni yangu imeandalifi vyema na kwa umahili zaidi kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imeonyesha dhahiri kuwa Wizara inaimarika. Aidha, kazi ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Wizara limeipatia Wizara hii hadhi ya kutosha mbele ya macho ya wananchi na wageni kutoka nje ya nchi. Kifuatacho sasa ni kazi zitakavyolingana na hadhi ya jengo hili hata kuzidi. Ninawatachia heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kwimba tunalo zao la Dengu. Soko lake halieleweki na ni la kusua sua sana. Mnunuzi hajulikani kwa uhakika na haileleweki wanunuzi wake wanarabitiwa kwa utaratibu gani. Wanunuzi wa zao hili ambalo ni mkombozi wa wakulima wa zao hili Wilayani Kwimba, Shinyanga na maeneo wanakolilima ni kama walangazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ombi langu kwa Wizara hii ni kuliangalia zao hili kama zao mbadala kwa zao la Pamba, pindi pamba inapogoma. Zao hili iwapo mnunuzi au wanunuzi wakihamasishwa na kuwekewa utaratibu mzuri na soko maalum likapatikana litainua sana hali ya kifedha/kiuchimi katika maeneo haya. Nashauri Mheshimiwa Waziri au Naibu wake akawatemelea wakulima wa zao hili Wilayani Kwimba na kwingineko kwa ajili ya kuwahimiza na kutoa elimu sawia ya zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na zao hili lipo zao la Mironge. Nashauri zao hili ambalo tofauti na mazao mengi ya kudumu, hili ni zao linalochukua muda mfupi toka kupanda na kuanza kuvuna. Iwapo zao hili na elimu muafaka itatolewa kwa wakulima wa maeneo kusikokuwa na mazao ya biashara ya kudumu, zao hili laweza kuwa mkombozi kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ushauri wangu ni kuwa elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi, elimu ambayo itapelekea wananchi kuanzisha ushirika wao wa mazao husika na kwa msaada wa Wizara hii wakionyeshwa jinsi ya kupata masoko ya mazao yao watahamasika kulima kwa wingi.

MHE. OMARI S. CHUBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa George Kahama, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba, pamoja na wataalam wote kwa hotuba nzuri ambayo ni ya kuleta ukombozi wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja hii, napenda niende kurasa 45 hadi 46 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, juu ya mikakati ya kutafuta masoko ya mazao ya kilimo. Katika eneo hili mpango wa kongamano hiyo ihusishe wakulima walete mazao yao ili waweze kupata wafanyabiashara ambao watakuwa tayari kununua mazao hayo kwa bei nzuri. Mazao hayo ni ufuta, mbata, mchele, asali, mbarika, nyonyo, maharage, mbaazi, machungwa na mengine ambayo yanaiza kutokana na kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umeishafika kwa Wizara kutafuta njia ya kuwawezesha wakulima mitaji kama wanavyofanyiwa wakulima wa tumbaku na mwani, katika kilimo hiki wanunuzi hutoa fedha kwa wakulima fedha za kulimia na wakati wa kuvuna yule aliyetoka fedha ndiye anauziwa mazao hayo. Hatua hii itaondoa bughudha kwa wakulima mfano ufuta ambao wananchi wanaonewa kutokana na mbinu za ujanja wa wafanyabiashara ambao ibada yao ni kuwanyonya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nachangia kila mwaka juu ya mtambo wa kukamua machungwa ambayo huwa yanaiza. Hapa namwomba Mheshimiwa Waziri amtume Dr. Turuka, aambatane nami twende Pemba, Msumbiji kutafuta wawekezaji kwenye machungwa kuepusha wananchi wa jimbo langu kurubuniwa na wafanyabiashara kutoka Kenya ambao wanaumizwa katika biashara hii. Naomba safari hii ifanyike mwezi Agosti mapema ili kuwahi msimu wa machungwa. Kwa kuwa kilio hiki ni cha siku nyingi naamini suala hili litapata kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho natoa shukrani zangu kwa ushirikiano mkubwa unaotolewa na Wizara kwa Kamati yetu ya uwekezaji na biashara na Wabunge binafsi wakati wowote wa shughuli zetu za kibunge na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri Mheshimiwa George Kahama, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezikiah Chibulunje na Katibu Mkuu, Dr. Ladislaus Komba na safu nzima ya watalaam kwa hotuba nzuri na utekelezaji mwema wa ahadi walizotupa katika mkutano uliopita wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakumbuka maombi yaliyoletwa mbele yako na Chama cha Ushirika cha Wakulima wadogo wa Chai wa Wilaya ya Rungwe kwamba waweze kuuza chai yao moja kwa moja kiwandani Katumba. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuteua Tume iliyokwenda Wilayani na kuwahoji wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililozuka ni kwamba mwaka mzima umepita tangu Tume hiyo ipite kule Wilayani lakini hakuna maelekezo au maagizo toka Wizarani yaliyopelekwa kwa wakulima hawa na uongozi wa umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Wizara kuhusu suala hili. Naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongozi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu na wataalam wote hotuba imeandikwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kuzungumzia kidogo kuhusu uboreshaji wa mazao ya biashara ambayo yanaweza kuuzwa nje ya nchi. Kama tutaendelea kulima kwa kilimo cha mkono, bado tusitegemee kama tutajikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kiwe kilimo cha kuelewaka ni lazima tulime kwa kutumia trekta, ushauri wangu ni kuwa mshirikiane na Wizara ya Kilimo na Chakula na kuwasaidia wananchi ambao wataonyesha jitihada za kuanzisha vituo vyta kukodisha matrekta kwa kutoa mikopo nafuu kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi ambao wangependa kuzalisha mazao ya kusindika hivyo inapotokea nafasi ya kushiriki maonyesho ya Kimataifa nje na ndani ya nchi wapewe nafasi ya kushiriki kwani mara nyingi wanaoshiriki ni wale wale tena bila kuwashirikisha waishio vijijini, mazao ya kusindika ndio yanayoweza kumkomboa mwananchi wetu, naomba Wizara hii itilie mkazo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SACCOS* ndiyo ukombozi, zimeonyesha kusaidia kupambana na umaskini vizuri hivyo ni vema tukatilia mkazo jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongozi kwa *CRDB* kwa kushirikiana vizuri na *SACCOS* zetu kwa kuziwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii ya Waziri wa Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapa rambirambi wafiwa wote ikiwemo familia ya Ndugu yangu Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Ibara 53 sehemu ya (d) imeelekezwa uimarisaji wa miundombinu ya masoko. Mheshimiwa Waziri pia anasisitizia kuwa miundombinu ya masoko itakuwa ya kudumu na endelevu. Nampogeza sana kwa hili. Lakini ukirejea kwenye ibara hiyo hiyo Kifungu cha (a) tunaelekezwa juu ya kukamilishwa rasmi kwa ya sera ya uandaaji wa masoko ya mazao ya kilimo. Wakati Kifungu (b) cha ibara hiyo hiyo inaeleza kujasirisha wakulima na wafanyabiashara wa mazao na bidhaa za kilimo na kuwaunganishia na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa mikakati hiyo ila tu inaonyesha duplication of resources and efforts katika ya Wizara yake na ile ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara imeandaa mikakati ya kukuza uuzaji wa bidhaa nje kwa kutumia fursa za biashara zilizo wazi duniani kama vile *AGOA*, *EBA* na *KKD*. Hapo hapo Wizara ya Viwanda na Biashara ili/na inatarajia kuhodhi majengo yaliyo Ubungo yanayojihuisha na *EPZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Wizara ya Ushirika na Masoko imekarabati miund mbinu ya masoko na kuwa na mikakati ya kujasirisha wakulima na wafanyabiashara za kilimo na kuwaunganishia na masoko, wakati fursa za *AGOA* na zingine zipo, je, masoko gani Wizara inatafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hayo masoko yaliyokarabatiwa angalau yasitumike kwa *EPZ* kwa mazao ya kilimo? Kuna sababu na kila haja ya Wizara hizi mbili kukutana na *ku-streamline strategies* ili kutumia rasilimali adimu za nchi kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuwa sehemu nyingi za aina hizi kwenye Wizara hizi ambazo lazima zitazamwe upya. Ikiwezekana *strategies Audit at ministerial ifanyike* ili kuainisha ipasavyo majukumu kamilifu kwa kila Wizara bila ya kurudiana majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa kazi nzuri anayoifanyia nchi hii hasa kwenye kuwezesha wananchi kijiunga na *SACCOS* na hivyo kuwawezesha kupata mitaji hasa kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahimiza Wizara uanzishaji haraka iwezekanavyo wa Benki tarajiwa ya ushirika ili malengo ya Sera ya Ushirika iweze kutekelezeka kwa urahisi na hasa kabisa kuongezea pato la wananchi kwa mazao yao kwa mfumo wa Stakabadhi za mazao kama alivyoainisha kwenye hotuba yake ibara 53 sehemu ya (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. ALLY MACHANO MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa vifo vilivyotokea kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambavyo vimetokea tukiwa hapa Bungeni kifo cha Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira wa Jimbo la Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu awape subira na uvumilivu ndugu na wapigakura wote wa Marehemu na Mola azilaze roho za Marehemu pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia kuchangia katika hotuba hii iliyopo mbele yetu kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa utendaji wao na matayarisho ya bajeti hii ambayo imeletwa mbele yetu ambayo tunaijadili, kwa upande wangu sina budi niseme naiunga mkono kwa sababu nahisi ina mwelekeo wa kuleta mafanikio mazuri kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie sehemu ndogo ambayo nitayatolea mapendekezo, kwanza, naomba Mheshimiwa Waziri akumbuke lipo jambo ambalo muda mrefu halizungumzwi sijui jambo hili limefikia wapi, jambo lenyewe ni lile la kugawana mali ambayo ilipatikana katika vyama vya ushirika vya Tanzania Bara na vile vya Tanzania Visiwani ambavyo kwa sasa vinafanya kazi zake kwa utaratibu mwingine ambao kwa sasa siyo ushirika kama ulivyokuwa wakati uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa wana uhusiano wa karibu lakini na utakuta kuna mambo yanahitaji ufanuzi namna gani mali hizo zimegaiwa ili wananchi wetu wayaelewe kwa sababu kwa muda huu wanayaaulizia na kama bado mali hizo hazijagaiwa tuelezwe ni muda gani na ni sababu gani zinazosababishwa hatua hiyo ichukue muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichangie katika hali ya masoko ya kuuza. Mazao yanayolimwa hapa nchini naomba Mheshimiwa Waziri aangalie hali ya wananchi kuuza mazao ya chakula ovyo nchi jirani kwa bei nafuu inaweza kutuletea upungufu wa chakula kwa muda mfupi na baadaye kuomba msaada tena kwa nchi jirani na huenda tukauziwa kwa bei ya juu kwa sababu wananchi wetu wanaouza chakula hicho wana shida zinazowakabili waendelee kuuza, lakini pia wahamasishwe wabakie na chakula cha kuwafaa baadaye kujiepusha na uhaba wa chakula kitakachowafaa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yamezungumziwa na wachangiaji wengi, mimi ningeomba Wizara hii iendelee kutafuta masoko ya kuuza matunda ambayo yapo mengi Tanzania ambayo hupatikana katika mikoa mingi hapa nchini kwetu yanaharibika ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Wizara iendelee kutafuta wahisani wa kutujengea masoko kama lile la Kibaigwa hata kama soko hilo litajengwa kwa kutumia mkopo, kwa hili sina budi kuwapongeza wote waliofanikisha mradi wa soko hilo la Kimataifa.

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri aliyoisoma leo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la bei za mazao yetu limekuwa la muda mrefu na huenda ikapelekea wakulima kukata tamaa na hatimaye kuamua kuacha kuzalisha mazao hayo. Wakati tukiwa na vyama imara vya ushirika, suala la bei lilisimamiwa vyema na pale bei zilivytetereka vyama hivi viliweza kuziba pengo kwa kuwasaidia wakulima katika upatikanaji wa pembejeo na zana zingine za kilimo ili kuwawezesha kuendelea kuzalisha. Katika mfano wa sasa wa soko huria, ambapo kila mwenye uwezo anaruhusiwa kununua mazao bado haijawa na mafanikio makubwa kwa sababu hata hawa wanunu si wenye uwezo usiotiliwa mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na matatizo mbalimbali yaliyovikumba vyama vya ushirika na hatimaye kupelekea kufilisika kwa vyama vingi vya ushirika, kikiwemo chama cha ushirika mkoani Mara, *Mara Cooperative Society (MARACOP)* bado mkombozi wa dhati wa mkulima wa Kitanzania ni vyama imara vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hususan wakulima ni vyema wakaelimishwa umuhimu wa ushirika na hasa wao wakielewa nafasi yao ndani ya vyama hivi vya ushirika. Lakini vyama vyetu vingi vya ushirika vimefilisika na hatua za kisheria hiajachukuliwa kwa wale wote waliohusika na ubadhilifu mkubwa wa fedha za ushirika. Hii ni dosari kubwa kwenye sekta ya ushirika. Wananchi wangependa kuona hatua zinachukuliwa kwa wale wote waliohusika na ubadhilifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufilisika kwa vyama hivi vya ushirika kuna madeni makubwa ambayo vyama hivi vinadaiwa. Hivi sasa chama cha ushirika cha Mara kipo chini ya mufilisi, lakini bahati mbaya sana baadhi ya mali hazijauzwa kwa maagizo toka Serikali. Hii imepelekea ucheleweshaji wa malipo ya madeni mbalimbali ambayo *MARACOP* inadaiwa. Wafanyakazi wa ushirika wa Mara bado wanadai stahili zao mbali na hii imechukua zaidi ya miaka saba hadi nane na wengine wamekwishapoteza uhai kwa matatizo na adha mbalimbali zilizowasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo ya hatua ambazo Serikali inachukua kuhusiana na matatizo yaliyoikumba *MARACOP* hasa kuhusu madeni ya watu mbalimbali na pia madai ya wafanyakazi na pia hatima ya mali zilizositishwa kuuzwa na Serikali.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii imo mbioni kukamilisha maandalizi ya sera ya masoko ya mazao ya kilimo (*Agricultural Marketing Policy*) na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wake, nilitaka kujua ni vipi Wizara hii ya Ushirika na Masoko itaiwezesha Zanzibar ili nayo inufaikie na fursa mbalimbali za mauzo ya bidhaa nchi za nje kama vile *AGOA*, *EAC*, *SADC* na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuelezwaa mustakbali wa soko la Karafuu nchi za nje, kwani kumekuwa na kilio kutoka kwa wakulima wa Karafuu huko Zanzibar kwamba biashara ya zao hili ni kwa nini hadi leo linadhibitiwa na Serikali? Kuna ugumu gani unaozuia wakulima wa zao la Karafuu kutoruhusiwa kuuza mazao yao nchi za nje ili kujiongezea kipato kutokana na ubora wa soko la nje kuliko bei inayolipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata faraja kuona kwamba Wizara hii inatambua kwamba mazao ya bidhaa zitokanazo na mifugo soko lake kwa kiwango kikubwa linategemea soko la ndani. Lakini taarifa tuliyoelezwa hapa Bungeni na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ni kwamba ulaji wa mazao yatokanayo na mifugo hapa Tanzania ni mdogo sana ukilinganisha na mahitaji yanayotakiwa na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Wizara hii kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza ni lazima kuandaa utaratibu wa kusaidia kusambaza uelewa kwa wananchi waone umuhimu wa kutumia viwango vinavyotakiwa kwa mazao yanayotokana na mifugo. Hatua hii italikuza soko la ndani ambalo ndio tegemeo kuu kwa wafugaji.

Pili, ni kuandaa mikakati ya kutoa elimu kwa wauzaji na wasindikaji wa mazao ya mifugo kwa mujibu wa matakwa ya soko la nje ili nchi yetu nayo ipate fursa ya kupenga katika soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhakikisha kwamba wazalishaji na wasindikaji wa mazao ya mifugo wanapatiwa mikopo kwa ajili ya kuwekeza kikamikilifu katika shughuli zao na hivyo kukuza *quality standards* zitakazowawezesha kupata soko la nje na bei iliyo bora. Huu utakuwa ni ukombozi kwa wafugaji, wasindikaji na wauzaji wa mazao yatokanayo na mifugo.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza hotuba hii kwa muda mrefu, kwa kweli nimeridhika sana na hatua ambazo zimechukuliwa na Wizara katika muda mfupi sana wa uhai wake. Ni vizuri nikiri kuwa kuna mapinduzi ya hali ya juu ambayo yamefanywa na Wizara ili kuhakikisha kuwa nchi yetu ambayo ni ya wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara inapata neema hasa tukizingatia kuwa wenzetu duniani kote wanachukua hatua madhubuti katika kufanya mabadiliko ambayo yananeemesha wananchi wao.

Kitendo cha Serikali kukubali Chuo cha Ushirika cha Moshi kiwe Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*The Moshi University College of Cooperative and Business Studies - MUCCOBS*) ni ushahidi wa waziwazi kuwa kweli Serikali ya Tanzania imekusudia kuleta mapinduzi ya hali ya juu ya kiuchumi. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa busara nami naahidi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Siha tutatoa kila aina ya ushirikiano kwa Taasisi hii mpya na muhimu ili iweze kukua kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kitendo cha kuamua kuanzisha *The Cooperative Bank* kwa ajili ya wana ushirika ni ishara ya wazi kuwa kweli sasa Serikali iko *serious* katika kupambana na umaskini. Ni kwa msingi huo naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda baada ya hayo yote kuchukua fursa hii kukumbushia tena tatizo la wananchama wa *Siha Kheyo Cooperative Society* ambao wamekuwa wanadai haki yao ya msingi na ya Kikatiba ambayo wanadai kuheshimiwa kwa maamuzi yao katika vikao mbalimbali ambayo yana nia ya kutatua matatizo yao ya kimenejimenti na uongozi.

Baada ya Bwana Baker, kukimbia bila kulipa gawio lao la miaka ya nyuma katika shamba la Kifufu, wanachama wameamua kuweka uongozi mpya madarakani lakini vikao hivyo vimekuwa vipindishwa na Mrajisi Msidizi wa Mkoa kwa kisingizio cha kusubiri kanuni mpya zitokanazo na sheria mpya ya ushirika ya mwaka 2002. Naiomba *centre* iingilie kati suala hili ili kuepusha mgogoro na malumbano yasiyo ya lazima.

Mwisho nakumbushia marejesho ya makato ya *KNCU* yaliyofanyika mwaka 1989 kiasi cha shilingi 519,000,000/= yaliyofanywa kwa maelekezo ya Serikali kama inavyodaiwa na Bodi ya Kahawa. Kumbukumbu zote zimewasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono hoja.

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na maafisa wote wa Wizara hii kwa vile Wizara hii ni muhimu sana, wananchi walio wengi wanaitegemea sana. Serikali kwa umuhimu wake kwa kuwa wanaushirika wengi hawapata utaalam wa kutosha ni vizuri Wizara iwe na mpango maalum wa kutoa mafunzo kwenye vikundi vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa ujenzi wa soko la kisasa pale Kibaigwa, jambo la kufurahisha hivi sasa wafanyabiashara wamepangwiwa eneo maalum ya kuuzia mazao yao badala ya mazao kuwekwa katika maeneo yasiyo na usalama. Ni vizuri Serikali isiishie hapo Kibaigwa tu, lakini ni bora ujenzi wa masoko uendelee Wilaya zote kwa sababu zipo Wilaya ambazo hazina masoko ya kuhifadhia bidhaa zao, hivyo masoko yajengwe kulingana na bidhaa zinazozalishwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Mkoa wa Tanga unazalisha sana zao la machungwa lakini hapana soko la kuhifadhia machungwa hayo. Hivyo wananchi na wakulima wanahitaji kupatiwa soko ili waweze kuwa na uhakika wa kujuwa mazao yao yatanunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ianzishwe Benki maalum ya Taifa ya Ushirika itakayotoa mkopo kwa masharti nafuu na kuviunganisha vyama vya ushirika na huduma za fedha ili kuwapunguzia matatizo ya kuhangaika kutafuta fedha za kuanzia biashara kwa wanaushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wana ushirika kuzalisha bidhaa hizo tatizo lililojitokeza ni mahala pa kuuzia bidhaa zao, kwa hivyo basi, naiomba Wizara hii iweke utaratibu maalum wa kuhakikisha kuwa bidhaa inayozalishwa inapatiwa soko la kuuzia. Lakini jambo lingine la kufanya Wizara ingeorodhesha Mashirika yote kila Wilaya ili kujua ni matatizo yapi yanayowakabili wanaushirika. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Asante sana.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa uwasilishaji mzuri wa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo matatu yafuatayo:-

Kwanza, naipongeza Wizara kwa kuanzisha mradi wa kuendeleza na kuboresha biashara na soko la zao la Kahawa unaofadhiliwa na mfuko wa Kimataifa wa mazao (*Common Fund for Commodities - CFC*). Napongeza utaratibu wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za mazao kwenye maghala kama dhamana ya kupata mikopo, baada ya kufanikisha katika mikoa ya Kilimanjaro na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakulima waeleweshwe ubora wa mfumo huu, ili kwa uangalifu na uaminifu mkubwa wa wakulima, watendaji na viongozi wao uwanufaishe kwa kuboresha soko na bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Benki ziombwe kutoweka riba kubwa itakayoondoa faida ambayo angeipata mkulima. Naomba pia maghala ya wakulima yakaguliwe na kupewa uthibitisho wa uimara wake kabla ya kuruhusiwa kutunza Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninalochangia ni kuishauri Serikali sasa ifanye kweli kuhusu hatua ya usindikaji wa mazao kabla ya kuyauza. Serikali iache kufanya majaribio au ushauri, bali iwe ni lazima, hatuwezi kupata ubora, madaraja na ufungashaji wa mazao wa hali ya juu, Serikali ikihimiza tu sheria ya kuhakikisha mazao yanasisindikwa kabla ya kuuzwa iwepo. Hali hii itaongeza ajira, bei na ongezeko la mazao kwani wakulima wataongeza uzalishaji. Japokuwa kilimo ni uti wa mgongo iwapo hakuna soko zuri, wakulima watapunguza uzalishaji na hali ya nchi kiuchumi haiwezi kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu na mwisho, ninalopenda kuishauri Wizara ni kutangaza soko la ndani. Mazao kama matunda na mboga mboga yanaweza kutumika vizuri hapa nchini na kuinua kipato cha wakulima. Hata hivyo soko la ndani bado liko chini sana na hivyo ulaji na utumiaji wa matunda na mbogamboga bado ni wa kiasi kidogo. Hii inathibitishwa na mazao mengi yanayooza na kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, ninashauri Serikali ione uwezekano wa kuanzisha vikundi vyta wazalishaji wadogo wadogo, kisha waanzishiwe viwanda vidogo vidogo ili wasindike matunda na mbogamboga, vifaa kutumika wakati wote baada ya kuachwa kuharibika. Aidha, ulaji au utumiaji wa matunda na mbogamboga vihimizwe kwa wananchi wote walau kila mlo mmoja kwa siku pasikose mboga na matunda. Lengo ni kuinua soko na kuboresha afya za Watanzania. Nawasilisha.

MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Pili, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya ya kufufua ushirika katika nchi yetu. Ushiriki ni mkombozi wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa Maofisa Ushirika ni wachache na kwa kuwa Maofisa ushirika ni muhimu sana katika suala zima la kutoa elimu ya ushirika kwa wananchi na hasa vijijini ambapo wakulima wengi wapo wanaishi. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuajiri Maafisa Ushirika kila Kata na kuwapatia vitendea kazi nya kutosha ikiwepo Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla?

Pili, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa wananchi wanaendelea na juhudi za kuunda vyama nya ushirika nya msingi, vyama nya ushirika nya wafugaji na *SACCOS* na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa wanalima/wanazalisha kwa wingi mazao ya mbegu za mafuta kama vile Karanga, Alizeti na Ufuta tatizo kubwa ni soko la kuza mazao hayo ili wananchi wapate fedha za kuboresha maisha yao, je, Serikali itakubaliana nami kwamba iwapo chama kikuu kitaundwa Wilayani Mpwapwa kitasaidia sana wakulima kuza mazao yao na pia wananchi watahamasika na kulima mazao hayo kwa wingi kwa vile soko lipo na kusaidia wakulima kupata mikopo kwa ajili ya kuboresha kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali iliahidi ndani ya Bunge hili Tukufu kuwa wataunda Bodi ya Mazao mchanganyiko yakiwemo mazao ya mbegu za mafuta kama vile Karanga, Alizeti, Ufuta na kadhalika, Bodi hii ndiyo itasaidia kuboresha hapa nchini. Je, Bodi hiyo imeundwa na kama bado kuna sababu gani za msingi za kutokuunda Bodi hiyo?

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga soko la mazao ya mbegu za mafuta Wilayani Mpwapwa kama Karanga, Alizeti, Ufuta na kadhalika?

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba ya Waziri, naiunga mkono mia kwa mia. Sasa ni ukweli usiofichika kwamba kuna mabadiliko makubwa na maendeleo mazuri katika kazi za Wizara hii Ushirika na Masoko umeendelea kuimarishwa na mfumo wa masoko ya mazao umeboreshwa zaidi. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Wizara kwa kufanya juhudi kubwa za kukipandisha hadhi Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Sokoine. Ingawa naipongeza Wizara kwa hatua hii, bado sikubaliani na mtindo wa kuunda Vyuo Vikuu Vishiriki kama cha Moshi.

Hoja yangu ni kuwa bado Chuo cha Ushirika Moshi kingekuwa Chuo Kikuu kamili bila ya kuongeza gharama za uendeshaji zinazotokana na kuwa Kishiriki na hii haitakuwa kitu kigeni na wala chuo cha ushirika Moshi hakitakuwa cha kwanza kuwa Chuo Kikuu kamili. Mifano ipo ya Vyuo vya Serikali na hata vya binafsi. Bila ya kuwa na *time frame* ya kuwa kishiriki, mtindo huu hautasaidia kuongoza vyuo vikuu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia ukurasa 33 hadi 48 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inazungumzia juu ya utekelezaji wa mpango wa kazi kwa mwaka 2003/2004 katika sehemu hii, Waziri hasemi lolote juu ya uanzishaji wa Bodi ya Mazao mchanganyiko ahadi ambayo amekuwa akitoa Bungeni. Hata katika kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2004/2005 ukurasa wa 55 hadi 66, Waziri yuko kimya kabisa kuhusu uanzishaji wa Bodi ya Mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea Wizara imeliacha wazo hili ambalo iliahidi italifanya kazi, tatizo ni nini? Je, ni kweli kuwa mazao kama Karanga, Alizeti, Ufuta, Kunde, Maharage, Mahindi na kadhalika hayahitaji chombo cha kuendeleza mazao haya? Je, ni kweli hakutakiwi utafiti wa mbegu bora za mazao haya? Je, ni kweli masoko ya mazao haya hayahitajiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa wakati wakulima wa Pamba, Kahawa, Chai, Mkonge, Tumbaku, Korosho (*traditional crops*) wameundiwa bodi na zinawasaidia sasa, je, wakulima wa *non-traditional crops*, mazao yasiyo asilia ya mchaganyiko ambayo ni tegemeo la wakulima wengi nchini wanasaidiwa na chombo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma niliwahi kutoa hoja Bungeni kuwa tusiendelee na utaratibu wa kutofautisha *traditional crops* na *non traditional crops*. Tofauti hii sasa imepitwa na wakati, *it is a colonial legacy* ambayo lazima tuiondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atoe maelezo ya kutosha kwa nini Bodi ya Mazao mchanganyiko haijaundwa hadi leo, kuna tatizo gani? Je, ni tatizo la *mind set* iliyopo Wizarani juu ya mazao mchaganyiko? Je, kutokuwepo umuhimu wa mazao haya katika uchumi wa Taifa? Tatizo ni nini?

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote katika Wizara hii.

Naipongeza Wizara kwa kuhamasisha na kuendeleza vyama vya ushirika, aidha, kuviwezesha baadhi ya vyama vya ushirika nchini kushindana katika ngazi za Kimataifa na kufanikiwa kupata ushindi (medali). Naiomba Wizara kuviendeleza vyama vya ushirika na kuviongezea uwezo pamoja na kuvionyesha nafasi yao kimasoko Kimataifa na kuviwezesha kutumia fursa hizo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 1980 tulikuwa na Jumuiya ya Washirika Tanzania. Jumuiya ambayo ilivunjika mwaka 1993. Wakati inavunjika

Washirika ilikuwa na wanachama au vyama vya ushirika 27 kati ya hivyo vyama 22 vya Mikoa ya Tanzania Bara na vyama vitano vya mikoa ya Tanzania Zanzibar.

Wakati Washirika inavunjika ilikuwa inamili mali na madeni, hata hivyo kwa wakati huo mali na madeni hayo hayakugaiwa kwa wanachama, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilikabidhi mali na madeni ya Washirika kwa Kabidhi Wasii (*Public Trustee*) ilipoanzishwa *Tanzania Federation of Cooperative (TFC)* ambayo inajumuisha vyama vya Ushirika vya Tanzania Bara tu walimtaka Kabidhi Wasii awakabidhi mali za Washirika na alipokataa kwa vile madai hayo hayakushirikisha vyama vitano vya Zanzibar Kabidhi Wasii alikataa, hatua ambayo ilipelekeea *TFC* kufungua kesi Mahakamani kwa kuwashitaki (wadaiwa) Kabidhi Wasii na vyama vitano vya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliingilia kati na kutaka shauri hilo litanzuliwe nje ya Mahakama, hatua ambayo vyama husika viliteua wataalam wanne, kati ya hao wanasheria wawili na Wahasibu wawili kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kwa madhumuni ya kutathmini mali na madeni ya Washirika, aidha, kutambua stahiki ya kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hiyo iliwasilisha ripoti yake tarehe 9 Mei, 2003 katika kikao kilichofanyika Moshi ambacho kilihuisha Halmashauri ya *TFC* na vyama vitano vya Zanzibar. Kikao kilipokea na kuithibitisha ripoti hiyo kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kwa vile *TFC* inaendelea kunufaika na mali za washirika imeendelea kupunguza maamuzi hayo mpaka leo vyama vitano ya Zanzibar bado havijapewa stahiki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudhi mbalimbali za vyama husika yaani vyama vitano kujaribu kufuatilia pia kuiomba Wizara ya Kilimo na Ushirika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kusaidia ufumbuzi wa tatizo hilo lakini bado hakuna mafanikio yoyote yaliyopatikana. Kutokana na hayo namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufanuzi wa yafuatayo:-

Kwanza kituo gani kinakwamisha kumalizika kwa tatizo hili unaviambia nini vyama vitano vya ushirika vya Zanzibar katika ufumbuzi wa tatizo hili. Naunga mkono kwa kutegemea majibu muafaka yenye kutoa ufumbuzi wa tatizo.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zao kwa kazi nzuri wanayofanya katika kujenga upya ushirika hapa nchini. Kazi kubwa kwa Wizara hii ili ushirika ushamiri upya ni kujenga mionganini mwa wanaushirika tabia ya kuthamini, kuheshimu, kulinda kwa uaminifu na kuendeleza mali za ushirika, kwa manufaa ya wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo sasa naomba kutoa maelezo, pongezi ushauri na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, uboreshaji wa wanaushirika wa Wilaya ya Muheza wafugaji wa ng'ombe wa maziwa. Tunaipongeza Serikali ya Uhlanzi kwa mchango wake mkubwa

kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga chini ya Chama Kikuu cha Wafugaji Mkoa wa Tanga (*TDCU*). Wiki hii, tarehe 27 Julai 2004 mradi mpya wa kopa ng'ombe lipa maziwa ulizinduliwa katika Wilaya ya Muheza, Mjini Muheza ambapo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, alikabidhi ng'ombe wa mradi kwa wanachama wa vyama vya msingi vya Ushirika chini ya Chama Kikuu cha *TDCU*, mpango ambao umedhaminiwa na Taasisi ya *Farm Friends (T) Ltd.* Chini ya uhisani wa *Farm Friend Netherlands* ya Uhlanzi. Mpango huu unakwenda sambasamba na mpango wa *Pingoni Youngstars Dairy Settlement* wenye lengo la kuongeza uzalishaji wa maziwa na kuboresha hali ya wafugaji, ambao ni wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wa hali ya juu, Wizara ya Ushirika na Masoko imekubali kuwapa mafunzo ya kibiashara wanachama hao wa ushirika wa wafugaji chini ya *TDCU*. Naipongeza sawa Wizara kwa uamuzi huo.

Pili, kuisaidia *TDCU* na *Tanga Fresh* kujenga kiwanda. Kwa kuwa *TDCU* imeonyesha kwa vitendo mpango wa kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa mpango shirikishi wa wafugaji wadogo wadogo na kwa kuwa inaonekana dhahiri kwamba Serikali haitaweza kuwapa *TDCC* kilichokuwa kiwanda cha maziwa cha *Tanga Dairy* ambacho kimeuzwa lakini hakizalishi wala kusindika maziwa basi Wizara ya Ushirika na Masoko ichukue jukumu kama changamoto kuisaidia *TDCU* kuandika mchanganuo na kuwawezesha kupata mkopo wa kuwawezesha kujenga na kuendesha kiwanda cha kisasa ili kusindika maziwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii *TDCU* itaweza kukabiliana na ongezeko kubwa la uzalishaji wa maziwa chini ya mpango endelevu kati ya *Farm Friends Netherlands* na Taasisi ya uzalishaji mitamba ya *Holland Dairies (T) Ltd.* vinginevyo wanaushirika watakosa mahali pa kuuza maziwa yao kwa mpango wa kopa ng'ombe lipa maziwa ulioanzishwa hivi karibuni.

Tatu, ombi la wananchi wa Muheza kujengewa Soko la Kimataifa la Matunda. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Muheza nawasilisha rasmi ombi kwa Wizara ya Ushirika na Masoko kuwzesha kujengwa kwa soko la Kimataifa la Matunda, Muheza. Sehemu kubwa ya machungwa na matunda mengineyo kutoka Muheza yanasa firishwa nchi jirani ya Kenya na pia katika masoko ya ndani ya nchi hasa Moshi, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa na Mbeya. Kwa msingi huo upo uwezekano kwa matunda hayo kuingia nchi jirani za Zambia, Malawi na *DRC* (Kongo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuboresha kilimo cha machungwa Wilayani Muheza, kwa lengo la kuwzesha kuboresha ubora wa machungwa na matunda mengine kuweza kushindana katika soko la Kimataifa, umeanza kufanyiwa kazi kupitia Taasisi (*NGO*) ijulikanayo kama *DAIPESA*. Nimefurahi kusikia kwamba Wizara ya Ushirika na Masoko inafahamu mpango huo na kwamba *DAIPESA* wamekabidhi Wizarani nakala moja ya ripoti ya kazi yao ikiwa ni pamoja na soko la machungwa nje ya Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maendeleo hayo na kwa kuzingatia uzalishaji wa matunda na mbogamboga katika Wilaya jirani za Lushoto, Korogwe, Handeni na Pangani, kuna haja ya kulipa uzito ombi la Muheza kujengewa soko la Kimataifa la Matunda. Naafiki kuwepo kwa mpango wa uendelezaji masoko Wilaya ya Muheza lakini hili liendelee kubaki kama ombi maalum.

Nne, ombi la ushirika wa wakulima wa Kijiji cha Kilongo, Kata ya Songa, wanakijiji hao wameanzisha ushirika wao na kukifanya Kijiji chao kuwa *SACCOS*. Wakulima hao kwa kusaidiwa na *NGO* ya *DAIPESA* wameandaa mpango wa kujenga ofisi yao na ghala la Kijiji wanaomba kutembelewa na Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa wakati muafaka kabla ya mwisho wa mwaka 2004. Mtazamo wa Wizara ndiyo utafuatia na maombi ya maandishi kutoka kwa wakulima hao na mimi nitafuatisilia ombi hili.

Tano, ushirika wa mafundi seremala mjini Muheza. Nimewahi kuzungumzia kuhusu ushirika huu mkongwe katika mji wa Muheza. Nilishauri wasaidiwe kutembelewa na kupewa ushauri juu ya matatizo yao ikiwa ni pamoja na kushindwa kuendeleza jengo lao la ghorofa walilokopa fedha Benki na sasa kukwama kabisa kuendelezwa. Sehemu kubwa ya deni sio *principal value* ila ni *interest commulative* na kutokana na kukosa kazi hasa walizokuwa wakipata kutoka Serikalini na Halmashauri, uwezo wao kifedha umepungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara itawezaje kuwasimamia na kuwashauri wanaushirika hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Balozi George Kahama, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dr. Ladislaus Komba, kwa hotuba hii nzuri na kazi nzuri sana ya ujenzi wa Vyama vya Ushirika, imara na endelevu pamoja na kuimarissha masoko bora na imara. Natoa pongezi za dhati kwa kazi nzuri katika kuongeza idadi na kuimarissha vyama vya ushirika na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano hai ni soko la mahindi la Kimataifa la Kibaigwa na ukamilishaji wa sera mpya na sheria mpya ya vyama vya ushirika zenye shabaha ya kutatua matatizo yaliyokuwa yanavikabili vyama vya ushirika pamoja na kufufua, kuimarissha na kuendeleza vyama vya ushirika katika sekta mbali mbali, hasa kwa *SACCOS*. Uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika nao unaleta matumaini makubwa sana licha ya Vyama vya Ushirika kuwa na hadhi ya kukopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine kama uandaaji na utekelezaji wa *Cooperative Reform and Modernisation Programme* na mipango mingine ya kuendeleza ushirika na masoko yanaleta matumaini makubwa sana. Hii ni pamoja na *ECGS*

kupandisha Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki kuboresha Idara ya Masoko, uchapishaji majarida na taarifa za masoko, mafunzo ya ushirika shirikishi, kuondoa vipozo vya ukaguzi, kuhamasisha ukoboaji wa mazao kabla ya kuyauza, kuimarisha soko la ndani, soko la nchi jirani na kuhimiza kwa kutumia soko kuondoa vipozo vya ukaguzi, kuhamasisha ukoboaji wa mazao kabla ya kuyauza, kuimarisha soko la ndani, soko la nchi jirani na kuhimiza kwa kutumia vema fursa zinazopatikana chini ya *AGOA*, *EBA* na kadhalika ni mionganoni mwa shughuli mahsusini ambazo Wizara inazifua tilia na kuzitekeleza kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimefarijika sana kuona jitihada za Wizara katika kukisaidia Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa Mkoani Tanga (*TDCU*). Bado chama hiki kinahitaji sana msaada wa Serikali katika kuongeza mtaji wake, kupata mitambo na vifaa, madawa, kuboresha Malambo majosho mafunzo, huduma zaidi za ugani na kuboresha masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, bado ipo haja ya Wizara kuongeza jitihada zake katika maboresho hasa katika kuendeleza mafunzo na uhamasishaji wa ushirika shirikishi. Aidha, motisha maalum kama vile kuwapatia mikopo nafuu kwa ununuizi wa pembejeo na mahitaji mengineyo, kadhalika ujenzi wa masoko na hatua nyingine zaidi kwa uboreshaji wa soko la ndani na kuviwezesha vyama vyetu kuhimili ushindani katika masoko ya dunia ni muhimu. Motisha nyingine inayoweza kuongeza ari ni kuwawekea malengo ya uzalishaji na mauzo kama msingi wa kuvishindanisha vyama mbalimbali na kuvizawadia vile ambavyo vinafanya vizuri kuliko wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia imetufunza kwamba udhibiti mzuri na uongozi makini ni muhimu katika kuhakikisha ushirika imara na endelevu. Hivyo hapana budi kwa *COASCO* na Wizara kuwa makini zaidi na wakali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya kuunda, kuendeleza na kuhudumia vyama vya ushirika Jimboni Mkinga ni makubwa na muhimu sana katika jitihada ya kujikwamua kiuchumi na Kijamii kwa jumla. Hivyo, tunatoa ombi maalumu kwa Wizara kufikiria kuongeza idadi ya Maafisa Ushirika pamoja na hatua na nyenzo nyingine za kukuzia ushirika Jimboni Mkinga. Zaidi ya Vyama vya Ushirika vya mazao na masoko, Jimboni kwangu vyama vya ushirika vya wavuvi, wachimbaji wadogo wadogo na wafugaji nyuki pamoja na *SACCOS* vina umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu ni kwanza, Benki ya Ushirika ianzishwe, pili, Serikali iendelee kukisaidia Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa Mkoani Tanga (*TDCU*) katika huduma za uzalishaji, ugani na masoko, tatu, Wizara iongeze jitihada katika kuboresha mafunzo na uhamasishaji wa ushirika hasa elimu shirikishi, nne, Serikali itoe motisha maalum kuwezesha vyama vya ushirika kupata mikopo yenye masharti nafuu, tano, Wizara ichukue hatua zaidi kuwezesha ujenzi wa masoko ili kuboresha Soko la ndani na sita Wizara isaidie vyama vya Ushirika kuhimili ushindani katika Masoko ya dunia. Aidha, vyama vya Ushirika visaidiwe kujiwekea malengo ya

uzalishaji na mauzo kama msingi wa kuvishindanisha na kuvizawadia vile ambavyo vinafanya vizuri zaidi.

Saba, Wizara na *COASCO* wawe wakali zaidi katika kuboresha uthibiti na uongozi makini katika vyama vya Ushirika ili kuhakikisha ushirika imara na endelevu, nane, ombi maalum kwa Wizara kufikiria kuongeza idadi ya Maafisa Ushirika na nyenzo za kukuzia Ushirika katika Jimbo la Mkinga na tisa, Wizara ihamasishe na kusaidia vyama vya Ushirika katika maeneo mengine ya kiuchumi katika Jimbo la Mkinga, hasa vyama vya ushirika vya wavuvi, wachimbaji wadogo wadogo wa madini, wafuga nyuki na *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Hoja ya bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko ambayo imewasilishwa leo asubuhi hii na Mheshimiwa Waziri ambayo mimi naiunga mkono na ningombwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tuiunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa niaba ya wapigakura wangu wa Jimbo la Chilonwa na wananchi wa Chilonwa kwa ujumla ningependa kutoa salaam za rambirambi kwa wananchi wa Majimbo ya Mbeya Vijijini na Ulanga Mashariki kwa kufiwa na Waheshimiwa Wabunge wao Marehemu Mheshimiwa Yetet Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, ambao walifariki tukiwa hapa Bungeni. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa niwape pole wale Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata maafa ya aina mbalimbali ikiwemo kufiwa na ndugu zao wa karibu pamoja na wengine kupata matatizo ya maafa ya mikasa ya ajali za barabarani wote hao nawapa pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nielekeze mchango wangu katika kujibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa kwa kusema na wengine kwa maandishi. Lakini ningependa niwashukuru wote kwa ujumla kwa michango yao mizuri waliyoitoa na nataka kuwaahidi kwamba tutaifanya kazi. Lakini kama ilivyo kawaida yetu Mheshimiwa Waziri mtoa hoja atakapokuwa anahitimisha hoja yake atawatambua wote mmoja mmoja kwa kuwataja majina. Tunawashukuru sana kwa sababu michango yao inatutia nguvu na kutupa ushauri ambao tutaufanya kazi. Nataka nitibitishie kwamba tutatekeleza yale ambayo yanawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni ya kutushauri na mingi ilikuwa ni ya kutoa maelekezo yote hiyo nasema kwamba tutaifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nijielekeza kwenye michango mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ni mingi na muda pengine hautatosha, lakini nitajitahidi kwa kadri itakavyowezekana na Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi ya kuhitimisha hoja, yale yatakayokuwa yamesalia tunaweza tukayatolea majibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilijitokeza hoja ya kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kadhaa, lakini hasa ilihuusu ahadi ya kuajiri Maafisa Ushirika katika kila Kata na kuwapatia vitendea kazi. Hii hoja ilitolewa na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na vilevile Mheshimiwa Robert Mashalla, aliitaja kwa namna moja au nytingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ninachotaka kusema ni kwamba Serikali iliainisha mahitaji ya watumishi 300 katika kuimarisha na kuendeleza Ushirika hapa nchini. Pengine hoja hii haikuelewaka vizuri tuliposema kwamba tumeainisha idadi ya watumishi 300 haikumaanisha kwamba Wizara itaajiri hawa watumishi 300 na kuwapeleka kwenye maeneo ya Wilaya na Mikoa ukizingatia utaratibu wa utawala wetu kwamba ni wa madaraka ya Mikoani na Wilayani watumishi hawa wanatakiwa wawe kule Wilayani.

Kwa hiyo, wajibu wa kuajiri ni wa Halmashauri zenyewe kuweza kuainisha mahitaji yao na vilevile kuomba vibali vyta kuajiri ili waweze wakatimiza mahitaji yao. Kwa hiyo, ningombu tu kusema kwamba itakuwa ni vizuri katika Halmashauri zote kwa idadi hii ambayo tulikuwa tumeainisha kila Halmashauri ijaribu kutoa mahitaji yake na kuomba kibali cha uajiri kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na Idara Kuu ya Utumishi ili watumishi hao waweze wakapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wetu kama Wizara tumetoea vitendea kazi vya Wizara kama tulivyokuwa tumesema kwenye hotuba, Wizara imefikia hatua mbalimbali za kutoa pikipiki pamoja na kutoa fedha kiasi kwa ajili ya kusaidia utendaji kazi wa watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile lilijitokeza suala ambalo Mheshimiwa Hasnain Murji, amelizungumzia kwa nguvu sana nalo ni la wafanyabiashara binafsi wasiruhusiwe kununua mazao moja kwa moja kutoka kwa wakulima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala nadhani Mheshimiwa Mbunge alikuwa analikazia kwa sababu ndiyo utaratibu wenyewe kwani hata kanuni pamoja na sheria zote ambazo zimetajwa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge zinakataza suala hili kwamba ununuzi wa mazao usiwe wa kiholela. Huu wa kumfuata mkulima mmoja mmoja nyumbani, kwenda kununua kwenye mashamba haupo kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba maadam Waheshimiwa Wabunge hapa wameliona hilo kinachotakiwa hapa ni ushirikiano tu

kuhakikisha kwamba jambo hili halifanyiki, lakini nataka nishauri kwamba kwa sababu kuna hivi vikao vya wadau vya mashauriano ambavyo vinakaa mara kwa mara kwa kila zao, ni vizuri basi tuelekeze ushauri wetu na wakati mwininge tufike mahali pa kutoa maazimio ambayo yatatuwezesha kuelekeza mazao haya tuyauze kwenye vituo maalum na hasa hasa kwenye Vyama vya Ushirika mahali ambapo vitakuwa vimekwishakuanzishwa na viko imara. Mfano, mzuri ni wenzetu wa zao la pamba ambao mwaka jana walikaa wakakubaliana katika msimu wa 2005/2006 kwamba ununuzi wa pamba utafanyika kupitia kwenye Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, nilikuwa nataka tu niseme kwamba hata katika mazao mengine ikiwemo na korosho itakuwa ni vizuri jambo hili likazingatiwa.

Lakini vile vile Mheshimiwa Robert Mashalla, amesema kwamba utaratibu wa ununuzi wa mazao hauzingatiwi kwa mujibu wa soko huria ni hayo hayo ambayo nimekwisha kuyaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Zahor Juma Khamis la mgawanyo wa mali za washirika. Kama mnavyofahamu ni kwamba washirika walikuwa ni Jumuiya ya wananchi chini ya uongozi wa Chama na wakati huo ilikuwa inajumuisha pande zote mbili za Muungano yaani Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba nimekuwa Naibu Katibu Mkuu kwa Jumuiya hiyo kwa miaka tisa. Kwa hiyo, nafahamu utaratibu wa mali hizi jinsi ulivyokwenda. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba suala hili Serikali hajashindwa kwa sababu kilichokuwa kinatakiwa hapa ni kutaka tu kufanya mgawanyo wa haki wa kutengeneza hesabu ambazo zinazoonyesha nani anastahili nini na nani anastahili kulipa deni lipi? Kwa hiyo, kilichokuwa kinafanywa ni kuangalia michango gani ilichangwa na pande zote mbili, Tanzania Bara na Visiwani na baadaye hesabu hizo zitakapokuwa zimeainishwa basi uweze mgawanyo huo ukafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa kuna *task force* ambayo inaendelea na kazi hiyo. Hesabu zilizokuwa zinatazamiwa zilikuwa zitoke kwa Kabidhi Wasii ambaye alikabidhiwa shughuli hizi na Serikali wakati ule shirika linavunjika, lakini kwa bahati mbaya hesabu hizo hazikukamilika vizuri, lakini sasa tumekubaliana kwenye kikao cha juzi ambacho kilifanyika tarehe 26 Julai, 2004 kwamba zichukuliwe hesabu zilizoko pale *TFC* ili ziweze zikaainishwa vizuri na kuhakikisha kwamba mgao huo unafanyika. Kwa hiyo, Serikali hajashindwa katika suala hili inaendelea na utaratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala ambalo limezungumzwa sana na Mheshimiwa *Major Jesse Makundi*, suala la watu ambao walifilisi Vyama vya Akiba na Mikopo vile vya *Mwika North, East SACCOS*. Suala hili tunalifahamu na kwa bahati nzuri tulishatuma timu ya wataalam kule tukaainisha hayo yote na hao watu waliofanya ubadhirifu walitakiwa wawe *surcharged*, kwa hiyo, tulichokuwa tunasubiri hapa ni utaratibu wa sheria mpya na kujiandaa sisi wenywewe kupeleka Afisa ambaye atakuwa yuko imara katika kusimamia suala hili la kuwa-*surcharge* hao watu na vile vile kuangalia vipengele kwa kulingana na sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge Nkenge, amezungumzia masuala mengine, lakini mengine ya msingi nitamwachia Mheshimiwa Waziri atayatolea ufanuzi. Lakini amezungumza suala la fedha za wakulima zilizokatwa kujekewa akiba kutozwa kodi na *TRA*.

Tungependa kusema kwamba hili tumelipokea kwa sababu ndiyo limetufikia tu nataka niahidi kwamba tutaendelea kulifutilia na tungeomba ushirikiano wake katika kulifutilia jambo hili ili baadaye tupate ufumbuzi wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambalo wameliongelea la kasi ya kuhamasisha Vyama vya Ushirika iongezeke na hasa katika maeneo ambayo Vyama vya Ushirika havijawa imara sana. Hili limeongelewa na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kusema tu kwamba suala hili ndicho Serikali inachokifanya baada ya kupitisha sera na sheria mpya na sasa hivi *Cooperative Reforms*, kazi ambayo tunatarajia kuifanya mwaka huu ni hiyo ya kuhakikisha kwamba uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika katika maeneo ambayo Ushirika haujawa imara itazingatiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia tu tutahakikisha kwamba kuna programu maalum itakayokuwa inahamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika katika Mikoa ya Mara, Dodoma na Singida kwa kuzingatia maelekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Aisha Magina, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya muundo wa sasa wa ushirika kwamba sasa hivi ushirika unakuwa *imposed*, hili siyo sahihi kabisa kwa sababu suala la *ku-impose* ushirika nadhani Mheshimiwa Mbunge pengine amefikiria ule utaratibu wa nyuma ambalo sasa hivi ni kama *history*. Ushirika tunaouanzisha sasa hivi ni *demand driven*, siyo ule amba ni wa kuagiza, tunahakikisha kwamba wanachama wenyewe wameamua wana tatizo gani na wanaanzisha ushirika unaolingana na utatuaji wa tatizo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si sahihi sana kusema kwamba ushirika tunaouanzisha sasa hivi ni wa *ku-impose*. Hata katika suala la *structure* ambalo Mheshimiwa Mbunge alilieleza kwamba kuna *Tanzania Federation Agricultural Cooperative* kitu kama hicho hakipo, tulichonacho sisi ni *Tanzania Federation of Cooperatives* ambayo wanachama wake si vyama vya mazao tu isipokuwa ni pamoja na vyama vingine kama vile *SCCULT* na *TICU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa ushirika vile vile unaamuliwa na wanachama wenyewe. Kwenye sheria tulichosema ni kwamba Chama cha Msingi cha Ushirika kitakuwa ndiyo nguzo ya mwanzo na utakuwa kwa kweli ndiyo msingi. Baada ya hapo ngazi nyingine ambayo inatambuliwa rasmi ni ile ya juu kabisa ambayo ni

federation. Hapa katikati ni uamuzi wa wanachama wenyewe kuamua ni muundo gani wanataka uwe wa ngazi ngapi kutegemeana na kazi ambazo zinahitajika zifanyike na hizo ngazi zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala ambalo Waheshimiwa Wabunge marafiki zangu kutoka Mikoa ya Shinyanga na Mwanza hapa wameliongelea hasa hasa wanaotoka Mkoa wa Shinyanga hili suala la *SHIRECU*. Mimi nataka tu niseme kwamba Serikali hapa kusema kweli ilistahili pongezi kubwa sana kwa sababu hali ya *SHIRECU* ilivyokuwa mwanzo ilikuwa si hali ya kuridhisha sana. Hivi sasa tunachosema ni kusaidia *SHIRECU*, maana mtu mmoja akazungumzia hapa suala la kwamba kunakuwa na *Government interference*, hii si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia masuala haya lazima tutofautishe mambo mawili. Kuna *interference* na *intervention*. *Intereference* ni lile suala la kuingilia shughuli za kila siku zinafanywa kwa maelekezo ya Serikali, lakini *intervention* ni wajibu wa Kiserikali ambapo mambo yanaharibika lazima kuwe na *intervention* ya Serikali ili kuvisaidia na huu ni wajibu ambao unatekelezwa kwa mujibu wa sheria kwa sababu sheria inaipa mamlaka Serikali kwamba *the government shall give protection to the cooperative by giving support and guidance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tunaitekeleza kwa njia hiyo kwa sababu huwezi kuona mambo yanaharibika wakati sheria inaelekeza kwamba lazima Vyama hivi visaidiwe ukaviacha tu kwa kuogopa kwamba kuna *interference*. Kwa hiyo, hapo hakuna *interference* isipokuwa kilichokwuwa kinafanyika ni *intervention* na *intervention* hiyo imesaidia sana kwa sababu matatizo yote yaliyoelezwa haya hayakuanzishwa na Serikali, matatizo haya yalianzishwa na uongozi ambao ulikuwepo huko nyuma na ndiyo maana Serikali ilipofanya hiyo *intervention* ikatoa uongozi ulikuwepo na kuweka hawa watumishi wa Serikali ambao walikuwa wanasimamia katika kuelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine ni kama vile mtu alikuwa mgonjwa yuko *ICU* baada ya kumpa dawa akapona akaenda kwenye Wodi ya kawaida unasema bado ni mgonjwa tu. Lazima ushukuru kwamba huyu katoka *ICU* sasa yuko kwenye wodi ya kawaida. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali ya *SHIRECU* na kwanza haya matatizo hayakuletwa na Serikali, Serikali iliikuta ikiwa katika mzigoo mkubwa sana na baada ya hapo sasa ndiyo tunawatoa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kauli ya Serikali kwamba hawa watumishi wa Serikali waliokuwa wanaisaidia *SHIRECU* katika kujikwamua na matatizo hayo maadam *SHIRECU* sasa wameshafanya uchaguzi juzi juzi, watumishi hawa tunawarudisha Serikalini ili iwekwe menejimenti ambayo itakuwa inaendesha shughuli kwa maelekezo ya Hal mashauri iliyopo. Lakini hiyo haimaanishi kwamba Serikali ikiona mambo yanavurugika isifanye *intervention* itaendelea kufanya hivyo kwa sababu huo ni wajibu wake wa kisheria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala ambalo limejitokeza kuhusiana na Wizara kuanzisha Benki ya Ushirika ili kutoa huduma za fedha kwa masharti nafuu kwa wanaushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumelieleza vizuri sana na hata katika kujibu maswali yetu hapa, tumejaribu kueleza jinsi ambavyo tunakusudia kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika, lakini tulisema kwamba Benki hii hatuwezi tukaianzisha bila utaratibu maalum japokuwa rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, amesema kwamba mambo ya *feasibility study*, sijui masuala ya rasimu hayatakiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kitu chochote ukikianzisha kwa pupa bila kufanya uchunguzi wa kutosha ndiyo mwanzo wa kuharibikiwa mapema. Kwa hiyo, hayo yote tunayofanya ya kuteua wataalam wa kuweza kutushauri ni katika kuhakikisha kwamba huko tunakokwenda tuweze tukafanya kazi nzuri. Mtu mwingine ananiuliza ni kwa muda gani tunesema huyu mtaalam wa kufanya hii kazi atakamilisha kufikia mwishoni mwa mwezi Septemba, 2004 itakapokuwa imekamilika baada ya hapo basi uamuzi utafikiwa wa namna gani benki hiyo itafanya kazi.

Mheshimiwa Venance Mwamoto, amehimiza suala la kuendeleza *SACCOS* kwani zinaonyesha kusaidia kupambana na umaskini. Hicho ndiyo tunachofanya na sasa hivi kuongezeka kwa *SACCOS* pamoja na kufanya kazi kwa nguvu sana ni kutokana na kazi ambayo inafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, amezungumzia Chuo cha Ushirika Moshi kingekuwa Chuo Kikuu kamili bila kupitia utaratibu wa kuachwa Chuo Kikuu Kishiriki. Madhumuni ya kukipandisha hadhi Chuo cha Ushirika Moshi ni kukabiliana na changamoto ya maendeleo ya ushirika nchini na kukidhi mahitaji ya kijamii kwa wakati tulionao. Mwelekeo huo unasababisha mabadiliko makubwa kukiandaa Chuo hicho kitaaluma. Utaratibu unaofuata Sera ya Elimu ya Juu hivyo yahitajika maandalizi ya kuwezesha kutekeleza mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka tu niseme kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesema nadhani hasa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba Chuo hiki kitakapokuwa kimeanzishwa kisipuuze taaluma yake na zile kozi ilizokuwa inazifanya za *Diploma* ya Ushirika na Vyuo vingine ambavyo viko chini yake. Hivyo havitaachwa na kusema kweli hivi vitakuwa ni sehemu ya hicho Chuo na vitaimarishwa zaidi ili viweze vikafanyakazi ya kuimarisha ushirika nchini na hapa tulichokifanya kusema kweli ni kukipandisha hadhi tu Chuo lakini kazi zake za kuzingatia ushirika itakuwa ndiyo *core function* yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, ametoa maelezo juu ya Chama cha Ushirika cha Kyeyo ambacho kimekwamishwa na Mrajisi Msaidizi, Kilimanjaro kuchagua uongozi mpya kwa ajili ya kungojea matumizi ya sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka hapa niseme kwamba Serikali imeshachukua hatua na suala hili, tumelipata kutoka kwake Mheshimiwa Mbunge tunataka tumpongeze sana kwa kutuletea suala hili kwa karibu sana na sisi tumeona kwamba hatutakaa kimya tuendelee kufanya maagizo tu, isipokuwa hivi sasa tumekwishatuma mtaalamu wetu ambaye yuko kule Kilimanjaro na wakati wowote ataleta matokeo ambayo yatakuwa na ufumbuzi wa tatizo hili. (*Makofit*)

Mheshimiwa Juma Kidunda, ameipongeza Wizara kwa kuajiri wasomi, ni jambo zuri ndiyo maana tunafanya kazi nzuri, kwa sababu tuna wataalam ambao wanatusaidia katika kufanya kazi hizi. Japokuwa rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, anasema kwamba wataalam wale wako pale halafu na semina zinaendelea.

Sasa semina hizi zinazoendelea si ndiyo wanatoa utaalamu kwa watu wengine ambao hawaelewi, sasa utakuwa umekaa na utaalamu, wewe ukishakuwa *Doctor* basi unakaa nao. Kwanza, utakuwa ni uchoyo, lakini vile vile utakuwa hautumii utaalamu wako kuwasaidia watu wengine. Kwa hiyo, semina hizi zitaendelea za kutoa mafunzo kwa watu wengine ili kazi hizi zitakopokuwa zinaanzishwa wote tuweze tukaenda sambamba pamoja na wataalamu wetu. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba wataalam tunao wanatusaidia lakini vile vile mafunzo na maelekezo wanayoyatoa ni kwa manufaa ya wananchi wengine pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Aggrery Mwanri, amezungumzia habari ya hatua gani zilizochukuliwa kuhakikisha marejesho ya shilingi milioni 519 kwa *KNCU* na Bodi ya Kahawa.

Suala hili tulikuwa tumeshaanza kulifanyia kazi kwa muda mrefu na kama tulivyokuwa tumeshasema mwanzo kwamba tunataka tufanye kazi kwa uhakika zaidi, tuliona kwamba ni vizuri kwa sababu kulikuwa na mabishano ya namna fulani. Tukaona kwamba suala hili tutumie timu ya wataalam ya ukaguzi ambao watalifuatilia kwa karibu na ndivyo tulivyofanya tumeshawateua wenzetu wa *Tanzania Audit Coorporation* ambao Serikali imekwisha walipa kufanya hiyo kazi. Kwa hivi sasa wameishaianza kazi na itakopokuwa imekamilika basi watatoa taarifa na hatimaye ufumbuzi utapatikana kutokana na hayo watakayokuwa wameshatuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko michango ambayo iliendelea kutolewa na Waheshimiwa Wabunge. Lipo suala linalohusiana na masuala ya masoko. Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, anaulizia vipi ujenzi wa soko la Makambako usipewe umuhimu wa kwanza katika kipindi hiki cha mwaka 2004/2005 na kuwa Makambako ina sifa zote zinazotakiwa kama vile kuunganishwa na reli ya *TAZARA* katika Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Serikali imelipokea na hasa katika kipindi hiki ambacho tunao mradi mkubwa wa kuendeleza masoko ya mazao ya kilimo. Mpango huu kama tulivyokuwa tumeshasema ambao unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuanzia, lakini ndiyo mpango ambao utasimamia utaratibu wa uendeshaji wa masoko ya mazao ya kilimo. Kwa hiyo, ni pamoja na Makambako itafikiriwa kwa sababu katika

mpango huu kwa kuanzia unahusisha Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na Kaskazini ambapo Makambako ni mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pengine niunganishe hapa na ushauri wa Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara, ilikuwa imetushauri kwamba tunapoangalia suala hili la kuweka masoko katika *Strategic Areas* tuangalie vilevile suala la kuhakikisha kwamba tunajenga soko moja ambalo litakuwa la kimkakati pale Segera kwa ajili ya matunda, nalo hilo tumesema kwamba tumelipokea tutakapokuwa tunaangalia yote haya kwa ujumla wake la Makambako na Segera, Serikali itayatilia maanani.

Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, anasema ni vipi Wizara ya Ushirika na Masoko itawezesha Zanzibar kunufaisha na fursa mbalimbali za mauzo ya bidhaa nchi za nje kama vile *AGOA, Eastern African Community, SADC* na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa suala hili si la Muungano, Wizara imekuwa ikishirikisha wafanyabiashara kutoka Zanzibar kushiriki katika fursa mbalimbali za mauzo ya bidhaa na nchi za nje kama vile *AGOA*, Jumuiya ya Afrika Masharika, Jumuiya ya Ulaya na Jumuiya ya *SADC* na hapa kusema kweli tuna ushirikiano mzuri tu kwamba hata katika maonyesho ya biashara yale yaliyofanyika Rostock, wenzetu wa Visiwani walihusika, walikuwepo Waziri wa Biashara Zanzibar na Maofisa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna ushirikiano wa karibu na kwa vyovoyote vile haya mengine yatakapokuwa yanatokea tutaendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, alisema Wizara itoe kauli kuhusu wakulima wadogo wa chai wa Wilaya ya Rungwe kuruhusiwa kuanza kuza chai yao moja kwa moja kiwandani Katumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni tatizo lolote linalojitokeza kwa mfumo wa kuuza majani ya chai Wilayani Rungwe kwa Kampuni ya *Wakulima Tea Company* kwenda kununua chai kwa mkulima, kwani hiyo kampuni ina uwezo na kuwa na magari ya kusafirisha chai toka vituo vya kununulia majani ya chai vijijini hadi kiwandani. Kama Mheshimiwa Mbunge atakavyokumbuka suala hili tulikuwa tumeshalishughulikia na yeze pamoja na viongozi wa chama hiki kinachohusika na tukaliundi timu ya wataalam walikwenda kufanya uchunguzi kule na haya yametokana na ile taarifa ambayo tulikuwa tumeishaipata.

Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni, amezungumza kuwa Wizara iendelee kujenga masoko ya kisasa kama lile la Kibaigwa katika Wilaya zote ambazo hazina masoko kama hayo. Ujenzi wa masoko utategemea mahitaji ya masoko kwa Wilaya husika na niseme tunaangalia vilevile na mipango mingine ambayo ipo kama nilivyokuwa nimesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, amezungumzia habari ya soko la zao la Dengu ambalo huzalishwa katika Wilaya yake ya Kwimba halieleweki na linasuasua. Wizara inalifuatilia suala hili na kusema kweli

mambo mengi haya ya masoko niseme tu kwa ujumla yatatafutiwa ufumbuzi na maelekezo rasmi tutakapokuwa tumeikamilisha ile sera yetu ya masoko ambayo tunatazamia kufikia mwezi Septemba, 2004 nayo itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani kwamba ni vizuri tufanye shughuli tukiwa na mwelekeo ambao ni wa uhakika badala ya kubabaisha babaisha. Kwa hiyo, ni pamoja na mazao yote ambayo sasa hivi bado hayana masoko maalum tunadhani kwamba sera ya masoko itakapokuwa imekamilika basi yatakuwa yamezingatiwa yote hayo.

Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, amezungumza kuwa wakulima waeleweshwe mfumo wa matumizi ya stakabadhi za mazao kwenye maghala kama dhamana ya kupata mikopo ili wanufaikie kwa kuboresha soko na bei nzuri. Uhamasishaji umefanyika katika mikoa ya majaribio ya pamba na kahawa. Kwa kuanzia na kazi hii bado inaendelea katika maeneo hayo pamoja na maeneo mengine mapya ya mazao hayo na mengineo. Ni mategemeo ya Wizara kuwa kasi ya kutoa elimu hii itaongezeka kwa kuwa Serikali imeshaukubali mfumo huu utumike na pia maandalizi ya sheria yanafanyika. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka baadhi yenu mlihudhuria ile semina ya jambo hili na bado tunatumaini azma ya kuendesha semina nyingine tena inayohusiana na suala hili na ufanuzi zaidi utatolewa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hasnain Murji, anazungumzia suala la kuhusu bei ya korosho katika msimu wa mwaka 2004/2005. Bei hii ya zao la korosho hupangwa kwa pamoja na wadau wote wa zao la korosho. Pengine hapa nataka tu niseme rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, alikuwa anazungumzia suala la kwamba Serikali kukaa pamoja na wafanyabiashara si jambo zuri. Vikao vile vinavyofanyika ni vikao vya mashaurino vya wadau ambapo Serikali inakuwepo pale kama mshauri.

Kwa hiyo, haiwezekani ukasema kwamba uwaachie hawa wanaohusika wakiwepo Vyama vya Ushirika na wafanyabiashara binafsi bila kuihusisha Serikali kwa sababu Serikali ndiyo inajua mipango na taratibu nyingi, kwa hiyo, Serikali inakuwa iko pale kushauri. Lakini haipo pale kwa ajili ya kupanga mikakati pamoja na wafanyabiashara binafsi. Kwa hiyo, katika kupanga bei, vigezo mbalimbali vinavyotumika ni pamoja na gharama za uzalishaji, ununuzi na uuzaji pamoja na mambo mengine haya yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimesema kwamba michango ni mingi lakini yote nia yake ni nzuri. Kwanza nataka niseme wachangiaji wote wametupongeza na kutupa moyo katika kazi nzuri ambayo tumeifanya. Sisi tunataka tuwathibitishie kwamba tutarudisha imani hiyo ambayo mmetupa kwa kutekeleza ushauri mliotupa na kuhakikisha kwamba ushauri wenu unazingatiwa na kwa sababu michango bado ilikuwa inaendelea kuwepo.

Nataka tu niseme kwamba tutaiunganisha vizuri ukiacha hiyo ambayo Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hapa kuitolea maelezo. Lakini hii

mingine ambayo ilikuwa ina majibu hapa tutaiandalia majibu rasmi ambayo tutayawasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge wahusika ili kila mmoja aweze kuona kwamba amejibiwa namna gani. Lakini nataka tu nirudie kusema kwamba michango yote ni mizuri, michango yote ni ya kujenga, inatupa moyo na sisi wenzeni tunafarijika sana tunapopata michango ya namna hii ya kututia moyo.

Nimalizie tu kwa kusema rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga nadhani enginee hajazisoma soma hizi nyaraka ambazo tumezazishilisha na tumezitumia, aweze kuona jinsi ambavyo nyaraka hizo zinavyosema na hatua tulioifika katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, toka tulipotoka kwenye kuaandaa ile taarifa ya Tume ya Rais kulikuwa hakuna vitu kama hivi vya *credit guarantee scheme* ambayo sasa hivi inatolewa kwa wakulima, kulikuwa hakuna masuala kama haya ya *warehouse receipts*, kulikuwa hakuna masuala ya uanzishaji wa Chuo cha Ushirika kuwa Chuo Kikuu na mambo kadha wa kadha.

Kwa hiyo, hii si rahisi au sio vizuri kusema tu moja kwa moja kusema kwamba toka Wizara hii imeanza hakuna chochote kilichofanyika, nadhani sio sahihi. Kwa bahati mbaya nasema amesema yeeye mwenyewe tu, lakini wachangiaji wote waliochangia wamesifu kazi inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda niwashukuru sana wale wote walioongooseza na kututia moyo na ningeomba basi tutumie nafasi hii kumsaidia mwenzetu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa sababu ndio amerudi tu hivi karibuni enginee bado hajaweza kuziangalia hizi sera aone jinsi tunavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge wote muunge mkono. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo niliiwasilisha leo asubuhi hapa Bungeni na kutoa maelezo na majibu ya ziada kwa mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda awali ya yote kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja yangu ama kwa kuongea Bungeni ama kwa maandishi au kwa kupiga makofi au kwa ishara ya kichwa. Wote nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yao yote ilikuwa ni mizuri kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema na ninaamini kwamba itatusaidia sana katika Wizara yetu kuweza kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ambayo tumekabidhiwa na Taifa katika kujenga ushirika imara katika nchi yetu na pia kushughulikia suala zima la masoko kwa mazao yanayozalishwa na watu wetu. Vile vile kuendelea kusaidiana nao matatizo yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, michango imekuwa ni mingi na kwa kweli muda tulionao tusingewenza kujibu hoja zote kwa mara moja, moja kwa moja. Lakini na mimi nathibitisha kwamba hoja zote zilizotolewa tutajitahidi kuzijibu kwa maandishi kwa kufuata utaratibu ambao tumejiwekea Serikalini.

Napenda kumshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa kunisaidia kujibu karibu hoja zote ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kuna hoja chache tu ambazo ama za kijumla au ni za kisera ambazo nitazitolea maelezo ya ziada. Lakini kabla ya maelezo hayo ya ziada napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuwataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge wafuatao, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, ambaye ndiyo aliywakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Aisha Philipo Magina, ambaye vile vile ye ye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Dr. James Msekela na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko. Wote hawa nawashukuru sana kwa michango yao ya kuongea Bungeni. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkyo, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Enock Kipole, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Lydia Boma na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro. Wote hao ninawashukuru sana. Kwa bahati mbaya kama kuna Mheshimiwa aliyechangia na sikumtaja naomba ajitambulisse halafu aniletee *ki-note* kadogo ili niweze kutamka jina lake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kutoa maelezo kwa majibu ya ziada kama ifuatavyo.

Mapendekezo na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, ushauri na mapendekezo yote ya Kamati tunayakubali na tutayaafanya kazi. Tunamshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri wao na kuendelea kutuunga mkono katika kazi zetu za siku hadi siku. Napenda nieleze machache kuhusu baadhi ya mapendekezo.

Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Aisha Magina, kwa hotuba yake nzuri. Namshukuru pia kwa kuunga mkono sera ya Serikali ya kuhimiza wananchi kujiunga katika Vyama vyta Ushirika kama njia mojawapo ya kuondokana na umaskini uliokithiri. Baadhi ya mapendekezo aliyojatoa ni mazuri sana na tutayaafanya kazi. Lakini mengi aliyojatoa ni yale ambayo tayari yapo katika sera yetu ya maendeleo ya ushirika. Kwa hiyo, nitamkabidhi baadaye nakala hii kama hana ikiwezekana akija nitamwonyesha kifungu kwa kifungu kusudi asije akapotea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo machache ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyataja ambayo ni ya kijumla ambayo ningetaka nisiaache hivi hivi labda niyatolee maelezo machache. Kwa mfano, kuna rai iliyotoka, na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza ni Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Robert Mashalla na Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, wao walitoa rai ya kutaka Bodi za Mazao ziwekwe chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa misingi kwamba iwe kama Wizara mama kwa kuwa Bodi zinashughulikia masoko ya mazao.

Ningeweza kusema tu kwa kifupi kwamba rai hii imetolewa na kwa kweli inazungumzika. Lakini napenda nitamke kwamba Bodi za Mazao zinafanya kazi nydingi. Kwanza Bodi za Mazao zinashughulikia masoko kama kazi mojawapo. Lakini vile vile zinashughulikia kuandaa na kuendesha mipango ya kilimo cha mazao makuu kahawa,pamba, korosho, tumbaku na kadhalika. Bodi pia ndizo zimepewa majukumu ya kusimamia *statutory functions* za Bodi zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo sijui wale wanaotoa pendelezo labda wangeuliza. Kilimo kingekuwa katika hali gani kama Bodi hizo zingehamishwa kutoka kilimo kwenda katika Wizara nyingine. Hasa tukiweka maanani kwamba kwa historia Bodi za Mazao huwa zinakwenda pamoja na Wizara ya Kilimo. Lakini nadhani rai hii inaweza kuzungumzwa kwa kuwa tuko katika mtindo wa kidemokrasia. Lakini pengine ni vizuri tukasubiri ile sera aliyoizungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri ambao tunaiandaa na ambayo itakuwa tayari mwezi Septemba, 2004 tuone hii itasemaje kwa sababu hii imehusisha wadau wengi pamoja na wataalam halafu tutakuwa na lolote la kusema. Lakini kwa sasa hivi tuko katika kipindi cha mpito na si vizuri kwa kweli kupangua mambo yalivyo kwa sasa, tutapata hasara kubwa zaidi kuliko kama tungeacha ikaendelea namna ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni hayo na ushauri wao. Dr. Diodorus Kamala, amezungumzia matumizi ya fedha za *STABEX* na akasema kwamba Wizara ya Ushirika na Masoko na mimi kama Waziri wake hatukuhusishwa. Ukweli ni kwamba mimi nilihuhsishwa na Wizara yangu imehusishwa. Pamoja na kwamba suala la *STABEX* kwa sasa hivi tunaweza kusema kwamba ni historia, lakini ukweli ni kwamba nilihuhsishwa na hapo nilipendekeza na pia Waziri Mkuu aliunga mkono katika pendeleko hilo na vile vile Waziri wa Kilimo na Chakula kwamba, sehemu kubwa ya fedha za *STABEX* zilipwe moja kwa moja kwa wakulima wa kahawa, ndivyo tulivyokuwa tumependekeza. Wenzetu ambao wanatoa fedha katika *European Union* hawakukubaliana na pendeleko hilo. Sasa tukumbuke usemi wa Kiingereza ambao unasema kwamba, *beggars are not choosers*. Tukakubali fedha zisitumike kwa kazi waliyokuwa wanapenda.

Mheshimiwa Hasnain Murji, amezungumzia habari za kuwa na mpango wa kuhakikisha kwamba korosho inabanguliwa kabla ya kuuzwa nchi za nje. Nadhani anaelewa na wengine wanaelewa kwamba Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula kwa sasa hivi iko katika harakati za kutayarisha *incentives* ambazo zitajadiliwa na wawekezaji wa ndani na wa nje kama motisha ya kushawishi wabanguaji korosho zote nchini kabla ya kuzipeleka nje katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi, hiyo *package of incentives* tunaitayarisha, tunaiandaa na bila shaka wote watafurahia nayo, tutakaa chini kwa pamoja tuweze kuizungumzia. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao wana joto katika suala hili wavute subira kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali mengine ambayo yanahu moja kwa moja Wizara nyingi. Kuna masuala yanayohusu moja kwa moja Wizara ya Kilimo na Chakula, aliyaeleza Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na Mheshimiwa Dr. James Msekela. Kuna mengine yanahu moja kwa moja na Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na vile kuna masuala hayo wameyazungumzia ambayo yanahu moja kwa moja Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Sasa yote haya nadhani kwa sababu yapo kwenye *Hansard* na wenyewe wako hapa nadhani kama ilivyo kawaida watayashughulikia kwa kushirikiana na sisi kutaweza kutoa majibu ambayo ya kuwatoshaleza Waheshimiwa Wabunge.

Kama nilivyosema, nilikuwa nimesahau kuyataja baadhi ya majina ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu na vile vile Mheshimiwa James Musalika na mwenyewe amechangia. Samahani sana nilikuwa sikupata majina yao mapema. Baada ya kutoa majibu hayo nazidi kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba michango yao yote tumeichukua na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko

Kifungu 1001 - *Administration and General* 1,187,343,700/=

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie sehemu moja ndogo tu. Wakati alipokuwa akifanya majumuisho katika mchango wangu nilimwomba atusaidie ufanuzi juu ya mgawanyo wa mali za vyama vile 22 pamoja na vile vitano ile iliyokuwa washirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amejibu vizuri lakini bado kuna nafasi ameziacha wazi kwamba tatizo lile hata katika hotuba yake ya mwaka 2003/2004 alilizungumza na naomba nikariri katika ukurasa 40 sehemu ndogo naomba uniruhusu ilisema hivi: "Vile vile mikutano hiyo iliwezesha kufikia muafaka kupitia Shirikisho la Vyama vyatanzania (TFC) na Vyama vyatanzania vitano vya Zanzibar kuhusu utaratibu wa kugawana mali iliyokuwa washirika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea mwaka jana hili suala limemalizika, sasa hivi anatuambia mazungumzo yanaendelea kufikia muafaka. Hesabu wenyewe walikwishafanya na wamekubaliana mgawanyo, tatizo liko wapi na pengine atuambie tu lini hili tatizo litamalizika? Ahsante.

MWENYEKIDI: Kwanza tuwekane sawa, waliosimama ni wengi mno. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge juzi au jana kuna watu walikuwa wengi sana walitaka kuchangia kwa kutaka ufanuzi. Lakini kwa sababu hotuba zilianza kuwa ndefu sana tukaingia kwenye *guillotine* na watu wengine walikuwa na mawazo mazuri.

Kwa hiyo, tunaomba mtu aende moja kwa moja kwenye *point* badala ya kuanza kuzunguka, hilo la kwanza.

Lakini la pili, unaruhusiwa kusimama mara mbili tu Kikanuni. Kama ni mara ya tatu ama unaotoa shilingi, ama unaunga mkono. Sasa Mheshimiwa Waziri maelezo kwa Mheshimiwa Zahor Juma Khamis.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la mgawanyo wa mali za Ushirika, kama nilivyokuwa nimelitolea maelezo hapa na kwa mujibu na hata maelezo yetu ya hotuba iliyopita mwaka 2003/2004, lilikuwa linafanyiwa mazungumzo kwa maana ya kwamba tulitaka mgawanyo huu uwe wa wazi na ambao unaonyesha haki. Kwa hiyo, tulichokuwa tunasema kwamba mazungumzo yanaendelea ilikuwa ni hiyo katika kutafuta hesabu ambazo zimekuwa zinatoa huo mgawanyo wa haki. Sasa nilisema hapa tulipokuwa tunatoa maelezo kwamba awali tulikuwa tunafuutilia hesabu ambazo zilikuwa kwa Kabidhi Wasii ambayo alikuwa

amekabidhiwa mali za ushirika baada ya ushirika kuvunjika. Lakini wakati vikao hivi vinaendelea, hesabu hizi zimeonekana kuwa hazipatikani kwa urahisi ambao ulikuwa unatakitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema basi katika kikao cha juzi cha tarehe 26 Julai, 2004 sasa tumekubaliana kwamba maadam wale waliokuwa wanahuksika na mali hizo wanafahamika, basi zitumike hesabu zilizopo sasa hivi badala ya kuendelea kuzitafuta zile ambazo ziliwa zinafuatiliwa kutoka kwa Kabidhi Wasii. Kwa hiyo, litakwisha muda si mrefu kwa sababu makubaliano sasa yamefikiwa ya kutumia hesabu zilizoko pale *TFC*.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu hicho japo sikusudii kumnyang'anya Mheshimiwa Waziri mshahara wake. Nimechangia kwa maandishi, nasikitika kwamba hakunitaja. Japo nilimpelekea *message* lakini nadhani anayo pale.

Nimemwuliza na imeulizwa na Wabunge wengine kuhusu Kiwanda cha *TANICA* cha Kusindika Kahawa kilichoko Bukoba. Mheshimiwa Waziri anajua kwamba Serikali sasa hivi inakazana kwamba *tu-ad vive* kwenye mazao yetu. Sasa tuna vikwazo pale ambavyo tumeuliza awali walionunua kwa nini hawajapewa na Serikali inachukua jitihada gani za kuweza kuwashinikiza ili waweze kupewa halafu wafanye utaratibu waweze kuongeza pale. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, nilimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilifanya utaratibu katika hilo suala la kuongeza *value* kwenye pombe ambayo imepikwa na kuchujwa kama wanavyofanya Uganda au Hakuna Matata. Je, Waziri alikuwa tayari kwenda kule ili kuweza kuwasaidia? Sio wao wanaanza wazo halafu linakwenda huko bila ya mtu wa kuwasaidia kuharakisha ili tuweze kufanikiwa. Ndiyo mambo ambayo nilitaka ufanuzi.

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nifafanue swali la kwanza alilouliza Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

Suala la Kiwanda cha *TANICA* linafanyiwa kazi kwa bidii sana, nafikiri katika hii wiki inayoanza Jumatatu litakuwa limemalizika. Hawa ambao wanetaka wafaidike na ubinafsishaji huo nafikiri watafaidika na ubinafsishaji huo kama Serikali.

MWENYEKITI: Kulikuwa na maswali mawili. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lile suala la pili, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, amesema la kwenda kuwasaidia katika hii *project* yao ya kutengeneza pombe aliyoita. Nataka kumhakikishia kwamba nilikuwa nasubiri wanilettee maandishi yaani *write-up* na nikishaipata nitajitahidi kwa kusaidia pamoja na kuwasaidia kwa upande wa gharama zitakazohusika za kutengeneza *feasibility study*.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi sina nia ya kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ila wakati nachangia nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali ilikuwa imekopa korosho kwa wakulima katika msimu wa mwaka 2000/2001. Mheshimiwa Waziri alishiriki vizuri sana katika kutusaidia kutafuta soko lile na mipango mizima ya kukopa zile korosho kwa wakulima.

Waziri alikwenda China, India, Singapore na sehemu zingine pia kwa ajili ya kutusaidia kutafuta soko hilo. Baadaye zile korosho ziliuzwa na hasara ikapatikana. Lakini hakunijibu kwamba sasa ile mikopo iliyokopwa kwa wale wakulima wa korosho mpaka leo hajjalipwa. Ukizingatia kwamba kwa mwaka 2000 hiyo hiyo kahawa walipewa shillingi bilioni 1.7 kwa ajili ya matatizo kama ya kwetu. Mwaka 2001/2002 katika pamba walipewa shilingi bilioni 3.79 na mwaka 2002/2003 pareto walipewa shilingi bilioni 1.5. Sasa kwenye korosho kuna tatizo gani hawa wakulima wanadai fedha yao imekuwa ni kero sana Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa tu nataka maelezo.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoahirisha kikao chetu mchana huu tumekutana na viongozi wanaohusika na zao la korosho kwa kadri ya tatizo alivyoliweka Mheshimiwa Hasnain Murji. Kwa sababu hii ndio mara ya kwanza kwamba tumeletewa tatizo hilo Wizarani *roughly* ni siku tatu zilizopita na hatukuweza kupata majibu. Lakini majibu tuliyopata ni kwamba Serikali haikuwakopa wakulima wa korosho fedha yoyote kwa mazao ya korosho. Kama Mheshimiwa Mbunge ana taarifa zaidi kuhusu wakulima wa korosho kukopwa atuletee ili zifanyiwe kazi. Kilichotokea mwaka 200/2001 si kukopeshana bali ni juhudzi za Serikali kuokoa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa sasa hivi kwamba kwa sababu wote tuko hapa kuanzia kesho tukutane na Mheshimiwa Hasnain Murji, halafu tuweze kukaa chini ili kuona namna gani tunaweza kutatua hilo tatizo kama kwa kweli litaonekana kwamba lipo. (*Makofii*)

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina masuala mawili tu. Nilishauri kwamba ushirika wa wafanyakazi katika Vyama Vikuu vya Ushirika ni wengi mno na kwamba wanahitaji kupunguzwa ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi. Hata kama ungevipa shillingi bilioni 10 haviwezi vikapata faida. Sasa na hili jukumu nikashauri kwamba Serikali ingechukua jukumu la kuwalipa mafao, wapunguzwe, waende, halafu wataendelea kuuweka utaratibu mzuri wa kulipana na Serikali kama Vyama vya Ushirika. Hilo lina maelezo gani?

Jambo la pili, ni Bodi ya Elimu ya Shinyanga ambayo kwa kweli ulikuwa ni uamuza wa RCC na Bodi hii inachangiwa na wakulima wa pamba, inachangiwa na wafanyakazi kwa mishahara yao, inachangiwa na wafanyakabiashara. Kwa hiyo, watu wote wa Shinyanga wanachangia mfuko huu kwenye Bodi. Bodi hii inajenga shule, inaendesha shule kwamba shule hazijamalizika majengo kuna makontrakta wanafanya kazi hajjalipwa na kuna Walimu hajjalipwa na Bodi hii. Sasa leo ukiondoa kama

tamko la Waziri Mkuu alivyokuwa anasema tunaondoa shilingi 5/= zote za Bodi maana yake nani atalipa mishahara, nani ataendesha, atalipa ma-*contractor* na ujenzi wa shule bado unaendelea kwa sababu sisi hatuna Shule za Sekondari Mkoa wa Shinyanga.

MWENYEKITI: Kwanza inakuwa ni tatizo sana kwa Waziri kusikia na kuelewa. Kwa sababu Mheshimiwa Leonard Derefa, anapiga kwa nguvu sana. Mheshimiwa Danhi Makanga, keti kwanza natoa maelekezo.

Mheshimiwa Leonard Derefa, anapiga makofi kwa nguvu sasa Waziri hawezu kuelewa vizuri. Tunataka tuombe jamani Waheshimiwa Wabunge, mimi mpaka siku nimesema labda tuweke vyuma kwenye kiti cha Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, pale na kwenye kiti cha Mheshimiwa Leonard Derefa. Sasa mwachieni mtu azungumze Waheshimiwa Wabunge, halafu tunapiga makosa ya kawaida. Isitoshe tumeletewa *notice* sisi kama viongozi mliotuchagua kwamba kuna watu wengine wana ugonjwa wa moyo, kidogo moyo unastuka, kwa hiyo, ukipiga makofi ghafla na alikuwa hana habari wanastuka sana watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana tupige makofi ya kawaida. Lakini la kwanza nataka nimsaidie Waziri alipokuwa anajumuisha alisema kwa sababu *SHIRECU* hawajafanya uchaguzi, baada ya uchaguzi wale wafanyakazi watarudi na watu wakapiga makofi. Labda kama Waziri ana majibu mengine kwa suala hilo hilo na swali lingine. Mheshimiwa Waziri maelezo. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe tu maelezo juu ya wingi wa wafanyakazi katika Chama cha *SHIRECU*. Nilipokuwa natoa majumuisho hapa nilieleza jinsi hali ilivyokuwa mbaya juu ya Chama cha *SHIRECU* kwa sababu ya menejimenti ilivyokuwa mbovu kwa sababu ndiyo ilisababisha na kuajiri watumishi wengi kupita kiasi. Lakini Serikali ilipoingia pale moja ya mambo iliyokuwa inayashughulikia ni pamoja na kushauri hayo ya kupunguza watumishi.

Kwa hiyo, sasa tuna imani kwamba maadam sasa hivi tumeshatoa maelekezo na watumishi wetu Serikali wataondoka mwezi wa nane unaokuja ni mategemeo yetu kwamba menejimenti mpya iliyochaguliwa itayazingatia hayo na Mheshimiwa Mbunge akiwa ni mmoja wa viongozi kule, basi ni wakati wake mzuri wa kuweza kushauri ili idadi hiyo ya utitiri watumishi walioko waweze kupunguza ili chama kiweze kufanya kazi kwa kadri ya mahitaji yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, juu ya Mfuko wa Elimu, mimi nadhani maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, asubuhi yalikuwa yanatosheleza kabisa. Maelezo yalikuwa ni kwamba katika kuondoa kipengele kile cha Mfuko wa Elimu ni kwa sababu kipengele kile kilikuwa kinahusu eneo moja tu. Pili, akaeleza kwamba si haki kuwabebesha mzigo wale wanaolima pamba tu na wakati mwingine katika suala hili inawezekana kabisa mtu mwingine akawa halimi pamba, lakini anazaa zaidi kwa hiyo, ina maana watakaokuwa wanagharamia ni wale ambaa wanalima pamba lakini watoto wake wanasomeshwa na ile hela ya mkulima. Lakini si hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu

asubuhi ameelezea kwamba iko mipango ya Serikali kwenye MMEM na MMES ambayo yote kwa pamoja inalenga katika kuendeleza hiyo elimu.

Kwa hiyo, mipango yote ambayo Mheshimiwa Mbunge anailezea kwamba itakuwa imekwama Serikali ina mipango hiyo ya kufidia kama alivyoeleza mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Danhi Makanga, naona hajaridhika bado.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sikueleweka vizuri, tunasema sisi kama Mkoa wa Shinyanga, si wakulima wa pamba tu waliobebeshwa mzigo huu, ni wananchi wote, wafanyabiashara, wafanyakazi maofisini, wanachangia mfuko huu. Kwa hiyo, tulivyoamua kwenye RCC na unafanyakazi nzuri kwenye mkoa wetu. Sasa kuna mizigo ambayo iko *pending*, kuna watu wamejenga, kuna madarasa yako kwenye *renter*, kuna mengine yako katika msingi, kuna shule zinaendeshwa walimu wanalipwa, mfuko huu ndiyo unalipa, sasa leo ukiukata ghafla vuu, maana yake unatoa wapi hela ya kuendesha sasa shughuli hizo? (*Makofi*)

Lingine la msingi kwamba mpango wa MMES nao una taratibu zake sisi tuliweka mfuko huu kama uamuza wa Mkoa. Sasa kama angegusa alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba atagusa maeneo lakini si kuondoa kabisa, vipengele vyote aligusa Mheshimiwa Waziri, amepunguza hakuondoa kabisa hakuna mahali ni hapa tu kwenye mfuko huu ndiyo amefuta kabisa. Sasa tunafanyaje katika shughuli hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Mkuu, tusaidie, maana inahusu hotuba yako.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Danhi Makanga, pamoja na wenzake tulipokutana kilio kikubwa kilikuwa ni kwamba wakulima wa pamba hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, tulikuwa tunaangalia maeneo gani ambapo tunaweza tukapata fedha tukamuongezea mkulima. Lakini la pili kama nilivyoeleza asubuhi hakuna mantiki ya kuweka jambo kama hili katika *price structure* kwa sababu haiwahuusu Morogoro, haiwahuusu Mara, haiwahuusu mahali pengine. Kwingine kote ambapo tunajenga Sekondari, siyo kwamba hatujengi, tunajenga, lakini kinachotakiwa ni uelimishaji wa wananchi, ili watu wachingie sekondari zao siyo kuwahiana kwenye mazao. Kwa sababu unapomkata mtu kwenye zao ni kama unamnyang'anya hivi. Hatutaki utaratibu huo, kwa hiyo, hatusema wananchi wa Shinyanga wasichangie elimu, wakachangie elimu ndiyo wa akina Mheshimiwa Danhi Makanga, sasa wakafanye hiyo kazi ya kuwahamasisha kwamba jamani katika sekondari yetu hii bajeti yetu ni kiasi hiki, kiwango kinachotakiwa sasa kwa kila kaya ni hivi. Huyo mtu atakwenda kutoa fedha hizo hizo alizopokea kwenye pamba yake. Lakini usimnyang'anyie kule.

Kwa hiyo, tunachosema tu hatuwezi. Wazungu wanasema *you eat your cake and have it at the same time*. Tukishaamua kuitafuna ni lazima tukubali haikutakuwa mkono. Lakini hatusema wala hili jambo halipigi vita ujengaji wa sekondari. Tena mimi nina hakika itachochea zaidi kuliko hii ya kukatakata kwenye mazao. Sehemu ambazo

wamejenga sekondari nyingi hawakuwa wanalima pamba wala wanakatana kwenye mazao. Wanachangishana kwa utaratibu ambao wananchi wote wanakubaliana ambao ni wa haki zaidi. Kwa hiyo, mimi nina hakika wenzetu watakwenda kufanya hiyo kazi na watafanikiwa mwakani watatuambia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nchi yetu ilipoamua mazao ya asilia watu binafsi wanunue vyama vya *union* hawakupewa muda. Maamuzi yalitolewa na mara moja wanunuzi binafsi wakaingia. Kwa hiyo, *union* hawakujitayarisha kwa ushindani. Matokeo yake *union* kama *MBICU* ikajikuta ina madeni na ikashindwa kulipa. Lakini katika ukurasa wa 14 na 15 wa hotuba ya Waziri Serikali imefidia madeni mengi tu ya *union* mbalimbali katika nchi yetu. Wakati zoezi la watu binafsi kununua mazao *MBICU* ilikuwa na deni siyo zaidi ya shilingi bilioni mbili, lakini bahati mbaya *union*, *MBICU* haikusaidiwa iliwekwe kwenye mfilisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mali nyingi ya *MBICU* ikafirisiwa. Lakini kwa sasa hivi kuna majengo, hoteli ya *MBICU* na ma-*godown* yako Mbinga na wakulima vyama vitano vinavyonunua kahawa sasa hivi vyama vya msingi.

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Mbunge, tuambie hasa unataka Waziri akusaidie nini?

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Ndiyo nakuja sasa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Basi nenda hapo hapo.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Nakuja, hivi vyama vitano vya msingi vinavyonunua Kahawa, Mbinga vinakosa sehemu ya kutunzia kahawa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, ilipe hilo deni ili vyama hivi vitano vya msingi Wilaya ya Mbinga, viwezi kutumia majengo hayo, viweze kutumia magodauni hayo na magodauni hayo na *MBICU* iwe mali ya hivi vyama vya msingi vitano. Ahsante.

MWENYEKITI: Maelezo Mheshimiwa Waziri kuhusu ma-*godown* hayo. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, ameonyesha wasiwasi katika maeneo mawili, la kwanza ni kuhusu madeni ya jumla. Katika utaratibu wetu wa utekelezaji wa mpango kamambe wa urekebishaji *form* ya *cooperatives* sasa hivi yangu wanaangalia madeni yote ya vyama vya msingi na vya vikuu kusudi tuweze kuzitafutia jawabu.

Kwa hiyo, kama atasubiri kidogo katika muda si mrefu mwezi Septemba, 2004 tutakuwa na jawabu kwa mambo yote haya. Lakini nataka kutahadharisha kwamba

madeni anayoyasemea yasiwe kwamba ni madeni ya wizi kama watu wamewekwa wabaya wakaiba fedha hilo ni jambo la kwenda kortini siyo jambo la kwenda Serikalini. Hilo moja. (*Makofi*)

La pili, la vyama vya msingi vitano kutumia *ma-godown* ya *union* yao awashauri watuletee mapendekezo halafu tutakuwa tayari kuyashughulikia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Umeridhika?

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Madeni hayo siyo ya wizi, madeni hayo yalikopwa benki, siyo wizi kwa hiyo, ningeomba ishughulikiwe kama walivyopanga. Ahsante.

MWENYEKITI: Nadhani Mheshimiwa Waziri, ameelewa. Tuendelee Mheshimiwa James Musalika.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho *Sub Vote 1001* sina mpango wa kutoa shilingi kwa mshahara Mheshimiwa Waziri, lakini nilitaka maelezo, nimechangia kwa maandishi kwamba wakati msimu ulipofungulia wa kununua pamba kuna wanunuzi walilinua kwa bei ya shilingi 300/= kwa kilo. Baada ya bei kuteremka wakasema sasa wanalipa shilingi 250/=, wameshachukua pamba na wameshatoa risiti, lakini walikuwa hawajalipa wamewakopa wakulima.

Sasa maghala mengi vijijini yamezuiliwa wananchi na sungusungu wanatoka hizo shilingi 300/= na siku ile tulikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulikubaliana kwamba zilipwe shilingi 300/= kwa wale ambao wameshanunua tayari. Naomba Serikali sasa itamke hilo, asubuhi Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakulitamka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa James Musalika, alikuwa katika kikao hicho ambacho kilikuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa makubaliano tulioafikiana katika mkutano huu ndiyo yatakayoteklezwa. Kwa hiyo, kama ana shida atakuja atuone ofisini. (*Makofi*)

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa sababu leo limetoka tamko la mtu mzito kwenye Serikali na hili limeachwa, mimi nikienda ofisini, mimi na yeze na nitapigwa simu leo nitamke kama tulivyokubaliana nitaeleweka? Kwa nini yeze asitamke kama Waziri? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewe kwamba Kauli ya Waziri Mkuu, haiwezi kufanyiwa maamuzi na Kamati ya Matumizi, hilo naomba tuwekane sawa na tusome hizi kanuni. Kauli ya Waziri Mkuu, haifanyiwa maamuzi na

Kamati hii kwa sasa. Sasa *unless* Mheshimiwa Waziri ana maelezo mengine ya ziada, tunaomba kama yapo atusaidie.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa James Musalika, aniamini kama mimi ninavyomwamini. Aje tukutane, alikuwa kwenye mkutano na mimi nilikuwa kwenye mkutano na wote tunajua tulikubaliana nini. Kwa hiyo, aje tuzungumze halafu kuanzia hapo tutaweza kulitatua tatizo lake.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Yangu mimi ni madogo na wala mshahara wa Mheshimiwa Waziri siugusi. Nilishapata jibu kidogo la kwanza. Suala langu ni madeni kwamba kule Jimboni kwangu kuna wananchi ambao wamekopa miaka mingi sana, Sambaru, Misoghaa na kadhalika na mpaka sasa hayo hayajaonekana. Sasa katika ukurasa wa 14, naona hapa kwamba Serikali imechukua hatua ya kufidia madeni kwa vyama vingine. Sasa niliomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie, je, kwa upande wa madeni haya ya Singida sisi atatusaidia namna gani? Hilo la kwanza.

La pili, katika mchango wangu nilieleza kwamba Vyama vya Ushirika katika Singida na hasa Singida Kusini ni duni sana. Nilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri nikamwomba watalaan wa kusaidia kuhamasisha ushirika na anilipa namshukuru, nimeshamshukuru na ninaendelea kumshukuru. Lakini toka tumeピta na wale watalaan kuhamasisha wananchi wamehamasika wanangojea Vyama vya Ushirika viundwe mpaka sasa hamna kitu. Inawezekana ni kwa sababu Halmashauri yangu ina watendaji wawili wa ushirika.

Je, katika hali kama hii ambayo Halmashauri ina watendaji wawili na kwa sababu katoa maelezo pale kwamba suala la kuajiri maafisa ushirika katika kata na tarafa mimi sikumuelewa vizuri kwamba hilo halipo au kama lipo sisi tukazungumze na Halmashauri ningeomba anisaidie katika hilo na hasa Singida anatusaidia vipi ili kuona kwamba Vyama vya Ushirika vinaundwa? Majedwali aliywewka kwenye ukurasa wa 72 na 73 unathibitisha kabisa. Kwa mfano, kuna vyama viwili tu vya ushirika vya wafugaji. Sisi ni eneo la wafugaji na wafugaji wako wengi na wangependa kupata Vyama vya Ushirika.

La mwisho katika ukurasa wa 49 ameelleza pale mipango ya miradi ya maendeleo nilitazamia kwamba huku mwishoni walau ataweka jedwali la kuonyesha kwamba hii miradi ya maendeleo ambayo imeelezwa ukurasa wa 49, 50, 51 mpaka nafikiri 54 labda mgawanyo wake ungekuwa vipi.

Sasa ningependa kujua mgawanyo wake uko vipi na hasa sisi Singida tutahusika vipi katika miradi hii ambayo ameieleza itakuwepo katika mwaka 2004/2005? Nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe maelezo ya ufanuzi ya maeneo matatu ambayo Mheshimiwa Mohamed Missanga, anahitaji kupata maelezo.

La kwanza ni juu ya madeni, kwanza nataka kusema kwamba Serikali haifidii madeni, tulichosema hapa kwamba ni kweli kuna madeni ya aina mbalimbali katika vyama vya ushirika wanadaiana na wafanyakazi mahali pengine wanachama. Tulichosema kwamba madeni yote haya yanaainishwa yaweze yakaonekana chanzo chake ilikuwa ni nini. Mahali pengine madeni haya yanatokana na ubadhilifu wa watumishi, ubadhilifu wa viongozi na wakati mwngine madeni haya yalitokana na uzembe.

Kwa hiyo, sasa yote yatakapokuwa yameainishwa ndiyo tunaweza sasa tukajua tufanye nini juu ya madeni haya. Kwa hiyo, tungeomba tu kwamba hili yasubiri mpaka tuweze hilo la kuianisha madeni haya, vyanzo vyake na kadhalika na ndiyo tunaweza tukalitolea maelezo kwamba tunafanya nini juu ya madeni haya.

La pili, linahusu uimarishaji wa vyama vya ushirika kule Singida, nimetoa maelezo hapa kwamba tumeandaa program maalum kwa mwaka huu wa fedha tunaoanza sasa kwa Mikoa ya Singida, Dodoma na Mara kwa kuzingatia kwamba maeneo haya ya vyama vya ushirika vimefifia sana na kwa hiyo, lazima tuviandalia programu maalum. Kwa hiyo, hizo shughuli ambazo zimechaanza za kupelekewa maafisa wachache kwenda kumsaidia ni sehemu tu, lakini pengine tutakapokuwa tumeanza kutekeleza hii programu maalum hayo mahitaji anayohitaji Mheshimiwa Mohamed Missanga, yanawenza yakatimizwa. (*Makofi*)

Kuhusu suala la watumishi, nilipokuwa natoa maelezo hapo nilisema kwamba watumishi wale tulioainisha kwamba watumishi 300 watahitajika ili kuimarisha ushirika nchini, tulisema tu kwamba tulionyesha mahitaji ambayo yatakuwa yanahitajika. Lakini kwa kila eneo itabidi sasa waainishe mahitaji yao na utaratibu wa kuomba kuwaajiri hawa ufanyike kupitia mamlaka zinazohusika ikiwemo TAMISEMI, pamoja na Idara Kuu ya Utumishi.

Sasa kama kwenye Halmashauri yake itaonekana kwamba wanahitajika maafisa ushirika pengine kumi au ishirini kwa kutegemeana na uwezo wao wa kuweza kuwalipa basi hilo linaweza likafanyika na mamlaka zinazohusika zitashirikiana nao katika kuwasaidia kutoa ajira ya wahusika.

Mwisho juu ya miradi ya maendeleo ambayo angependa tuyaanishe lakini nadhani hapo tungenesubiri tuone utaratibu huu ambao tunaundaa wa programu maalum tuliyoeleza katika hotuba hii pengine inaweza ikasaidia kuonyesha kwamba hii miradi ya maendeleo Singida itahusika vipi.

MWENYEKITI: Ahsante sana, naona Mheshimiwa Mohamed Missanga, ameridhika.

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi naomba katika maelezo hasa tangu hotuba ya mwaka jana niligusia sana suala la STABEX ambalo liliacha sana nyuma wakulima wa

zao la kahawa na mikoa ambayo ilikuwa imepangiwa, sisi tumekwenda kule tukawaambia wananchi kwamba badala ya ule utaratibu wa zamani wa kuwapeni pesa sasa imeingizwa kwenye barabara na tukaanza kujua kabisa kwamba kuna barabara zitakazotengezwa, kwenye jimbo langu tu niliondoka hapa na hansard inayoelezea na milioni 600 na nikawapa matumaini.

Sasa leo Waziri wa Ushirika na Masoko na Waziri wa Kilimo na Chakula, wanaposema kwamba ule mpango haupo na zile hela zimekwenda wapi? Yaani hivi wananchi wanakuwa wanapata picha ipi katika hilo?

Sasa naomba ufanuzi aidha, Serikali yenyewe igharamie yale maeneo ambayo wamekosa kile kiwango cha fedha, ili zile barabara zitengenezwe kwa sababu bado kuna wakulima wa kahawa kule hawatuelewi sisi. Zao la kahawa sasa naomba maelezo hapo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Maelezo Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja.

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hapa kwamba fedha za *STABEX* kwa ajili ya kutengeneza barabara zipo na sasa hivi *consultant* anaandaa mpango huo kwa kuanisha ni barabara gani zitakazotengenezwa. Sasa mimi nafikiri kwenye Bunge la mwezi Oktoba itakuwa ndiyo wakati mzuri zaidi wa kupeana taarifa hiyo kazi itakuwa imefikia wapi. Lakini hata ukirudi jimboni ukawahakikishie wananchi, kwamba fedha za *STABEX* zitatumika kutengeneza barabara utakuwa unasema ukweli. Kitu ambacho siwezi kukuambia sasa hivi ni barabara ipi. Ahsante.

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niombe tu kwamba barabara ipi itatokana na mkoa ule kwa sababu unazo barabara zinazoleweka. Lakini nilikuwa najua kwamba Mkoa wa Kigoma tumevangiwa shilingi milioni 600 na ikizingatiwa kwamba wakulima wanaolekea kwa mfano mimi na Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, tuna wakulima wengi sana wa kahawa na waliwahi kupata hela kipindi cha mwaka 1992 au 1993 za *STABEX*. Kwa hiyo, ilipotangazwa wakajenga matumaini. Sasa kwa nini barabara hii isiwalhusu wao na kuna shilingi milioni 600, sasa iwalhusu barabara ya Mwandiga, Manyovu uwape hizo hela zikafanye kazi hiyo. Je, anakubaliana na hilo? (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu kusema ni shilingi milioni 600 au ni shilingi bilioni moja ama shilingi ngapi. Mimi nimetoka Kigoma juzi na nawasifu sana wakulima wa Kigoma wanalima kahawa nzuri kuliko mahali pengine popote nchini, hongereni sana. Tuna hakika mtapata haki yenu ya hizo fedha za barabara ziliozopo. (*Makofi*)

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka maelezo tu katika kitabu hiki cha hotuba nyuma wake wameweka Soko la Kimataifa la mahindi, linazungumzia chai sasa wapi, kuna kitu kingine kipyra mahindi na limejengwa

Soko la Mataifa ambayo haya mazao haya mengine hawana soko la namna hiyo. Nataka maelezo, katika ukurasa wa 53 kuna programu vile vile ya *ADB* vile vile kuhusu *feeder roads* na masoko kujengwa. Soko la Kibaigwa asilimia 70 au 80 ya mazao yanatoka Kiteto.

Sasa ninachoomba kama katika hii programu ambayo umeipata usipoimarisha masoko ya Engusero na Dongo itakuwa vigumu. Nashukuru kwanza Waziri wa Kilimo na Chakula kwamba ameleta mradi mzito wa *PEDP* pale ambao utaimarisha Soko la Kibaigwa la Kimataifa kwa hali ya juu. Je, katika Wizara hii katika hizi kilomita hizi, maana bila barabara sasa *feeder road* kuja katika Soko la Kimataifa kama lilivyotangazwa la kimataifa kama hakuna barabara ya kuleta chakula pale haya yatakuwa magofu kwa hiyo, naomba nijue kwamba hilo yale masoko madogo ya kuimarisha soko la kimataifa mnao utaratibu huo? Nataka tujue hapa kwamba sasa soko la kimataifa linaimarishwa vipi? (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, utaratibu gani? Wanao utaratibu, huo utaratibu gani?

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema ukurasa wa 53 barabara na masoko madogo wameelewa vizuri sana swali langu. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Eee, lakini lazima Mwenyekiti naye aelewé vile vile. Sasa Mheshimiwa Waziri, soko la Kimataifa na barabara. Anaomba maelezo.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa anachosema Mheshimiwa Benedict Losurutia, kwamba katika programu hizi za kuendeleza masoko uko mradi ambao tumesaidiana kujenga soko la Kibaigwa ambao *Rural Markets Project*.

Lakini tunao mpango mwengine ambao tulishautolea maelezo hapa ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu unaohusisha uendelezaji wa masoko ya mazao ya kilimo ambao nimeusema hata hapa nilipokuwa nafanya majumuisho ambao unahusisha mikoa ya Nyanda za Kusini, pamoja na Mikoa ya Kaskazini, Mkoa wa Manyara ukiwa mojawapo ambapo *component* mojawapo ni kuimarisha miundombinu ikiwemo pamoja na barabara. Kwa hiyo, katika kuimarika na kuendeleza kwa utekelezaji wa mradi huo, suala hilo litazingatiwa. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* 198,120,600/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* 453,724,600/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 4001 -*Co-operative Development* 4,673,868,800/=

MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niko kwenye kifungu hiki *Sub Vote 4001 Co-operative Development* (kuendeleza Vyama vya Ushirika).

Nilikuwa nimechangia hapa asubuhi ya kwamba kuna wizi, ubadhirusi, ujambazi uko kwenye vyama hivi na sikusikia tamko la Serikali na kutamka kwao yamkini hiki wakafanya juhudhi za kurusha fedha zile kabla sijafika kule na itakuwa nafuu ya wananchi wangu. Mheshimiwa Waziri, naomba tamko. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri maelezo kabla hajafika kule kwenu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko tulishalitoa nadhani pengine wakati nilipokuwa nafanya majumuisho hapa nilitoa tamko pengine ambalo halielekei kule ambapo anasema yeye.

Mimi nilichosema ni kwamba baada ya kuona kwamba kuna matatizo haya ya ubadhilifu wa fedha za *SACCOS* kule tulipeleka timu yetu ya watalaa ikawafanya ukaguzi na ikawabaini wahusika ambao wamefanya ubadhilifu huo.

Kwa hiyo, tumesema kwamba wale watakuwa *surcharged* kwa maana ya kuwa-*surcharged* ni kwamba kila mmoja atafuatiliwa kama ni kumfilisi na kadhalika. Kwa hilo ndiyo kwamba Serikali sasa hivi inawa-*surcharge* wale wote waliohusika na ubadhirifu huo. (*Makofi*)

MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa tamko hilo hakika tutafanikiwa naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 4002 - *Marketing Development* 823,184,800/=

(*Kifungu kulichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* 548,719,000/=
Kifungu 4002 - *Marketing Development* 3,518,100,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mhesimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo tu, moja lilishatangazwa na Mheshimiwa Spika asubuhi. Lakini sasa hivi kuna tangazo kutoka kwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, kwamba Jumapili tarehe 1 Agosti, 2004 saa tano asubuhi Ukumbi wa *VETA*, Dodoma kutakuwa na Mkutano wa Wabunge wote wanaotoka Mikoa inayolima pamba.

Pili Kamati ya Kilimo na Ardhi, tatu, Wabunge wanaotoka Mkoa wa Mbeya, hili ni tangazo limekuja rasmi hapa, tunaambiwa kwamba kesho kuna semina hapa, kwa hiyo, Mwenyekiti ni yule yule wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka, saa tatu asubuhi. Baada ya matangazo hayo, sasa naahirisha Bunge hadi Jumatatu saa tatu asubuhi. Bunge limeahirishwa.

(Saa 01.34usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 2 Agosti, 2004 saa tatu asubuhi.

